

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 15 Mei, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 200

Mgongano wa Kiutendaji – Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma

MHE. LEONIDAS T. GAMA aliuliza:-

Wananchi wa Songea Mjini wamekuwa wakiitumia Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma kama Hospitali yao ya Wilaya hivyo kufanya kuwepo na mgongano wa kiutendaji katika Mamlaka ya Mkoa inayoitambua Hospitali hiyo kama Rufaa ya ngazi ya Mkoa na Mamlaka ya Wilaya. Tarehe 10 Januari, 2016, Mheshimiwa Waziri wa Afya alifika kuona hali halisi na juhudhi za wananchi wa Songea Mjini za kujenga Kituo cha Afya Mji Mwema ambacho kimefikia hatua kubwa, hivyo wakamwomba Waziri kituo hicho kipandishwe hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya, Songea Mjini.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiacha Hospitali ya Mkoa ifanye kazi ya Rufaa Kimkao?

(b) Je, Serikali haioni haja ya kupunguza msongamano katika hospitali hiyo kwa kuanzisha Hospitali ya Wilaya Songea Mjini?

(c) Je, ni lini basi Serikali itakipa hadhi Kituo cha Afya cha Mji Mwema, Songea Mjini ya kuwa Hospitali ya Wilaya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, Mbunge wa Songea Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma inatakiwa kutoa huduma za rufaa kama

inavyofanyika kwa Hospitali zote za Mikoa nchini. Hata hivyo, mahali ambapo hakuna Hospitali ya Wilaya, wagonjwa hawazulili kwenda katika Hospitali ya Mkoa kwa ajili ya matibabu. Mpango uliopo ni kuimarisha Zahanati na Vituo vya Afya ndani ya Halmashauri ili viweze kutoa huduma kwa wagonjwa wengi ili kupunguza msongamano katika Hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakusudia kuboresha Kituo cha Afya cha Mji Mwema ili kiweze kutoa huduma bora za matibabu kwa lengo la kupunguza msongamano katika Hospitali ya Mkoa kwa sasa. Serikali itatoa kipaumbele kwa mpango wowote wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea juu ya uanzishwaji wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mji Mwema kimeshaombewa kibali kuwa Hospitali. Timu ya Wataalam kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeshakagua kituo na kuelekeza yafanyike maboresho ya miundombinu inayohitajika ili kiweze kukidhi vigezo vya kuwa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea, imepanga kukutana tarehe 17 Mei, 2017 ili kujadili utekelezaji wa maelekezo ya Wizara ya Afya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gama.

MHE. LEONIDAS T. GAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nataka nimjulishe kwamba Hospitali ya Rufaa hiyo ya Mkoa wa Ruvuma ina msongamano mkubwa sana wagonjwa na hasa akinamama wajawazito na watoto. Kwa mfano, hivi sasa Hospitali ya Mkoa ina vitanda 13 tu kwa ajili ya akinamama wajawazito na watoto. Akinamama hawa kwa wastani wa siku ni wagonjwa 25 mpaka 35 wakitumia vitanda 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lipo tatizo la msingi kweli kweli; pale katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa akinamama wajawazito wanunua dawa, damu, mipira ya kujifungulia na vifaa vingine vyote vya kujifungulia, wanunua wenyewe. Sasa nauliza: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa za akinamama wajawazito na watoto zinatolewa katika kiwango kinachotakiwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa vile hivi sasa tunategemea sana Kituo cha Afya cha Mji Mwema ambacho Mheshimiwa Naibu Waziri amesema bado hakijafika mahali kikapandishwa hadhi ya kuwa hospitali kamili. Je, Serikali ni lini italeta gari ya wagonjwa kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wanaofika katika Kituo cha Afya cha Mji Mwema hasa akinamama wajawazito na watoto?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nipokee malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge kwamba pale akinamama wanunua dawa, vifaa tiba na mambo mengine; hili Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ameshali-*cite* pale, ina maana jambo hilo lipo. Katika ziara zangu kwa maeneo mbalimbali nilikuwa nikitoa maelekezo kwamba Serikali inapeleka fedha katika Vituo vya Afya hasa katika Halmashauri zetu; lengo kubwa watu wapate dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa mara kadhaa kwamba kwa kipindi cha sasa suala la uzembe kwamba Serikali inatoa fedha lakini watu hawazitumii kama inavyokusudiwa (kununua dawa na vifaa tiba), niliwaeleza *DMOswote* na Waganga Wakuu wa Mikoa sehemu nilizopita kwamba wahakikishe fedha zinazokwenda lazima ziweze kutumika kama inavyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue *concern* hii, lakini hata hivyo, nafahamu kwamba Rais wetu

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alitoa fedha kwa ajili ya kununua vitanda katika Halmashauri zetu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na hivi vitu vimeshakuwa tayari, naomba na yeye avipokee aende akakabidhi mwenyewe pale. Lengo kubwa ni kupunguza changamoto katika maeneo yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kwamba hakuna *ambulance*; mara kadhaa nimekuwa nikitoa ufanuzi hapa ikiwezekana mchakato uanze katika Halmashauri zetu. Naomba niseme kwamba kilio hiki cha Mheshimiwa Mbunge tumekisikia, japokuwa suala la *ambulance* lazima lianzishwe katika Halmashauri kuonesha yale mahitaji, lakini tutaangalia nini kifanyike sasa kushirikiana pamoja Serikali Kuu na Halmashauri ya Songea ili tupate *ambulance*. Wapi itakapotoka, hiyo haijalishi, lakini cha msingi tupate *ambulance* kwa ajili ya wakazi wengi sana nikijua wazi kwamba hata watu kutoka eneo la Namtumbo wanakuja pale Songea kwa ajili ya kupata huduma ya afya. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mapunda.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa uzito unaoikabili Hospitali ya Mkoa wa Ruvuma ni uzito ule ule unaoikabili Hospitali ya Wilaya ya Mbinga hasa ikizingatiwa Wilaya ile inahudumia Halmashauri kubwa tatu, yaani Halmashauri ya Nyasa, Halmashauri ya Mbinga Mjini na Halmashauri ya Mbinga Vijiji, lakini vile vile sehemu ya Halmashauri ya Songea Vijiji: Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna haja ya kutimiza ile ahadi yake aliyoiahidhi ya kuiboresha ile hospitali ili kuweza kupunguza mzigo mkubwa kwenda Hospitali ya Mkoa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli

Mheshimiwa Mbunge anakumbuka kwamba tulikuwepo kule Mbinga na tumebaini hizo changamoto, ndiyo maana katika mipango yetu ya sasa, tumeamua kwamba Kituo cha Afya cha Kalembo ambacho ukiangalia mahitaji, sasa yamekuwa makubwa.

Kwanza tuboreshe Kituo cha Afya cha Kalembo ambacho siyo muda mrefu sana tunaenda kufanya ukarabati mkubwa sana wa *theater* na wodi ya watoto pale; lengo kubwa ni kwamba huduma ziweze kupatikana vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ndiyo maana wenzenetu kule wa Nyasa tume-*cite* Kituo cha Afya cha Mkiri ambacho tunaenda kufanya huduma hiyo hiyo vilevile. Lengo letu kubwa ni katika maeneo hayo mawili, Nyasa na pale Mbinga, tukiweka huduma za kutosha zitasaidia wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwalongo, Mheshimiwa Dau na Mheshimiwa Japhary. Mheshimiwa Mwalongo, si ulisimama!

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Hospitali ya Wilaya ya Njombe, Kibena ni hospitali ambayo sasa inasomeka kama Hospitali ya Mkao na inahudumia watu wengi sana. Pale kuna tatizo kubwa la watoto njiti na hakuna chumba cha kutunzia watoto hawa njiti. Je, Serikali iko tayari kutusaidia kupata chumba cha watoto njiti pale ili tuweze kuokoa maisha ya hawa watoto? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, anataka kujua tu kama mtamsaidia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuchukue *concern* hiyo, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anafahamu tulikuwepo pale Hospitali ya Kibena. Tutajadili kwa pamoja ili tuone nini tufanye ili eneo lile ambalo ni Makao Makuu ya Mkao pale sasa, japo katika hospitali ile

angalau tuweze kupata *centre* maalum kwa ajili ya watoto njiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa pamoja kujadili nini tufanye kwa ajili ya Hospitali ya Kibena pale iweze kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dau, halafu Mheshimiwa Japhary.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo la Songea Mjini linafanana sana na tatizo liliopo katika Wilaya ya Mafia. Wilaya nzima ya Mafia haina hata Kituo kimoja cha Afya. Ukizingatia kwamba alipokuja Waziri Mkuu tulimwomba suala hili na mchakato tumeshauanza katika ngazi ya Wilaya. Je, ni lini sasa Serikali itatupatia Kituo cha Afya angalau kimoja pale Kilongwe kwa kuongeza hadhi ile zahanati iliyopo pale?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipofika Mafia tulienda katika hicho Kituo cha Afya na nikatoa mapendekezo kadhaa likiwemo suala zima la makazi ya watu katika maeneo yale, lakini tulikubaliana kwamba wafanye mchakato na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dau, kwa sababu Mafia jiografia yake lazima tuboreshe huduma ya afya na nilitoa maelekezo pale mbele ya *DC* na mbele ya Mkurugenzi nini kifanyike kituo kile kiweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Dau kwamba Serikali imechukua ile, tutafanya kila liwezekanalo hasa eneo la Mafia katika kile Kituo cha Afya ambacho nimekitembelea mwenyewe, tutafanya uboreshaji mkubwa katika kipindi kinachokuja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Japhary.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Halmashauri ya Manispaa ya Moshi imekuwa na maombi ya muda mrefu ya Hospitali ya Wilaya na tulikuwa tayari na majibu ya Serikali kwamba wakati wowote watajibu maombi yetu, lakini mpaka sasa hatuoni mwelekeo wowote. Nini tamko la Wizara ya TAMISEMI katika suala hilo la Hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Moshi? (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOÀ NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kweli Halmashauri mbalimbali hazina Hospitali ya Wilaya na siyo Moshi peke yake. Ndiyo maana wakati fulani nilikuwa naongea na dada yangu Mheshimiwa Esther hapa, alileta *special request* na Mheshimiwa Mbunge najua tupo karibu sana. Tukaona kwamba basi angalau tuongeze suala zima la kimkakati la afya katika eneo hilo, japokuwa tuna hospitali yetu kubwa pale ambayo tunaitegemea, ipo chini ya Kanisa ya KCMC, lakini ni lazima tuboreshe huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukaona katika kipindi cha sasa tuboreshe kwanza Kituo cha Afya cha Uru Mashariki ambapo siyo muda mrefu, ndani ya miezi miwili tutapeleka fedha za kutosha pale kufanya marekebisho makubwa sana. Tutajenga *theater* na wodi nyininge pale na vifaa mbalimbali vitawekwa pale. Lengo kubwa ni kupunguza changamoto za wananchi katika eneo lile.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha.

Na. 201

Deni la Pembejeo Mbinga

MHE. MARTIN M. MSUHA aliuliza:-

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016 Mawakala wa Usambazaji Pembejeo kwa Vocha katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga wanaidai Serikali jumla ya Sh.824, 000,000/=

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa deni hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016, Serikali ilitoa ruzuku ya pembejeo kwa utaratibu wa vocha kwa mikoa 25 ya Tanzania Bara. Kazi ya kusambaza pembejeo hizo kwa kaya za wakulima wanufaika wapatao 999,926 ilifanywa na makampuni na Mawakala wa Pembejeo katika Halmashauri zipatazo 144 zilizonufaika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha na uhalali wa madai ya makampuni ya Mawakala waliota huduma ya pembejeo katika Wilaya hizo, Wizara imefanya uhakiki wa awali ambao umefanyika katika baadhi ya mikoa yenyе kiasi kikubwa cha madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uhakiki wa awali imefanyika katika mikoa nane kati ya mikoa 25 ya Tanzania Bara iliyopata ruzuku. Matokeo hayo yameonesha upungufu mkubwa katika madai hayo. Hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki katika mikoa yote kwa makampuni na Mawakala wote

waliosambaza pembejeo katika msimu wa 2015/2016 katika kipindi cha mwezi mmoja. Baada ya uhakiki huo madeni yote halali yatalipwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msuha.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile madeni haya yamechukua muda mrefu; je Serikali iko tayari kufikiria kulipa pamoja na riba kwa Mawakala hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwepo na tatizo la pembejeo ambazo hazina ubora; je, Serikali ina mpango gani kuimarisha ukaguzi wa maduka ya pembejeo za kilimo ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata pembejeo zenye ubora stahiki? Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na madeni ulipwaji wake kucheleweshwa na hivyo kustahili kulipwa riba; nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ucheleweshwaji wa ulipwaji umetokana vilevile na kasoro ambazo hata Mawakala wenywewe wanahusika katika kasoro hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba suala la pembejeo limekuwa ni moja kati ya maeneo ambayo kuna wizi mkubwa sana wa fedha za umma. Kwa hiyo, ukiona kwamba kuna ucheleweshaji kidogo ni kwa sababu tunataka tufanye malipo sahihi, hatutakubali tena fedha za umma ziibiwe na wajanja wachache kwa kisingizio kwamba huduma imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tunathamini mchango mkubwa sana wa Mawakala wa Pembejeo katika kuendeleza Sekta yetu ya Kilimo, lakini niwaeleze tu kwamba hili ni eneo ambalo

Serikali imepoteza fedha nyingi sana. Katika ukaguzi wa awali ambao tumefanya kama Wizara katika mikoa nane ambayo imepata ruzuku kubwa, walikuwa wanadai shilingi bilioni 36. Kati ya hizo ni shilingi bilioni nane tu ambazo zimeonekana zinaweza kulipwa bila utata. Kwa hiyo, unaweza kuona ni kwa kiasi gani tumekuwa tukipoteza fedha nyingi kwa kukimbilia kulipa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, naombeni wale mnaotoka maeneo ambayo pembejeo ya ruzuku imepelekwa, mtufahamishe upungufu unatokea kule. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Keissy kwa sababu yeye amekuja mbele na kutueleza kuhusu udanganyifu uliofanywa na Mawakala katika Jimbo lake. Vilevile juzi Mheshimiwa Flatei Massay, naye kaeleza upungufu uliotokea Wilayani kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kulipa madeni yale ambayo ni sahihi, lakini kwa bahati mbaya sana kuna Mawakala ambao hawana makosa lakini wanapata matatizo kwa sababu ya makosa ya Mawakala ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lazima niseme udanganyifu huu haikufanyika na Mawakala peke yao, hata Maafisa wa Serikali wamekuwa ni sehemu ya mfumo mbovu ambao umekuwa ukiibia fedha Serikali. Kimsingi tu, katika Serikali ya Awamu ya Tano hili hatutaki litokee na ndiyo maana tumebadilisha mfumo na kwa sasa hatuna tena mfumo wa vocha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Ulega.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Swali lilitolizwa na Mheshimiwa Martin Mtonda kuhusu madai ya Mawakala wa Pembejeo Mbanga Vijijini linafanana kabisa na tatizo lilitopo Wilaya ya Masasi Mkoa wa Mtwara na hasa Jimbo la Ndanda; kwamba katika msimu wa kilimo wa mwaka 2016 wakulima wa korosho

na hapa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba hasara nyingine huwa zinasababishwa na watumishi wa Serikali wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jambo hili pia limetokea Mtwara kwa wakulima wa korosho baada ya wamiliki wa maghala kwa kushirikiana na Watendaji wa Chama Kikuu cha Ushirika kuwaibia wakulima pesa zao na kesi zinaendelea kwenye Mahakama. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kutoa pesa zilizopo kwenye Mfuko wa Wakfu na kufidia hasara hii waliyoipata wakulima wakati wao wanaendelea na wale watu waliopo Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.
(Makofii)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uwezekano wa Serikali kulipa fedha ambazo kwa sasa zipo kwenye Mfuko wa Wakfu kwa ajili ya kufidia zile fidia, ingekuwa ni jambo jema, lakini kwa sababu suala lenyewe bado liko Mahakamani, ni vizuri tukasubiri tupate majibu, kwa sababu inawezekana kule Mahakamani, wale ambao tunafikiri wamesababisha hasara ikaja ikatokea uamuzi tofauti. Kimsingi tunataka kila mtu abebe mzigo wake ili kama wale watakuwa wamehusika kulingana na hukumu ya Mahakama, wenyewe watabeba jukumu la kurudisha fedha za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya sisi kama Serikali ni kuhakikisha kwamba matatizo kama haya hayatokei tena. Ndiyo maana tunavyozungumza, tayari Bodii za Vyama vya Ushirika zaidi ya 200 Mtwara na Lindi zimevunjiwa, ni kwa sababu tunajaribu kuwalinda wakulima wasiendelee kuibiwa na watu wachache ambao sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hizo kesi ziko Mahakamani na Afisa ye yote wa Ushirika au wa Serikali

ambaye atabainika kuhusika katika upotevu wa fedha za wakulima, naye vilevile atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha ubora, ni swali ambalo liliulizwa awali ambalo linahusiana na hili. Sasa hivi Serikali ina mpango wa kuagiza mbolea kwa mkupuo (*bulk procurement*) na hii itasaidia sana sisi tuweze kuchagua mbolea ambayo tunahakikisha kwamba inakuwa na ubora. Kampuni yetu inayohusika na ubora wa mbolea itahakikisha kwamba mbolea yote inayoingia ni bora lakini vilevile hata kwa mbegu...

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. Mheshimiwa Mipata.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Mwaka 2016 Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Mkoani Rukwa na alipata nafasi ya kuonana na Wakala wa Mkoa wa Rukwa. Kama tunavyoju, Mkoa wa Rukwa ni mchangaiji mkubwa sana wa uzalishaji wa chakula hapa nchini. Mpaka sasa hakuna kilichopatikana katika madai haya na Wizara imekuwa ikitoa majibu ya namna hii hii kila siku; haioni kama inadidimiza kilimo katika nchi hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawakala wamekata tamaa na ndiyo walikuwa wanatusaidia mkoani kwetu na sasa chakula kitapungua Mkoa wa Rukwa kwa sababu ahadi ya Waziri Mkuu ambaye aliongea na Mawakala, haijatimizwa kwa sababu ya majibu ya kila siku kama haya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Mbadilishie majibu leo. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba majibu yamekuwa ni kama haya kwa sababu huo ndiyo ukweli, kwamba ni vigumu sana sisi kukimbilia kulipa madeni ambayo tunafahamu kuna wizi ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi tunachofanya ni kuhakikisha kwamba tunaondokana na mfumo ambao unarahisisha wizi na ndiyo maana mfumo wa kununua mbolea kwa mkupuo hatutakuwa tena na tatizo la kuanza kuwa na madeni kwa sababu mbolea itakuwa inanunuliwa dukani kama *Coca Cola*. Kwa hiyo, tunachosema, watuvumilie tu, hatuwezi tukalipa fedha ambazo ni wazi ni za wizi. Tuna ushahidi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ulega.

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba inaondoa migogoro hii ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo na kwetu sisi wakulima wa korosho, hapa juzi Serikali imetutangazia kutupatia *sulphur* kwa maana ya pembejeo ya kilimo bure. Je, Serikali imejipangaje katika usambazaji wa *sulphur* hii ya bure ili iweze kutufikia kwa wakati na ya kutosha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuja kueleza wakati wa hotuba ya bajeti yetu Ijumaa kuhusiana na hatua mbalimbali ambazo tumechukua kuboresha mifumo ya usambazaji wa pembejeo katika mazao mbalimbali ikiwepo zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niseme tu kwamba *sulphur* itagawiwa kwa utaratibu ambao umewekwa na Bodi ya Korosho. Kimsingi, hatuamini kwamba itawezekana tena *sulphur* ichelewe, kwa sababu kwa sasa maana yake inakuwa inatolewa bure na yule ambaye anagawa inakuwa ni Bodi. Kwa hiyo, tusubirie tutasikia kuhusu huo utaratibu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Flatei.

Na. 202

Minara ya Mawasiliano ya Simu

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Wananchi wa Mbulu Vijiji ni hawana mawasiliano ya simu wala minara katika Kata za Tumati, Yaeda, Ampa, Gidhim na Gorati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka minara katika Kata hizo ili kupata mawasiliano?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, ilainisha maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Mbulu likiwemo Jimbo la Mbulu Vijiji na kuyaingiza maeneo hayo katika miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa. Kijiji cha Yaeda Ampa kutoka Kata ya Yaeda Ampa kimeingizwa katika zabuni ya mradi wa kufikisha huduma ya mawasiliano kwa maeneo ya mipakani na kanda maalum. Zabuni hii ilifunguliwa tarehe 27, Aprili, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yetu kuwa Kijiji cha Yaeda Ampa kitapata kampuni ya kufikisha huduma ya mawasiliano na kuondoa kabisa tatizo la mawasiliano katika kata hiyo. Aidha, Kata za Tumati, Gidhim na Gorati zimeingizwa katika orodha ya miradi itakayoteklezwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka nimpe taarifa kwamba katika Kata ya Hayderer kuna mnara wa *Airtel*/umeanzishwa, una miaka miwili, haujamalizika kabisa, uko kwenye *foundation*. Sasa kwa kuwa Kata za Yaeda Ampa na Tumati zinakaribiana. Je, Wizara iko tayari sasa kujenga mnara katikati ya kata hizi ili angalau katika mnara huu uliotangazwa *tender*, kata hizi mbili zikapata mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa maeneo mengi mitandao haifiki, maeneo ya Endagichan, Endamasak, Enargatag, Runguamono, Munguhai, Gembak na Gidamba. Serikali sasa ituambie, ina mpango gani tena wa kuingiza vijiji hivi na kata hizi ili angalau basi Jimbo langu lipate mawasiliano? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Umeona swali hili wamesimama Wabunge 42! Kwa hiyo, jibu kwa kifupi, uwajibu wote hao 42.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafuatilia mnara wa *Airtel*/ambao amesema umekaa kwa muda mrefu katika kiwango cha msingi. Tutafuatilia tuone tatizo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu ombi la kujenga katikati ya zile kata mbili; tumelipokea na tutalifuatilia na vilevile vijiji vyote ambavyo amevitaja tumepokea ombi hili, tutaangalia namna ya kuyashughulikia ili hatimaye vijiji hivyo vyote vipate mawasiliano. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Adadi, Mheshimiwa Nape, Mheshimiwa Bilago. Tuanze na hao kwanza.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Matatizo ya mawasiliano ya Mbulu Vijijini yanafanana sana na matatizo ambayo yapo kule katika

Tarafa ya Amani Jimbo la Muheza hususan kwenye Kata za Misarai, Kwezitu, Mbomole na kwingineko. Sasa Serikali ina mpango gani kupeleka minara kwenye sehemu hizo na Tarafa hiyo ambayo kwa kweli mawasiliano ni tabu sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kupeleka mawasiliano ya uhakika katika Tarafa ya Amani tukiunganisha kata zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Namwomba Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab tuwasiliane ofisini ili tupitie kwa pamoja, tuone kata gani imesahaulika katika zile ambazo Serikali tayari imezingiza katika mipango yake ya kutekeleza mawasiliano kwa wote.

MWENYEKITI: Ahsante. Nimeshawataja Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Bilago.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la mawasiliano ya simu katika Jimbo la Mtama ni baya kuliko ilivyo katika Jimbo la Mbulu Vijijini, kwa sababu katika Tarafa tano; Tarafa tatu mawasiliano ya simu ni tabu sana, wakati mwingine inabidi upande juu ya mnazi au juu ya kichuguu ili uweze kuwasiliana. Tulianza kupata matumaini baada ya Kampuni ya Viettel kuanza kusambaza minara, tukadhani hali itarekebishika, lakini inaonekana kama kazi ile kama imesimama hivi.

Sasa ni lini kazi ile itakamilika ili wananchi wangu waweze kufaidi matunda ya kazi nzuri ya mawasiliano ya simu katika Jimbo la Mtama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Anataka kujuu ni lini, tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, haikubaliki kati ya tarafa tano, tarafa mbili tu ndiyo zipate mawasiliano ya

uhakika, hiyo haikubaliki. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutalifuatilia hili, nini hasa kimesababisha ujenzi wa minara katika maeneo hayo kusimama na baada ya hapo tutaangalia namna ya kushughulikia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo lillipo Mbulu Vijiji linafanana kabisa na tatizo lillipo Wilaya ya Kakonko. Wilaya ya Kakonko Kata za Nyamtukuza, Nyabibuye, Warama, Muhange, Kasuga na mwambao wote wa Burundi, simu zinaingiliana na mitambo ya Burundi na hivyo wananchi wa Wilaya ya Kakonko maeneo hayo yanayopakana na Burundi wanapata hasara kubwa sana kwa kuongeza vocha ambazo zinaliwa na mitandao ya Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *commitment* ya Serikali hapa; Serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha kwamba wananchi hawa hawapati hasara katika matumizi yao ya simu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo aliyoyataja, kama alivyosema, yako mpakani na tuna mipango maalum ya kushughulikia maeneo ya mipakani. Nitakwenda kuangalia ni kwa nini hasa eneo lake bado halijaboreshwa kwa namna ambavyo ameeleza?

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kutokana na muda wetu, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

Na. 203

Utafutaji wa Mafuta na Gesi Mlimba

MHE. SUSAN L. KIWANGA aliuliza:-

Serikali inafanya zoezi la kimya kimya la utafutaji wa mafuta na gesi katika Jimbo la Mlimba bila kutoa taarifa rasmi kwa wananchi juu ya zoezi hilo:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mchakato huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Kilosa Kilombero unaofanywa na Kampuni ya *Swala Energy* ilianza mwezi Februari, 2012. Kampuni hiyo ilianza kufanya utafiti wa awali wa kijiolojia kwa ajili ya kutambua aina na sifa za miamba iliyopo na kutoa taarifa ya mitetemo (*seismic data*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na tafiti hizo, kampuni ilionesha uwezekano wa kuwepo kwa mafuta na gesi asilia katika eneo hilo. Eneo lilioloainishwa kwa ajili ya uchimbaji wa kisima hicho lipo katika Kijiji cha Ipera Asilia katika Hifadhi Tengefu ya Bonde la Kilombero. Uchimbaji unatarajiwaka kuanza mwezi Septemba, mwaka 2017 baada ya utafiti kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari, 2017, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) ilianza kutoa elimu kuhusu utafiti wa mafuta na gesi asilia na fursa zitakazopatikana kwa wananchi wa Mlimba hasa katika maeneo yanayozunguka mradi huo. Elimu hiyo itahusu pia athari za mazingira na ushiriki wa wananchi katika miradi

mbalimbali kwa manufaa ya wananchi pamoja na Taifa kwa ujumla.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Najua Naibu Waziri haya majibu amepata kwa wataalam, lakini ukweli ni kwamba katika Jimbo la Mlimba hakuna Kijiji kinachoitwa Ipela Asilia. Ipela Asilia ipo Wilaya ya Malinyi, Halmashauri mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyofuatilia Malinyi, Madiwani hawana taarifa yoyote, hata Baraza la Madiwani halina taarifa yoyote kuhusu hizi taarifa, wanaona tu watu wanaingia na kutoka. Ni kweli kabisa pale uwezekano wa mafuta upo mkubwa sana, wameshachimba kisima kimoja cha mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swalilangu; kwa kuwa eneo hilo ni eneo nyeti, wanapatikana wale wanyama wasiopatikana duniani (puku), lakini Serikali inakwenda kutoa kibali cha kuchimba hayo mafuta na wananchi wanaozunguka hili eneo wamekatazwa kabisa kufanya shughuli za kibinadamu katika eneo hili.

MHeshimiwa Mwenyekiti, nataka majibu ya Serikali, ni lini sasa watakwenda kuwaelimisha hawa wananchi na kuwapa wao maeneo ambayo wanaweza wakaendeleza shughuli zao za kilimo wakati mradi huu unaendelea na elimu hajijatolewa katika kijiji hicho ambapo ni Kata ya Njiwa na Kata ya Itete; nimezungumza na Madiwani usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalilangu la msingi; kwa kuwa amesema Mlimba; Mlimba katika Kata ya Mofu, Bwawa la Kibasila kuna utafiti ulifanyika na Mzee Magoma alikuwa Mkalimani wa wale Wazungu na ukweli ni kwamba Bwawa la Kibasila Kata ya Mofu, Kijiji cha Ikwambi kuna uwezekano mkubwa wa kupata mafuta kwa sababu kuna mikondo miwili inayotoka Ihenga na Mofu na Ikwambi na mkondo

mwingine unatokea Mngeta, inakutana pale, kwa hiyo, wakasema kuna uwezekano mkubwa wa kupata mafuta.

Sasa nauliza swali hili kuhusu Jimbo la Mlimba; ni lini sasa Serikali itakwenda katika Jimbo la Mlimba ikibidi waonane na huyu Mzee Magoma awaambie hali halisi, kwa sababu kuna uwezekano mkubwa wa kupata mafuta, lakini leo wamenijibu swali la Malinyi. Kwa hiyo, swali langu bado halijakidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu. Mheshimiwa Waziri mhusika.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipande kusema tu kwamba hatutakwenda kwa mzee yejote kumuuliza uwezekano wa mafuta kupatikana, kwa sababu hili ni suala la kitaaluma, tutachukua utafiti uliofanywa *Seismic Surveys* ambayo kuna 2D na 3D, hizo ndizo zitakazotupeleka kule. Kwa hiyo, hatutakwenda kwa mzee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tena, mbali ya mchanganyiko wa majina, tunaomba radhi kama tumechanganya majina, lakini utafutaji wa mafuta, nataka kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, sehemu nyingine duniani watu wametafuta mafuta wameyakosa, lakini baada ya kubadilisha mbinu na namna ya kutafuta mafuta, wengine wakaja wakayapata. Kwa hiyo, hili ni jambo la kitaaluma na kitaalam, halina mjadala wa mambo ya kisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu hilo ni kwa wote.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga. Kwa niaba yake Mheshimiwa Musukuma, hayupo; Mheshimiwa Susan Lyimo.

Na. 204

Matumizi ya Shisha

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. NAJMA MURTAZA GIGA) aliuliza:-

Matumizi ya SHISHA yamegundulika kuwa ni miongoni mwa aina ya uvutaji wa sigara ambao wauzaji wengine huchanganya na aina mbalimbali za dawa za kulevyu na vimeo vikali na kusababisha vijana wadogo kuathiriwa kwa kiasi kikubwa.

Je, kwa nini Serikali hadi sasa inaendelea kuruhusu matumizi ya SHISHA kwenye baadhi ya migahawa na hoteli kubwa ambayo inatumiwa na watu wa rika zote?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Giga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali mara baada ya kuona kuwa matumizi ya shisha yanaleta athari kubwa kwa afya za binadamu, kutohana na utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya, Serikali ina mpango mkakati wa kutengeneza utaratibu wa kudhibiti na kutungia sheria kupiga marufuku utumiaji, uuzwaji na usafirishwaji wa shisha nchini Tanzania ili kuweza kuokoa afya za Watanzania walio wengi ambao ni nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tukiwa tunasubiri kutungwa kwa sheria na kanuni, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaelekeza kupiga marufuku matumizi ya shisha na utekelezaji ulishaanza kutekelezwa mikoani ikiwemo Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Kilimanjaro na mikoa mingine.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini ni wazi kwamba siku za nyuma kulikuwa na mgogoro kati ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Bwana Siro kuhusiana na suala hili. Naomba kujua wakati ambapo Polisi walisema hakuna, lakini Mkuu wa Mkoa alikuwa anasema zipo.

Je, huu mgogoro umeishia wapi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hakukuwa na mgogoro wowote kati ya Kamanda wa Kanda Maalum na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ni viongozi wanaofanya kazi kwa pamoja na mara zote maelekezo ya Kamati ya Ulinzi na Usalama imekuwa ikielekezwa kwenye utekelezaji na shughuli hiyo imeendelea kufanyika na kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaelekeza na Mikoa yote imeitikia na sisi kama Wizara tunawaaelekeza wote wanaokuwa *field* kuhakikisha kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yanafanyiwa kazi bila kupunguza hata nukta.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante nami nataka kujua hapo kwamba kwa kuwa wakati shisha linapigwa marufuku, huku nyuma kuna watu walikuwa wamepewa leseni ya kufanya hiyo biashara kwa sababu ilikuwa inaonekana ni biashara halali. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu hilo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Selasini jiandae.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yote yanayohusu afya za Watanzania ni kipaumbele cha Serikali na kwa kuwa ni kipaumbele cha Serikali, jambo la kwanza tunalofanya ni kuokoa maisha ya

Watanzania. Wakati tunafanya hivyo, ndiyo maana tunasema tunaliwekea utaratibu mzuri wa Kisheria na hivi tunavyoongea, ukienda kwenye ukurasa wa 15 wa kitabu cha hotuba ya Waziri wa Afya, ameongelea utaratibu ambao utachukuliwa na tayari alishatungia kanuni. Kwa hiyo, inasubiria mashauriano ya mwisho ndani ya Serikali ambayo yanazingatia *concern* aliyoitoa Mheshimiwa Shangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Shangazi, n kwa kutambua kwamba hilo jambo lilikuwepo lakini ni lazima tuzingatie afya za Watanzania na tuzingatie utaratibu ambao utaweka utaratibu wa kisheria wa kudumu ili kuweza kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinalindwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vijana wengi wanaotumia shisha, bangi, madawa ya kulevyaa na pombe kali kali hizi, wanatumia kutokana na kukata tamaa katika maisha; nami siamini sana katika kutunga sheria, kuwakamata na kuwaadhibu. Mfano mzuri, juzi Waziri Mkuu Serikali ilipiga marufuku utumiaji wa viroba, lakini sasa kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri kilevi kingine kimeanzishwa. Sasa vijana wanaanza kuvuta gundi kitu ambacho ni kibaya zaidi. (*Makofii*)

Sasa Je, sisi kama Taifa, Serikali kuna utaratibu gani wa kuwasaidia vijana hawa ambao wengi wamekata tamaa ili waweze kupata matumaini katika maisha na waache mambo hya bila lazima ya kutunga sheria au kuwakamata?

MWENYEKITI: Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti nimshukuru sana Mheshimiwa Selasini kwa swali lake la nyongeza. Kubwa ambalo tunalifanya sasa hivi ili kuwaepusha vijana wa Kitanzania na matumizi ya tumbaku na vileo ni kuendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia Luninga na redio, lakini pia

tumechapisha vijarida mbalimbali ili kuonesha madhara ya tumbaku pamoja na matumizi ya pombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, wale ambao walikuwa tayari wanatumia kwa mfano, madawa ya kulevyta, tumeanza mpango wa kuongeza vituo vyta kutoa dawa (*Methodone*). Kwa hiyo, siyo tu Dar es Salaam lakini tutaanzisha Mbeya, Arusha, Tanga, Kilimanjaro pamoja na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kubwa ni kwamba leo ni siku ya familia, kwa hiyo, tunatoa wito kwa wazazi, walezi kutimiza wajibu wao wa msingi wa malezi bora kwa watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa sababu nimepata pia fursa ya kusema leo ni Siku ya Familia Duniani. Kwa hiyo, familia bora ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Ni kweli, Waheshimiwa Wabunge, wananchi, wazazi, hili suala siyo la Serikali peke yake. Kila mzigo mkiipa Serikali itashindwa, hawa watoto wanaoumia ni wetu, ni sisi wenyeewe ndiyo tunawalea siyo Serikali. Mheshimiwa Ditopile.

MHE. MARIAM D. MUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. Swali langu, je, kwa tafiti ambazo zimefanywa nchi nydingi sana, ikiwemo kwa nafasi kubwa nchi za Kiarabu, sigara ina madhara makubwa, mara dufu kuliko hii Shisha na kila siku tunasema ajira, ajira. Biashara ya Shisha ilikuwa inaa jiri vijana wengi sana na kweli wamepata matatizo tangu hili zuio.

Swali langu kwa Serikali; je, mlifanya utafiti wa kutosha wa kuona kwamba hii Shisha ina madhara makubwa kuliko sigara? Nashukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mariam kwa kutaka kujua kuhusu utafiti wa jambo hili. Nimhakikishie tu kwamba jambo hili lilifanyiwa utafiti na Wizara ya Afya na hivi vitu ambavyo vina vilevi, ubaya wake ni kwamba vijana wetu hawavitumii peke yake, wanachanganya na vitu vingine, kwa hiyo, wanaongeza makali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, nimhakikishie Mheshimiwa Mariam kwamba vijana bado wana fursa nyingi sana na nitolee mfano wa kwake yeche mwenyewe, ni mmoja wa vijana wanaofanya vizuri sana kwenye kilimo na yeche ni shahidi na amefanikiwa sana; ni mmoja wa Waheshimiwa Wabunge vijana waliofanikiwa sana kwenye kilimo. Kwa maana hiyo, vijana wengine wanaweza wakaiga mfano ule, wakalima mazao ya biashara. Mheshimiwa Mariam analima ufuta, wao nawakaribisha walime alizeti ama mazao mengine yanayostawi katika mikoa yao ili waweze kufanya biashara iliyohalali isidhuru maisha ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira ya kudumu, ndiyo maana Mheshimiwa Rais ana mpango wa muda mrefu wa kukuza uchumi kwa kuhakikisha kwamba fedha zote zinatumika vizuri ili kuweza kutengeneza uchumi wa viwanda, uchumi unaojitegemea, uchumi unaotengeneza ajira nyingi ambazo zitakuwa zinaingiza kipato halali kwa vijana na afya za Watanzania.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Bobali.

Na. 205

Miundombinu Mibovu ya Gereza Kingulungundwa

MHE. HAMIDU H. BOBALI aliuliza:-

Gereza la Kingulungundwa liliopo Wilayani Lindi linakabiliwa na uhaba mkubwa wa Nyumba za Askari na miundombinu mibovu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha makazi ya Askari katika Gereza hilo?

(b) Gereza hili lipo umbali wa kilometra tatu kutoka barabara kuu inayotoka Dar es Salaam kwenda Lindi, lakini wakati wa masika, barabara hiyo haipitiki kwa gari kutokana na kujaa tope na maji. Je, Serikali haioni kuwa kukosekana kwa mawasiliano ya barabara kutoka Gerezani ni jambo la hatari?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu kuwa lipo tatizo la uchakavu na upungufu wa nyumba za Askari wa Jeshi la Magereza nchini na hali hiyo inatokana na baadhi ya nyumba kujengwa kabla ya uhuru ama katika maeneo mengine ambapo zilijengwa kwa matumizi ya muda wakati ikitabu ujenzi wa nyumba za kudumu na za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya nyumba za Askari Magereza hivi sasa ni nyumba 14,500 wakati zilizopo ni nyumba 4,221, hivyo kuwepo kwa upungufu wa nyumba 10,279 ambaa unasababisha baadhi ya Askari kuishi nje ya Kambi. Kwa sasa Serikali ina mpango wa kuwajengea Askari Magereza nyumba 9,500 na mara baada ya mpango huo kukamilika tunategemea kumaliza kero za makazi ya Askari Magereza nchini likiwemo Gereza alilolitaja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imeendelea na mpango wa kuzifanya ukarabati mkubwa baadhi ya nyumba kwenye baadhi ya Magereza na kujenga nyumba mpya. Ni nia ya dhati ya Serikali kuendelea kuboresha nyumba za Askari nchini zikiwemo za Gereza la Kingulungundwa kwa awamu. Kwa sasa, Jeshi la Magereza linajenga nyumba 320 za Maafisa na Askari hapo

Ukonga na fedha ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameshatoa ni shilingi bilioni 10 na shilingi bilioni tano tayari zilishatolewa kwa ajili ya ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara inayotoka barabara kuu ya Dar es Salaam kuelekea Gereza la Kingurungundwa imekuwa haipitiki kwa gari wakati wa masika. Kimsingi barabara hiyo ipo chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Lindi vijiji na ndiyo yenye jukumu la kuifanya matengenezo barabara hiyo kwa kuwa haiishii Gerezani tu, bali inaendelea kwenye vijiji vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Magereza limeshafanya mawasiliano na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lindi Vijini ili barabara hiyo iweze kutengenezwa na kuepusha adha inayojitokeza wakati wa masika.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini majibu aliyonijibu ni *too general*. Mimi niliulizia suala la Kingulungundwa lakini ametoa takwimu nyingi za Magereza ya Ukonga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı langu la kwanza la nyongeza; nahitaji kufahamu hizi nyumba 320 ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema zinajengwa huko Ukonga na maeneo mengine; je, katı ya hiso, Kingulungundwa zinapelekwa nyumba ngapi? (*Makofı*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalı la pili, katika Gereza lile, kuna shida kubwa ya maji ambayo inasababisha wakati mwingine wafungwa na Askari watumie muda mwingi kabisa kutafuta maji. Kama inavyofahamika, hili ni Gereza maalum kwa Mkoa wa Lindi, limewekwa mbali kidogo na makazi ya wananchi kwa kazi maalum ambayo nadhani Mheshimiwa Waziri anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kupata *commitment* ya Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itawapatia maji Gereza la Kingulungundwa na jirani zao wa Mjimwema ili kuondoa adha ambayo wanaipata wafungwa na Maafisa wa Gereza lile? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Bobali, *Goal Keeper* wa Timu ya Bunge ya Wabunge wa Yanga, kama ifuatavyo:- (*Makofii*)

Moja, suala la nyumba za Ukonga; tulikuwa tunaelezea tu *commitment* ya Serikali kuhusu nyumba za Askari Magereza kwa maana ya kwamba zinajengwa kule, tunaendeleza ili kutatua tatizo hilo na tunakamilisha nyumba nyingine ambazo ziko katika hatua za mwisho ili Askari waweze kuhamia, hatuzihamishi zile za Ukonga kwenda Gereza lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upande wa maji, hata wakati napitisha bajeti, Mheshimiwa Salma Kikwete aliniambia hatashika shilingi, lakini anaomba siku nikipita Lindi niende kwenye Gereza hilo kujionea tatizo hilo la maji. Mheshimiwa Mbunge amelitaja jambo hili, naweka uzito, nitakapozungukia kule, nitahakikisha napita kujionea lakini hoja hiyo tumeshaipokea kama Serikali kuhakikisha kwamba tunaweka kipaumbele kuweza kuhakikisha kwamba suala la maji linaenda sambamba na hilo la barabara ambalo lilikuwepo kwenye swali la msingi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nditiye.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Gereza kuu la Wilaya ya Kibondo pamoja na kuhudumia Watanzania na mahabusu kwa wafungwa, linahudumia vile vile mahabusu na wafungwa kutoka nchi jirani ya Burundi kwa maana ya Wakimbizi kwa wingi sana. Lina upungufu mkubwa sana wa maji na Shirika

la Kuhudumia Wakimbizi la *UNHCR* liliahidi kwamba litasaidia kuleta mradi wa maji kwa Gereza lile na taarifa tulishazitoa mpaka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Je, Srikali imefikia hatua gani kuwalazimisha sasa wale watu wa *UNHCR* walete maji katika Gereza hilo la Kibondo? Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri bajeti yake imepita wiki iliyopita, ndiyo kwanza amepata pesa, anashughulikia matatizo yenu yote. Sasa ukijibu, jibu kwa Magereza yote yaliyokuwepo.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana. Nampongeza Mheshimiwa Nditiye kwa kufuatilia jambo hili na mara kwa mara tukionana, amekuwa akinikumbushia jambo hili hili. Nimwambie tu kwamba, kati ya wiki hii mpaka wiki ijayo, timu ya Wawakilishi wa Shirika la Wakimbizi Duniani hapa kwetu nchini, pamoja na wadau wanaoshughulikia masuala ya wakimbizi, watazungukia Mkoa wa Kigoma, watazungukia makazi likiwemo Gereza hilo na moja ya ajenda kubwa wanayokwenda kufanya ni kuangalia miundombinu jinsi inavyoweza kusaidia uwepo wa watu wengi katika Makambi pamoja na Magareza kama hilo ambalo amelitaja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Lathifah Chande.

Na. 206

Hitaji la Kiwanda cha Ufuta - Liwale

MHE. LATHIFAH H. CHANDE aliuliza:-

Uzalishaji wa zao la ufuta limeongezeka kwa msimu wa mwaka 2015/2016 na kusababisha kushuka kwa bei ya ufuta sokoni:-

Je, ni lini Serikali itajenga kiwanda cha kukamulia ufuta Wilayani Liwale?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa mavuno ya zao lolote yakiongezeka, bei yake sokoni inaweza kushuka. Sera ya Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iweze kujenga viwanda na kuwekeza katika biashara. Kufuatia uhamasishaji huo, Mkoa wa Lindi una jumla ya viwanda 11 vya kukamua mafuta, viwili vikiwa mahususi kukamua mbegu za ufuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jukumu la msingi la Serikali limebaki katika kuhamasisha sekta binafsi, Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji ili kuwekeza katika usindikaji wa mafuta ya ufuta Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Wizara yangu katika kuhamasisha wajasiriamali wa Wilaya ya Liwale waweze kuwekeza katika usindikaji wa mbegu za ufuta. Kiwango cha ufuta kinachozaishwa Wilaya ya Liwale kwa sasa kinakidhi uwekezaji mdogo na wa kati ambaio wananchi na wajasiriamali walliopo wakihamasishwa wanaweza kuwekeza katika usindikaji wa mbegu za ufuta.

Mhesjhimiwa Mwenyekiti, mashine ndogo sana ya kukamua mafuta ya ufuta, inakadiriwa kuwa na gharama kati ya shilingi milioni 10 mpaka 15 na mashine ndogo ni kati ya shilingi milioni 16 mpaka 200. Mashine ya kati inayoweza kukamua na kuchuja mara mbili (*double refinery*) inagharimu kati ya shilingi milioni 200 mpaka 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika wananchi wakihamasishwa wanaweza kuijunga katika vikundi na kuweka mitaji yao pamoja na kuweza kununua mashine

ambayo ina uwezo wa kuchuja mara mbili (*double refinery*) yenye kuzalisha mafuta yenyeye soko zuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai pia kwa Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wananchi walio katika Majimbo yenye kuzalisha mbegu za mafuta waweze kushiriki katika kuanzisha viwanda vya kukamua mafuta kwa viwango mbalimbali. Wizara itakuwa nyuma yao kutoa ushauri na mafunzo ya kiufundi pamoja na kuelekeza mahali mashine zinapopatikana kupitia Taasisi zake za *SIDO*, *TEMDO* na *TIRDO*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lathifah.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kutoptaka na kwamba *demand* ya Soko la Dunia ni ufuta mweupe, lakini Tanzania tumekuwa tukillima ufuta wa *brown ambao* bei yake inakuwa haina thamani kubwa kama ilivyo ufuta mweupe: Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia wakulima wa ufuta nao waweze kuanza kulima ufuta mweupe ili kuweza kuongeza kipato? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni juu ya Kiwanda cha Korosho kilichopo Lindi, Kiwanda cha *TANITA* ambacho kilikuwa kinaendeshwa na Serikali na kiliweza kuwapatia ajira wananchi wengi. Sasa hiki Kiwanda cha Korosho, *TANITA*, kimebinafsishwa ambapo hamna shughuli yoyote inayoendelea baada ya ubinafsishwaji huu na kupelekea wananchi kukosa ajira. Je, Serikali ina mpango gani juu ya kukifufua kiwanda hiki kutoptaka na kwamba Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ni Tanzania ya viwanda? Ina mpango gani juu ya kufufua hiki kiwanda na viwanda vingine vingi vilivyoko Mkoani Lindi? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Hoja yake ni lini? Wewe mpe ahadi tu, ni lini?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lathifah ameuliza swali lake la kwanza wakati muafaka; bajeti ya Wizara ya Kilimo

inafuata nami nitamhimiza Waziri wa Kilimo kwamba tulete mbegu zinazozalisha ufuta mweupe ambao una soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kiwanda cha korosho, Serikali ina mpango gani? Mpango wetu ni kuhakikisha kwamba viwanda vyote vilivyobinafsishwa vinafanya kazi. Hatuendi kwa kasi inayotakiwa kama nitakavyoeleza kwenye bajeti yangu kesho kutwa, ni kwa sababu viwanda vingine vina matatizo ya mikataba ya kisheria, lakini dhamira yetu ni hiyo na tutahakikisha viwanda vyote vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na viwanda hivi, wako wawekezaji wanakuja na nitahakikisha Mheshimiwa Mbunge tunashirikiana kwamba Waheshimiwa Wabunge wanaokuja waende Lindi na nimeshazungumza hata na ndugu yangu, viwanda vingi vitakwenda vitaanzishwa ikiwemo na kufufua vile nya zamani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Khadija Nassir na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Swali langu ni kwamba, kwa kuwa Mkoa wa Pwani wanalima sana matunda ya aina mbalimbali na kwa kuwa kiwanda kipo eneo moja tu Mkuranga ambacho sasa hivi kinazalishana kiwanda kingine kinajengwa Chalinze. Je, ni lini Serikali itawashawishi wenyе Kiwanda hicho kuhakikisha wanakuwa na maeneo maalum ya kuwasaidia wakulima kwenda kupeleka mazao yao na kuza badala ya kutafuta magari na kupeleka mpaka kwenye kiwanda? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, ni lini?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kiwanda cha Evelyn kinachokausha matunda asilia na Kiwanda cha Sayona kitakachochakata matunda ya aina zote, mara wanapoanza uzalishaji wataweka *collection point*. Evelyn

wakati wowote atazinduliwa na kuanza kazi, mboga tunategemea aanze mwezi wa Tisa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir, jiandae Sophia.

MHE. KHADIJA N. ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali imekuwa ikiagiza tani laki nne za mafuta kila mwaka, wakati tuna malighafi za kutosha hapa nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mazao hayo ipasavyo ili kuweza kuokoa fedha za kigeni zinazopotea kwenye kuagiza mafuta hayo nje ya nchi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, ni lini? Kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatumia mafuta tani laki nne kwa mwaka na *70 percent* inaagizwa kutoka nje. Tunahamasisha ulimaji wa alizeti; tuna mpango wa kulima migaze au michikichi Kigoma na Pwani; pindi tutakapokuwa tumejitosheleza, tutaweza kuzuia mafuta kutoka nje. Hatuwezi kufanya makosa ya kuzuia mafuta kutoka nje, matokeo yake ni kwamba mafuta yatapanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma wakiwa tayari, Pwani wakawa tayari na alizeti zikawa za kutosha, hatutazuia ugavi kutoka nje. Ugavi kutoka ndani utazuia mafuta yasije. Sisi ni *memberwa WTO* na katika mpango wa *WTO*, bei ni nguvu ya soko inayomzuia mshindani asiingie kwenye soko letu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa nchi za Uturuki, Ujerumanu na Italy wanakunywa sana chai ya Tanzania. Je, ni lini Serikali itapeleka Kiwanda katika Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya wakulima wa chai ili waweze kuuza chai yao ambayo ni nyingi ikaweza kusaidia katika hizo nchi nyingine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, swali tofauti lakini lijibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo ni nguvu ya soko. Mheshimiwa Sophia tumeshazungumza kwenda kwenye maonesho ya Kimataifa kwenda kutafuta hayo masoko. Leta hizo *order* zako kusudi *demand pool* iwashawishi watu wachakate chai. Kuna watu wana chai hawana soko, sasa wewe nimeshakuruhusu uende kwenye maonesho. Nenda basi ulete hizo *order*. (*Kicheko/Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Sima.

Na. 207

Maeneo ya Uwekezaji Singida Mjini

MHE. MUSSA R. SIMA aliuliza:-

Singida Mjini ni Mji unaokuwa kwa kasi sana na tumetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji:-

Je, Serikali iko tayari kuleta wawekezaji?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-

Mheshimimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamashajili wa uvutiaji wa uwekezaji ni jukumu la msingi la Serikali. Katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 imeelezwa wazi kwamba malengo ya Serikali ni kuongeza kasi ya kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje katika sekta zenye tija kwa Taifa. Hivyo, Wizara yangu

imekuwa ikihamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini ikijumuisha Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kivutio cha msingi cha uwekezaji ni uwepo wa maeneo ya uwekezaji. Hivyo, Serikali imeendelea kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Mikoa na Wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Kutokana na juhudhi hizo, hadi kufikia Aprili, 2017, jumla ya Mikoa 13 imewasilisha taarifa ya utengaji wa maeneo katika mikoa yao. Napenda kuchukua fursa hii kuupongeza Mkoa wa Singida kwa kuitikia wito huo na tayari wametenga hekta 6,595.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha kuanzia mwaka 1996 hadi Aprili, 2017, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania, imefanikiwa kuandikisha miradi 33 kwa ajili ya Mkoa wa Singida yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 997.879. Kwa muhtasari huo, kazi iliyofanyika katika uhamasishaji uwekezaji Mkoani Singida, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Singida kuwa Serikali itaendelea kuvutia wawekezaji kuwekeza katika Mkoa wa Singida. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sima.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, namwomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Jimbo la Singida Mjini kwamba miradi hiyo aliyoitaja, miradi 33 iliyosajiliwa yenye kutoa ajira zaidi ya 4,000 itaanza lini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa Serikali imehamia Dodoma na yako Mashirika ndani ya Wizara, Ofisi za Kanda zipo Dodoma: Je, Mheshimiwa Waziri, sasa upo tayari Mashirika hayo kwa mfano *TFDA, TBS* na mengine kuanzisha Ofisi za Kanda Singida Mjini ili kuweka ufanisi wa kazi hiyo? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile miradi 33 niliyoisema, nimesema kuanzia mwaka 1996 mpaka Aprili, 2017, mionganoni mwa viwanda hivyo ni kiwanda cha mafuta cha *Mount Meru*, kimeshaanza kazi. Viwanda hivyo vimeshaanza kazi; na mojawapo ya viwanda hivyo ni Kiwanda cha Maziwa anachokijasiria Mheshimiwa Kingu. Tumeshaanza kazi. Tanzania sasa tunajenga viwanda. Sasa labda anieleze wapi anataka mimi nisukume kwa nguvu kusudi mambo ya nchi yetu yaendelee vizuri na yeye yamnyooke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha kanda za *TBS* na *TIRD*, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna tija kuwa Dodoma ukaanzisha *Branch Singida*, kwa sababu unaweza kuondoka asubuhi ukafanya kazi Singida, ukarudi hapa, ukarudi tena, ukarudi tena. Kwa hiyo, itabaki Dodoma na itakuwa rahisi hata Mheshimiwa Waziri kwenda na Mheshimiwa, rafiki yake wakaweza kuhamasisha shughuli za viwanda.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka halafu Mheshimiwa Aweso.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuelekea kwenye nchi za viwanda; na ninavyofahamu mimi ili twende huko, lengo kubwa ni kuchakata mazao yanayolimwa hapa nchini; lakini kama ambavyo swali namba 206 lilitivojibiwa, sijaona mkakati unaowekwa kwenye zao la ufuta. Ni namna gani Serikali imejipanga kutangaza ili tupate wawekezaji kwenye kusindika mazao ya ufuta?

Vile vile...

MWENYEKITI: Aaaah, Mheshimiwa vile vile viper? Wewe kaa sasa. Mheshimiwa Waziri. (*Kicheko*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua haya maneno ya mkakati

na vipaumbele yanaleta shida. Nilivyosema kwenye swalii la msingi Na. 206 nimesema, viwanda vidogo na viwanda vya kati ni viwanda tunavyoweza kuvimudu. Nikaenda zaidi nikasema sisi Waheshimiwa Wabunge tuwe wa kwanza, kwa sababu sisi ni watu ambaa tunafuatwa na watu, ni *influential*, ukianzisha kiwanda wewe cha shilingi milioni 200, watu wa kwenu wote wakianzisha viwanda, viwanda vitatekelezwa. Ndivyo hivyo nilivyosema.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Aweso.

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mkoa wa Tanga ni miongoni mwa Mikoa ambayo imetenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Je, Serikali ina mkakati gani ya kufufua na kuwekeza viwanda vipyaa? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa na uwezo hili swalii nisingelijibu, kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ananilazimisha nisome hotuba ya bajeti yangu kabla ya muda na shughuli ni kesho kutwa. Nimejipanga kwa ajili ya Tanga na Jumatano nitawaonesha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya, ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, kwa niaba yake, Mheshimiwa Munde.

Na. 208

Ujenzi wa Viwanda vya Pamba

MHE. MUNDE T. ABDALLAH (K.n.y. MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU) aliuliza:-

Wilaya ya Igunga ni miongoni mwa Wilaya zinazolima pamba kwa wingi nchini:-

Je, ni lini Serikali itajenga au kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchambua pamba, kutengeneza nyuzi na nguo na hata mafuta ili kutekeleza azma ya Serikali ya kujenga nchi ya viwanda?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI
alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele kikubwa katika kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini (*mass consumption*), zinazotoa ajira kwa wingi na zinazotumia malighafi za ndani ya nchi kama inavyojieleza kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano. Bidhaa hizo ni pamoja na nguo zitokanazo na pamba inayolimwa maeneo mbalimbali nchini ikiwepo Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha uzalishaji katika mnyonyoro mzima wa thamani katika zao la pamba unaofanyika, Serikali iliandaa mkakati wa kuendeleza zao la Pamba, Nguo hadi Mavazi (*Cotton to Clothing Strategy – C2C*) uliozinduliwa mwezi Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huo ambao utekelezaji wake unaendelea, unahamasisha uendelezaji wa zao la pamba na uongezaji wa thamani wa zao hilo kuanzia kuchambua pamba, kutengeneza nyuzi na nguo na hata kuongeza thamani ya mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya uwekezaji katika Sekta ya Viwanda, Wizara yetu imendaa mkakati wa kuharakisha ujenzi wa viwanda (*Fast Tracking Industrialization in Tanzania*) na imekamilisha utafiti juu ya vikwazo zinavyochelewesha uwekezaji nchini. Ni imani yangu kuwa

utekelezaji wa maandiko tajwa hapo juu na juhudhi za uongozi wa Mkoa wa Tabora zitatuwezesha kuvutia uwekezaji Wilaya ya Igunga.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Munde.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri pale manonga tuna Kiwanda cha kuchambua pamba cha siku yingi ambacho kina utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuja tukaongea na Mheshimiwa Waziri, akatuahidi kumwita Rajan na Igembensabo ili kuja kutatua tatizo hili na hatimaye kiwanda hicho kiweze kufanya kazi ili wananchi wa Igunda waweze kupata ajira na sehemu rahisi ya kuuza pamba zao. Je, Mheshimiwa Waziri amefikia wapi kuwaita watu hao ambao alituahidi kuwaita hapa Dodoma ili kuja kupatanaao mwongozo ili tuweze kujua tunaanzaje kuhusu kiwanda kile cha Manonga *Ginnery? (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Tabora umekuwa na adha kubwa ya ukosefu wa viwanda; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara alituahidi kwamba amepata mwekezaji Mchini wa kiwanda cha kujenga Tumbaku Tabora; na lilitokea tatizo pale *Airport* hatimaye yule mwekezaji hakuweza kuja Tabora kuongea na sisi ili kuweza kujenga Kiwanda hicho cha Tumbaku. Je, Mheshimiwa Waziri, mpaka sasa *status* ya mwekezaji huyo ambaye alikuwa anakuja Tabora akapata matatizo *Airport* imefikia wapi? *(Makof)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kujadiliana na Rajan juu ya *Manonga Ginnery*. Tatizo ninalolipata kuhusu Rajan, aliyerithi kiwanda yuko nje ya nchi. Kwa hiyo, nawasiliana naye kupitia mtu wa kati, lakini naomba mwendelee kunikumbusha, mwendelee kunishinikiza kusudi tuweze kufikia suluhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana hawa Rajan hawana *interest* tena na kiwanda na hawako tayari kununua na mwendelee kuwapa shime watu wa Igembensabo waendelee na nia hiyo, tutafikia muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la tumbaku; sina mpango tena na yule Mchima ila natafuta wawekezaji wengine wa kuweza kuwekeza kwenye zao la Tumbaku kwa kujenga Kiwanda. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chegeni halafu Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, suala la zao la pamba na usindikaji wake au kuongeza thamani ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Busega kuna vinu ambavyo ni vya viwanda vya Pamba kama cha Ngasamo na *Sir Ginnery*. Maeneo yote haya yamekuwa na viwanda ambavyo vimesimama, havifanyi kazi na hivyo kipelekea wananchi wengi na wakulima wa pamba kushindwa kuuza pamba yao kwa bei yenye kuongeza thamani. Je, Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani? Pamoja na suala la Manonga na kwingineko ambako kuna viwanda ambavyo havifanyi kazi vizuri, kama Serikali kuna namna gani ya kuweza kuboresha viwanda hivi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri. Unajua Mheshimiwa Waziri unajibu vizuri, kwa kifupi na kwa uhakika. (*Kicheko/ Makof*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, chanda chema huvi kwa pete. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye eneo la pamba, nenda kwenye mkakati wa pamba mpaka mavazi, ukurasa wa 91 majibu yote yako pale. Tutaweza kufaidika na pamba kama zamani, soko litakapokuwa linaweza kuvuta (*the demand pull*) na mojawapo ya mambo ya kufanya ni kuongeza ufanisi katika zao la pamba. Mwaka 2016 kwa kutumia *ways and measures* baada ya *ku-control* watu wasichafue pamba, nyie ni mashuhuda bei imepanda kidogo, tutaendelea na nikuahidi Mheshimiwa Mbunge tukitoka hapa nitakupa huo ukurasa namba 91 nilikuja nao nilijua itajitokea uone mambo mazuri. *The productivity*, pamba ina tatizo kwa sababu hakuna tija katika uzalishaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devotha na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Saada.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mkoa wa Morogoro ni mionganini mwa mikoa ambayo ilikuwa na viwanda vingi sana. Baada ya ubinafsishaji, viwanda vingi vimekufa na vingine vimegeuka kuwa ma-*godown*. Je, Serikali ina mpango gani wa uhakikisha inafufua viwanda hivi viweze kutoa ajira kwa wakati wa Mkoa wa Morogoro? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Wanakuchokoza.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Devotha nawe umewahisha shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isionekane mimi ni bingwa wa kukwepa maswali, Mheshimiwa Devotha hakuna kiwanda kitabaki *godown* Morogoro. Tajiri namba moja alisimama Morogoro na *microphone*, akasema kama ningekuwa na

Waziri wa Viwanda, Viwanda vya Morogoro vingefanya kazi, alikuwa ananisema mimi. Viwanda vyote unavyovisema, vinafanya kazi sasa. Kiwanda cha *Canvas* kitaanza ku-role Kiwanda cha *MOPROCO* kitaanza kutengeneza mafuta nami mambo yataendelea kunyooke. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saada.

MHE. SAADA SALUM MKUYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake, lakini Mheshimiwa Waziri najua kwamba karafuu ya Zanzibar ndio Karafuu ambayo ni *quality* duniani kote. Je, Wizara ya Biashara na Viwanda ya Tanzania ina mkakati gani kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda ya Zanzibar kuhakikisha kwamba tunajenga kiwanda ambacho kita-*absolve* karafuu ya Zanzibar kwa ajili ya kutengeneza *products*, kusafirisha nje lakini vile vile kupatia vijana ajira kama ambavyo tunaelezwa na ndio mategemeo yetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Zanzibar ilikuwa ni kwamba Makatibu Wakuu wa Wizara ya Viwanda Zanzibar na wale wa Tanzania kwa upande wa Bara wakutane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nitoe maelekezo kwamba wanapokutana sasa, kwa sababu najua wanansikiliza; na suala la Karafuu na Kiwanda na lenyewe waliunganishe walete majibu hapa tuweze kupata suluhu ya kutengeneza Kiwanda Zanzibar. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Sasa ni kipindi cha Wageni waliopo Bungeni.

Tunao Wageni sita wa Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Elimu na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako

ambao ni wadau wa maendeleo; Ndugu Alice Birnbaum - Mwenyekiti wa Wahisani wa Elimu kutoka Ubalozi wa Canada nchini Tanzania. *Welcome to the Parliament. (Makof)*

Ndugu, Tanya Zebroff - Afisa kutoka Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (*DFID*), *Welcome*. Ndugu John Lisingu - Afisa kutoka Idara ya Maendeleo ya Kimataifa, (*DFID*), karibu. Pantelee Kapichi - Afisa kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Elimu (*UNICEF*) karibu; Ndugu Mwanahamisi Singano - Mratibu wa Wahisani wa Elimu, karibu Bungeni; na Ndugu Beatrice Omary - Mshauri Elekezi wa Elimu Ubalozi wa Canada nchini, Tanzania. *(Makof)*

Wageni 12 wa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya ambao ni Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimboni kwake Nyasa Mkoa wa Ruvuma wakiongozwa na Ndugu Ndunguru Marcus. Karibuni Dodoma. *(Makof)*

Pia tuna wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wanafaunzi waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni.

Tuna Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari na Msingi 13 zimekuwa 10 bora Jimboni Mbulu Vijijini. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Flatei Massay. Karibuni Bungeni. *(Makof)*

Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa William Ngeleja, anaomba Waheshimiwa Wabunge kuwapa matokeo ya mashindano yaliyofanywa *weekend* hii kati ya *Bunge Sports Club* na *Iringa Veterans*. *Bunge Sports Club* walishinda goli moja; na goli hilo lilitfungwa na Mheshimiwa Ali Hassan King. Bunge Queens walishindana na Chuo cha Hombolo, Bunge Queens goli 30 na Chuo cha Hombolo goli 15. Nyota wa mchezo huo ni Mheshimiwa Tulia Ackson, Naibu Spika. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mwenyekiti Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) naomba nisisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara anajibu swal i Mheshimiwa Kafumu liloulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Munde ametoa jibu la mkato kabisa kwamba hana mpango na yule Mchima. Halafu akasema, tunaangalia utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nauliza kama jibu hilo la mkato kabisa ni sahihi bila kueleza kwamba yule Mchima alipata matatizo gani ili kusudi siku nyingine matatizo kama yale yasijitokeze. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68, sitaisoma kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye hapa ndani Mheshimiwa Naibu wa Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa hivi Mamlaka ya Mapato Tanzania inafanya utaratibu wa kufanya *updateya TIN* kwa ajili ya wafanyabiashara na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utaratibu huu, imeonekana kwamba kuna watu wengi aidha walikuwa wamenunua magari na kuyauza kwa watu mbalimbali au magari yao yalipata ajali, lakini wanapokwenda kufanya *updates*, *TRA* wanawaambia kwamba *TIN* zao zinadaiwa. Jambo hili limeleta mkanganyiko mkubwa sana, Watanzania wengi wanapofika *TRA* kwa ajili ya kuingiza mizigo mipya wanatakiwa kwanza walipe hiyo *balance* wanayoambiwa ndani ya *TIN* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo wanataka kufanya utaratibu wa kuanza kushika mali mbalimbali za watu ambao inaonesha kama wanadaiwa na *TRA*. Sasa naomba meza yako itueleze. Je, zoezi hili ambalo lilikuwa halifahamiki kwa Watanzania wengi kwamba gari lako linapokuwa *grounded* inabidi utoe taarifa *TRA* au unapouza kuwe kuna mkataba; ni sahihi kufanyika wakati huu au kuna maelekezo mengine? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naanza na Mwongozo wa Mheshimiwa Kakunda. Mheshimiwa Kakunda suala la uwekezaji nakupa fursa ya kuonana na Mheshimiwa Waziri baadaye ili akueleze vizuri majibu yake na mpango wake. Waziri huyu yuko *active* na anafanya kazi nzuri sana za viwanda. Kwa hiyo, nafikiri mtalelewana tu.

Mheshimiwa Mwambe, licha ya kuwa mwongozo wako hauendani na Kanuni zetu kwamba siyo jambo lilitotokea Bungeni mapema, lakini ni jambo ambalo linagusa jamii ya watu wengi sana na linaleta mahusiano kidogo ya sintofahamu kati ya *TRA* na wananchi. Licha ya kuwa *TRA* wana nia njema, sasa nakuagiza na namwagiza Waziri wa Fedha mkutane baadaye Kantini, myazungumze na mjaribu kuya-sort out. (*Makofii/Kicheko*)

Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali
kwa Mwaka 2017/2018 – Wizara ya Elimu,
Sayansi na Teknolojia**

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kuchangia, tunaanza na Mheshimiwa Mama yetu Salma Kikwete na Mheshimiwa Doto Biteko ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nitoe pongezi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika kuboresha elimu. Pamoja na hayo, niwapongeze Walimu wenzangu wote nchini Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya katika sekta hii ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niwapongeze Walimu wenzangu, wengi wao wameweza kuijendeleza katika maeneo tofauti kuanzia ngazi za chini, hadi kufikia eneo lingine la *Masters* na *Ph.D*, hongereni sana Walimu wenzangu popote pale mlipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la elimu na tunazungumzia uboreshaji wa elimu. Tunasema kwamba tunataka tuboreshe; katika maboresho haya, ninachokizungumzia, Walimu hawa wanapojiendeleza ni vema kabisa baada ya kumaliza masomo yao, wasiombe nafasi za kwenda aidha Sekondari au kwenye Vyuo. Kwa sababu tuko kwenye maboresho, msingi wowote ni muhimu sana katika jambo lolote lile. Kwa hiyo, Walimu hawa ni vema wabaki kwenye zile shule kama ni wa Msingi wamejiendeleza wamepata *Diploma* au wamepata *Degree* wabaki pale, lakini kitu kikubwa ni vema kabisa Walimu hawa waboreshewe maslahi yao kulingana na elimu yao waliyokuvanayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye eneo la Mafunzo ya Ualimu. Nimeona Walimu wengi wamepata fursa juu ya maeneo hayo, lakini sijaona mafunzo kwa eneo la Elimu ya Awali. Sera inatuambia kwamba kwenye kila Shule ya Msingi kuwe na darasa la elimu ya awali. Sasa kama tunataka tuboreshe, ni lazima tuanzie kuboresha kwenye Elimu ya Awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ithibati katika ukurasa wa 19 aya ya 37. Tumeambiwa kwamba kulikuwa na suala zima la ukaguzi, Walimu 7,727 walikaguliwa; Msingi 6,413, Sekondari 1,314. Ni vema kabisa, lakini lengo

ilikuwa kukaguliwa Walimu 10,818. Hawa ni baadhi tu ya waliokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukija kwenye eneo hili, ili tuweze kuboresha elimu yetu hapa nchini Tanzania, hili eneo la ukaguzi ni lazima lipewe kipaumbele. Kuwe na pesa ya kutosha na kuwe na vitendea kazi. Ili kuboresha eneo hili, ni lazima Walimu wakaguliwe mara kwa mara. Unaweza ukakuta ndani ya miaka; nazungumza haya kwa sababu nina uzoefu juu ya eneo hili, mimi ni Mwalimu kwa taaluma. Unaweza ukakuta zaidi ya miaka miwili au mitatu Mwalimu hajakaguliwa. Sasa unategemea ubora wa elimu hapa utakujaje kama hakuna mtu wa kumsimamia huyu Mwalimu? Kwa hiyo, hili eneo ni lazima lipewe kipaumbele cha namna ya pekee. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza haya, napenda nizungumzie eneo la Shule ya Lindi Sekondari. Nimeona maeneo mengi wameboreshewa, wameambiwa itaboreshwa hili, itatengenezwa Shule hii, itafanya hivi, lakini Sekondari ya Lindi ilipata tatizo la kuungua moto; na moto ulikuwa mkubwa na ulipoteza karibu madarasa yasiyopungua sita pamoja na eneo la Mikutano. Serikali hapa mnatuambiaje juu ya shule hii iliyoko Mkoa wa Lindi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mimba. Suala la mimba ni tatizo na suala la utoro ni tatizo. Sisi kama wanawake tunawapenda sana na ni lengo letu Waheshimiwa Wabunge wanawake kuwatetea watoto wa kike na mwanamke yejote yule ambaye anaomba nafasi ya uongozi. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Sawasawa.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili la mimba, hasa mimba za utotoni, sikubaliani na kwamba watoto wakipata mimba warudi tena shulenii. Hili sikubaliani nalo hata kidogo! Sababu za kutokukubaliana nazo ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunazungumzia suala la mila, desturi, utamaduni na mazingira... (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Imani ya dini.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, na dini. Hakuna dini yoyote inayomruhusu mtoto wa kike kupata mimba kabla ya wakati. Biblia inasema na *Quran* inasema. Tunapofanya mambo yetu ya msingi tuangalie vilevile mambo yanayohusu imani zetu za dini. Suala la mtoto kurudi shulen, tutafute njia nyingine mbadala. Sisi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuna Kanuni zetu na ndizo tunazozifuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwenye suala la mimba, sheria inayofuata hapa mtoto akipata mimba asirudi shulen. Kama hapa ingekuwa sisi kama Wabunge hatuna sheria na kanuni, ingekuwa tunafanya mambo kila mtu na jambo lake, lakini sheria zinatubana. Nataka kwa hilo sheria zibane. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Taarifa!

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka sheria ibane. Mtoto akipata ujazito asirudi shulen, atafutiwe njia nyingine ya kuweza kumsaidia mtoto huyu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salma subiri kidogo. Mheshimiwa Keissy!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, watoe shuhuda hapa, Mbunge ye yote mwanamke aliyeanza mapenzi shulen, elimu yake ilikwendaje? Namuunga mkono mzungumzaji mia kwa mia. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salma, endelea.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Nashukuru sana kwa kuniunga mkono. Naomba wanawake wote waniunge mkono na wanaume vilevile waniunge mkono. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Kama hivyo ambavyo sisi tunawatetea...

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Tuwatetee katika mazingira...

MWENYEKITI: Waheshimiwa taarifa ya mwisho, naona sasa mnamtua kwenye flow. Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Sawa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mbunge wa Viti Maalum Lindi, Mama Salma Kikwete kwamba kati ya waathirika wengi Tanzania ni pamoja na Mikoa ya Mtwara na Lindi. Tunataka sasa atueleze, anataka watoto wetu wasisome kwa sababu wanapata mimba wakiwa wadogo? (*Makofi/vigelegele*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Taarifa hiyo siikubali, naikataa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. SALMA R. KIKWETE: ...pamoja na kwamba kwamba watoto hawa wanapata mimba katika umri mdogo; lakini ni lazima tuwatengenezee mazingira wezeshi. Mazingira wezeshi tukisema warudi shulen i watoto hawa, ina maana wengi watapata mimba.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa mwachen!

MHE. SALMA R. KIKWETE: Wengi watapata mimba katika umri mdogo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuyumiliane humu ndani. Kila mtu ana fursa ya kusema hoja yake.

MBUNGE FULANI: Kabisa!

MWENYEKITI: Mkianza huku na huku watataka.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Doto Biteko ajiandae Mheshimiwi Almasi.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia na kabla sijasema ma...

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge. Waheshimiwa tunaomba utulivu ndani ya Bunge. Nitaanza kutaja majina sasa, Mheshimiwa Waitara!

MHE. MWITA M. WAITARA: Naam Mheshimiwa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge, mumwongezee dakika yake moja Mheshimiwa Doto.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa hotuba yake hii aliyoileta kwenye Bunge letu hili. Nampongeza vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kwa kazi kubwa anayofanya kwa ajili ya kuinua elimu ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza sana Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa taarifa yao ambayo kwa kweli ilikuwa inajieleza vizuri, sana na nimetoa ushauri ambao mimi binafsi nauona ni ushauri wa msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Confucius* ambaye ni Mwanafalsafa wa Kichina aliwahi kusema maneno haya, akasema kwamba ukitaka kupanga kwa ajili ya mwaka mmoja, basi panda mpunga. Ukitaka kupanga kwa ajili ya miaka 10 basi panda miti na ukitaka kupanga kwa ajili ya miaka 100 ijayo, basi mwelimishe mwanao au mtoto wako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo moyo wa Taifa hili. Taifa lolote ili liweze kuendelea na tafiti zimeonesha, kuna uhusiano wa moja kwa moja wa ukuaji wa elimu na ukuaji wa uchumi; hivi vitu vinakwenda pamoja. Taifa ambalo limeendelea kielimu kwa vyovyote vile linajikuta linaendelea vilevile kiuchumi. Kwa hiyo, tunajadili Wizara ambayo ni muhimu sana kwa nchi yetu; na kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kuchapa kazi kwa sababu bila hivyo Taifa letu hili tutachelewa sana kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kutoa elimu bure kwa Watanzania. Uamuzi huu, unaweza ukaonekana wa kawaida kwa sababu ni kawaida, hata mbuzi huwa haoni umuhimu wa mkia wake mpaka uondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe taarifa kwamba kabla ya elimu bure, Wilaya ya Bukombe watoto waliokuwa wanaandikishwa darasa la kwanza mpaka la saba walikuwa 45,000 peke yake. Baada ya kuanzishwa kwa elimu bure, sasa hivi watoto walio darasa la kwanza kwa elimu ya msingi yote, wanafika 75,000. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba wapo watoto wengi zaidi ambao walikuwa wanaacha shule, walikuwa wanashindwa kwenda shule kwa sababu ya michango na ada hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahitaji kumtia moyo Mheshimiwa Rais, tuitie moyo Serikali iendelee kuwekeza zaidi kwenye elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na yako mambo ambayo nataka nichangie kidogo. Jambo la kwanza ni ukaguzi wa elimu. Suala la ukaguzi wa elimu lilishaelezwa kwa kila aina ya lugha, hapa Bungeni na nje ya Bunge. Ukaguzi wa Elimu wa Tanzania una hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi ku-*suggest* na vyombo vingine viliwahi kupendekeza kwamba ili ukaguzi wa elimu uweze kuwa imara ni lazima tuutoe kwenye mikono ya Wizara uwe wakala wa kujitegemea. Serikali ilishawahi kuahidi hapa Bungeni kwamba inaanzisha mchakato wa kufanya ukaguzi kuwa wakala wa ukaguzi. Ahadi hiyo nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu sasa hivi, wala hakuna kinachozungumziwa, kana kwamba hakuna kitu kilichowahi kusemwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano. Kwenye kijarida cha elimu (ninacho hapa), cha Januari hadi Machi, mwaka 2013, ukurasa wa nne, Mheshimiwa Waziri wa Elimu alisema yafuatayo: "Katika jijihada zake za kuipa mamlaka zaidi na uwezo na hivyo kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa shule na Vyuo vya Ualimu, Serikali inakusudia kuibadili Idara ya Ukaguzi wa Shule iliyoko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, kuwa Wakala wa Kujitegemea. Imeandikwa humu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Kamati ya Bunge lako iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Margaret Sitta mwaka wa fedha 2013/2014, ilikuja na mapendelekezo hayo hayo ya kuifanya ukaguzi kuwa Wakala Maalum wa Elimu na Waziri wa Elimu wakati huo, mimi sijawa Mbunge, nilikuwa nje, kwa sababu mimi ni mdau wa elimu, aliahidi kuwa jambo hilo linafanyiwa kazi. Nataka kujua Mheshimiwa

Waziri, hivi hili jambo limeishia wapi? Hivi hili jambo lilikuwa tu ni kwamba tumalize kipindi hicho cha bajeti hiyo, halafu maisha yaendelee? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa elimu hauwezi kuendelea kwa mfumo tulionao. Wakaguzi wana hali mbaya; Wakaguzi hawana kila kitu, kuanzia rasilimali mpaka uwezo wa rasilimali watu. Wakaguzi ni wachache, shule ni nyngi. Lazima sasa tuangalie utaratibu mpya wa kuhakikisha kwamba Walimu hawa na wao tunaweza kuwapatia fursa ya kukaguliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, iliwahi kusemwa iwepo Bodi ya Wataalam wa Walimu. Hii Bodi kwenye kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaiona. Hivi hata hivi vyeti feki tunavyozungumza, kama kungekuwa na Bodi ya Kudhibiti Walimu ingekuwa imeweza kulgundua hilo mapema. Hili lilishawahidi kuahidiwa humu humu Bungeni na Mheshimiwa Shukuru Kawambwa wakati ule akiwa Waziri kwamba Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha Bodi ya Walimu. Hii bodi iko wapi? Mbona na yenyewe sioni! Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja kujibu, atusaidie kutupa majibu sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na wengi ni suala la vitabu. Nami nataka nizungumze kidogo hapa, nimevisoma hivi vitabu. Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye hotuba yake ukurasa wa 21, amesema kwamba vitabu hivi vina makosa ya kimaudhui na hivyo uchambuzi wa kina unafanyika ili vitabu vilivyochapisha mwaka 2016/2017, kubaini endapo vina dosari; nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, vitabu hivi siyo tu kwamba vina makosa ya kimaudhui, vina makosa mengi, wala havifai kupelekwa sokoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu tu aliyechapisha pengine ni Serikali, anapata kigugumizi. Mwaka 2016, Mei hapa hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri alitueleza kwenye hotuba yake ukurasa wa 55, kipengele cha tatu, akasema hivi:

"Mheshimiwa Spika, vimeandikwa na kuchapishwa vitabu nakala 6,862,000. Akasema hivi, katika vitabu hivyo, vitabu 2,807,000 vimebainika kuwa na makosa na kwa hiyo, wamemwambia aliyevichapisha avirudishe akavichape upya."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vilivyochapishwa na Serikali vina makosa luki. Nitakupa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha kwanza cha *English, Form Four*, kina makosa 34 kwa uchambuzi wangu. Kina makosa ya mpangilio; yaani ukurasa wa kwanza kwenye jedwali (*table of content*) lenyewe lina makosa. Anasema *Preface* iko *roman* (ii) ukienda kwenye kitabu iko *roman* (iii), ukiangalia *chapter one*, anasema iko ukurasa wa nne, ukienda kwenye kitabu ndani, iko ukurasa wa kwanza. Ni makosa mengi ambayo siwezi kuyaeleza! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Kidato cha Tatu, kina makosa 12 ya kimantiki na nimwambie Mheshimiwa Waziri, siyo makosa ya kimaudhui, ni makosa ya kimantiki, makosa ya kimaudhui, makosa ya kiuandishi. Kwenye mwongozo wao walionao, huu hapa ninao. Unataka kitabu chochote kilichozidi kurasa 100 kifungishwe au kiwe *binded* kwa kutumia gundi, lakini ninacho kitabu kiko hapa, kina zaidi ya kurasa 100 lakini kimegundishwa kwa pini. Hata ubora wa vitabu vyenyewe haupo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais anahangaika kutafuta fedha kwa ajili ya watoto wa Tanzania. Haiwezekani Mheshimiwa Rais atenge shilingi bilioni 18.77 kila mwezi kwa ajili ya watoto. Baba anatoa fedha kwa ajili ya watoto wake wapate chakula kizuri, wanaenda kupewa matango pori! Nyumba hii ambayo ni ya kwetu sisi Wabunge, Nyumba hii ya Mheshimiwa Ndugai na Mheshimiwa Tulia Ackson ikubali mambo haya yatendeke mbele yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie, ni shilingi ngapi zimetumika? Tumeambiwa

zaidi ya shilingi bilioni 100 zimetumika kuchapisha vitabu vibovu hivi. Hizi fedha ni kama zimepigwa kiberiti na sasa hivi viko kwenye mzunguko vinafundisha watoto kuwapatia maarifa ambayo ni *substandard*. Tunapeleka wapi Taifa hili? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, Walimu wa Tanzania baada ya kuliona hili waliweka pembeni vitabu vyenu wakaachana navyo, wakaanza kufundisha kwa maarifa yao wanayoyajua. Hivi hata wingi wa neno *sheep*; neno *sheep* peke yake, kuna wataalam ambao wanakaa kupitia vitabu hivi, nimewasoma. Kuna mtaalam wa *curriculum*, kuna wataalam wa kutoka Vyuo vya Ualimu, kuna wataalam wanaotoka *NECTA*, kuna wataalam wa... (Makofi)

(*Hapa kengele lilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Almas na Mheshimiwa Maftaha ajiandae.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo kwa kweli ndiyo msingi wa maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea kuchangia napenda pia nitoe shukrani nydingi kwa Mheshimiwa Rais na Mawaziri wote wa Wizara hii ya Elimu. Vile vile nijikite kwenye mambo haya manne ambayo nitayaongelea, moja shule za ufundi lakini mambo ya *VETA*, tozo ya *SDL* na mimba za utotonii. Naomba nianze na suala hili la mimba za utotonii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limekuwa linaomba tuletewe sheria itakayozuia watoto kuolewa wakiwa wadogo. Bunge hili limepitisha sheria kali sana kwamba mtu ambaye atampachika mimba mtoto wa shule, afungwe miaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa, watu wanachangia tena Bunge hili linaruhusu watoto kupata mimba wakilwa mashulenii. Hii ni kinyume! Bunge linaomba tulete Sheria ya Kuzuia Watoto Kupata Mimba lakini Bunge hili hili leo linataka tupitishe kanuni au ruhusa watoto wapate mimba shulenii. Tunajikanyaga! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Muislamu na niko wazi kabisa na nina hakika dini zote zinakataza mambo ya zinaa kabla ya ndoa. Kwa hiyo, ni vigumu sana mimi kwa imani yangu ya dini kuruhusu watoto hawa watiwe mimba halafu warudi shulenii. Ina maana niwaruhusu wapate mimba kabla ya kuolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono kama Bunge hili litaruhusu watoto wa shule waolewe, wazae ndipo warudi shulenii. Kinyume chake ni kosa kubwa sana. Pia nimepitia takwimu; wanasema kama huku-*research usiseme*; tatizo la mimba shulenii mwaka 2015 jumla ya watoto wote wa *primary and secondary school*/3,937 ndio waoliacha shule kwa sababu ya kupata mimba, lakini watoto walioacha shule kwa makosa mengine ya utoro 139,866. Hili ndiyo tatizo kubwa sana, siyo la mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuruhusu watoto wapate mimba warudi shulenii, itaharibu nidhamu ya shule kabisa. Watoto sasa hivi wanaogopa kupata mimba kwa sababu wanajua watafukuzwa shule, sasa tukiruhusu wapate mimba wakasome, itakuwaje? Serikali imeshaweka muundo wa watoto wanaopata mimba wakarudi nyumbani kama mama watoto, wasome elimu ya watu wazima ambayo inaanzia Shule ya Msingi mpaka Chuo Kikuu, wanakosa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuruhusu watoto walioitwa mama, wanajua mambo yote ya kulea mtoto wakakae darasa la saba tena, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kidini nakataa, lakini Bunge hili limelaumiwa kutunga sheria zinazokanganyana zenyewe; huku tunakataza watoto wasifanlywe zinaa wakiwa wadogo chini ya miaka 18 na mtu akifanya kosa afungwe miaka 30. Huku tunaruhusu hiyo tena ifanyike kuwa watoto wapate mimba warudi shuleni. Hii sheria itatukanya wenyewe, haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maoni yangu ni kwamba watoto hao wanaoacha shule kwa kupata mimba wafukuzwe kabisa. Waliowatia mimba wafungwe miaka 30 na watoto wasirudi shuleni kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni la kwanza. Naomba sasa niongelee mambo ya Elimu ya Ufundu. Mfumo wa elimu unaotolewa sasa hauwezi kulingana na matakwa ya Mheshimiwa Rais ya kujenga nchi ya viwanda na hili naomba lisikilizwe vizuri sana. Mimi ni zao la Elimu ya Ufundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka iliyopita kulikuwa na Shule ya Ufundu, Moshi; kulikuwa na Shule ya Ufundu, Ifunda. Shule zote zilikuwa zikipeleka wanafunzi waliotoka *Form Four* kwenda Chuo cha Ufundu (*Technical College*) na hao walichagua ufundu tangu mwanzo, walikuwa kama Fundi Umeme miaka minne ya Sekondari, inaitwa *Trade School*, baadaye kama wewe ni *Civil Engineer*, utaanzia mambo ya *engineering* kuanzia *form one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michoro wanayochora Chuo Kikuu leo ya *technical drawing* niliichora nikiwa *Form One*. Tulikwenda pia Chuo Kikuu cha Ufundu (*Technical College*) tukachukua miaka mitatu, tukajaliwa watoto wanaoitwa Mafundi Sadifu (*Technicians*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, tumefanya kazi nje, tukarudi tena Chuoni, tukasoma *Diploma* ya *Engineering*. Kwa hiyo, tuna miaka 10 katika ufundu uliochagua ukiwa *form one*. Kama ni *electrical*, ni miaka minne *form one* mpaka *form four*, kama ni *Civil*, ni miaka minne *form one* mpaka *form four*, lakini miaka mitatu ya

ufundi inakuwa jumla saba. Ukirudi kuchukua Diploma, una miaka kumi katika ufundi. Tulizalisha mafundi kama mimi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mifumo miwili ambayo ilikuwa inajulikana waziwazi. Mfumo wa *Academicians form one mpaka form four, form five, form six* na Chuo Kikuu cha *Engineering* au cha *Udaktari*. Ufundu tulianzia Sekondari ya Ufundu, Chuo cha Ufundu, unarudi unapata fundi anaitwa *Diploma Engineer*, hawa ndio ambao wanaendesha kampuni nydingi mnazoziona leo, ndiyo wako viwandani. Mfumo huu ulifutika kwenye Awamu ya Pili ya Uongozi wakati Mheshimiwa Mungai (Marehemu) alipofuta shule za ufundi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi suala hili haliwezekani tena. Tuna *Artisan* kutoka *VETA*. Hawa watu wa *VETA* ni wa chini kabisa katika Elimu ya Ufundu, lakini baadaye kutoka hapa mpaka hapa, hakuna ma-*technician*, mafundi sadifu hawapo.

Mheshimiwa Rais anaongelea ufundi, viwanda vya ufundu, viwanda vya kuzalisha mali; wanaoendesha viwanda hivi ni mafundi sadifu. Mafundi *VETA* wana-repair mashine zikiharibika na kadhalika. Namwomba Mheshimiwa Rais afikirie kuendeleza elimu ya viwanda, afikirie kurudisha mfumo wa zamani wa *Diploma Engineers* ambao walifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, sisi waajiri tunaona kwamba *VETA* kuwekwa chini ya Wizara ya Elimu ni kosa. Kufanya kosa siyo kosa, kujisahihisha ni bora. Tunapenda *VETA* iwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ambako ndiko tunafanya uendelezaji wa stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzenetu Kenya *Polytechnic* walilinda mambo hayo na matokeo yake, hela tunayochanga sisi kama *SDL* inakwenda kusomesha watoto *High Learning Institution*, tungependa sisi hela yote iende *VETA*, lakini vile vile tungeomba pia *VETA* yote katika mfumo mpya

wa kuanzisha Mfumo wa Elimu ya Ufundu irudi tena katika Wizara ya Kazi ambako ndiko tunaendeleza stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi waajiri tunapata taabu sana katika suala hili, tunaona kwamba *VETA* imewekwa sehemu ambayo labda kwa makosa ambayo hatuyajui, lakini tunaomba sasa *VETA* irudishwe tena Wizara Kazi ili iweze kuendeleza ujuzi wa wafanyakazi lakini vile vile ujuzi wa wanafunzi wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi bado naumia na tozo. Najua tunaongelea tozo ya *SDL* ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu. Napata ukakasi! Ningependa kuongelea tozo ikiwa chini ya Wizara ya Kazi, lakini iko Wizara ya Elimu. Hii inatupa tabu sisi waajiri kuchangia kwa sababu tunaona tozo hii inakwenda kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini vile vile naomba sana Serikali ichukue ushauri ambaao nimeutoa. Ahsante sana kwa kuniruhusu niongee. (*Makof*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, hakuna mwongozo sasa hivi, kaa chini. Mheshimiwa Maftaha dakika tano, halafu Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia dakika hizo tano ulizonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwamba ili tuweze kuwa na wanafunzi ambaao wanafundishika vizuri *level zote za elimu*, iwe sekondari kwa maana ya kwamba *O-level na A-level* lakini Vyuo vya Ufundu, *Universities* ni lazima tuanze na uwekezaji katika elimu, pale tunasema *Pre-Primary Education* yaani Elimu ya Msingi na Elimu ya Chekechea kabisa kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi ye yote ambaye amefundishwa vizuri, akiwa chekechea, elimu ya awali, mtoto huyu atakuwa na uwezo mzuri wa kuweza kufundishika vizuri atakapokuwa Shule ya Msingi. Akifundishwa vizuri shule ya msingi, atafundishika vizuri sekondari, elimu ya kidato cha nne lakini pia kidato cha tano na kidato cha sita, hata anapofika /level/ ya elimu ya juu, kwa maana ya Chuo Kikuu, atafundishika vizuri na mwisho wa siku tutaweza kuwa na wasomi wazuri katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana kwa kuona kwamba sasa hivi katika nchi yetu kuna mkanganyiko wa usimamizi wa elimu. Tuna Wizara ya Elimu, tuna Wizara ya TAMISEMI, mimi nashangaa sana na nazungumza haya nikiwa Mwalimu, lakini pia nikiwa Msimamizi wa Elimu, kwamba tunavyoangalia Wizara ya Elimu, kwamba imepewa kusimamia miongozo, ni jambo la ajabu sana. Tunataka Wizara ya Elimu isimamie elimu, tunataka Wizara ya Elimu isimamie miundombinu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninavyozungumza, ukija Mtwara Mjini pale kwa mfano, tuna Shule ya Msingi Mbae, ina madarasa mawili; haina vyoo, lakini ina wanafunzi zaidi ya 630 halafu leo hii tunasema kwamba eti wanafunzi Mtwara na Lindi hawafanyi vizuri katika mitihani yao. Hatufanyi vizuri kwa sababu hatuna miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mikoa ya Mtwara na Lindi hatufanyi vizuri katika elimu kwa sababu pia Walimu hawatoshi. Shule za Msingi, Shule za Sekondari hatuna Walimu wa kutosha. Tunaomba Wizara itusaidie hili. Mko mzyma wa Mtwara tuna upungufu wa Walimu, hawatoshi, watuletee Walimu tuweze kufanya vizuri kama ilivyo katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dakika zangu ni chache, naomba nizungumze suala hili ambalo Serikali ya Awamu ya Nne ililanzisha. Mimi nilikuwa Msimamizi wa elimu wakati huo, nilikuwa Mkuu wa Shule, Mchingga Sekondari kwa miaka mitano. Tulipewa miongozo ya kusimamia elimu

kupitia *BRN*, lakini tangu mwaka 2016 hatuoni kuna nini? Kwa nini huu mpango unaoitwa *BRN (Big Result Now)* ambao Serikali iliiga kutoka nchi ya Malaysia. Ule mpango ulikuwa ni mzuri kwa sababu ule mpango ulikuwa unaleta usimamizi katika elimu kwamba Mwalimu anapofanya vizuri, anapofundisha vizuri, mwisho wa siku anakuja kupewa *motivation* kupitia Wizara ya Elimu na TAMISEMI, lakini sasa hivi *BRN* haitajwi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba kama kweli tunahitaji matokeo mazuri katika elimu, turudishe huu mpango wa *BRN* katika elimu, ulikuwa unasaidia sana kuchochea Walimu kuweza kufanya kazi, Walimu kuweza kufundisha kwa sababu walikuwa wanapewa motisha pale ambapo wanafaulisha vizuri masomo yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuboresha elimu linaendana sambamba na kuboresha maabara. Kulikuwa na mpango wa kujenga maabara, nami kipindi kile nikiwa Mkuu wa Shule, tuliweza kujenga maabara nyingi sana, lakini mpaka leo tunavyozungumza zile maabara hazina vifaa, hazina kemikali, hazina Walimu wa sayansi ambao watakuja kufundisha yale masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kweli tunahitaji kuipeleka elimu yetu mbele, lazima Wizara ya Elimu iliangalie suala hili la maabara tupeleke kemikali mashulenii. Jambo la umuhimu zaidi ni usimamizi wa elimu kwa Wakuu wa Shule. Wakuu wa Shule ndiyo nyenzo pekee ambapo tukiwatumia ipasavyo, hawa Walimu wanaweza kusimamia elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa elimu bure hivi sasa hasa katika Shule za Mikoa ya Lindi na Mtwara, hakuna michango inayokusanywa, hakuna pesa za ulinzi wala taaluma na hizi shule maeneo mengi ziko vijijini, ziko maeneo ya vijiji na Halmashauri zenyewe...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo dakika kumi, ajiandae Profesa Norman Sigalla, Mheshimiwa Jumanne Kishimba na Mheshimiwa Ester Mahawe.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja muhimu sana ya elimu kwa sababu naamini wote humu ndani tunatekeleza majukumu yetu kwa sababu ya elimu. Hakuna Mbunge ambaye hajaingia darasa la kwanza awe yumo humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimesikitishwa sana, sana, sana na maneno aliyosema Mheshimiwa Salma Kikwete, ni mwanamke mwenzangu, lakini sishangai kwa sababu hata mume wake aliwahi kusema kwamba watoto wa shule wanaopata mimba ni viherehere vyao. Nimesikitishwa zaidi kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wote wawili ambao ni wanawake nao pia walikuwa wanapiga makofi. Jambo hili linasikitisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu naamini kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokuwa anajibu swalii la Mheshimiwa Mama Sitta hapa Bungeni ilikuwa ni kiini macho tu, kwa sababu alisema *by March* angeleta mwongozo huo na hii ni Mei hajaleta na leo anampigia makofi Mheshimiwa Mama Salma Kikwete. Hii inaonesha ni jinsi gani humu ndani watu ni wanafiki, hawaishi/hawatembeil katika maneno yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa hapa Tanzania tunataka tuwe na elimu jumuishi au elimu shirikishi kwamba kila mtoto asome.

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimueleze mchangiaji kwamba kwenye Bunge hili kila mtu ana uhuru wa kutoa mawazo yake na kitu anachoamini. Kwa hiyo, tusilazimishane kuhusu kuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi sipendi kuondoa viboko mashulenii na sipendi kuondoa utaratibu wa watu waliofanya mambo ya hovyo kuondolewa. Kwa maana hiyo, wote wanaowapa mimba wanafunzi tutawafunga na wanaopata mimba wataondoka mashulenii, wewe kama unaamini vinginevyo changia ile iliyo ya upande wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank kaa, Mheshimiwa Susan endelea.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Tunataka tumpe taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Taarifa ni ya Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sipoeki taarifa yake kwa sababu nilikuwa nam-refer Naibu Waziri aliyetoa majibu humu ndani na leo anamshabikia Mheshimiwa Mama Salma Kikwete ambaye anaenda kinyume na kitu ambacho alikisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la vitabu, nililianza juzi na bahati mbaya sikuwa na muda lakini nashukuru sana Mheshimiwa Doto Biteko ameliongea. Niseme ni wazi kwamba hapa ndani au katika Bunge lako baadhi ya Mawaziri wanaleta utani. Suala la vitabu ni zito sana. Wote tunatambua kwamba nchi hii ina ukosefu

mkubwa wa Walimu na kwa maana hiyo vitabu vingekuwa vimetengenezwa vizuri watoto wangeweza kuvisoma na kuvielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo ambalo linasikitisha Mheshimiwa Waziri anasema watawachukulia hatua, tunataka kujua toka mwaka jana wakati tumekuwa na tatizo hili, amewachukulia hatua watu kiasi gani? Jambo hili linasikitisha kwa sababu leo Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu ndiye aliyekuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu. Kwa hiyo, ina maana hivi vitabu vibovu vimetengenezwa chini yake lakini leo amekuwa *elevated* kuwa Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea suala la Kiingereza nchi hii, tunajua watoto wadogo ni *tabula rasa* kile wanachokipata mwanzoni ndio kina-stick katika ubongo wao. Leo ukichukua kitabu hiki cha Klingereza kwanza *title* yenye, '*I learn English language, this is not English*'. Hata hivyo, ukienda katikati ukurasa wa 127 kinasema, *look at this insects* lakini ua (*flower*) limewekwa kama ni *insect* (mdudu).

MBUNGE FULANI: Aaaah.

MHE. SUSAN A. J LYIMO: Sasa mtoto wa darasa la tatu unamwambia leo kwamba ua ni mdudu anakuwa anajua kwamba ua ni mdudu. Kuna huyu mtu anaitwa Dkt. Elia Y. Kibga ambaye ndiye *Acting Director* amesaini, ajue kwamba Mungu anamwona watoto wake hawasomi vitabu hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni kwamba hivi vitabu sio tu vina matatizo ya kimaudhui bali pia vina matatizo makubwa ya kimantiki. Tunaomba vitabu hivi viondolewe mashulenilakini kubwa zaidi tunaomba Tume au Kamati Maalum iundwe ipitie vitabu vyote kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita kuona makosa makubwa yaliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vitabu hivi vimeshasambazwa takribani nakala milioni 16. Kama kila

nakala ni Sh.5,000 bado usambazaji maana yake tuna zaidi ya shilingi bilioni 100 tumezipoteza, hela hizi zingeweza kabisa kujenga zaidi ya madarasa 500. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba tunaomba kabisa Bunge lako Tukufu liunde Kamati/ Tume Maalum iende ikachunguze uchapishaji wa vitabu hivi. Pia isiruhusu Taasisi ya Elimu kuwa ndiyo inayotunga vitabu bali kuwe na chombo ambacho kitasimamia kuhakikisha kwamba vitabu hivi vinakuwa vizuri kwa ajilli ya watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye suala la vitabu nije kwenye suala la ripoti ya *CAG*. Wote tunajua kwamba *Mlimani City*, nadhani kila Mbunge amepita pale, mkataba wa *Mlimani City* ni mbovu haijapata kutokea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *CAG* ya 2005 inaonesha wazi kwamba ilikuwa inatakiwa pale *Mlimani City* pawe na hoteli ya *three stars* lakini mpaka leo hii tunaongea baada ya miaka 14 hakuna hoteli imejengwa pale. Mbaya zaidi mkataba huo unasema kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinapaswa kupata 10% ya *gross profit*, lakini cha ajabu mpaka leo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinapata 10% ya *net profit*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaleta hasara kubwa na ndiyo sababu leo tunazungumzia miundombinu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa mfano, Bweni Namba Mbili (*Hall Two*) limefungwa toka mwaka jana hakuna mwanafunzi yeyote anayekaa pale kwa sababu ya uchakavu. Hizi fedha zingeweza kusaidia kufanya ukarabati wa jengo lile. Kwa hiyo, tunaomba sana hii ripoti ya *CAG* ifanyiwe kazi ili mapato ambayo yanaenda kwa mmiliki wa *Mlimani City* yawe yanaenda 10% ya *gross profit* na sio ya *net profit*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo nataka Wizara itusaidie na hii pia inatokana na *CAG* ripoti. *CAG* ripoti inasema 94% ya shule zilizoanzishwa nchini zinatoa

huduma bila ya kusajiliwa. Hata hivyo, ni Wizara hiyo hiyo inapoenda kusimamia shule za *private* hata kama umeongeza darasani mwanafunzi mmoja tu shule inafungiwa. Mtuambie ni kwa nini 94% ya shule hazijafanyiwa usajili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa nije kwenye suala zima la ukaguzi, limezungumzwa sana na hata leo tumesema kwamba bila ukaguzi elimu yetu haiendi. Hata hivyo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukaguzi ni kidogo sana..

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam maarufu kama Magufuli Hosteli. Pamoja na kwamba Waziri hajaeleza gharama halisi lakini inajulikana kwamba gharama za *hostel* zile ni shilingi billioni kumi, *that means* kila jengo moja ni shilingi millioni 500. Haiwezekani na haingii akilini na nimejaribu kuongea na wahandisi, haiwezekani jengo linachukua takribani wanafunzi 390 liwe lina gharama ya shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *CAG* akafanye *special audit* kuona ni kiasi gani kimetumika na kama ni kweli ni shilingi milioni 500 mimi niko tayari nitatoa shilingi milioni zangu 500 Serikali injengee jengo kama hilo ili tuweze kuwaweka vijana wengine, kabisa. La sivyo labda naweza nikasema pia naweza nikaachia Ubunge kama kwell jengo moja la ghorofa tatu limejengwa kwa shilingi milioni 500. Mimi naamini hii ilikuwa ni siasa na kama ni hivyo basi tunaomba hata hizi hela za vitabu zijenge hosteli nyingine katika vyuo vingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mloganzila, mimi niseme kwa mara ya kwanza Tanzania imejenga hospitali kubwa ya Kimataifa na imekamilika toka mwaka jana mwishoni lakini mpaka leo hajafunguliwa rasmi kwa sababu tu haina watumishi. Naiomba Serikali na namwomba Mheshimiwa Rais, kama alivyotoa vibali kwa wale madaktari walioshindwa kwenda kuajiriwa Kenya, atoe vibali ili hospitali ile iweze kufanya kazi. Kwa sababu hospitali ile ni kubwa

sana, ina vifaa vingi sana na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kama Mjumbe wa Kamati umeenda umeiona lakini imekaa pale kama *white elephant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana hospitali ile ifanye kazi kwa sababu itaingizia Taifa kipato kikubwa kwa sababu wagonjwa wengi watatoka nje ya Tanzania watakuja kutibiwa pale, kwa hiyo vipatikane vibali kwa ajili hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ualimu. Najua mengi yamezungumzwa kutokana na matatizo ya walimu na mimi niseme kama mwalimu. Elimu ni mwalimu. Mwalimu akipata mazingira bora ataweza kufanya kazi yake vizuri lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mulugo anaomba kuwatambulisha viongozi wa shule binafsi Tanzania wapo watano na wanaongozwa na Mwenyekiti wao Mzee Totela na Katibu Mheshimiwa Magero na chama chao kinaitwa *TAMOGOSCO*. Ahsante. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, Mheshimiwa Kishimba ye ye atachangia jioni nafasi yake ataichukua Mheshimiwa Agnes watafuatia Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Amina Molet.

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kuishukuru Serikali yangu ya CCM kwa kuendeleza elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka nichangie mambo machache yafuatayo. Ukitu hotuba ya Waziri wa Elimu na jitihada zetu zote za elimu inaonesha kupelekea

kuimarisha au kutengeneza kitu kinaitwa *quality education* lakini bila kuangalia sana *relevance of the education system*. Niiombe sana Serikali yangu, tatozo tulionalo Tanzania na nchi nyingi za kiafrika sio *issue ya quality education* tu, ni elimu stahiki kwa kiwango gani elimu inawezesha kupambana na mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wote tunajua Tanzania 77% ya wananchi wetu ni *agricultural population* kwa hiyo ungetegemea shule ya msingi na sekondari zifasili kilimo, ungetegemea shule za sekondari na msingi yaani *basic education zi-articulate* hiyo, zibebi mzigo huo wa changamoto ya kilimo lakini haiko hivyo. Mwanafunzi anaanza darasa la kwanza mpaka anafika *form six* hajakutana na kilimo lakini akimaliza *form six* tunamtaka aende akalime haiwezekani, haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu ni moja. Ni muhimu sana masomo ya darasa la kwanza mpaka kidato cha nne yawe yamebeba *elementary education* ya kilimo yaani unatumiaje mbolea ya UREA, DAP, Minjingu, unalimaje mahindi, kahawa, korosho na mazao mengineyo. Turidhike mwanafunzi akiishia kidato cha nne atakuwa amepata elimu inayomtosha yeye kujajiri ili wanaoenda vyuo vikuu wawe ni wale tu wanaostahili kwenda vyuo vikuu, sio kulazimisha kutanua wigo hata wale ambao hawajafaulu kwa kukidhi viwango vyya vyuo vikuu tushushe alama za kuingia chuo kikuu ili tu watu wengi waende, tutakuwa tunapoteza rasilimali za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu ilione jambo la vyuo vikuu binafsi. Vyuo vikuu binafsi kwa mujibu wa *ownership* ni *private institutions* lakini *establishment* yake ni *public institutions*. Ni sera ya Serikali ndiyo iliyoanzisha vyuo vikuu binafsi. Ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu vizuri na Waziri anafahamu vizuri Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne ndiyo waliopelekea kuanzisha vyuo vikuu binafsi kwa sababu tulipoanzisha shule za sekondari za kata swalii likaja

watakapomaliza wataenda wapi, tukafungua utaratibu wa kuanzisha vyuo vikuu binafsi. Njiombe sana Serikali yetu hasa *TCU*kupeleka wanafunzi kwenye vyuo vikuu binafsi sawa na vyuo vikuu nya umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi nadhani hawajui vizuri, ni lazima tufahamu hata wakuu wa vyuo vikuu binafsi wametokana ama na Chuo Kikuu Dar es Salaam ama Sokoine ama Mzumbe. Kwa hiyo, elimu inayotolewa kwenye vyuo vikuu binafsi ni sawa kabisa na inayotolewa kwenye vyuo vikuu nya umma. Naomba sana tusivitizame vyuo vikuu binafsi kama vile viro viro tu au kama vimejileta tu hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo naomba fedha za mishahara zinazokatwa kwa walimu wa vyuo vikuu binafsi kwenda kuchangia *Loan Boardna contribution* zingine zote wanazotozwa vyuo vikuu binafsi ziondolewe. *Treatment* ya vyuo vikuu binafsi iwe sawa na *treatment* ya vyuo vikuu nya umma. Ni jambo la muhimu sana kwa sababu vyuo vikuu binafsi ndivyo vinavyopelekea kutengeneza ajira kwa watu wetu, lakini pia vinakidhi haja ya kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata maeneo ya kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye *entry qualification* na hasa kwa walimu wa vyuo vikuu. Ukisoma maelekezo ya *TCU*ili uingie kuwa mwalimu kwa vyuo vikuu kwa kawaida ni lazima uwe ama na *first class or upper second* ya *GPA* kati ya *3.6 or above*. Naomba sana *TCU* mkumbuke kabisa kwamba kwa wale waliosoma zamanii hasa walio-graduate vyuo vikuu miaka ya 90 au nyuma kidogo, darasa tulikuwa tunakuwa wanafunzi 60 au 30 lakini *first class* anakuwa mwanafunzi mmoja au wawili ndiyo tulivyokuwa tunafaulu hivyo. Tumefaulu ni mwanafunzi mmoja ni kwa *first class, upper second, good upper second*, lakini kuna watu ambao baada ya kumaliza wamekwenda kwenye *field*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *an engineer* ambaye ame-graduate kwa *lower second* Chuo Kikuu Dar es Salaam huyu

ni *civil engineer* akaenda ku-practice 10 years anaporudi kutaka kufundisha sasa ameshapata *degree* yake ya uzamili (*master degree*) bado unamtaka awe na 3.6 *GPA*, unasahau *added value* aliyo-*accrue* kwenye ku-practice *engineering* inamzidi aliyeko chuoni. Ndiyo maana naomba sana *TCU* pamoja na kuweka hivyo vigezo wekeni dirisha la watu wale wenye sifa za ziada walio-practice ili kuwa sasa na walimu ambao si tu wamejikita kwenye kufundisha *theory* lakini wanaweza kufundisha *theory* na *practice* kwa sababu kwanza wame-practice.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hili litakuwa muhimu sana kwa sababu hivi tunavyosema inakuwa ni mtihani mkubwa pale ambapo mwali mu amemaliza *degree* ya kwanza, akamaliza *master degree na degree* ya uzamivu akiwa shuleni, kwa hiyo, ye ye ni *master of a school*. Sasa ni muhimu sana ku-recruit Walimu ambao wako nje ya mfumo wa vyuo vikuu ambao wame-practice kwenye *field* hizo ili waweze kuwfundisha wanafunzi wetu elimu ambayo ni ya vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea hiyo *relevance of education*, niombe sana ni vizuri *primary education* kama wenzetu wa Kenya walivyo tutoke darasa la kwanza mpaka la nane sio *six years*. Kwa sababu lengo letu ni lazima *u-manage* katika wanao-*graduate* na *your ability to employ those people*. Mfumo wa elimu uliopo sasa hivi wote sisi shahada zetu zimejikita kwenye kuajiriwa sio kujiajiri. Ndiyo maana ni vizuri Mheshimiwa Waziri aelekeze vyuo vikuu vito au vitengeneze mitaala yenye kutosha wanafunzi kujiajiri. Hapa tulivyo hata waki-*graduate* watu 100,000 *what next?* Serikali haina uwezo wa kuajiri na *degree* zetu si za kujiajiri ni za kuajiriwa. Tusipobadilisha hili tutakuwa na *graduates* ambao hawalisaidii Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi kidogo kuhusu wanafunzi wanaopata mimba. Nisikitike kidogo, maana yake najuliza kidogo, sasa hivi ilivyo ni kwamba mwanangu mie ambaye anasoma sekondari akipata mimba yuko *form one, form two, form three*

anaachishwa shule, lakini kama mimi baba yake nadhani kwamba bado anahitaji kusoma nitampeleka kwenye shule ya *private* ninayotaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mfumo upo. Maana yake majadiliano mengi ni kama vile mfumo huo haupo aah upo. Binti yako amepata mimba anaachishwa shule lakini akiishalea mtoto ukitaka mpeleke *form one* shule nyingine ni ruksa, ukitaka mpeleke kwenye mfumo mwengine wa elimu ni ruksa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu nataka tutazame vizuri, ukiangalia tatizo la mimba kwa mfano *primary education* mwaka jana kwa maana ya taarifa ya *BEST* ni wanafunzi 251 kwenye lakini utoro ni 82,850, sasa Wabunge wengi tunajikita kwenye kuangalia 251 *vis-a-vis* 100,000. Ni vizuri ifahamike vizuri, hivi mwanafunzi wa miaka 12 tunamlea kwa *do not* au kwa *counseling*. Maana yake mwanafunzi ukimwambia mwanangu ukipata mimba aah unaendelea na shule, *the yeskwenye mapenzi zitakuwa nyingi kweli*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana mimi nasema wale wanaowapa mimba wanafunzi wapewe adhabu kali mbali na miaka 30 wapewe jukumu la kuhakikisha hatma ya elimu ya huyo aliyepewa mimba. Sheria iweke *clearly kwamba you shall be responsible on the fate of that girl including handover* yake ya *education*. Maana watoto hawa ni wadogo, kwa hiyo ukifungua *paradox seriously* utaingia darasani kufundisha watoto thelathini wana mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa anakuja Mheshimiwa Agnes, ajiandae Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Amina Moel.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza nitoe pongezi sana kwa

Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kutoa elimu bure kwa wanafunzi. Imefikia hatua sasa vijijini watoto wengi wanakwenda shulenii, hakuna watoto wanaokaa majumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kipekee nimpongeze Waziri Mheshimiwa Profesa Ndalichako. Kwa kweli mama anafanya kazi nzuri sana, tuko nyuma yake na Mungu amsimamie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Magufuli ampe Mheshimiwa Profesa Ndalichako pesa ya kutosha ili arekebishe mambo mengi ndani ya elimu ili mambo mengine ambayo yanaleta shida ndogo ndogo yakae sawa. Kwa mfano, elimu ya shule za Serikali, shida siyo kwamba eti wanafunzi hawaelewi au Walimu hawafundishi. Hata kama wewe nyumbani kwako ukiwa una njaa huwezi kufundisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iwaangalie hawa Walimu kwa macho mawili kwa sababu Walimu ndiyo wamemfundisha Rais, wamemtoa Mbunge lakini Walimu wanafanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee suala la kupandishwa madaraja kwa Walimu. Ni muda mrefu sasa Walimu wanalamikia suala la kupandishwa madaraja na hasa vijijini. Mkoani kwangu Mara Walimu wengi wanalamika hawajapandishwa madaraja. Namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana hili kwa macho mengine kwani hawa Walimu wanapopata motisha wanaweza kufundisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine Mkoani kwangu Mara, Wilaya ya Rorya, Kijiji cha Kinesi, Tarafa ya Suba, kuna shule moja ya Isango. Hiyo shule ameuziwa sijui ni mtu gani, tangu mwaka 2014. Shule hiyo ilikuwa inasaidia watoto wengi sana na Mkoa wa Mara tuna uhaba wa shule.

Mheshimiwa Waziri hii kesi iko Mahakamani muda mrefu sana, nimwomba sana alisimamie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Magufuli huko aliko namwomba, yeche na mtu wa vitendo aangalie suala hili la Shule ya Isango ili irudi mikononi mwa Serikali na wananchi. Wananchi wa Ranya wanaweza wakaiendesha shule ile na wako wadau ambao wako tayari kwa ajili ya kuiendeleza. Sasa hivi imekaa kama gofu wakati Mkoa wa Mara tuna upungufu wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la ongezeko la tozo chefuchefu kwa hizi shule za watu binafsi. Nasema tozo chefuchefu kwa shule za watu binafsi kwa sababu, hizi shule zimeongeza na kupandisha kiwango cha elimu, kwa hiyo, tunapowawekea kodi nyingi ina maana kwamba tunataka kuwakwamisha wasiendelee au tunawakomesha wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema tunawakomesha wananchi kwa sababu hizi tozo zinapokwenda kwa hawa wakuu wa shule au wamiliki wa shule anayezilipa ni mwananchi. Yule Mkuu wa Shule unapomwongeza na yeche zile asilimia anaongeza ada kwa mwananchi. Katika mazingira ya kawaida tunawaonea wananchi, hatuwaonei hawa wenye shule. Kwa hiyo, hili suala tuliangalie mara mbili kwa ajili ya kupandisha kiwango cha elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Ndalichako, kipekee na-*declare interest* kwa sababu mimi pia ni mwanafunzi ambaye nimesoma hayo masomo ya *QT*. Wameongea humu Wabunge wengi lakini hawajaongelea suala hili. Kipekee nimwombe Waziri aangalie vile viwango vya ufaulu vishuke kidogo kwa hawa wanafunzi wanaosoma masomo ya jioni kwa sababu wanapokuwa wanawekewa *marks* za juu sana na wengi wao ni watu wazima, wanatoka maofisini, wanakuwa wamechoka wanawaza mambo mengine inakuwa ni vigumu kufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri washushe kidogo viwango hivi ili watu wengi wapate moyo wa kusoma. Mheshimiwa Waziri naamini hili atalichukua kwa mikono miwili ili hata wale amba ni vilaza wenzangu na wao wakasome hii elimu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Mara tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa shule za msingi na sekondari na hasa vijiji. Wilaya ya Ranya, Tarime, Serengeti, Bunda, Butiama na Musoma Vijiji, nimwombe sana kiongozi wangu atuongezee Walimu ili wale wanafunzi na wao waweze kufundishwa vizuri. Kwa sababu wanakuwa wanafunzi wengi sana lakini unamkuta mwalimu labda mmoja au wawili. Kwa hiyo, kipekee nimuombe Waziri atusaidie kutupatia Walimu Mkoani Mara.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ester Mahawe ajiandae Mheshimiwa Amina Molel.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mungu kwa ajili ya kutujalia afya sisi wote tulioomo humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na pole kwa wanafunzi waliopoteza maisha kule Arusha na nimpe pole mmiliki wa shule ya Lucky Vincent. Pia niwashukuru sana wale Wamarekani waliokuja kuchukua wale majeruhi watatu na kuwapeleka Marekani kwa ajili ya matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa *declare interest*, mimi ni mdau wa shule binafsi. Nimwombe sana Mheshimiwa Mwigulu Nchomba, hivi navyozungumza magari mengi ya shule katika kila mkoa yanakamatwa na kuwekwa *yard*. Gari asubuhi limetoka na wanafunzi nyumbani, linapeleka wanafunzi shule, wakienda kushusha watoto magari yale yanachukuliwa yanapelekwa *yard* kwamba gari hili bovu, tumepata *pressure* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zitafungwa ndani ya wiki mbili kuanzia sasa. Tunaomba wamiliki hawa wa shule binafsi wapewi nafasi ili wakati ule wa mwezi wa saba kipindi shule zikiwa likizo hayo mapungufu yaliyoko kwenye hayo magari yakafanyiwe kazi lakini wawaache watoto sasa hivi waendelee na shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza kuona kwamba tunafanya vitu kwa kukurupuka. Hawa ma-*traffic* walikuwepo barabarani miaka yote wakati hawa watoto wanaenda shulen na hayo magari. Leo imetokea ile ajali imekuwa mateso kwa wamiliki wengine. Mheshimiwa Mwigulu tusaidie kwenye hili, wasitishe hilo zoezi. Shule zitakapofungwa mwezi huu wa Saba magari yatarekebishwa halafu ndiyo michakato mengine iendelee. Hilo ni ombi kwa Mheshimiwa Mwigulu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la hivi vitabu. Mimi nina maswali kama matano na Mheshimiwa Profesa Ndalichako atakapokuja hapa tunaomba atusaidie. Je, ni nakala ngapi za vitabu vya darasa la kwanza, la pili na la tatu vilivyokwishesambazwa. Pili, vitabu vimetayarishwa kwa gharama za walipa kodi Watanzania ambavyo ni vibovu, nani anawajibika kwenye hili? Fedha kiasi gani zimetumika kuandika, kuchapisha na kusambaza vitabu hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi vilitumia muda wa miaka mitatu kuiandaa, tunasema vitabu hivi sasa havifai viondoke sokoni, je, ni muda gani zaidi utatumika mpaka tupate vitabu mbadala wa hivi? Sisi wamiliki wa shule binafsi, mfano mimi nimenunua vitabu vya shilingi milioni 18, najiuliza nalipwa na nani gharama zile? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Mulugo amenunua vitabu zaidi ya shilingi milioni 30, nani analipa gharama hizo? Wakati hawa watu wa *TET* wanaandaa huu mtaala, tuliomba kwamba wawashirikishe watu wengine mbalimbali kwa maana hata kutoka kwenye sekta binafsi ili waweze kupata *inputs*, wakajifunga

vyumbani, wakakataa ushauri, leo wamekuja na vitu vibovu, nani anawajibika? Kwenye vitabu nimemaliza, ninavyo hapa ni upuuzi mtupu unaendelea hapa. Hata Kiingereza cha mtoto wa *English Medium* wa darasa la tatu hawezি kutunga vitabu vya namna hii. Sijui ni wataalam gani walitumika kutunga hivi vitabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya vitabu naomba nielekee kwenye suala zima la kodi kwenye shule binafsi. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba leo mnielewe, wakati mmiliki wa shule binafsi anaposimama na kuzungumza habari ya kodi 15 tunazizungumza, niliwahi kuzisoma hapa Bungeni mkashika vichwa, hatujitetei sisi maana kodi hizi mnazilipa ninyi ambao watoto wenu wanasona kwenye hizo shule, tunawatetea akinamama ntilie na wananchi wa Tanzania kwa ujumla wao. Maana kama kwenye shule ada ingekuwa Sh.200,000 inakuwa Sh.400,000 kwa ajii ya hizi kodi na anayezilipa ni wewe mwananchi sio mimi mwenye shule, mimi ni wakala tu wa kuzikusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaposimama hapa, ile *negative attitude* kupitia kwa wamiliki wa shule tulipo humu Bungeni iondoke kwamba hawa watu wamekuja kutetea maslahi yao binafsi. *After all* kipele kinachokuwasha wewe mgongoni mwako unakijua wewe mwenyewe na maumivu yake, sasa nisiposema mimi atasema nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* majengo ya shule yalivyo makubwa unatakiwa ulipie *property tax*. Sheria ya Elimu ya mwaka 1977 iliomba watu binafsi waweze kuisaidia Serikali kutoa elimu kwa nchi hii. Sheria ya Elimu ya mwaka 1977 inatutambua sisi kama watoa huduma, Wizara ya Fedha inatutambua sisi kama wafanyabiashara, tushike lipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya nchi yetu inasimamiwa na Wizara zaidi ya moja, Wizara ya Elimu, TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Afya, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi yaani nazungumzia *SUMATRA* huko

kwenye mabasi na kadhalika, kwa hiyo, kila mtu anakupiga kivyake. Kusema ule ukweli *it is like a crime for you owning a school in this country*, wakati Uganda na Kenya mtu anayetaka kuanzisha shule anasaidiwa na Serikali *almost 60%*. Leo sisi watu wamejitoa, halafu haya mambo yangekuwa yamewekwa bayana wakati unatafuta usajili wa shule kwamba kuna kodi hizi na hizi, *these are the criteria* hakuna mtu angeanzisha shule kwenye hii nchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna dirisha la wawekezaji kusamehewa kodi wanaokuja kuchukua *Tanzanite* zetu, ardhi zetu, malighafi mbalimbali lakini mwekezaji Mtanzania ambaye ye ye ndiye ana uchungu na Watanzania wenzake, anayewekeza kwenye elimu ya nchi hii hana msamaha wa kodi hata kwenye vitu tu kama *cement*, bati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ya wenye shule 100 ukiwapima wote wana *pressure* na sukari labda wasiokuwa na maradhi haya ni wawili. Ni tabu tupu. Kama Serikali tu yenye we inashindwa kutengeneza miundombinu mizuri na kutoa elimu bora kwa watu wake sembuse mtu mmoja? Ifike mahali Serikali itambue juhudini zinazowekwa kwenye hizi shule na watu binafsi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nimwombe Mheshimiwa Profesa Ndalichako, ilikuja barua kutoka kwa Kamishna wa Elimu kwamba hakuna mwanafunzi kukaririshwa darasa. Naomba nisome *effect* ya hilo suala la kutoikumkaririsha mtoto darasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, matokeo ya mwaka jana na mwaka juzi ya kidato cha nne, wanafunzi waliopata *division one* mpaka *division three* ni 53,000. Mwaka 2015 wanafunzi waliopata *division four* na zero 354,000. Wanafunzi waliopata *division one* mpaka *three* mwaka 2016 ni 54,000 na wanafunzi 347,000 waliopata *division four* na zero. Yet mnatuambia hakuna kukaririshwa darasa, hivi tunawaandaa watoto wamalize darasa la saba na *form four* au tunawaandaa ili elimu wanayoisoma iwasaidie? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, huko kwetu kwenye shule za binafsi ni mapatano ya mzazi na mwenye shule, kila shule ina *joining instruction* kwamba mtoto wako asipofikia hii *marks* kwa kweli hawezi kwenda mbele na mzazi ana *sign* na tunakubaliana. Imetokea tu mzazi mmoja amekwenda kulalamika huko Wizarani ndiyo inakuja kuandikwa waraka wa namna hii, *this is not fair!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunashangaa ufaulu ambao ni mbovu kiasi hiki, watoto wanaofaulu *division one* mpaka *three* ni 54,000 kwenye malaki ya wanafunzi unatoa waraka kama huu. Naomba Wizara ya Elimu itazame hivi vitu. Wakati mwingine wanapotoa maamuzi ya namna hii watushirikishe. Ninayezungumza ni Mwenyekiti wa wadau wa shule binafsi Tanzania niko humu humu ndani. Tunaomba tushirikishane hivi vitu vingine maana tunaumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wanafunzi zaidi ya laki saba kwenye shule za binafsi Tanzania. Tumeajiri zaidi ya watu 45,000 Walimu na wasio walimu, kuna *matrons*, madereva, wapishi na kuna kila kitu. Tunachangia uchumi wa nchi hii kwa kununua vyakula na mahitaji mengine, sisi sio watu wadogo, tunaomba tutambulike kwenye hii nchi kwamba tunasomesha Watanzania wenzetu. Hakuna Mchina atakayekuja kujenga shule hapa, hakuna Mwingereza atakayekuja kujenga shule Tanzania ili Watanzania wasome. Wakiwasaidia kwenye elimu watawatawala namna gani? Sisi ndiyo wenyewe uchungu na Tanzania na ndiyo maana tumewekeza kwenye elimu. Kwa hiyo, tunaomba juhudhi zetu zitambulike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunacheza na *referee mchezaji*. Watoa elimu nchi hii ni TAMISEMI na watu wa shule binafsi lakini sisi tumekuwa watu wa kupokea maelekezo kutoka TAMISEMI, kutoka Wizara ya Elimu, tunaletewa tu hatushirikishwi. Kuwe na chombo maalum ambacho *kita-regulate* elimu ya nchi hii ili kuwe na *fair play* kati ya watoa elimu. Tuanzishe chombo kinaitwa *Tanzania Education and Training Regulatory Authority* ili kama kuna

shule ya msingi ya Serikali haina choo ifungwe kama inavyofungwa shule ya mtu binafsi ambayo haina choo. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae Mheshimiwa Ikupa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na hatimaye kuweza kusimama leo hii katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwape pole wazazi wote waliopoteza watoto wao katika ajali mbaya ya gari la shule iliyohusu shule ya Lucky Vincent, Mkoani Arusha. Niwape pole sana na Mwenyezi Mungu awajalie ili waweze kuendelea na mambo mengine na wale watoto pia waliokwenda jana kupata matibabu nje, Mwenyezi Mungu awajalie wapone na warudi kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nitoe pongezi za dhati kwa sababu amechangia kwa kiasi kikubwa watoto wenye ulemavu na hasa wazazi lakini walezi kuhakikisha kwamba wanawapeleka watoto wao shule ili waweze kwenda kupata elimu. Miiongoni mwa watu ambao walikuwa ni waathirika wakubwa katika suala zima la elimu ni watoto wenye ulemavu ambao kutokana na mila, desturi na tamaduni zetu wazazi kwa mitazamo tu hasi waliwaacha na kuwafungia nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ujio wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kuleta elimu bure hata wazazi wenye wameona kwamba ni wakati muafaka wa kuwapeleka watoto wao shule. Kwa hiyo, nampongeza sana na niseme tu kwamba kwetu sisi tunaona

Mheshimiwa Rais Magufuli ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Waziri pamoja na Naibu wake na hawa ni akinamama. Wanasesma siku zote uchungu wa mwana aujuaye mzazi. Niwapongeze sana lakini pamoja na pongezi hizo na pongezi za ujumla kwa Serikali vilevile basi nizungumzie changamoto zilizopo katika suala zima la elimu na hasa kwa watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu pamoja na kwamba hivi sasa shule nyingi watoto wamejitokeza na kwenda kupata elimu lakini nikianza na suala zima la miundombinu pamoja na kwamba Serikali imetoa vifaa, pongezi sana kwa hilo Mama Mheshimiwa Profesa Ndalichako lakini bado miundombinu ni tatizo na ni kikwazo kwa watoto wenyewe ulemavu kuweza kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia miundombinu ni kwa ujumla kuanzia madarasa lakini pia umbali na tatizo lingine kubwa zaidi ni vyoo. Pamoja na jitihada ambazo mmezonesha mnakwenda kujenga vyoo katika shule za msingi na shule za sekondari watoto wenyewe ulemavu wanapata shida sana wanapokuwa shulenii kwa sababu miundombinu ya vyoo inawafanya wasiweze kufika katika maeneo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika vyoo vingi ambavyo vinatumia na wanafunzi wote kwa ujumla na hasa ukiangalia tundu moja wakati mwingine linatumika mpaka na watoto 25-30 kwa huyu mtoto mwenye ulemavu, mfano tu mtoto mwenye ulemavu anayetambaa, niambie mazingira yale anaifikaje chooni? Inakuwa ni vigumu sana. Kwa hili, niwaombe tulete sheria kwamba kila shule ni lazima kuwepo na vyoo ambavyo vitawawezesha watoto wenyewe ulemavu kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, nalishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nimshukuru Katibu pamoja na Spika kwa sababu wanaelewa kwamba

Bunge hili limetujumlisha wote lakini pia miundombinu ni rafiki inayotuwezesha kwenda katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na kwa sababu watu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania na wao wanakarabati hizi shule muwape mwongozo kuhakikisha kwamba katika kila shule wanayokwenda kukarabati wahakikishe vyoo viwili vinakuwepo kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na Walimu Wakuu waweke utaratibu maalum ambao utawezesha hawa watoto peke yao wenye ulemavu kwenda katika vile vyoo na wasiweze kuingia hao wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ni kweli kwamba Serikali imetoa vifaa kwa ajili ya watoto wenye ulemavu lakini kwa walimu bado ni tatizo. Ni tatizo kwa sababu gani? Kwa mujibu wa mwongozo wa huduma kwa watumishi wa umma wenye ulemavu ambao unasema nyenzo na vifaa vya kuongeza uwezo wenye ulemavu Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kwamba watumishi wenye ulemavu wanapata huduma zitakazowasaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu kama vile nyenzo na vifaa ili kuwasaidia kuongeza kiwango chao cha kujitegemea katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwongozo huu unawataka waajiri na siyo kwa Wizara ya Elimu peke yake ni waajiri wote kwa ujumla na bahati nzuri yupo hapa Mwenyekiti wa Waajiri hili pia alibeve na kusitiza waajiri wote wanaowaajiri watu wenye ulemavu wanahakikisha ni kwa namna gani watu wenye ulemavu wanaweza kufika katika sehemu zao za kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu nachangia Wizara ya Elimu, hawa Walimu wana changamoto nyingi, hawana nyenzo muhimu ambazo zinawawezesha wao kuweza kufanya kazi zao kwa ukamilifu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuimba na kuishauri pia Serikali kuhakikisha kwamba inawawezesha Walimu hawa.

Ukiangalia katika Wizara ya Elimu hawa Walimu wenye mahitaji maalum wengi ndiyo wanaopata ajira kwa wingi huku, kwa hiyo, tuhakikishe tunawawekea miundombinu pamoja na kuwapa nyenzo ili waweze kufanya kazi zao pasipo usumbu. Vilevile kuhakikisha wanawekwa maeneo ya karibu ili basi wasipate shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba kumekuwepo na utaratibu ambapo Serikali inaratibu wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma katika shule tofauti, tofauti, mfano, shule ya Buigiri na Furaha kule Tabora na nyinginezo. Wanafunzi wenye ulemavu ambao wanakwenda kusoma kwenye shule hizo kwa sababu ya mila, tamaduni, desturi na mitazamo, wazazi wengi wanaona kwa nini ampeleke mtoto lakini sasa hivi wanakwenda na Serikali ikaweka utaratibu kwamba hawa wanafunzi wakati wa likizo inawasafirisha kuwarudisha nyumbani lakini mwaka jana mmefuta huu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Mama yangu anapofuta huu utaratibu hawa watoto wanabaki kule shuleni mwaka mzima. Kwa mzazi mwenye mtoto mwenye ulemavu mfano shule iliyopo Shinyanga ambayo sasa hivi imekuwa kama ni kituo wengi wamekwenda kuwatupa pale watoto hawarudi hata nyumbani. Sasa ule utaratibu wakiondoa kwamba hawawachukui tena kuwarudisha nyumbani yaani pale ndiyo inakuwa nyumbani kwao na kama mnavyojua tukasome lakini pia turudi nyumbani ili kujumuika na wazazi wetu. Wakituacha maeneo ya shule wasipotrudisha nyumbani ni sawa na wametutupa kwa maana kwamba sisi tunakuwa sasa ni watoto wa pale pale mpaka tumalize shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ye ye ni mama na siku zote mama ndiyo mwenye uchungu, apigane hawa watoto warudi nyumbani kwao, kuwepo na usafiri utakaowapeleka na kuwarudisha nyumbani. Ndiyo wamewaandalia mazingira lakini pia wakiwaacha kule miaka yote inakuwa ni kama vile adhabu

au ukizaliwa mtu mwenye ulemavu basi inakuwa ni kama vile ndio mkosi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasimama hapa na kutoa michango ni kwa sababu jamii ilituwekeea mazingira mazuri, wazazi wetu walikuwa wanajua umuhimu huo na ndio maana wakatusomesha na leo hii tuko hapa. Sasa tusipowaandalia mazingira mazuri tutawapata wapi akina Amina na Ikupa wengine.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ikupa halafu wajiandae Mheshimiwa Hamida na Mheshimiwa Tauhida, mtagawana dakika tano tano.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii adimu. Nami moja kwa moja niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa, Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo wameyashughulikia masuala haya ya watu wenye ulemavu kuitia Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako pamoja na Mheshimiwa Stella Manyanya wamekuwa ni mama zetu kwa maana kwamba wamekuwa ni wasikivu sana. Muda wote ambapo tumekuwa tukiwahitaji kwa ajili ya masuala ya watu wenye ulemavu wamekuwa wakipatikana kirahisi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa ni mpungufu wa fadhila nisipoishukuru Serikari kwa jinsi ambavyo imetoa kipaumbele cha elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu. Kwa sababu ya muda nitataja baadhi ya maeneo na si kwa umuhimu basi hakuna mengine. Kuna ukurasa wa 22 aya ya 45; ukurasa wa 23 aya ya 46, lakini kuna ukurasa wa 26 aya ya 53, hiyo nitaomba niisome kwa sababu ni kitu kigeni kidogo. Inasema:-

"Imeandaa Kiongozi cha Mwalimu wa Masomo ya Sayansi kwa wanafunzi wasioona na wenyewe uoni hafifu. Uwepo wa kiongozi hiki utasaidia wanafunzi wasioona wa sekondari kwa mara ya kwanza kuwezeshwa kusoma masomo ya sayansi".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni habari njema sana kwa watu wenyewe ulemavu. Pia shukrani zangu zinaendelea ukurasa 29 aya ya 55 mpaka (56) na ukurasa wa 30 aya ya 57 mpaka 59.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze sana Serikali, wakati Mheshimiwa Waziri akisoma hotuba yake siku ya Jumamosi alikiri kwamba kuna changamoto ya miundombinu na vifaa saidizi. Niombe tu Serikali tunaongelea mambo ya elimu jumuishi lakini haiwezi kuwa kama miundombinu haitaboreshwani. Kwa hiyo, niombe Serikali liendelee kutoa kipaumbele kwa habari ya uboreshaji wa miundombinu ili elimu jumuishi iweze kuwezekana katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hili niombe Serikali kwamba katika vyuo vyetu vya ualimu, kwa sababu sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa Walimu wa elimu maalum, kwa hiyo katika vyuo vyote vya ualimu nchini elimu hii ifundishwe. Kwa hiyo, Mwalimu anapotoka chuoni anakuwa ana ufahamu ama uelewa wa elimu maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapoongelea elimu jumuishi ni pamoja na Walimu, tusipokuwa na Walimu wa kutosha ambao wanafahamu elimu maalum hili halitawezekana. Kwa hiyo, niombe Serikali iweke mkazo ama iweke msisitizo kwamba katika vyuo vyote vya ualimu elimu maalum ifundishwe ili mwalimu anapotoka pale anapokwenda shule yoyote ana uwezo wa kumfundisha mwanafunzi mwenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Walimu wenyewe ulemavu. Inawezekana Serikali ikawa haina takwimu

sahihi za Walimu wenye ulemavu lakini Walimu hao wapo. Kwa hiyo, niiombe Serikali iwe na takwimu sahihi za Walimu wenye ulemavu ili waweze kujua changamoto na mahitaji walionayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pPamoja na ugawaji wa hivi vifaa ambavyo vimegawiwa lakini Walimu hawa wasipoangaliwa itakuwa pia ni kazi bure. Kwa maana kwamba Serikali ikiwa na takwimu sahihi za hawa Walimu wenye ulemavu itawawezesha ili waweze kuwa na sifa, maarifa na weledi kama Walimu wengine. Walimu hao wanahitaji pia kujengewa uwezo kwa njia ya mafunzo. Kwa hiyo, niiombe Serikali pia itoe kipaumbele sana kwa ajili ya mafunzo ya hawa Walimu wenye ulemavu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee tena kwa mara nyingine kwa sababu nimeshawahi kuongea kwenye Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali ione sasa umuhimu wa kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu ya Tanzania. Kwa nini nasema hivyo? Kila siku hapa tunalalamika kuhusu wakalimani wa lugha ya alama lakini kama hii lugha ya alama itafundishwa kwenye elimu yetu kuanzia darasa la kwanza mpaka *form four*, huyu mtu tunamuandaa kuwa Mwalimu, Mbunge, Daktari, Polisi, kiongozi wa madhehebu ya dini, kwa hiyo atawenza kuwasiliana na mtu ambaye ni kiziwi kwa urahisi. Kwa hiyo, niombe sana Serikali yangu sikivu ilione hili na kwa hapo baadaye tutengeneze kizazi ambacho kitakuwa kinaweza kuwasiliana na viziwi kwa urahisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee pia takwimu za watahiniwa wenye ulemavu kuanzia darasa la saba, *form four* mpaka cha kidato cha sita. Kwa nini nasema hivi? Mheshimiwa Profesa Ndalichako atakuwa ni shahidi hapa katikati nilimsumbuwa sana kwa habari ya uhamisho wa mwanafunzi ambaye alikuwa na ulemavu. Hizi takwimu za watahiniwa zitasaidia wakati wa *selection*. Unapomalizika mtihani wa darasa la saba Serikali ikafahamu kwamba tuna

wanafunzi wenye ulemavu wa aina hii kwa hiyo watawapangia shule kutokana na aina ya ulemavu walionayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe sana Serikali kuwa na takwimu sahihi za watahiniwa wenye ulemavu, hii itasaidia kwa habari ya *selection*. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwamba ule uhamisho ulifanikiwa na mtoto anaendelea na masomo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niishukuru Serikali sana kwa sababu mimi ni mwakilishi wa watu wenye ulemavu kuhusiana na wale watoto mapacha walioungana kule Iringa, Consolata na Maria ambao kiukweli Serikali imesimamia elimu yao na watoto wanakiri kwamba hakukuwa na shida kwao kwa sababu hata wakiwa pale shulen i wakati wa kidato cha sita walijengewa kajumba ambako kalikuwa ni maalumu kwa ajili yao peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili niongeze, ulemavu wa jinsi hii, Mheshimiwa Profesa Ndalichako yule mtoto ambaye nilimwomba uhamisho kwa ajili yake, amepangiwa shule ya Jangwani, lakini bado kuna changamoto kwa sababu ulemavu wake unahitaji usaidizi, yaani anahitaji mtu wa kumsaidia hawesi kushika kijiko kula mwenywewe. Kwa hiyo, niiombe Serikali ione jinsi gani ya kuandaa wasaidizi kwenye hizi shule kwamba anakuwepo matroni maalum kwa ajili ya watoto wa jinsi hii. Matroni atamuogesha, atamsaidia kwenda chooni lakini pia atamsaidia hata chakula na kumfulia nguo. Kwa hiyo, niombe Serikali pia hili iliangularie kwa jicho la tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na si kwa umuhimu naomba niongelee Bodi ya Mikopo. Nimekuwa nikiomba na imekuwa ni kilio changu cha muda mrefu kwamba wanafunzi ama watoto ambao wanafanikiwa kufika kidato cha tano na sita mpaka kufika chuoni ni wachache sana. Kwa hiyo, hii elimu bure inayotolewa naomba Serikali itolewe bure kwa watu wenye ulemavu yaani mtoto mwenye

ulemavu kama atafanikiwa kuingia kidato cha tano na mpaka kufika chuo, asomeshwe bure na Serikali kwa sababu wako wachache. Kwa hiyo, hata gharama ni ndogo haitakuwa kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu kwa leo ni hayo, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Hamida dakika tano na Mheshimiwa Tauhida dakika tano.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Niendelee kumpongeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa uwasilishaji wa bajeti ya utekelezaji wa mambo mbalimbali kuhusiana na masuala ya elimu kwa kipindi hiki cha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali kwa mafanikio makubwa ya kuhakikisha upande wa elimu unaendelea kuboreka. Hata hivyo, pamoja na mafanikio na jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali yetu bado tuna changamoto kubwa katika maeneo mbalimbali zinazowafanya watoto wetu washindwe kabisa kuendelea na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona suala la ujauzito ni changamoto kubwa sana kwa watoto wetu wa kike. Vilevile bado tuna changamoto zingine kama vifo na utoro mashuleneni umekithiri kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, lazima tujipange katika kuhakikisha utoro mashuleneni unaondoka kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado vifo vingi vinasababisha watoto wetu kushindwa kuendelea na masomo. Naiomba sana Serikali ijpange vizuri kuhakikisha kwamba maji salama yanapatikana katika maeneo yote kwa sababu maeneo mengi hatupati maji salama. Watoto wetu wanakunywa maji ambayo si salama na yanawasababishia matatizo ya kiafya na kwa sababu hospitali, zahanati ziko

mbali sana, si vijiji vyote vina hospitali, kwa hiyo, mtoto anapopatwa na ugonjwa wa kuharisha asipopata tiba kwa haraka kwa kweli inamsababishia kifo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali izingatie suala la upatikanaji wa maji katika maeneo yote ili kuhakikisha watoto wetu wanapata maji safi na salama na kuendelea kuimarisha afya zao ili waweze kumaliza elimu kama ambavyo wametarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali yetu kwa kukarabati vyuo vikongwe katika nchi hii. Katika mkoa wetu wa Lindi tuna *TTC Nachingwea*, chuo kile ni kikongwe kinahitaji kukarabatiwa kwani miundombinu yake ni mibovu na kimechakaa. Kama mimi ningekuwa Bwana Afya ningefunga kile chuo, kwa kweli kinasikitisha sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kukturazama chuo kile kwa jicho la huruma sana ili kiendelee kudumu kwa muda mrefu na kiweze kuzalisha Walimu kwa sababu mahitaji ya Walimu bado ni makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishukuru sana Serikali imeweza kukarabati Chuo cha Ufundı kilichopo Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Ruangwa. Tunashukuru sana chuo kile kimekarabatiwa na sasa kimeanza kupokea wanafunzi 28 na wameshaanza mwaka huu wa kwanza. Niombé sana Serikali kuharakisha kujenga mabweni kwa sababu bado tunahitaji watoto wa kike na wao waweze kushiriki katika kupata mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kike anapolala kwenye nyumba ya kupanga tunamtengenezea nafasi ya kushindwa kuendelea na masomo. Kwa hiyo, bado tunahitaji mabweni yajengwe pale ili watoto wa kike waweze kukaa katika mabweni na waendelee na masomo na itasaidia Wilaya nyingine zilizopo Mkoa wa Lindi watoto kuja kushiriki kupata mafunzo katika Wilaya ya Ruangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna mategemeo makubwa sana na Chuo chetu cha *VETA* kilichopo Mkoa wa Lindi katika eneo la Lindi Manispaa na hili nalizungumzia kila mara.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Tauhida.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii kwa kuchangia Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa na jitihada yao wanayoifanya, kwa kweli sisi kama Watanzania tunaiona wenyewe kwa macho. Kinachonifurahisha na kuniridhisha zaidi ni kwamba Mawaziri wote wawili ni wanawake. Mara nydingi wanapofanya kazi wanawake mimi kama Tauhida huwa najisikia ufahari mkubwa lakini hatuachi kusema mambo madogo madogo ili waweze kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mimba kwa watoto wa kike linahitaji umakini kwenye kutoa uamuzi. Ukiangalia suala hili kwa pande zote mbili kwa hoja zinazojengwa basi kila mmoja ana tafsiri yake. Naamini kwamba Waheshimiwa Wabunge ni watu makini na watatoa maamuzi sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye ukurasa wa 28 na 29 wa Taarifa ya Kamati, kuna sheria zinazomhusu mtoto wa kike, naomba ziangaliwe na zifanyiwe kazi. Nasema zifanyiwe kazi kwa sababu sheria ambayo ilitakiwa iletwe ni anayempa mimba mtoto wa kike kuwekwa ndani. Imani yangu ni kwamba atakayempa mimba mtoto wa kike akiwekwa ndani nina uhakika kwamba suala la mimba kwa wanafunzi litakoma au suala la mimba kwa watoto wa kike litakoma kwa sababu mtiaji mimba ataogopa kuwekwa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba ifike wakati kama wananchi na Watanzania tukubaliane kwamba mtoto wa kike anatakiwa apewe elimu ya kutosha, tusiwe watu wa kufumba maneno. Suala la kufumba maneno ndiyo limetufikisha hapa leo kutokubaliana.

TAARIFA

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba Bunge liliopita tulifanya marekebisho ya Sheria ya Elimu Na.60 katika kifungu (b) ambacho kimetoa adhabu ya miaka 30 kwa mtu yejote atakayempa mimba mtoto wa kike. Pia kimetoa adhabu kwa mtu yejote ambaye atasaidia kupatikana kwa mimba kwa mtoto wa kike na kifungo chake ni miaka mitano au faini ya shilingi milioni tano. Kwa hiyo, jambo hili tayari Serikali imeshalifanyia kazi, naomba nimpe taarifa hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tauhidha.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mchengerwa kwa ufanuzi na maelezo mazuri, nayakubali kwa kuwa mwanasheria ametoa jambo la ziada zaidi kutukumbusha, naikubali taarifa yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri amesikia kwa sehemu, naomba aweke mkazo kwenye maeneo hayo, yeye ni mama, ni mwanamke, hatupendi kuwa na Taifa wanawake wakakosa fursa ya kufanya kazi, kwa sababu tu ya hali ambayo wao hawakupendezewa nayo na wala hawakukubaliana nayo. Umri mtoto anaopata mimba ni mdogo, anarubuniwa, nafikiri ni wakati wa kulishawishi Bunge hususan wanawake wenzangu tuliotoka kwenye Viti Maalum kwamba tuje na mikakati ya makusudi na sheria za makusudi, mtoto mwanamke atafutiwe jinsi ya kulindwa aendelee na masomo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiamue kwa utashi tu, tusifikie wakati tukaamua bila kujua nini athari yake mbele. Ningeridhia sana kama ingekuwa bakora hii na sisi

tuliokuwemo ndani ingetukamata. Nazungumza kama ingetukamata kwa sababu watoto wengi wanaothiriwa na hili ni watoto wa vijijiini, watoto wa kimaskini. Nazungumza hivi Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tunaishi mitaani tunaelewa nini kinachoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtoto ye yote wa mtu aliye po humu ndani, tena namshangaa baba ye yote anayesimama humu ndani akadhani kwamba hakielewi kinachoendelea kule nje. Mtoto anayepata fursa ya kusoma ni mtoto wa mwenye pesa, ndio anayepata fursa ya kusoma, tufikie wakati tuwafikirie na walioko chini. Nazungumza mtoto yoyote wa mwenye pesa akishika ujauzito, ikifika mwezi mmoja au miwili anaenda kutolewa mimba kimya kimya inapita, baba ndani ya nyumba yake haelewi mtoto wake kama katolewa mimba maana haugui lakini isitoshe mtoto huyo huyo atatafutiwa shule ya mbadala kwenda kusoma. Inaniwia vigumu kutokuitendea nafsi yangu haki, nataka apewe fursa mtoto wa kike kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kwangu mimi ni kigezo Wabunge wangapi wa kike humu mnaendelea kusoma. Wabunge mmebeba mimba zaidi ya tano ya sita mmezaa na mnakaa na waume zenu. Tuwatafutie mustakabali watoto wa kike tunawafanyaje, tunawasaidiaje? Huwezi kuwa Mbunge wa Viti Maalum uliyeteuliwa na wanawake wenzio... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Othman Omar dakika 10, ajiandae Mheshimiwa Lucia Mlowe dakika tano na Mheshimiwa Pascal Haonga dakika tano.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Pia napenda nifikishe salamu kwa Mheshimiwa Waziri kutoka kwa

Mkuu wa Idara ya Fizikia pale Dar es Salaam kwamba aende akawatembelie. Kuna maabara yao imechoka, vifaa vyao vimechoka, kwa hivyo aende wakashauriane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nieleze tu kwamba mimi ni Mwalimu, nafundisha masomo ya sayansi na hisabati. Nakumbuka katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia kuhusu tatizo la masomo ya sayansi katika nchi yetu. Akasema kwamba uchumi wa viwanda unategemea kwa kiasi kikubwa rasilimali ya watu wenye ueledi wa masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile akasema kwamba changamoto tuliyonayo hapa Tanzania mpaka sasa hivi ni vijana wetu kutopenda kusoma masomo ya sayansi na hisabati. Akienda mbali zaidi Mheshimiwa Waziri Mkuu kusema kwamba changamoto tuliyonayo ikiwa wanafunzi na vijana wetu hawatajitalidi iko hatari ya viwanda vyetu kuja kuwategemea wataalam kutoka nje na hivyo Watanzania kubakia watazamaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri nilifikiria angalau angetoa mwelekeo au kujibu hii hotuba ya Waziri Mkuu, jinsi gani anajipanga kwenda kutoa suluhisho la matatizo ya masomo ya sayansi lakini naona hotuba iko kimya. Kama Waziri mwenye dhamana wa Wizara hii tunapenda awaeleze Watanzania changamoto hii ya vijana wetu kutopenda kusoma masomo ya sayansi anakwenda kuitatua vipi? Ukitilia maanani wajibu wa Wizara yake ni kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na mahitaji tuliyonayo ya nchi sasa hivi ni vijana waliosoma masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa pili ni kuimarisha matumizi ya sayansi na hisabati. Tatu ni kuendeleza wataalam wa ndani wa sayansi na hisabati. Haya ni majukumu ya Wizara ambayo yameandikwa katika kitabu hichi lakini mpaka sasa hivi pamoja na changamoto hizo sijaona vipi anakwenda kilitatua tatizo hili la wanafunzi ambaeo hawapendi kusoma masomo ya sayansi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimjulishé Mheshimiwa Waziri na Watanzania ni kweli usiopingika kwamba vijana wetu kusoma sayansi sasa hivi hawataki. Tatizo kubwa linalowasibu ni kwamba wale ambao wanajaribu kufuatilia masomo ya sayansi hawapendi kusoma hisabati. Huwezi ukaisoma sayansi ikiwa utaiacha hesabu, unaweza ukaisoma hesabu ukaiacha sayansi lakini huwezi ukasoma sayansi bila hisabati. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwalau mu sana Walimu wetu wa sekondari, kwa sababu wanafunzi hawa japokuwa wakifika pale sekondari wanaanza kuchanganyikiwa, kwa sababu hawa wanafunzi wameanza kupoteza mwelekeo kutokana na *primary* waliyotoka walikuwa hawana msingi mzuri wa masomo ya hisabati. Kwa hiyo, msingi wa hisabati unajengwa pale ambapo wanafunzi wako *primary* wakifika sekondari ikiwa hawana msingi huo wa hesabu basi masomo haya ya sayansi watayasi kia tu na ikiwa wataya fuata yatawa angusha njiani. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijielekeze kwenye dhima nzima ya Wizara ya Elimu. Waziri kasema katika kitabu chake hiki hapa kwamba, moja ya dhima ya Wizara yake ni kuinua ubora wa elimu na mafunzo, pia kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania wenye kuelimika lakini pia wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa hili. Nataka kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri hapa kwa sababu kuna idadi kubwa ya Watanzania hasa walio katika sekondari wanapenda kujielimisha lakini taratibu zilizowekwa zinawarudisha nyuma kupata elimu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia mfano mimi mwenyewe mwaka 2009 nilipata nafasi ya kwenda kusoma Shahada ya Uzamili pale chuo kikuu na tulikuwa wanafunzi 11, kati ya hao wanafunzi saba walikuwa ni *Tutorial Assistance* kutoka vyuoni, mmoja alitoka Arusha. Hawa walikuwa wanapata mikopo kutoka elimu ya juu Mheshimiwa Waziri tulibakia wanafunzi wawili ambao tulitoka sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijuliza kwamba wenzetu wanatoka kwenye vyuo, sisi tunatoka sekondari sote tuna lengo moja la kulitumikia Taifa hili lakini wenzetu wanasoma pale vyuoni kwa raha kabisa. Tulibakia wanafunzi wawili ambao tumetoka sekondari hatuna msaada wa aina yoyote, kwa hiyo, tukabakia tunabangaizabangaiza mpaka tukamaliza chuo. Ukiangalia hii siyo haki kuona kwamba wanafunzi wote tuna lengo moja la kujenga Taifa hili wengine wakapewa msaada huu lakini wengine wakanyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo lililotukuta lilitupelekeea sisi wawili kusoma kwa shida kubwa sana mpaka ulipofika wakati wa kuandika *dissertation* ilibidi tutafute njia nyingine ya kukabiliana na maisha. Mimi nilitafuta *school* ya karibu pale iko Kawe ambapo viongozi wengi mnapeleka watoto wenu pale. Nataka nikupe siri kidogo ya ile shule ya *private* ambayo iko *top ten* katika kiwango cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokigundua kinachozingatiwa pale kwanza ni ubora wa Walimu. Maslahi ya Walimu yanazingatiwa, unapoingia pale unasomesha kwa raha kabisa, unaondoka nyumbani umeacha chakula unakuja pale huna tatizo la aina yoyote. Suala la pili ni idadi ya vipindi havizidi 20 kwa wiki, ni vipindi vinne kwa siku moja. Ina maana ukiwa unafundisha vipindi vinne kwa siku moja unapata wakati wa kutosha wa kumsaidia mwanafunzi, unapata wakati wa kutosha wa kusahihisha madaftari, unapata wakati wa kutosha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlowe dakika tano na Mheshimiwa Haonga dakika tano.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja

hii ya Wizara ya Elimu. Nami niungane na Watanzania wenzangu kuwapatia pole wazazi wa Arusha kwa kufiwa na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na miradi ya Wizara ya Elimu hususani fedha za miradi kutopelekwa kwa wakati. Nikiwa mwanakamati wakati tulipotembelea miradi tuligundua kwamba fedha haziendi kwenye miradi au kama zinakwenda basi zinakwenda kwa kuchelewa. Kwa mfano, mradi wa Chuo Kikuu cha Sokoine, mwaka jana walitengewa shilingi bilioni nne lakini mpaka Machi fedha hizi hazikwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nydingine ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo walitengewa shilingi bilioni 9.4 hadi Machi fedha hizi ziliikuwa hazienda. Niwaombe Waziri wa Elimu na Naibu wake fedha hizi zitakapotengwa safari hii mhakikishe zinakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee *campus* ya Mloganzila. *Campus* hii kwa kweli ni mfano, imekamilika mwaka jana na hii ina vifaa vyote vya kisasa lakini hakuna watumishi. Niombi Serikali kuhakikisha watumishi wanapatikana kwa ajili ya *campus* hii kwa sababu ni aibu kwetu sisi Watanzania kuwa na *campus* kama hii halafu haina wafanyakazi, hii inaonesha kwamba hatukuwa tumejipanga. Kwa hiyo, niombi Serikali ipeleke watumishi katika *campus* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee suala la watoto wa kike kurudi shulenii au kutorudi shulenii baada ya kupata ujauzito. Mimi kama mama na kwa ye yeyote ambaye ana uchungu wa mtoto au uchungu wa kuzaa, nafikiri jukumu la huyu mtu au la mzazi huyu ni kutetea kwamba mtoto wa kike akipata ujauzito kwa sababu anapata ujauzito huu kwa kurubuniwa si kwa kutaka na kwa mazingira magumu na wengi wanakuwa hawana fedha, hiyo ndiyo inayowasababishia kupata ujauzito. Kwa maana hiyo, naomba Serikali watoto hawa warudi shulenii mara baada ya kujifungua. (*Makofii*)

TAARIFA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayeongea, kitendo cha kuwaruhusu wanafunzi wanaopewa ujauzito kurudi shulenii kuruhusu ngono. Kama anakubaliana na hilo basi namwomba Mheshimiwa Mbunge aiombe Serikali iweke bajeti ya *condom* kwa ajili ya shule hizi. (*Makofii*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naikataa taarifa hii kwa sababu akina baba ndiyo mnaosababisha matatizo haya ya watoto wetu kupata ujauzito. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa mnatumia muda vibaya yule ana dakika tano tu.

MHE. ESTER A. BULAYA: Anapotosha.

MWENYEKITI: Haya *Chief Whip* toa taarifa yako.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mchangiaji kwamba kwa sababu ngono inasababishwa na wanaume na wenyewe pia wafukuzwe shule. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlowe endelea.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naipokea taarifa hiyo. Kwa asilimia kubwa hata kama sheria imekwishawekwa watu hawachukuliwi hatua yoyote, wanaopata matatizo ni watoto wetu wa kike, ndiyo wanaoathirika. Kwa hiyo, niiombe Serikali kulifirkira suala hilo kwa sababu imekuwa ina kigugumizi kulipitisha jambo hili. Niiombe tafadhali Mheshimiwa Waziri atusikilize safari hii walipokee suala hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la shule za *private*. Mimi pia na- *declare interest* kwamba, nina shule ya *private*, tena shule hii ni ya watoto yatima. Kwa kweli watu wa shule za *private* wanapata matatizo mengi sana. Tatizo la kwanza ni kodi nyingi halafu wanafuatiliwa sana wakati watu wa *private* wanakuwa wana vigezo vyote tofauti na shule za Serikali. Wana Walimu wazuri ambao wamegharamiwa kwa hela nyingi na wanalipwa vizuri, wana vifaa vyote vya shule, wananaunua vitabu vyote vya kutosha kwa ajili ya wanafunzi lakini bado Serikali inawabana.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haonga ajiandae Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa ya kuchangia Wizara hii. Nitachangia maeneo makuu mawili, nitaanza na madai ya walimu lakini pia nitazungumzia Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la madai ya Walimu. Mwaka 2016 Walimu zaidi ya 80,000 wamepandishwa madaraja lakini wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 200, fedha hizi hadi leo hazijalipwa. Tunajua kabisa kwamba haya madai ambayo ni shilingi bilioni 200 ni

fedha ambazo Serikali ingekuwa makini na inawajali Walimu ingekuwa imeshalipa. Leo tutaanza kutafuta mchawi ni nani, kwa nini watoto wetu wanafeli wakati tunajua kabisa kwamba Walimu wetu wana madai makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kulipa madeni haya kwa sababu Walimu wetu wengi wanakata tamaa sana. Walimu wakiendelea kukata tamaa matokeo tutayaona muda si mrefu na tusianze kutafuta mchawi ni nani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu fedha za Walimu wa maeneo mbalimbali nchini waliosimamia mitihani ya kidato cha nne mwaka 2015. Mheshimiwa Naibu Waziri nimewahi kumwona na kuwambia Wilaya ya Mbozi Walimu wanadai Serikali zaidi shilingi milioni 170, walismamia mitihani ya kidato cha nne, 2015 akasema atashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba Walimu hao hadi leo hii hawajalipwa hizo fedha za kusimamia mtihani wa kidato cha nne mwaka 2015. Naomba niulize, ni nani Mbunge humu au Waziri hapa ndani ambaye anaidai fedha Serikali za mwaka 2015 ambazo hajalipwa hadi leo hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa masikitiko makubwa kabisa wale Walimu wanasema kwamba wameshakata tamaa. Ukitikia Mwalimu anazungumza kwamba amekata tamaa, hili jambo kwa kweli madhara yake ni makubwa sana na haya mambo yatasababisha watoto wetu wafeli. Mheshimiwa Waziri naomba tafadhali Bunge litakapokuwa limeahirishwa mwezi Juni achukue angalau muda akaonane na wale Walimu wa Mbozi. Walimu hawa wanadai Serikali zaidi ya shilingi milioni 170 walismamia mitihani hawajalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya madai ni vizuri wakayalipa kwa sababu Walimu wetu kuendelea kudai nadhani sio afya na haitaleta picha nzuri katika matokeo

yanayokuja. Kama wanataka kusubiri majuto tutayapata ila majuto ni mjukuu. Namwomba Mheshimiwa Waziri chonde-chonde katika hili afike Mbozi akawasikilize Walimu wanaoidai Serikali fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Bodi ya Mikopo. Bodi ya Mikopo leo hii inafanya mambo ya ajabu sana Mheshimiwa Waziri na kama inawezekana ivunjwe. Maana kinachotokea wale watoto yatima ambao hawana baba wala mama wananyimwa mikopo. Mheshimiwa Waziri nimemwona juzi, nimemletea mwanafunzi ambaye baba na mama yake amekufa na nimempelekea na *Death Certificates* za wazazi wote wawili hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mwanafunzi alinyimwa mkopo na yuko *CBE* mwaka wa kwanza. Mwanafunzi huyu niliyempelekea hivyo viambatanisho vyote alishawahih kuomba apatiwe mkopo kwa sababu hiyo na hadi *appeal bado amenyimwa*. Tunao watu wa aina hii wengi sana katika Taifa hili ambao wamepoteza wazazi na wamenyimwa mikopo. Kama huwezi ukampa yatima mkopo unampa nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazo taarifa kwamba watoto wa Mawaziri ndio hao wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu wanapewa 100%. Mheshimiwa Waziri, kwa kweli suala hili tafadhali naomba mlichukulie kwa umakini sana, kuwanyima watoto wa maskini mikopo hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine mikopo hii ukiangalia wako wengine waliosoma...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Serukamba ajiandae Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti

ya Wizara ya Elimu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kuandika historia kwamba na sisi tunashiriki mazishi ya kuua elimu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya nina vitabu hapa na namshukuru sana Mheshimiwa Biteko aliyeanza kulisema hili jambo. Waheshimiwa Wabunge ukiangalia vitabu hivi kwa namna yoyote ile huu ni wizi. Kwa namna yoyote ile hii ni kuua kizazi cha kesho, lakini vitabu hivi vimepitiwa na vimewekewa ithibati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hawa watu wa *Tanzania Institute of Education*, naomba leo niliombe Bunge hili tuazimie wote walioandika vitabu hivi waende gerezani, haiwezekani! Vitabu hivi wamekaa watu ma-*specialist* wamevitunga, wameviangalia, wanavipitisha, vinasomwa na watoto wetu, haiwezekani. Waheshimiwa Wabunge ukichukua vitabu hivi, nitawasomea sentensi chache, '*which is wrong between a pen and a ruler, 21st Century?*' Huku ndani kila unakoenda unajiliza ni Tanzania hii kweli? Haiwezekani Waheshimiwa Wabunge. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge suala la vitabu hivi tusilifanyie mzaha hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu hapa wanasema, '*When, End and How*'. Hata neno 'and' hawawezi kuandika na ni *specialists* walikaa wamepitisha vitabu hivi, vina makosa. Hiki kitabu cha Kingereza, hiki ni kitabu cha Jiografia. Kuna sehemu *carbon dioxide* imeandikwa *canon dioxide*, kweli jamani! Hapa kuna kitabu, *standards* wenyewe mmesaini, lazima kiwe na gundi, hapa wamebandika tu *stepple pin* na hiki chenyewe cha kujifunza na kusoma hakina hata ithibati, kina mhuri tu wa *Tanzania Institute of Education*. Waheshimiwa Wabunge, ukisoma makosa hapa ni mengi sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makosa haya ni aidha hawa walioandika hivi vitabu na waliovipitisha, nadhani watakuwemo kwenye orodha ya watu wa vyeti *fake*. Kama hawa hawamo, *then* tuna tatizo kubwa zaidi. Maana haiwezekani mmekaa na mnajua Waheshimiwa Wabunge

zimetumiwa shilingi ngapi, shilingi bilioni 108. Shilingi bilioni 108 za Watanzania zimeandika vitabu ambavyo havisomeki. Hivi siyo vitabu! Halafu mnataka Wabunge tukae hapa tushangilie kama mambo ni mazuri, hili lazima tulikatae. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukishakosea kwenye kitabu tunaua *generation* ya kesho *unless tumeamua* kuwa wabinafsi. Naomba sana tuache ubinafsi, tuombe kwanza vitabu hivi viondolewe kwenye *circulation* ya Wizara ya Elimu. Pili, naomba sana, watu wote walioshughulika na vitabu hivi lazima waende kwenye mkondo wa sheria. La tatu, tuombe Waziri wa Elimu anapokuja hapa, hawa watu lazima walipe shilingi bilioni 108 za Watanzania, haiwezekani. Haya yanatokea kwa sababu hatujali na inawezekana kwa sababu watoto wetu hawasomi huko ndiyo maana hatuoni kama ni jambo kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini liko suala hapa linasemwa la shule za binafsi. Nataka niwarudishwe kwenye historia, siku za nyuma miaka ya 80, 90 shule za sekondari za Serikali hazikuwepo zilikuwa chache hawa watu wa *private* wakaja wakatoa huduma kwa Watanzania hawa. Leo tumejenga Shule za Kata, haiwezekani sasa zile hazifai tuzitupe kwamba wale ni wafanyabiashara tuachane nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono tuanzishe *Regulatory Authority* ya kusimamia *standard* za elimu Tanzania ili kama shule iwe na wanafunzi 45 ndiyo *standard*, iwe ya Serikali iwe ya *private* ambayo imezidisha ichukuliwe hatua. Maana sasa zinazochukuliwa hatua ni za *private*, zile za Serikali hawana vyoo ni sawa, hawana Walimu ni sawa, wanafunzi wako 300 ni sawa, haiwezekani! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nasema lazima tufike sehemu tutoe huduma lakini pia naomba shule hizi za *private* tuziangalie kwa jicho lingine. Jamani, watu hawa kwanza wanatoa *service* kwa Watanzania, lakini pia wanaajiri watu na wanalipa kodi. Kwa hiyo, tutengeneze utaratibu tuwapunguzie mzigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la kurudia darasa. Mimi nimesoma seminari wakati tunaanza tulikuwa wanafunzi 51, *by the time* tunafika *form three* tumebakia 28. Wengine wanabaki huko nyuma kwa sababu pale seminari ili upande darasa ni lazima upate wastani wa 50. Wakati tunafanya mtihani wa *form two* ili upande *form three* Serikali ilikuwa wastani ni D, seminari waliweka wastani ni C, wameamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha msingi ambacho tumesema kwenye Kamati, Serikali muweke *standards* ili mtoto anayekwenda shule ya *private* anapoanza tu ile *form one* aambiwe kwamba hapa usipopata *marks* hizi hupandi darasa, mzazi akikubali amechukua *choice* yake yeye mzazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli mnataka liwe Taifa ambalo watoto wanasoma moja kwa moja mpaka *form four?* Waki pata *division four* tunasema mwaka huu kufaulu ni kwingi sana lakini ukifanya *analysis* ya kufaulu ni *division four*. Hili Taifa ni letu wote, naombeni Waheshimiwa Wabunge tulisimamie, tusiache kuna watu pale Wizara ya Elimu wanafanya wanayoyataka sisi tunanyamaza, haiwezekani! (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana Wizara ya Elimu ukienda kila mtu anatoa *circular*. Zinakuja *circular* nyingine hata Waziri hajui, lakini *circular* ilishakwenda. Ukienda TAMISEMI wanafanya wanachotaka, kila mtu anafanya anachotaka, hapana. Jamani Taifa lolote ili lione kane limeendelea ni elimu ya watu wake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni sana tuzisimamie vizuri lakini tupunguze utitiri wa kodi kwenye shule za *private*, hawa wanatoa huduma, wanasomesha Watanzania. Kazi hii wamefanya kwa muda mrefu, haiwezekani leo ghafla tuwaache, wameajiri watu. Naombeni sana Serikali, nendeni mkakae muwaite watoa huduma hawa muongee mkubaliane vitu vya kufanya vile ambavyo Serikali inaweza kusaidia isaidie kwa sababu tutapata kwingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Waziri anapokuja kuhutubia leo aje na majibu ya kutuambia hivi vitabu vinatoka kwenye *circulation*. Aje na majibu ya kutuambia kwamba haiwezekani hivi vitabu vinasomwa na watoto wa Kitanzania. Lazima hawa walioandika vitabu hivi, nasikia kuna wengine mpaka vyeo wamewapa, *how?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli, unampa cheo kwa kitabu hiki cha Kiingereza au ndiyo maana wanataka kila mtu aongee Kiswahili saa hizi maana Kiingereza imekuwa tabu. Ndiyo maana kila mtu anasema Kiswahili, Kiswahili, Kiswahili, Kiswahili, ni kwa sababu wameshafanya haya? Waheshimiwa Wabunge tusikubali kuingia kwenye historia na sisi tulishiriki kuua kizazi kijacho. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nisiunge mkono hoja mpaka Waziri atakapokuja hapa kuniambia hivi vitabu wanavifanyaje? Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sixtus wajiandae Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Elimu. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri amekuwa msikivu, mkarimu, akipigwa simu anapokea na tukimpelekea matatizo yetu ya elimu anatusikiliza kwa utii na uadilifu mkubwa. Nimwombee kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwa na hilo hilo sikio la usikivu, liambatane vilevile na kusikia hoja ambazo tunaziwasilisha tunapochangia bajeti yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walatini wana msemo, *non scholae sed vitae discimus*, wakimaanisha *we do not learn for school but we learn for life*. Mfumo wetu wa elimu lazima

utambue kwamba tunatengeneza maisha yetu, maisha ya watoto wetu, maisha ya wajukuu zetu na maisha ya kizazi kijacho. Mjadala unaoendelea ni uthibitisho tosha tumejikwaa kwenye kutengeneza kizazi chenye matumaini ndani ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata vitabu vinavyokinzana, tunapopata mifumo ya elimu inayotofautiana kwenye Taifa lilelile, inayonung'unikiwa upande mmoja na upande mwingine ni tafsiri tosha Mheshimiwa Waziri ana kazi kubwa ya kufanya kwenye hili. Nimwombe hoja zinazohusu hadhi, *value, quality* ya elimu yetu, azibebe vizuri na azifanyie kazi kwelikweli, tukifanya hivi tutatengeneza Taifa ambalo lina matumaini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mifumo mizuri sana siku za nyuma na wote tumepitia kwenye mifumo. Mkono wa kulia na wa kushoto haufanani. Hata huohuo mkono wa kulia una vidole vitano vyenye urefu tofauti na Mwenyezi Mungu katuumba hivyohivyo tulivyotofautiana na ye ye ana makusudi ili tutegemeane. Haiwezekani wanafunzi wote Tanzania nzima wakawa na upeo sawa, wakawa na fikra sawa, wakaenda sawasawa. Ndiyo kuna watu amba Mwenyezi Mungu kawaumba wanafaa kuwa wanasyansi, madaktari, watu wa *art*, watu wa kilimo na wengine watu wa biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii iko wapi *SHYCOM*? Mtu toka akiwa mtoto mdogo anajua akipenda biashara basi kuna *form five* na *form six* iko *SHYCOM*. Ziko wapi zile Shule za Ufundzi za Ifunda, *Mbeya Tech, DarTech, Arusha Tech* ziko wapi leo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tunapokwenda kusema tunatoa elimu za ugoko, tusiangalie tulikodondokea tuangalie pale tulipojikwaa. Nimwombe Waziri, hata mnaposema *university* sijui zote ziko sawa, mimi namwambia hakuna kitu kama hicho, ni kanuni ya maisha. *University* ya Mzumbe lazima itakuwa tofauti na *University* ya Tumaini kwa hoja za kihistoria, kwa hoja za *infrastructure*,

kwa hoja ya *curriculum*, kwa hoja zote utakazotaka kuziweka. Mimi nimwombeni sana, hili jambo ni lazima tuliweke vizuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kukaririshwa madarasa. Hili wala hatuhitaji kuweka utaratibu kwamba watu wote wapite kutoka darasa la kwanza mpaka la saba bila kukaririshwa darasa, sasa kuna haja gani ya kufanya mitihani na mitihani tunafanya kwa ajili ya nini? Mitihani hii imewekwa kwa ajili ya *ku-control human behavior*. Usipopata tishio huwezi ukafanya au uka-*behave, it is human nature*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *human nature* siku zote jinsi ilivyo lazima umwekee utaratibu wa kumfanya akae kwenye mstari. Moja kati ya vitu hivi ni pamoja na kuweka mitihani, lingine usipofikisha wastani tutakufukuza, ni kama tulivyoweka sheria na taratibu nyingine. Sasa huku mnasema waende tu kwa nini mkifika *university* kuna *ku-carry over*, kuna *supplementary, this is contradiction!* Tunaji-*contradict* sisi wenywewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema hii elimu tunaiburuzaburuza, sawa twendeni lakini mimi niwaambieni kama *university* mnasema kuna *ku-supp*, tafsiri yake ni kwamba tunataka tutengeneze *a certain quality of education, the same i-apply* kwenye ngazi zote. Walatini wanasma, *repetitio est mater studiorum...*

MBUNGE FULANI: Wachaa.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mambo uliyoyafanya toka ukiwa darasa la kwanza ndiyo yanayokujenga wewe mpaka unapokuwa *university*. Sasa huku aende holela halafu akifika *university* ndiyo kwanza apate utaratibu, haya mambo hayawezekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme lingine, hili naomba niseme kwa utaratibu kidogo, ni jambo ambalo limegusa hisia nyingi sana za watu, ni suala la mimba za utotonii, mimba za shuleni, yule anayepata mimba aendeleee na

mafunko au arudi akajifungue na atafutiwe utaratibu mwagine wa masomo. *The same spirit* tunayo iweka kwenye kuitengeneza elimu ya nchi yetu izingatie mila na desturi, izingatie taratibu lakini vilevile izingatie mazingira mazuri yanayofanya kitu kinacho itwa *social structure vis-a-vis social responsibilities*, maana yake nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii yetu hii imekaa katika makundi ya rika, tunatarajia mtoto wa darasa la kwanza mpaka darasa la saba atakuwa na *behavior* fulani inayoendana na jamii. Atakayekwenda *university* *ata-behave* tofauti na atakayetoka hapa akawa baba, mfanyakazi, mzee mpaka kikongwe, hiyo ni *social structure* imetengenezwa. Mwenyezi Mungu ameumba kuna muda wewe utasoma, kuna muda utapevuka utazaa, kuna muda utakuwa baba, kuna muda utakuwa kiongozi, kuna muda utakuwa mzee umezeeka baadaye una-rest in peace.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea juzi, nashukuru waliosema hapa wengi tulikuwepo, wa kwanza Mheshimiwa Mama Sitta alikuwepo, wa pili Mheshimiwa Susan Lyimo alikuwepo, Mheshimiwa Ndassa alikuwepo, tuliongelea kuhusu wale watoto wa Shinyanga waliopata mimba wakiwa watoto, tulilia na kusikitika. Tukajipanga kule tukasema tuje hapa Bungeni tushinikize Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inaruhusu mtoto wa kike aolewe akiwa na miaka 14 tuifute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunataka watoto wazae warudi shulen. Tunajichanganya wenyewe hatujui tunakotaka kwenda. Leo hii tuna ajenda kubwa sana ya kuhakikisha Sheria ya Ndoa inayomkandamiza mwanamke tuiondoe halafu huku wazae, hivi sisi tumelogwa, hatujui tunachokitaka. Basi niwalize swali moja, kama tunaruhusu mimba mashulen, kuna *mechanism* gani ambayo tumeiandaa kuhakikisha kwamba hawa watoto hawataoana mashulen? *This is a contradiction! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe mama zangu na mimi natokana na mama, naelewa...

TAARIFA

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,
naomba kumpa taarifa msemaji anayeendelea kuchangia
atofautishe ndoa na mimba za mashulenii. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa endelea.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
nashukuru. Ndiyo hapo unapopata tofauti kati ya kuelimika
na elimu. Ukipata tofauti kati ya kuelimika na ellimu hutapata
shida. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani unaposema huyu
mtu asiolewe akiwa chini ya miaka 18, tafsiri yake nini? Hata
Sheria ya Ndoa wanakuambia ndoa haiwezi ikawa ndoa
mpaka mke na mume waingiliane. Tafsiri yake kama
wanaingiliana maana yake kuna mimba. Yaani vitu vingine
jamani wala hatuhitaji kutafuta misamiati, hatuhitaji kutafuta
maneno ya kupakana matope.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize na neno moja,
naomba nilinde kwenye muda wangu. Najua hili jambo lina
hisia, hasa kwa mama zetu hata kama mimi ningekuwa
mama nisingependa mwanangu limkute baya. Kihistoria sisi
tuliotoka kwa mama zetu tuna mapenzi ya dhati sana kati
ya mama na mtoto, mama siku zote hupenda mwanaye
yasimkute mabaya. Katika upendo huu wa mama kumpenda
mwanae kuna maeneo upendo humletea madhara mtoto.

TAARIFA

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti,
Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sixtus usubiri kidogo. Mheshimiwa Kangi.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa nzuri Mheshimiwa Mapunda. Alipokuwa anazungumzia Wabunge kwamba hivi ni nani ambaye ameturoga, mambo haya pia Mtume Paulo katika Wagalatia 3:1 alipokwenda kuhubiri injili kwa Wagalatia, baadaye aliporudi kule kwenda kuwaona wana hali gani akakuta tena wamekengeuka wamemgeuka Mungu akawaambia, enyi Wagalatia ni nani aliwearoga?

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa, endelea Mheshimiwa Sixtus.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Na iwe kama ulivyonena nani amewaroga. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida niwaombe sana jambo hili tulitazame katika mapana, ni jambo liliogusa hisia, hakuna mstari ulio-*clear* unaoweza kutofautisha mimba ya mtoto anayepata chini ya miaka 18 na ndoa. Tukihalalisha hilo basi tukubaliane kimsingi tunataka ile Sheria ya mwaka 1971 iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Edwin Sannda, hayupo, Mheshimiwa Omari Kigua ajiandae Mheshimiwa Keissy.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana wa leo ili niweze kusema maneno machache juu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Nimpongeze sana mama yangu pale Mheshimiwa Profesa Ndlichako na Naibu Waziri Injinia Stella kwa kazi kubwa sana mliyoifanya pamoja na uongozi mzima wa Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maeneo mengi ya kuchangia lakini nitaanza hasa na pongezi hususan ya ujenzi wa hosteli ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hili ni jambo jema sana kwa sababu Mheshimiwa Rais pengine na ushauri wako ameona awaondolee usumbufu watoto wetu. Wizara iliamua kujenga hosteli za Mabibo lakini Mabibo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pana umbali kidogo lakini hili lengo la Mheshimiwa Rais kujenga hosteli pale ameondoa usumbufu mkubwa sana kwa sababu hosteli hizi zimelenga hasa watoto wa maskini. Wapo wenye uwezo ambao wana magari ya kwenda na kurudi vyuoni mfano Waheshimiwa Wabunge hapa wana watoto wanaosoma pale wana uwezo/magari ya kwenda na kurudi vyuoni lakini hosteli zile zitasaidia sana watoto wetu na kuondoa usumbufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi hosteli za chuo kikuu aangalie sasa namna ambavyo anaweza kusaidia kujenga hosteli katika shule zetu za kata. Waheshimiwa Wabunge wanazungumzia hapa watoto wetu kupata mimba lakini sisi tunaotoka katika majimbo ambayo ni ya vijijini kule tunaona watoto wetu wanatoka mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri, najua Wizara ya Elimu na TAMISEMI wanashirikiana lakini leo hii lawama zinakuja kwa Waziri wa Elimu. Nimwombe, tuone umuhimu wa kujenga hosteli hususan kwa watoto wetu wa kike katika shule za vijijini hususan katika shule zetu za kata. Hii itaongeza uwezo wa *ku-perform* watoto wetu ufaulu utaendelea kwa sababu watapata utulivu wa kusoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie juu ya suala la udhibiti na ukaguzi wa elimu. Wabunge wengi wamelizungumzia hapa na pengine kitendo hiki cha kukosa udhibiti wa elimu katika shule zetu hizi za sekondari na shule ya msingi ndiyo imepelekea vyeti feki. Leo hii ni takriban wafanyakazi 11,000 au 12,000 wana vyeti *fake*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri hili jambo lisipite hivi hivi, tuone umuhimu wa kufanya tathmini na kufanya *research* ndogo tatizo lipo wapi, ni *NACTE* au ni nani kakosea? Kwa sababu haya tunayozungumzia hapa tunazungumzia Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kat, tunazungumzia ajira, leo hii inaonekana Watanzania wengi wana yeti *fake*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri aone namna ambavyo itanyika *research* ndogo na taarifa ije Bungeni hapa tuone tumekosea wapi aidha ni *NACTE* au ni nani ametufikisha hapa tulipo. Pia naomba wale wote ambao wameshiriki katika kutufikisha hapa sheria ichukue nafasi yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni juu ya ujenzi wa vyuo vya *VETA*. Tunakwenda kwenye nchi ya viwanda. Sio wote ambao watapata fursa ya kwenda sekondari au kwenda katika vyuo. Vyuo vya *VETA* vitasaidia watoto wetu ambao hawajapata fursa waweze kusoma. Ukiangalia hapa maeneo mengi katika wilaya zetu hayana vyuo vya *VETA* mfano katika Jimbo langu la Kilindi toka 2010 tunazungumzia kujenga chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Kilindi. Mwaka wa fedha mwaka jana walisema kwamba Wilaya ya Kilindi itakuwa ni mionganoni mwa wilaya chache ambayo itajengewa chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha aniambie nini hatma ya Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Kilindi. Kwa sababu Halmashauri ya Wilaya Kilindi ilishatenga eneo kubwa sana takriban heka 20 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*. Tunahitaji Chuo cha *VETA* kwa sababu kitasaidia vijana wetu wa Wilaya ya Kilindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo suala la kidato cha tano ni muhimu sana. Sisi tunatoka maeneo ambayo miundombinu ni mibaya sana wapo vijana amba

wamefaulu lakini wameshindwa kwenda kidato cha tano katika maeneo mengine kwa sababu wazazi hawana uwezo lakini Wilaya ya Kilindi haina shule ya kidato cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule nyingi sana takriban tano ambazo zina sifa ya kuwa na kidato cha tano. Mfano shule ya Kikunde, Mafisa, Kilindi Asilia, hizi shule zina sifa, zina Walimu wazuri na miundombinu mizuri. Hivi tatizo liko wapi Mheshimiwa Waziri, kwa nini hatuna shule ya kidato cha tano? Nimwombe sana aone namna ambavyo na sisi tunaweza tukapata shule ya kidato cha tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni motisha kwa Walimu wetu. Nimepitia katika hotuba hii hapa ni kwamba wanatoa motisha kwa Walimu Wakuu lakini hawa Walimu wengine vipi? Kwa sababu motisha siyo pesa tu unaweza ukampeleka semina, ukawapeleka Walimu kusoma, hizo ni motisha. Tositengeneze *gap* ya Walimu, tuwape motisha Walimu wote na hii itasaidia pia kuinua kiwango cha elimu Tanzania hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka pengine Mheshimiwa Waziri aliangalie ni suala la uwiano wa upangaji wa Walimu, hapa pana tatizo kubwa sana. Kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya *performance auditor* aliyoifanya ni kwamba kuna mikoa Tanzania hii Mwalimu mmoja anafundisha darasa la watoto 26 lakini maeneo mengine mwalimu mmoja anafundisha watoto 46 maana yake ni nini? Maana yake maeneo yale ambayo Mwalimu mmoja anafundisha watoto 46 elimu haitakuwa nzuri na Walimu wengi sana wako mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kushirikiana na TAMISEMI pitieni tena kuona uwiano na upangaji wa Walimu ulivyokaa kwa sababu Walimu wengi wako mijini, vijiji kule hakuna Walimu. Kuna baadhi ya shule Walimu wanagawana *topic* ya somo moja labda la historia au sayansi, hili haliwezekani. Hebu tuone namna ya ku-*balance* uwiano wa Walimu Tanzania nzima ili maendeleo ya nchi hii yawe kila kona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo machache, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Keissy ulikuwa na dakika tano lakini ziko dakika tano zingine subiri. Nakuomba radhi kwa hilo, namwita Mheshimiwa Abdalla Haji Ali dakika tano, halafu utamalizia Mheshimiwa Keissy.

MHE. ABDALLA HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote kutujalia kama hivi alivyotujalia. Pia nakushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ndogo na mimi nichangie angalau machache katika mengi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa langu ni moja tu, napenda kuzungumzia kidogo suala la utafiti kwamba Taifa lolote duniani haliwezi kuendelea ikiwa halitatilia maanani suala zima la utafiti wa sayansi na teknolojia. Suala zima la utafiti wa sayansi na teknolojia ni lazima lipewe kipaumbele ndio maendeleo yapatikane katika nchi. Tanzania si kisiwa ni nchi kubwa, Tanzania ni nchi hai na ipo hatuvezi kuwa kinyume na teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania chombo kikubwa kinachodhibiti masuala ya utafiti ni Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Hiki ni chombo kinachodhibiti masuala ya utafiti na ndio chombo mama wa mambo yote ya utafiti yanayofanyika hapa Tanzania. Chombo hiki kazi yake kubwa kisheria ni kufanya utafiti katika nyanja za sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa yaliyoendelea tunaona kwamba wamekuwa wakitenga asilimia kubwa ya bajeti yao katika kuendeleza masuala ya utafiti. Hapa kwetu Tanzania tunaona kwamba Serikali inakuwa inaitengea sana Tume hii katika kufanya utafiti lakini tukiri kwamba pesa

zinazotengwa katika kufanya utafiti hazitoshi, ni kidogo. Hapa Waziri mwenye dhamana wewe ndio mwenye kilio, ulie na sisi wa kando tkuone tulie pamoja Serikali ikuongezee mapato juu ya suala zima la utafiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia takwimu za hizi karibuni za miaka iliyopita utaona viwango vilivyokuwa vikitolewa kwa ajili ya Tume hii. Mwaka 2010/2011 kilichotengwa ni shilingi bilioni 30, lakini kilichotolewa hakikuzidi shilingi bilioni 19. Aidha, mwaka 2011/2012 zilitengwa shilingi bilioni 25.7 lakini kilichotolewa kwa ajili ya masuala ya utafiti hakikuzidi shilingi bilioni 7.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 zilitengwa shilingi bilioni 21.4 zilitotolewa ni shilingi bilioni 12.8. Mwaka 2013/2014 zilitengwa shilingi bilioni 16 na hapa kwa bahati mbaya hakuna chochote kilichotolewa. Mwaka 2014/2015 zilitengwa shilingi bilioni 16.5 na zikatoka shilingi bilioni 3.8 na mwaka 2015/2016 zilitengwa shilingi bilioni 4.3 na hakujulikana kitu gani kilichotokeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naishauri Serikali, Taifa lolote linalotaka kuendelea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Keissy.

MHE. ABDALLA HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa nawapongeza Wizara ya Elimu hasa Profesa Ndalichako, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi wanayofanya. Namshukuru sana alinisaidia hata pesa kwa ajili ya *high school* yangu ya Kirando kwa ajili ya kujenga mabweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia mada moja tu kuruhusu watoto walioko shuleni kupewa mimba na kurudi kusoma. Ndugu zangu hapa Bungeni akinamama walio wengi wanaongoza mapambano mtoto asiolewe chini ya miaka 18. Leo kuna wasichana wanavunja ungo wana miaka 10 mpaka 12, wanawenza kupata mimba na mnaruhusu waende mashulenii. Mtoto ye yote anayefanya mapenzi na shule elimu yake inapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wanithibitishie baadhi ya akinamama hapa walikuwa wanafunzi na tuko nao hapa, kama walianza mapenzi mapema huko shuleni elimu yake ilikuwaje? Wakituthibitishia walianza mapenzi bado wako shuleni na elimu yake ilikuwa pale pale mimi nitawaunga mkono, watueleze. Mimi kama Muislam, dini yangu inaniambia kabisa nisikurubie zinaa. Sasa kama Muislam anasimama hapa ana-*support* mtoto wa shule aanze zinaa huyo siyo Muislam, amekiuka maadili yake ya dini moja kwa moja.

TAARIFA

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba aya ya Quraninasema, *walaa takrab zinaa inahu kana fahshatan wasaa sabilla*. Maana yake usiikaribie zinaa mpaka pale ambapo Mwenyezi Mungu atakuwezesha kuolewa au kuo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy hebu endelea.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kabisa, naunga mkono. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia ndugu zangu tusizalishe kundi la watoto wa mitaani. Watoto ambao watakuwa hawana walezi, watakuwa wazururaji hakuna atakayekubali mimba za watoto wa shule. Kwa hiyo, mnataka kuongeza watoto wa barabarani moja kwa moja, hatuwezi kukubali.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wengi mpaka sasa hivi tunajua siyo waaminifu, ndiyo watafungulia sasa, wataanza kuishi na watoto wetu mashuleni, hiyo hatutakubaliana. (*Makofi*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

TAARIFA

MWENYEKITI: Nampa nafasi moja Waziri Kivuli wengine tulieni. Mheshimiwa Lyimo.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nilitaka kumpa taarifa kwamba hatuzungumzii suala la mapenzi shuleni kwa sababu suala la mimba mtoto anaweza akapata mimba kwa kubakwa na wote tunajua kwamba shule ziko mbali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nataka kumpa taarifa kwamba mwaka 2008 nimezunguka nchi mzima kufuatilia *issue* hiyo na tulikubaliana na hicho anachokisema hata Mashekhe na Mapadri walikubali kwamba hili jambo ni la muhimu sana kwa sababu, naomba niseme tu kwamba kama hatutaruhusu hiyo hali ni kwamba ule mzunguko wa umaskini utakuwa unaendelea.

MWENYEKITI: Sasa umempa taarifa inatosha.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa kwamba suala la mimba halitokani na mapenzi suala la mimba ni *by choice* au *by chance*. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa endelea.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza taarifa yake naikataa na huyo Shekhe aliyekwambia siyo Shekhe ni shehena. Hakuna Shekhe atakuambia tukakurubie zinaa huyo siyo Shekhe ni mnafiki wa Mashekhe! Shekhe yejote hawesi kwenda kinyume na *Quran* huyo ni mnafiki wala siyo Muislam, nakwambia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusicheze na kuongeza watoto wa mitaani. Kwanza kuna UKIMWI, Sheria za Ndoa siku hizi kwa Mapadri na Mashekhe huolewi mpaka upimwe UKIMWI ndio ndoa inafungwa. Leo utashirikishaje watoto wafanye zinaa shuleni hawapimwi UKIMWI. Ndugu zangu tusikubaliane, mimi napinga hoja zenu, mmeekaa wanawake mnataka kutuendesha, mwisho mtaruhusu ndoa za jinsia moja au ndoa za kusagana hapa, acheni.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Nithibitishie wewe kama kweli ulianza mapenzi bado uko mwanafunzi.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, anapotosha.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nimeshapokea taarifa Waziri Kivuli wenu, inatosha, endelea Mheshimiwa Keissy.

MBUNGE FULANI: Anapotosha.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Tuelezeni kati yetu nani alianza mapenzi bado mwanafunzi? Nashaanga Mwalimu mmoja anasimama hapa...

MBUNGE GULANI: Unapotosha, unapotosha.

MWENYEKITI: Omba nafasi uchangie jioni.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Anasema turuhusu mimba, hao Walimu wa namna hiyo ndiyo siyo waaminifu. Inawezekana waliwapa watoto wetu mimba tuwachunguze, tuwachukulie hatua huko walikokuwa wanafundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana walikuwa wanaishi kimapenzi na wanafunzi. Ni makosa kabisa kuishi na mwanafunzi na makosa kabisa kutembea na mtoto chini ya miaka 18. Mtu aliyebacka kifungochake ni miaka 30, tuache sheria ichukue mkondo wake lakini hatuwezi kuruhusu sisi kuwaozesha watoto wako shulenii.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ndiyo hiyo, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofii)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Tunza Malapo dakika tano, watafuatia Mheshimiwa Grace Tendega dakika tano na Mheshimiwa Edwin Sanda.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano tutaanza na Mheshimiwa Tendega, ajiandae Mheshimiwa Tunza na Mheshimiwa Sannda.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba hii. Naomba niungane na wenzangu kwa kuwapa pole wafiwa wote wa watoto waliopata ajali Mkoani Arusha, Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na maneno ya wanazuoni ambayo yanasema ukitaka Taifa bora, boresha elimu; ukitaka kuboresha elimu boresha walimu na ukitaka Taifa la watu wanaojiheshimu, heshimu walimu. Ninazungumza hivi kwa sababu walimu wetu kwa kweli wamekuwa na kinyongo cha kufanya kazi yao, wengi wamekuwa na malalamiko mengi na wamekuwa hawapati haki zao. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu zamani walikuwa wakipata posho ya mazingira magumu ya kazi na hasa wale wa vijijini ili yawavutie, lakini sasa hivi hakuna posho hizo. Napenda kusema kwamba mimi pia ni mwalimu, wakati huo tukifundisha kulikuwa na posho, wale walimu wa sayansi walikuwa wana posho ya ziada ya walimu wengine wa

masomo ya *arts* na biashara, maslahi hayo yalikuwa yanatia moyo na mwalimu anafundisha kwa nguvu kubwa sana na wanafunzi walikuwa wakifaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile unaona kwamba kada hii ni kada inayofanyakazi kwa saa 24. Mwalimu anaandaa somo, mitihani na anasahihisha, mwalimu anapanga matokeo, muda wote wa siku mwalimu anafanya kazi hizi, lakini Serikali hii imekuwa haiwalipi posho ya kufundishia walimu ambayo ilikuwa ni kilio chao cha siku nyingi na walimu wamekuwa hawapati hizo posho. Tunaomba Serikali iangalie suala hili ili walimu wetu waweze kupata posho ya kujikimu na waweze kufanya kazi vizuri, hasa walimu wanaokaa kwenye mazingira magumu. Tumeona wengine wakifuata mishahara yao wanafunga shule kabisa. Mimi nina shule yenye walimu wawili kutoka mkoani kwangu, wakati wa kufuata mishahara mmoja anabaki, mwenzake anakaa na darasa la kwanza mpaka la saba. Kwa kweli, hii ni kazi kubwa kwa walimu, tuwatizame kwa jicho lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi hawapo, tunaomba Waziri alitizame suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa suala la vitabu. Vitabu ndiyo moyo wa mwalimu katika kufundisha, tuna mitaala, vitabu na vilevile tuna masuala mengine ambayo yapo katika ufundishaji. Mwalimu akikosa kitabu, akipata kitabu ambacho kinamwongoza mwanafunzi vibaya Taifa zima litakwenda kwenye fikra hizo na tutatengeneza Watanzania wenye fikra ambazo zimepotoshwa. Vitabu hivi kama tulivyokwisha kuviona na wenzetu wamevionesha hapa asubuhi vimekuwa na mapungufu mengi, hivi Serikali inataka tuende wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu, alikuwa kwenye Bodi ya Taasisi ya Elimu na amefanya kazi anajua jinsi ya kuandaa vitabu anafahamu kabisa. Baada ya kumaliza kazi hii inatakiwa watu wa

kuhakiki, kuna *panels* za masomo ambazo zinatakiwa zipitie. Kweli kama *panel* zile zilipitia na makosa haya yakatokea basi hawa waliofanya kazi hiyo wachukuliwe hatua, kwa sababu hii ni hasara kubwa kwa Taifa letu, Watanzania na watoto wetu wanakwenda kufundishwa vitu ambavyo vitawapoteza na vitawapotosha. Kwa sababu wanasesma unapopata elimu ya msingi bora ndiyo itakayokuongoza mpaka kwenye maendeleo ya baadae. Hivyo, ukimkosea mtoto hapa toka kwenye msingi kwa kweli utamfikisha mahali ambapo siyo panakotakiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala sasa la ufundishaji hasa kwa watoto wa kike na masuala ya mazingira ya watoto wa kike katika elimu. Tumeona kwamba kuna changamoto nyingi...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kuisha)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Tunza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka niwakumbushe kidogo hili suala la vitabu kuonekana vina makosa humu Bungeni siyo jambo geni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Susan Lyimo alisema hapa kwamba hivi vitabu vina makosa na Mheshimiwa Simbachawene alitoka kule kuja kuangalia na akajibu kwa mbwembwe na kejeli kwamba anachokisema Mheshimiwa Susan Lyimo siyo kweli. Sasa Mwenyezi Mungu kila siku yupo na wanadamu, nashukuru tu kwamba tumeona, kila mtu ameona ama amesikia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu, naomba uchukue hatua stahiki, tumepoteza pesa, lakini pia tumewapoteza watoto kwa maana wamepewa *knowledge* ambayo siyo sahihi. Wakati sijaingia Bungeni nilikuwa namsikia sana Mheshimiwa Mbatia anazungumzia mambo ya mtaala na vitabu vina mapungufu,

lakini tumechukua hatua gani naona kila siku hali inazidi kuwa mbaya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Elimu nafikiri una jukumu kubwa la kuangalia na inawezekana kwenye somo la Sayansi labda alipelekwa mwalimu wa historia maana hivyo vitu vipo, watu wanaangalia zaidi mshiko (kipato) kuliko kuangalia maslahi ya Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyuo vya Ualimu mwaka jana nillizungumzia na leo ninalizungumzia. Mradi wa *ICT implementation* katika *Teachers Education; serverzote* sasa hivi kwenye Vyuo vya Ualimu ambako mradi ule umepita hazifanyi kazi, lakini ukifungua kitabu cha hotuba ya Waziri anazungumza zaidi mfano, hata pale ukurasa wa 27 anazungumza suala la kuhakikisha TEHAMA inafundishwa, kuhakikisha walimu wanaandaliwa na TEHAMA na vitu kama hivyo. Nikuhakikishie tuma watu wako ama nenda mwenyewe kwenye Vyuo vya Ualimu vingi kama siyo vyote hakuna *computer* na kama zipo ni mbovu na pia *server* hazifanyi kazi na wala hawapewi *GB* wala kitu gani, tunategemea hiyo TEHAMA itaendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati tuna upungufu wa vyumba vya madarasa 158,674; lakini kwenye bajeti mwaka ujao wa fedha tumetenga kujenga vyumba vya madarasa 2000 tu kama pesa itapatikana. Kwa maana hiyo, kwa mahitaji haya 158,674 kila mwaka tukijenga vyumba vya madarasa 2000 maana yake tutatumia miaka 79 ili tuweze kukamilisha. Nafikiri inatakiwa kuwe na mkakati wa makusudi, madawati tunajua yalipatikana yaliyo mengi mengine yapo nje yanalowa mvua yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Waziri ili kusudi tuboreshe elimu yetu na watoto wetu wakae katika vyumba vya madarasa kunahitaji pia mkakati wa makusudi. Wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri naomba anijibu maswali yangu haya rahisi, tunaposema *quality education* Tanzania tunamaanisha nini? Pia napenda kujua falsafa yetu ya elimu sasa hivi ni nini? Bado ni ile elimu ya ujamaa na kujitegemea ama kuna kitu kingine? Kama ndivyo basi tujue mitaalaa

ambayo tunaitumia kweli inawafanya watoto wetu kwenda kwenye kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wakaguzi ama sasa hivi wanaitwa Wadhibiti Ubora. Mheshimiwa Waziri nikuombe kile kitengo kipo chini yako, Wizarani kwako, naomba ukipe kipaumbele kwa umuhimu wake, kwa sababu bila ukaguzi kwenye elimu ni sawa na hakuna. Maana yake hawa Wadhibiti Ubora wa elimu ndiyo *CAG* kwenye elimu, ndiyo wanaangalia kila kitu na kujua kuna matatizo gani. Inawezekana hata hili suala la vitabu leo tusingekuwa tunaliongelea hapa kama wangkuwa wanafanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Kwanza kabisa napenda kuipongeza Wizara chini ya majemedari wetu wawili hawa wana mama kwa kuwasilisha hotuba nzuri kabisa ya bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Lakini na mimi nitumie fursa hii fupi nichangie machache, kimsingi nataka nizungumze kwenye upande wa ufundi, leo nitajikita kwenye ufundi tu sitaongelea kitu kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mipango mizuri, utekelezaji ambao umefanywa huko nyuma lakini nataka nizungumzie ufundi kwa maana ya ufundi wa elimu na mafunzo kwa maana ya ufundi stadi na ufundi sanifu. Hapa tunazungumzia vyuo kama vile *DIT, Mbeya Technical, Arusha Technical* tunazungumzia pia *VETA* pamoja na *FDC* vile Vyuo vya Maendeleo. Huko nyuma tulikuwa navyo kwa maana halisi ya ufundi, lakini baadae tumekuja kutoka kila mmoja anataka awe meneja apate *degree*, avae tai kama

Mheshimiwa Sannda wakati tunahitaji mafundi wakae *site* tuweze kupata weledi na umahiri katika utekelezaji wetu wa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunajikuta tunaishia kwenye kazi zenyе ubora wa viwango vyа chini kwa sababu ya upungufu na ukosefu wa mafundi kule *site*, kila mmoja *manager* lakini *technicians* na *artisans* tatizo limekuwa ni kubwa sana. Ningependa sasa nimeona mipango na maelezo mengi ya huko nyuma na mipango kwa ajili ya 2017/2018, lakini ningependa Mheshimiwa Waziri unaporudi baadaye wakati wa kuhitimisha utueleze kidogo kuhusu sera na dhamira ya dhati ya kuhakikisha utekelezaji wa mipango hii na mikakati unakwenda kutekelezwa kwa maana ya kutenga bajeti nzuri ya utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya dhati itakuwepo tu pale ambapo tutawekeza kwenye vyuo hivi vyа ufundi, turudishe *polytechnics*. Sasa tuna Vyuo vingi Vikuu vinatoa *degree* mbalimbali katika fani mbalimbali, lakini pia hatuwezi kutoka moja kwa moja kila mmoja akawa meneja, tunataka tujenge kundi kubwa la mafundi ambao watakwenda kuwa weledi katika utekelezaji pia watajijengea stadi za maisha za kuweza kujajiri badala ya kila mmoja kusubiri kwenda kuajiriwa ofisini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona dhamira hii ya dhati kabisa katika uwekezaji kwenye hili. Tunahitaji tutenge bajeti yake lazima iakisi kwamba hapa tunataka kwenda kutekeleza hii mipango. Tutaongea mambo mazuri kweli kitabu chako kimeeleza vitu vizuri sana, lakini kwenye bajeti haipo hivyo katika nyanja hii. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri, Wizara kwa ujumla na timu yako yote, suala la fani na mafunzo ya ufundi sanifu na ufundi stadi siyo kitu tena cha kukisubiri au kukifikiria labda tutakifanya baadae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zama hizi tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda; uchumi wa viwanda bila hawa watu tutakuwa tuna-*import skills* nje sana. Tunahitaji watu

wetu a ndani ili waweze kwenda na kuiwezesha azma hii ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujikita kwenye uchumi wa viwanda. Jambo langu kubwa ninaloweza kusisitiza tutenge bajeti na tuwe na dhamira ya dhati kabisa ya kuweka bajeti ya kutosha kwa ajili ya elimu na mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo kama Chuo cha Ardhi kilikuwa chuo mahiri kabisa, watu wanavyokwenda kujifunza kule wanakwenda kujifunza muda mwangi ni mafunzo ya vitendo. Nadharia inakuwepo, lakini sehemu kubwa ya ufundishaji wao na mafunzo yao ni sehemu ya vitendo, kiasi kwamba wanapotoka pale shulenii ni watu ambao wameiva, wamepikwa wakapikika vizuri kabisa wanaweza kuwa tayari, wanasema wengine *you hit the ground running* ili uendelee na kupambana na maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapende tu kusisitiza kurudisha na kuweka *focus* kwenye vyuo kama Chuo cha Ardhi, *Mbeya Technical, Arusha Technical* na vingine vyaa namna hiyo. Pia huku nyuma tulikuwa na shule za ufundi, ukitoka *form four* unaenda kuanza shule za ufundi kama ilivyokuwa Ifunda. Kwa hiyo, unaanza kupikwa kutoka hapo, ukija kwenda kwenye *technical colleges* huko ni mtu ambaye tayari mzuri kweli kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunataniana tunasema wale *ma-engineer* waliokuwa wanakwenda *site* wanaajiriwa na makandarasi, waliotoka Chuo Kikuu wamesoma Uhandisi kabisa na wale waliotoka *DIT* ukiwaweka pamoja huyu wa Chuo Kikuu yeye ni mwepesi, mweupe kabisa. Tunataka watu watakaoenda kufanya kwa vitendo badala ya wengi kuwa na ndiyo tutakapoendeleza vizuri uchumi wetu wa viwanda na kujenga viwanda vingi na vikawa na wataalam wengi wa kuviwezesha vikastahimili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu kubwa kwa siku ya leo katika Wizara yako Mheshimiwa Waziri nilipenda sana niongelee suala la ufundi na sitazungumzia kitu kingine chochote. *VETA* pamoja na *FDC* najua ndiyo mmevichukua

sasa hivi Vyuo vya Maendeleo basi tuwekeze zaidi huko, tuhakikishe kwamba na kwenyewe tunakuhuisha ili tupunguze hii kelele ya kila mmoja akimaliza siku hizi vijana wana hitaji msaada sana wa kutafutiwa ajira basi kila mmoja anakutumia *CV*yake ukiona ni *degree*, waite kwenye usaili utaona kasheshe yake, uivaji haujaka a vizuri, lakini tungekuwa na watu ambaao ni wataalam anaweza akatoka ameshajifunza stadi za ufundi na stadi za maisha anaingia mwenyewe anajasiria viwanda. Anaanzisha kazi kelele na tazito kubwa tulilonalo la ajira litakuwa limepatiwa ufumbuzi mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mimi nafikiri ya kwangu ni hayo na nitakuwa nimetunza muda kweli. Ninakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mashimba hayupo, Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Mtolea ajiandae.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ni Mashimba au Kishimba? Mheshimiwa Kishimba yupo.

MWENYEKITI: Yupo?

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Kishimba yupo.

MWENYEKITI: Kama yupo basi aendelee kuchangia.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa shukrani nyingi kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika Wizara ya Elimu.

Kwanza napenda kutoa shukrani nyingi kwa Serikali kwa kutoa elimu ya bure kutoka darasa la kwanza mpaka la kumi na kbili. Mpango huu wa elimu bure umetusaidia sana kupunguza kero nyingi majimboni kwetu pia Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Tanzania kama haitafanyiwa mabadiliko makubwa itaendelea kuwa chanzo cha mateso, umaskini kwa wazazi, watoto na kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Wakati wakoloni walipoleta elimu zaidi ya miaka 100 iliyopita walikuwa na maana nzuri sana, leo baada ya mabadiliko makubwa ya dunia, uchumi na teknolojia kwa ujumla wake ni vigumu sana kuendelea na mfumo wetu wa elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano kwa nchi ya Uingereza; wanapomaliza wanafunzi mfano, milioni moja kutakuwa na *retirement* ya wafanyakazi karibu laki tisa au laki tisa na nusu ambaao ni asilimia 90 mpaka 95. Kwa hiyo, wale wanafunzi laki moja ambaao watakuwa hawana ajira watakuwa chini ya Serikali wanaweza kulipwa na kutafutiwa kazi polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu, wakimaliza wanafunzi milioni moja kutoka chuo na shule zote watakaopata kazi ni wanafunzi 50,000. Kwa maana hiyo ajira yetu ni asilimia tano peke yake ya wanafunzi. Kwa tofauti hii ya uwiano wa ajira kati ya waliotuletea mfumo huu wa elimu na waletewa, hata ikitokea miujiza hatuwezi kutengeneza ajira hata kwa asilimia 20. Ni jukumu la Wizara kuchukua mawazo ya Wabunge yanayoweza kufanyiwa maboresho ili kulitattua hili tatizo ambalo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaotoka Mikoa ya Kanda ya Ziwa tungeomba kutoka darasa la kwanza mpaka kidato cha nne kwa shule za kutwa tupewe elimu ya kawaida na tupewe elimu ya mazingira yetu. Kanda ya Ziwa tuna shughuli zetu za kawaida kama ufugaji, uvuvi, biashara, madini, tungeomba Wizara ya Elimu itupatie elimu hii kutoka darasa la kwanza ili mtu anapomaliza *form four* awe *ana-balance* ya elimu mbili. Kwa hiyo, ataamua mwenyewe aendelee kwenda kwenye ajira ya Serikalini au sehemu nyingine au arudi akajajiri kuliko mtindo wa sasa hivi baada ya mtu kumaliza *university* anarudishwa nyumbani. Akirudi nyumbani anakukuta wewe mzee umezeeka, huna kitu cha kufanya anakuja na karatasi inayoitwa *degree*. Tatizo

hili ni tatizo la Watanzania wote, kila mtu ni mwathirika wa hili tatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunamuomba Waziri ajaribu kuangalia upya muda wa kukaa shulenii. Kama hatuna ajira ingekuwa vizuri mtoto amalize *university* akiwa na miaka 15 au 17 ili awakute baba na mama yake *at least* wana nguvu kwa maana hakuna kazi ili waendelee pamoja akiwa bado mdogo ni rahisi kufanya naye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna tatizo la watu wa vyuo vikuu; vyuo vikuu vinaendesha nitaita kama aina ya utapeli mamboleo. Wanachukua pesa kwa wananchi, wanalaazimisha wananchi kukopa, wanachukua pesa, shilingi milioni 10 mpaka shilingi milioni 30, baada ya miaka mitatu wanakurudishia mtoto ana karatasi inaitwa *degree*. Wao ndiyo kwanda pekee kilichobaki duniani ambacho hakiwezi *ku-suffer, viwanda* vyote vinateseka sasa hivi lakini vyuo vikuu hakuna mahali vinateseka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaombwa Wizara ilete sheria hapa ili wanapotaka kusajili hao wanafunzi waeleze kazi walizonazo ili wao waende kwa waajiri waende wakatafute hiso kazi kabla hawajasajili wanafunzi. Waeleze mshahara ndiyo waseme sasa lipa kiasi hiki mtoto wako atakwenda kufanya kazi hapa. Hii itasaidia ndugu zetu maprofesa na wamiliki wa vyuo kulijua soko la ajira, itabidi wakakutane na waajiri. Kwa sasa hawakutani na waajiri, wao wanatayarisha wanafunzi wanaacha wazazi na wazee wote nyumbani wanakuwa maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usukumani tunakaribia kumaliza ng'ombe, tunalipia vyuo tunabaki na karatasi inayoitwa *degree*, lakini ukienda kwa mwajiri akiikataa ina maana hiyo *degree ni valueless* (haina thamani yoyote). Kwa hiyo, tungemuomba Waziri alete sheria hapa Bungeni ili vyuo vikuu viweze kubanwa na vyenyewe viende vikatafute ajira, badala ya mtindo wa sasa hivi wa vyuo kutumia nguvu ya Serikali na mawazo ya kusema elimu ni ufunguo wa maisha, matokeo yake sasa elimu ni kibano cha maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kidogo suala la *VETA*; humu ndani wote tuna magari, lakini sijasikia mtu ye yeyote anasema anapeleka gari yake *VETA*, wote tunauliza wapi ambapo kuna *garage* nzuri ya *Toyota* tunaambiwa ipo Mwembeni, tukifika pale Mwembeni hatuulizi cheti chochote, ningemuomba Waziri awafikirie sana watu wa *garage* maana yake ndio wanaofanya kazi kubwa kwa sasa hivi. Kama wao anaweza kuwa-*indicate* kama *VETA* ili wanafunzi wetu wakaenda kwenye *garage* za Miembeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri ni kwamba *garage* hizo hazina masharti yoyote ya kusoma, unaweza kusoma miezi sita kama umeshaelewa unaweza kuendelea na shughuli zako. Tofauti na sasa hivi unapeleka mtoto *VETA* kujifunza kupaka rangi miaka mitatu, fundi bomba miaka mitatu akirudi anakuta teknolojia ya bomba imeshamalizika inakuwa hakuna chochote. Hawa wakiona ametoka *VETA* wote huku mtaani hawamtaki, wanasema huyu ni *soft*, lakini anayetoka kwenye *garage* anapokelewa vizuri sana maana yake ni *practical*. Tunaweza kuapeleka kwenye maeneo ya sofa, maeneo mengi sana ambayo yapo sasa hivi, yanatosha kabisa kuweza kusaidia *VETA* badala ya mtindo wa sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, namuomba Waziri, pamoja na yote hayo, anisaidie kwenye Jimbo langu la Kahama shule Nne za sekondari ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu kuwa *High School*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo kwa leo, nashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Mtola ajiandae.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4, mwezi wa Tano, mwaka huu, 2017, nilisimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu, nikitoa pole kwa familia ya ndugu Chanjale aliyepigwa risasi kule Ikwiriri Kata ya Umwe, na leo nimesimama kwenye Bunge hili Tukufu nikitoa

pole kwa familia ya mmoja wa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM aliyepigwa risasi zaidi ya nane jana, Ndugu Alife Mtulia ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi kutoka Rufiji pia ni mkazi wa Jimbo la Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio haya yanayoendelea katika eneo letu la Pwani yanadhamiria kutukwamisha kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo nami nataka niendelee kuwasihii wananchi wa Rufiji, Mkuranga na wakazi wa Kibiti kuendelea kuchapa kazi na kuendelea kuwa na imani na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Hapa nataka niwakumbushe tu kwamba hakika Mwenyezi Mungu amekadiria maisha ya kila mwanadamu, na tunaamini kabisa kwamba mwanadamu anapozaliwa miezi mitatu tu akiwa tumboni mwa mama yake tayari Mwenyezi Mungu anakuwa ameshamuandikia mambo yake yote katika dunia. Qurani inasema *Kulla maagh yuswibana inna maagh katana llaahu lanah ikimaanisha kwamba hakika* Mwenyezi Mungu ameshamkadiria mambo yake kila mwanadamu aliyezaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwanza kabisa wananchi wa Rufiji tunatambua sana umuhimu wa elimu na umuhimu wa elimu hii kwa sisi wenyewe imani ya kiislamu tunatambua kwamba *wahyi*/wa kwanza kabisa Mtume wetu Muhammad kuupokea ilikuwa inahusu elimu. Katika Sura ile ya *Iqra* ambayo Mtume wetu alikabidhiwa na akiambiwa asome, niseme mbele ya Bunge lako hili Tukufu kwamba umuhimu wa elimu umesikilizwa katika kila sehemu na wananchi wa Rufiji wamepata bahati kubwa ya kupata Mbunge ambaye ni msomi na ana uwezo wa kusaidia kuwapambania katika jambo hili la elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza sana Serikali, nimpongeze sana Waziri wa Elimu. Kwanza kabisa Waziri wa Elimu alivunja historia na rekodi kwa kufika Rufiji kwa mwaliko wa Mbunge, alifika Rufiji akajionea hali ya miundombinu ya shule zetu za Rufiji, wananchi wa Rufiji wamenituma nikuambie wanakupongeza sana na uchape

kazi sana. Wako nyuma yako, lakini kwa namna ya kipekee kabisa wanakushukuru sana kwa kutoa shilingi milioni 259 kwa ajili ya ukarabati wa shule ya sekondari ya Utete. Wananchi wa Rufiji pia wanakupongeza Mheshimiwa Waziri kwa kukubali ombi la Mbunge la kutoa kibali cha shule ya sekondari Umwe ambacho kilikaa kwa zaidi ya miaka kumi kutosajiliwa. Wananchi wote wa Ikwiriri wanakupongeza sana na wanakukubali kweli, tunakuombea afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamenituma, wameniambia kwamba walikupa maombi ya kukarabati shule yetu ya sekondari ya Muhoro pamoja na shule ya sekondari ya Ikwiriri. Hali ya miundombinu ya shule zetu umejionea Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sasa utusaidie. Kwa sababu katika Mkoa wa Pwani, Rufiji umeweza kutupatia shilingi milioni 259 tu, tunakupongeza. Wananchi wa Kibiti pia kupitia kwa Mbunge wao, Mheshimiwa Ally Seif Ungando, wameniambia pia nikuambie wanakupongeza sana kwa kutoa kiasi cha shilingi 1,700,000,000 kwa kukarabati shule ya sekondari Kibiti, wanaomba pia uwasaide kukarabati shule ya sekondari Zimbwini, shule ya sekondari Bungu, shule ya sekondari Mlanzi pamoja na shule ya sekondari Nyamisati ambayo umetoa shilingi milioni 260 pamoja na shukrani kwa kutoa shilingi milioni 253 kwa kukarabati shule ya sekondari Mtanga kule Delta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Rufiji umetoa kwa shule moja, nikuombe sasa utusaidie wananchi wa Rufiji, wapo wengi hapa wanaomba wapatiwe viatu kwa kuwa wana miguu, binafsi miguu sina.

Kwa hiyo, nikuombe lile tamko lililowahi kutolewa na Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Kwanza la miaka ya 1970 la kuboresha elimu katika maeneo ya watu ambao walikuwa hawajasoma sana, leo hii tumejionea Maprofesa hapa kama Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, ni miongoni mwa watu waliosoma wakati ule ambapo waliweza kusaidiwa na Mwalimu Nyerere na wakapata elimu kwa kuwa maeneo yao hayakuwa na mwamko wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuomba watu wa Rufiji sasa utusaidie, utuletee mwamko wa elimu kwa kuboresha miundombinu ya shule zetu na wananchi wanaamini kabisa kwamba maombi yao haya utayachukua, utayapokea na kuyafanya kazi. Pia kwa namna ya kipekee wanaomba utusaidie kwa kupitia Mfuko wa Elimu utuboreshee shule yetu ya msingi Umwe, shule ya msingi Mgomba, shule ya msingi Muhoro, shule ya msingi Ngarambe, na ninamuomba Waziri wa TAMISEMI pia alichukue hilo na aone umuhimu wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaboresha suala zima la elimu katika maeneo yetu ya Mkoa wa Pwani, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa namna ya kipekee kabisa, tuwaangalie wananchi wa Pwani; kama ambavyo alifanya Mwalimu Nyerere, haitakuwa dhambi kufanya ili kuwapa manufaa wananchi wa Mkoa wa Pwani ambaao kwa kweli wameathirika kwa hali na mali kutokana na tatizo la kukosa elimu. Nikuombe wakati Mheshimiwa Waziri unahitimisha hapa utusaidie suala zima la mikopo, Bodi ya Mikopo iweze kuwaangalia wananchi wa Rufiji, watu wa Mkuranga, watu wa Kibiti na watu wa Kisarawe ambaao wamekosa elimu, wakati wa mgao huu wa Bodi ya Mikopo basi waweze kufikiriwa kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rufiji wamenituma, wameniambia kwamba wanacho Chuo cha Maendeleo pale Ikwiriri (*FDC*), ulifika mwenyewe ukajionea, wanaomba chuo kile sasa kiwe ni Chuo cha *VETA* kwa sababu kutoka Rufiji kwenda Kibaha kufuata elimu hii ya *VETA* ni mbali sana kwa zaidi ya saa sita. Wanaomba sasa Chuo hiki cha *FDC* uje utuambie mtakiboresha ili kiwe ni Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mnaboresha elimu kwa watoto wetu, tunaomba muangalie, yapo maeneo Rufiji ambapo hakuna shule, ni umbali mrefu, kwa mfano kule Mtanange kijijini kwangu wapo watoto zaidi ya 500 ambaao hawasomi kabisa, lakini yapo maeneo Kata ya Mgomba kule Mupi, wapo watoto wengi ambaao hawasomi kabisa. Tukuombe Mheshimiwa Waziri tuletee wataalam wako

waweze kuangalia ni namna gani wataboresha elimu. Ninaamini kabisa iwapo tutaboresha elimu tatizo hili ambalo linaendelea leo hii halitakuwepo tena kwa sababu tutakuwa na wasomi wengi eneo letu la Rufiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, zipo shule ambazo tunahitaji kukarabati, tunakuomba kupertia Mfuko wa Elimu utusaidie. Kwa mfano, ipo shule ya msingi Mchengerwa iliyopo kule Mianganaya ambayo nimeanza ujenzi wa darasa moja lakini pia tunayo shule ya msingi Kilindi ambayo imetoa madaktari wengi lakini shule hii ni shule ya miti tu na watoto wetu wanapata taabu sana inaponyesha mvua na wakati mwininge jua linapokuwa kali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wakizungumzia suala zima la kuwaruhusu watoto wetu waliopata ujauzito kuendelea na masomo. Mimi ninaomba niwakumbushe sana Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili iwapo wataendelea kulisogeza mbele sana wakumbuke wanavunja Ibara ya Tano ya Katiba kwa kutaka kuwaruhusu watoto wetu kushiriki kwenye shughuli za ngono.

Mimi ni muislamu, nilisema hapa, nitashangaa sana kuona Wabunge waislamu wakishabikia suala hili na kutaka watoto wetu washiriki kwenye shughuli za ngono. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Qurani inatuambia nilisema hapa, nataka nirudie inasema kwamba *wallah takrabu zinah inah kanah taishatan wasahalan sabilah*. Waislamu tumezuiwa kabisa, na jambo hili iwapo tutaendelea kuwasaidia watoto ambao wamepata ujauzito waendelee na masomo ni sawana kwenda kuongeza mafuta katika moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe, wakati ule ambapo... (*Makof*)

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: ...Wazungu wanaondoa biashara ya utumwa, miaka ile ya 1800...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: ...nataka niwakumbushe, wakati Wazungu wanaondoa biashara ya utumwa miaka ile ya 1800...

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

T A A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa. Mheshimiwa Mchengerwa, subiri taarifa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba hiyo hoja ya wanafunzi kuolewa warudi shulenii siyo suala la uislamu wala Ukristo ni hoja ya mtu binafsi, ni mawazo yake na mtazamo wake. Kwa hiyo, naomba tu kwamba hili asije akatugawa kidini humu ndani, kuna wakristo na waislamu na wengine hawana dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa tu mchangiaji, awe makini sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa aliyoitao ni sahihi, suala hili syo la udini lakini nataka niseme tu kwamba suala hili ni muhimu sana kwa Watanzania wakalitambua...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: ... ni vema Watanzania sasa wakalea watoto wao kwa misingi ya elimu

ya dunia na elimu ya ahera, ndio maana nikasisitiza hapa kwamba kuliweka jambo hili ni kusisitiza na kuwataka watoto wetu washiriki katika mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 Februari, 1835, Lord Maclay, mmoja wa Wabunge mashuhuri kule Uingereza aliwahi kusema kwamba Afrika hatuwezi kuitawala mpaka pale ambapo tutaweza kudhibiti elimu yao na kuhakikisha kwamba wanafanya mambo kutokana na tunayotaka kuyafanya. Ninaamini, nimeona Wazungu wakiwepo katika Bunge lako hili Tukufu na ninaamini... (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: ...ninaamini suala hili wapo watu wana-engineer ambao wanalitaka jambo hili. Mheshimiwa Lord Maclay alisema maneno haya, naomba niwanukuu kwa kiingereza:

"I have travelled across the length and breadth of Africa and I have not seen one person who is a beggar, who is a thief such wealth I have seen in this country, such high moral values, people of such caliber, that I do not think we would ever conquer this country, unless we break the very backbone of this nation, which is her spiritual and cultural heritage and therefore, I propose that we replace her old and ancient education system, her culture, for if the Africans think that all that is foreign and English is good and greater than their own, they will lose their self esteem, their native culture and they will become what we want them, a truly dominated nation"

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya siyo ya kwangu ni maneno yaliyowahi kutolewa tarehe 2 Februari, 1835. Ninaomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge iwapo wanasisitiza jambo hili wakumbuke Bunge liliopita tulifanya marekebisho ya sheria hapa, Sheria Na. 253. Kwa mujibu wa marekebisho haya ya Sheria Na. 353, kifungu cha 61 ambacho kilitoa mamlaka kwa Serikali kuhakikisha kwamba watoto wote wanaoshiriki katika masuala ya

uasherati pamoja na ngono wadhibitiwe. Kuliruhusu jambo hili ina maana kwamba tunakinzana na kifungu hiki cha Sheria Na. 61 ambayo Bunge hili lilitunga kifungu hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa wa Sheria ya Elimu, kifungu cha 60(b) ambacho kimetoa mamlaka...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtolea, dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Aisharose.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona dakika hizi za lala salama nami niweze kuchangia mawili matatu katika Wizara hii inayoshughulika na mambo ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotokea mjadala hapa wa kuitaka Serikali ibadilishe Sheria ya Ndoa ili ukomo au mwanzo wa umri wa kuolewa uwe kuanzia miaka 18 na kwenda juu kuna kundi huwa linapinga sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kundi hilo linalopinga kupandisha ukomo wa kuolewa watoto wa kike ndiyo hilo linapinga watoto wanaopata ujauzito kurudishwa tena shulen. Tafsiri tunayoipata hapa ni kwamba kumbe wabakaji na wanaotutilia mimba watoto wetu inawezekana wengine wapo humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge kama wazazi, mtu kuanza kupinga kumpa fursa mtoto wa kike ambaye pengine alifanya kosa kupata mimba au ilitokea bahati mbaya amebakwa, unasimama mapovu yanakutoka hapa eti hutaki mtoto huyu kurudi tena shulen ni jambo la aibu sana. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

TAARIFA

MWENYEKITI: Taarifa, subiri Mheshimiwa Mtalea.

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba katika Bunge lililopita tulipitisha Sheria Na. 353, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria tulitoa maelekezo kwa Serikali wakati wanaandaa Kanuni kuwaangalia watoto ambao wanapata ujauzito kwa kubakwa au kwa kufanyiwa masuala mengine yoyote waweze kusaidiwa na Serikali. Kwa hiyo, Bunge hili lilipitisha sheria kwa marekebisho tuliofiga kura wengi hapa Wabunge.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ahsante, ameshakuelewa. Mheshimiwa Halima vipi?

MHE. HALIMA J. MDEE: Nataka kumpa taarifa naona anatumia Uenyekiti wake kupotosha hapa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hapotoshi ninyi mlipata mimba wakati mpo shulenii?

MWENYEKITI: Sema Mheshimiwa Halima Mdee unataka kusemajje halafu ukae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hapa tunazungumzia watoto wa kike ambao ama walibakwa kwa sababu ni watoto wadogo ama walirubuniwa kwa sababu ni watoto wadogo, ama walilazimishwa ndoa za utotoni kwa sababu Sheria yetu ya Ndoa inaruhusu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante umeshaelewaka, Mheshimiwa Mtalea endelea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwiskeyki, kwanza hiyo taarifa ya Mchengerwa siipokei kabisa.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza unaposema Bunge lililopita maana yake una-refer Bunge la Kumi, Bunge la Kumi Mheshimiwa Mchengerwa hakuwa Mwenyekiti na wala hakuwa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya maisha tunayoishi hatushindani kutokufanya makosa, tunashindana kwa namna gani unajifunza kutokana na makosa ambayo umeyafanya. Hivi ni nani amefanya kosa la makusudi kati ya aliyebakwa akapata au kijana anayejifunza kuvuta dawa za kulevyia? Serikali hii juzi tumepitisha hapa bajeti ya Wizara ya Afya, Serikali inatenga pesa kwa ajili ya vituo vya *methadone*, inatumia mamilioni ya fedha kwa ajili ya kuwapa fursa vijana ambao wametumia dawa za kulevyia sasa wanatafuta nafasi ya kujifunza kutokana na makosa yao, wanatafuta nafasi ya kujirekebisha ili wawe raia wema. Ndiyo kazi ya Serikali kuwajengea miundombinu wananchi ili wawewe kuwa wananchi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtoto aliyepata mimba ama kwa kubakwa au kwa kurubuniwa unamnyimaje fursa ya kurudi shulen? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti...

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimalize maneno kwa sababu tu mtoto wako anasoma shule nzuri.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Taarifa.

MWENYEKITI: Hapana Mheshimiwa Mchengerwa kaa

chini. Waheshimiwa Wabunge wote wakae abaki Mheshimiwa Mtalea peke yake. Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Halima kaa chini.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwe wageni wa nchi hii, Waziri wa Elimu anafahamu, moja ya changamoto kubwa za elimu katika nchi hii ni kwamba hizo shule ziko mbali na watoto wetu wanakoishi. Watoto wanatembea umbali mrefu kuzifuata shule, hakuna *hostel* za kutosha kwamba hawa watoto wakae *hostel* wasome huko mpaka wamalize shule zao. Mtoto anapewa *lift* ya bodaboda mwaka mzima, hivi mtoto huyu kweli ana ujasiri gani atakataa kutongozwa na dereva wa bodaboda anayempa *lift* kwa mwaka mzima? Wewe mtu mzima pamoja na Ubunge wako hapa ukipewa *lift* mfululizo siku 30 tu lazima mtakuwa bwana na bibi. Leo mtoto mdogo, watoto hawa wadogo wanarubuniwa, wanapata mimba, tunashindwa kweli kuwa na huruma kweli? (*Makofii*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Waheshimiwa sipoeki taarifa yoyote sasa, Mheshimiwa Mtalea maliza.

MBUNGE FULANI: Kaa chini.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukru sana na ukijiona unanyeshewa wewe ingia ndani, ujue upo nje, ndio maana manyunu yanakukuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ambayo watoto wetu wanakwenda shulenii siyo rafiki kiasi hicho, kwamba unaweza ukadhibiti wasipate mimba. Wakati Serikali inaendelea na jitihada zingine za kuhakikisha watoto watakuwa wanapata *hostel*, shule zitakuwa karibu na makazi yao, pia tuwape fursa wale ambaa tayari wameshapatwa na matatizo. Inatugharimu kiasi gani... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Aisharose, lakini atasubiri tutakwenda kwa Mheshimiwa Bilago, Mheshimiwa Aisharose na Mheshimiwa Fatma Toufiq atafuatia.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bilago una dakika tano.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama huna utafiti huruhusiwi kuongea jambo ambalo hujafanya utafiti. Hapa ndani kuna Wabunge walitembea nchi mbalimbali, kuna Wabunge walitembea nchi hii kufanya utafiti wa jinsi watoto wetu wanaobeba mimba mashuleni watarudi kusoma. (*Makofii*)

Sasa watu wanaposimama hapa na kueleza watoto wanaobeba mimba wasirudi mashuleni tunashindwa kuwashangaa, halafu watu hao ndiyo wanaosimama na kusema tunataka *fifty fifty*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapata wapi *fifty fifty* wakati ndani ya *fifty* moja kuna watu walibeba mimba na hawakuruhusiwa kuendelea kusoma? Unataka hiyo *fifty* uipate wapi wakati wanaobeba mimba ndiyo *fifty* yako halafu hawarudi shulenii. Kila mtoto ana haki ya kupata elimu, anayebeba mimba utotonii isiwe ni laana, mimba ya utotonii siyo laana na kama mnadhani ni laana wamo Wabunge humu walibeba mimba za utotonii na leo ni Wabunge, (*Makofii*)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Wataje, wataje.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti,

Waziri wa Elimu, leta *re-entry policy* juu ya hili tuendelee. Nchi za jirani wamefanikiwa Zambia wanakwenda vizuri na wale watoto tumewauliza, ukiwaliza wale watoto wanasema kabla ya hii *re-entry policy issue* ya mimba ilikuwa kubwa baada ya *re-entry policy* mimba zimeshuka mashulenii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo nilitaka nizungumzie ni makato kwenye mishahara ya walimu bila ridhaa yao. Walimu wanakatwa mishahara yao bila ridhaa.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mchengerwa kaa chini. Mheshimiwa Bilago kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, humu ndani hakuna mijadala ya dini na tunatakiwa tuvumiliane, kila mtu awe na imani yake. Tukianza kila imani isimame huyu a-quote hiki, huyu a-quote hiki hatutavuka. Kwa hiyo, nawaomba, naelewa hisia za watu, naelewa kila mtu ana imani yake na katika majukumu manne ya Wabunge la mwisho ni dhamira binafsi ya kila Mbunge kukubali au kukataa yale yanayoletwa hapa, lakini haimaanishi tuanze mvutano. Ninaomba kila Mbunge ana fursa, ni huru ya kuchangia na imani yake na mawazo yake tuvumiliane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Bilago endelea.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe. Nilikuwa nazungumzia makato yanayotokea kwenye mishahara ya walimu bila ridhaa yao. Miongoni mwa makato hayo ni pamoja na makato ya Mwenge, pamoja na makato ya bima za maisha, kuna kitu kinaitwa *National Insurance Corporation*, wanakwenda mashulenii wanachukua *cheque number* za walimu zilizobandikwa ubaoni kwenye mbao za matangazo wanakwenda kuingiza makato bila ridhaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko ni walimu zaidi ya 14 wanakatwa hizo fedha tena hazionekani kwenye *salary slip* wala haziko kwa mwajiri wao, mshahara ukilingia anaona *message* imeingia makato yamefanyika shilingi 56 zimetoka kwenye mshahara wako, akienda kuchukua *bank statement* anakuta makato yameenda *N/C*, akiwasiliana na watu wa *N/C* wanamwambia hatuna habari hiyo, akimuuliza mwajiri hana habari, sasa hili hatuwezi kulivumilia mtu anakatwa makato ambayo hayana ridhaa yake, huu ni wizi lazima ifike mahali haya makato yasimame walimu wafaidi, wanufaikie na mshahara wao. Kama vile haitoshi, mwalimu akiwahi kuchukua ule mshahara, mwezi huo *N/C* hawakati wanashindana wanagombania mshahara nani aanze kuutumia.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu mlisimamie hili na Shirika la Bima za Maisha waache huu ujambazi wa kukata mishahara ya walimu bila ridhaa yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu mashulen; tunaomba Mheshimiwa Waziri Elimu na TAMISEMI mshughulikie suala la miundombinu mashulen. Miundombinu ni pamoja na uhaba wa walimu, tunao uhaba mkubwa sana wa walimu. Hili tunalojidanganya kwamba walimu wamezidi, walimu ni wengi siyo kweli. Tuende tukawahesabu *physically* mashulen, idadi ya walimu ni ndogo kabisa ukilinganisha na *enrolment* ya wanafunzi iliyofanyika, hawa walimu hawatatisha mpaka maisha, tukubali walimu waajiriwe wa nchi hii ili wafundishe kizazi chetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda kukimbia lakini hili mnisaidie Wabunge tulijadili kwa pamoja, mimi naangalia hili suala la vyeti *fake*. Suala la vyeti *fake* linatupeleka kugumu zaidi. Najiuliza kama mwalimu amepatikana na cheti feki, je, aliyefundishwa na mwalimu huyo naye siyo *fake*? Hana elimu *fake*? Kwa sababu tusi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Aisharose, ajiandae Fatma Toufiq.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kipekee nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Naunga mkono hoja na nimpongeze sana Mheshimiwa Ndalichako na Naibu wake Mheshimiwa Injinia Manyanya pamoja na timu nzima kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuleta mageuzi katika sekta ya elimu. Bila elimu bora hakuna Taifa bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua elimu ndiyo uti wa mgongo kwa Taifa lolote lile. Nikimnukuu Marehemu Nelson Mandela aliwahi kusema; "*Education is the most powerful weapon you can use to change the world*" akimaanisha elimu ndiyo silaha kubwa inayoweza kuibadilisha dunia. Kama kweli tunataka kuibadilisha dunia ya Tanzania ni vema sasa tukawekeza zaidi katika elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mimba za utotoni. Suala hili limekwamisha jitihada za watoto wa kike kufikia malengo yao. Mkoa wa Singida ni mionganini mwa mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni. Kwa mwaka 2015 kulikuwa na mimba za utotoni 11,513 ambazo zilikuwa chini ya umri wa miaka 20. Mionganini mwa waliobeba mimba hizi walikuwa ni wanafunzi walioacha shule na wale walioolewa, idadi hii ni kubwa sana na inasikitisha, ni lazima tutafute suluhu ya jambo hili ili wanafunzi wa kike waweze kusoma vizuri na kuweza kufikia ndoto zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali kuja na mkakati au programu au kampeni katika shule zetu ambayo itamsaidia mtoto wa kike kuweza kujitambua, kujiamini, kujithamini utu wake, kuwa na *vision* na kuweza kufikia malengo. Tunataka mtoto wa kike wa Tanzania hii aweze kujitambua, aweze kujua anataka kwenda wapi na atafikaje huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukajenga *hostel* nydingi zenyé uzio mrefu, lakini bila ya kumtengeneza mtoto wa kike, kumjenga kisaikolojia, kumpa elimu ya kutosha kuweza kujitambua itakuwa ni kazi bure na mimba za utotoni zitaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali iliendesha zoezi la uhakiki wa vyeti vyá taaluma kwa watumishi wa umma. Naipongeza Serikali kwa hatua hii kwani itasaidia kupata watumishi wenye sifa zinazostahili, lakini mionganí mwa watumishi waliokumbwa na kadhiya hii ni walimu. Ningependa kufahamu ni walimu wangapi wa shule za msingi na sekondari walioathirika na zoezi hili la uhakiki wa vyeti na je, Serikali imechukua hatua gani za kuweza kuziba nafasi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ukiangalia shule nydingi nchini zikiwemo za Mkoa wa Singida zina uhaba mkubwa wa watumishi walimu. Kwa Wilaya ya Ikungi tu kuna upungufu wa walimu 348 hao ni walimu wa sayansi na sanaa na kwa Wilaya ya Singida Vijijini katika shule za msingi kuna uhaba wa walimu 754, idadi hii ni kubwa sana ukijumlisha na wale waliotumbuliwa katika zoezi la uhakiki wa vyeti hili hii inakuwa siyo nzuri. Naiomba Serikali yangu iangalie jambo hili kwa ukaribu na ipeleke walimu wa kutosha hasa katika Mkoa wa Singida. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu ndiye mdau mkubwa katika elimu, tukiweza kumtengeneza kisaikolojia na kimaslahi tunaweza tukamuwezesha mwalimu huyu kufikia malengo yake. Kila siku hapa tutakuwa tunaimba elimu yetu imeshuka viwango, ifike wakati sasa walimu wapewe stahiki zao, walimu wawezeshwe kuwa na mazingira bora ya kufundishia kwa maana ya kuwa na nyumba bora za makazi, maslahi bora, miundombinu bora ya kufundishia hapo tutakuwa tumemwezesha mwalimu kuweza kumfundisha mtoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni maabara, Watanzania walio wengi wamejitlea kwa hali na mali

kuhakikisha shule zetu zinapata maabara, maabara nyingi hazina vifaa na hazina miundombinu inayoridhisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali yangu kwa kusambaza vifaa vya maabara mashulenii lakini nielezee masikitiko yangu katika Mkoa wa Singida ni shule 18 tu ndio zilizopata mgao wa vifaa vya maabara. Idadi hii ni ndogo sana ukilinganisha na mikoa mingine na kama tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda tutafikaje huko bila ya kuwa na wataalam wa kutosha ambaa watakuwa wameandaliiwa vizuri katika maabara zetu? Nakuomba sana Mheshimiwa Ndalichako najua wewe ni msikiku, uuangalie kwa kipekee Mkoa wa Singida kwa kupeleka vifaa vya maabara vya kutosha pia vitabu vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Idara ya Ukaguzi. Serikali imekuwa ikitumia rasilimali nyingi kuboresha elimu hasa katika shule za sekondari. Nadhani ifike wakati sasa tuwekeze nguvu kubwa katika idara zetu za ukaguzi vinginevyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. Ni lazima ukaguzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu upewe msukumo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta sera ya elimu bure, sambamba na hilo naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Elimu kwa bajeti hii ambayo imeletwa mbele yetu ambayo leo hii tunaizungumzia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina baadhi ya masuala ambayo ningependa kuyachangia na iwapo kama muda utaniruhusu basi nitaendelea zaidi, lakini katika mambo ambayo ningependa kuyachangia ni pamoja na udhibiti wa elimu, suala la upatikanaji wa vitabu shulenii ambalo wengi wetu wamegelizungumzia, sambamba na hilo ni uanzishwaji wa bodi ya kitaalam ya walimu, suala la programu ya lipa kulingana na matokeo pamoja na elimu ya kujitambua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 85 amezungumzia kuhusu kuboresha mazingira ya elimu kwa wadhibiti ubora wa elimu. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuamua kwamba watajenga ofisi 50 kwa ajili ya udhibiti wa elimu. Pamoja na pongezi hizo bado kuna changamoto nyingi sana na naaminii kabisa Mheshimiwa Waziri analitambua hilo hasa kwenye ofisi zetu za udhibiti wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi natokea Mkoa wa Dodoma, tuchukulie ofisi yetu ya Udhibiti wa Elimu Kanda ya Kati. Kwa kweli baadhi ya vifaa hakuna, suala zima la samani, vitendea kazi na kadhalika. Hali kadhalika magari hayatoshelezi, sasa hapa tunazungumzia kuhusu kuboresha elimu, bila kuwa na vifaa vya kutosha je, tutafikia hili lengo kweli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niishauri Wizara hebu haya ambayo tunayazungumza hapa wayafanyie kazi, pamoja na kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba watanunua kompyuta 100, lakini sambamba na hilo kwamba kuna baadhi ya Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa, mimi naona idadi hii bado ni kidogo ni budi Wizara ikaongeza vifaa vingi zaidi kwa ajili ya utendea kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba ofisi nyingi za Udhibiti wa Elimu ni za kupangisha, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwa sababu kwanza ya ucheleweshaji wa *OC*, wale watendaji wanaokaa katika

ofisi hizi kwa kweli wamekuwa wakipata taabu sana na karaha kwa sababu *OC* imekuwa ikichelewa pengine miezi sita mpaka miaka miwili, kwa hiyo hii kwa kweli inawalectea karaha sana. Ninaishauri Wizara ni vizuri sasa ikaweka mkakati wa uhakika wa kupeleka *OC* kwa muda unaotakiwa ili kusudi watu hawa wasipate karaha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna hili suala la elimu bure ambapo kwenye sera ya elimu bure inatakiwa kwamba kila mwanafunzi wa sekondari katika ile *capitation fee* inatakiwa shilingi 1,000 ipelekwe kwenye Idara ya Ukaguzi au Udhibiti wa Shule. Kwa masikitiko makubwa naomba niseme kwamba pesa hizi mara nyingine huwa hazifiki na hivyo kuchelewesha kabisa utendaji wa udhibiti elimu. Ninatoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri kwamba pesa hizi zimekuwa zikikatwa, lakini zikikatwa zimekuwa zikipelekwa katika akaunti ya Wizara na baadaye ndiyo zinakuja kupelekwa kwenye akaunti za Kanda. Hebu waone ili kupunguza urasimu ni vizuri kwamba pesa hizi zikikatwa zipelekwe moja kwa moja kwenye Ofisi za Kanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la upatikanaji vitabu pia na udhaifu. Wenzangu wengi sana wamelzungumzia na hapa nina kitabu cha *Steps in Primary Mathematics Book Four for Tanzania*. Kitabu hiki kimetungwa na Mtunzi ambaye anaitwa Kireri K.K.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu kina maajabu sana, maajabu yake ni kwamba hapa nina vya huyu mtu mmoja ambaye amevitunga Ndugu Kireri K. K. Katika vitabu hivi ukweli ni kwamba yaliyoandikwa humu huwezi ukaamini, naomba jamani kwanza nilikuwa najiuliza hivi kweli *EMAC* ipo? Kwa sababu kuna baadhi ya vitabu vina ithibati ya *EMAC*, lakini kuna vitabu vingine havina ithibati ya *EMAC*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana kwamba hapa kuna *issue ya pirating*, tuone Wizara ifanye utaratibu wa kwenda katika kila shule na kufanya ukaguzi wa kujua kwamba vile vitabu halali ni vipi na visivyo halali ni vipi. Nina-

declare interest mimi ni mwalimu *by profession* na nimekuwa Afisa Elimu Vifaa na Takwimu kwa zaidi ya miaka kumi, hiki kituko nihachokiona hapa ni cha ajabu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ushauri wangu kwamba Mheshimiwa Waziri, wenzangu wengi wamelizungumza hili, ninaomba sana iundwe Tume Maalum ambayo itakwenda kila shule kuona vitabu hivi kama viro sahihi. Pia walimu na Maafisa Elimu wajaribu kuangalia hivi vitabu kabla hawajavinunua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani tulikuwa na utaratibu wale wachapaji na wachapishaji wakiwa wanataka kukuuzia vitabu, lazima wakuletee *sample*, na wakikuletea *sample* ni lazima ile *sample* lazima uipitie kabla hujainunua, jambo la kushangaza ni kwamba hivi vitabu ukiviona hakika ni kituko kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu hii *Teachers Professional Board*, hili jambo limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu sana, ukurasa wa 80 katika hotuba ya Waziri imezungumzia lakini niseme kwa masikitiko makubwa sana hili jambo limeanza kuzungumzwa tangu mwaka 2009 na leo hii tuko 2017. Sasa ndugu zangu kwa kweli hili jambo itabidi kulifanyia haraka kwa sababu nilitegemea kwamba katika Bunge lijalo huu Muswada uwe *tabled*, lakini inaonyesha kwamba katika huu ukurasa wa 80 kwamba watakamilisha utaratibu wa uwanzishwaji, ina maana kwamba hata taratibu hazijakamilika, hebu naomba niishauri Wizara kuharakisha hii *Professional Board* ili walau walimu waweze kuona hii *Professional Board* ili kusudi tuepuke hao walimu ambao wanaingia katika hii fani bila utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake pia ukurasa wa 88, kwenye suala la Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo. Niipongeze sana Serikali kwa kuamua kujenga shule ya kisasa kabisa katika Mkoa wa Dodoma, najua kwamba sasa hivi Dodoma ndiyo imekuwa Makao Makuu ya Chama na Serikali,

ninapenda tu nimuombe Mheshimiwa Waziri kwamba isiwe shule moja tu, kwa sababu sasa hivi ujio wa watu katika Mkoa wa Dodoma utakuwa ni mkubwa sana. Kwa hiyo, Serikali na Wizara ione isiwe shule moja tu ziwe shule zaidi ili kusudi kuweza ku-accomodate wale watu ambao watakuwa wamefika katika Mkoa wa Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo wenzangu wengi wamelizungumzia ni kuhusu elimu ya kujitambua. Niungane na Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la mimba za utotoni ni tatizo kubwa sana katika jamii yetu. Sambamba na hilo kila mtu ana mtazamo wake wa kulibeba jambo hili, ila tu ninachowea kushauri ni kwamba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana katika mfumo wa elimu hivyo ni vyema Wizara ikajiwekea malengo mahususi (*prioritise list ya issues*) ambayo yanatakiwa kuwa *addressed mwanzo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ubora hafifu wa ufundishaji, hakuna mfumo maalum (*pedagogical skills*) ambao unatumika katika kufundisha mashulenii, jambo hili linatakiwa kupewa kipaumbele cha juu kabisa kwani lina *impact* kubwa sana katika kuelimisha.

Katika mfumo wa sasa tunakosa walimu bora ukilinganisha na miaka ya zamani (mpaka 1990) ambapo walimu wengi walikuwa wana *dedication* kubwa sana katika kufundisha na kuelimisha. Walimu walikuwa na uelewa mpana wa masomo wanayoyafundisha, walikuwa na *more ethics* na walikuwa *creative* katika kuhakikisha somo lake husika linaeleweka na kupendwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa wa kufumua upya utaratibu wa upatikanaji wa walimu (mchujo na mafunzo), kuboresha malipo kwa walimu na mazingira rafiki ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazingira duni ya kusomea wanafunzi, kuna haja kubwa ya kufanya *assessment* katika kila Wilaya na kwamba kila Wilaya itoe *list* ya shule ilizonazo katika kila Kata, hali ya shule husika na kadhalika ili kuweza kupanga mipango na utekelezaji wa mikakati husika na kuweza ku-*address challenges* kama matundu ya vyoo, madarasa, maabara, vitendea kazi (mazingira duni ya kujifunzia).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya usawa (wa kike na wasiojiweza); *still* ipo dhahiri hasa kwa watoto/vijana wa kike, wasiojiweza/walemevu. Mazingira ya sasa katika shule nyingi kuanzia za awali mpaka vyuoni nyingi hazina mazingira rafiki ya kuwawezesha wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kuweza kuhudhuria masomo au hata shughuli za *practicals* ama shughuli za michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosa falsafa ya elimu yetu, hii ipo dhahiri katika utahini, shulenii, udhibiti wa ubora wa elimu katika uandaaji wa elimu. Je, nchi yetu inasimamia katika nini? Dira ni nini? Kuna *link* yoyote katika mlengo wa uchumi wa katii na uchumi wa viwanda? Hii ipo *reflected* vipi katika *education system* yetu? Haya ni masuala muhimu ya kuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwajibikaji mdogo kwenye elimu, hakuna *policy* yoyote itakayoweza kutekelezwaa bila kuwa *translated* kwenye bajeti. Ni muhimu kuweka bayana Wizara ya Elimu na TAMISEMI kuonesha (*ku-tally*) zimepanga kujenga madarasa mangapi. Zimeletwa shilingi ngapi kwa mwaka 2017/2018? Wizara ya Elimu ina mpango mkakati gani wa kumaliza tatizo la madarasa?

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na

Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jitihada zenu za kuboresha sekta ya elimu nchini

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi, nilishauri na Baraza la Madiwani likapitisha hoja yangu ya kuwa na malengo ya na *A-level*/kila tarafa. Karagwe tuna tarafa tano lakini ipo *A-level*/moja tu. Ninaomba Wizara itusaidie kwenye vipaumbele vya kukamilisha malengo ya *A-level*/mbili kama ifuatavyo:-

Nyaboyonza sekondari bwalo moja, jiko moja, bweni moja na vitanda; Kituntu sekondari bweni la wavulana; Bisheshe sekondari si *A-level* ila sekondari hii tunaomba msaada ikamilike haraka kusaidia watoto wanaotembea umbali mrefu kupata elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda madaraja imekuwa tatizo kwa Karagwe, mapunjo ya mishahara, walimu wengi Karagwe kuanzia mwaka 2013 hadi sasa hawajalipwa hiyo fedha na madeni tayari yamehakikiwa na orodha ya walimu wanaodai CWT walipewa orodha hiyo mpaka sasa walimu hawajui muafaka ni lini wanalipwa.

Aidha, kwa walimu Karagwe kuna usugu wa kutopandishwa madaraja kwa zaidi ya 13. Utakapokuja kuhitimisha naomba uniambie tatizo hili linasababishwa na nini? Kwa nini mshahara unachelewa kurekebishwa ili uendane na tarehe ya kupandishwa daraja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yanayodaiwa na walimu yanakuwa na makato, na hii si haki kwa walimu. Serikali iweke utaratibu wa kulipa riba kwa madeni ya walimu ili walimu hawa wapate *time value of money* pamoja na *consideration* ya *inflation* (mfumuko wa bei).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi sana kupitia Mfuko wa Jimbo na michango yangu binafsi kusukuma kazi za uboreshaji wa elimu ya msingi Karagwe. Naomba Wizara iingilie kati kwenye shule ya msingi Ahakanya na shule ya msingi Rwentuhe ambapo walimu na wanafunzi wanasonic kwenye miti. Tayari nilishampa picha za shule

hizi Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Ndalichako. Pia shule ya msingi Rweizinga kwenye kijiji cha Mgurika, kata ya Bweranyange kuna baadhi ya wanafunzi wanasomea kwenye darasa la udongo liliozekwa na majani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni mbili za kupanua Chuo cha *VETA* cha *KDVTC* haziifika kwenye chuo, ninaomba Wizara itusaidie kupata fedha hizi.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai na leo hii tunaweza kujadili bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuonesha azma yake ya kuwa muumini mzuri wa elimu na kupata *Ph.D* yake akiwa kwenye lile Bunge la Tisa kama Waziri. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hili muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu ni tumrudishie mwalimu heshima yake. Madeni ya walimu yalipwe, walimu wapewe motisha, walimu wapatiwe vifaa vya kufundishia, walimu wapatiwe/wajengewe nyumba za kuishi hasa vijijini, walimu wapandishwe madaraja kwa wakati, walimu waruhusiwe kuijendeze na kadhalika. Kwa kuwa walimu ndio wanaofundisha fani zote, mishahara yao iboreshwe. Ualimu ni wito utunukiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya kufundishia iwe kiingereza kuanzia shule ya msingi ili tuweze kuingia kwenye soko la ajira la Afrika ya Mashariki (*East Africa*) na kwininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni mazingira duni ya kujifunzia yanayosababishwa na miundombinu katika maeneo husika kama maji, umeme, vyoo pamoja maabara. Ninapongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kumaliza zoezi la madawati, lakini nalo limezaa tatizo la madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu isiziachie Halmashauri tatizo hili kwani si sahihi sana hasa ukizingatia

kuwa uwezo wao ni mdogo na mambo ya kutekeleza ni mengi sana kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu bila malipo, juhudzi za Serikali kutoa elimu bila malipo kwa watoto wote zinaendelea na mimi ninaziunga mkono na kuzipongeza sana. Wadau wa elimu na jamii wanazo hoja kuhusu ubora wa elimu wanayopata watoto, mjadala huu ni wetu sote. Ni jambo jema hasa tunapoelekea awamu ya nne ya mapinduzi ya viwanda inayoitwa *exponential age*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha elimu hii inabidi wadau wote washiriki kikamilifu na kwa uaminifu mkubwa. Aidha, ninaomba Serikali itoe hela za kutosha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, naomba kuwasilisha.

MHE. HALIMA ALI MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 37, aya ya 65 inazungumzia kuhusu Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Ninaishauri Serikali kwanza, iongoze bajeti ya Wizara hii ya Elimu ili wanafunzi wengi waweze kunufaika na mikopo hiyo na pili, kwa kuwa takwimu zinaonesha ufaulu wa wasichana katika elimu ya juu ni mdogo ukilinganisha na wavulana, basi naishauri Serikali hawa wasichana waliojitalahidi kufanikiwa wapewe mikopo kwa asilimia 100 ili iwe ni motisha kwa wengine wajitalahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya walimu, elimu ni walimu, chonga mzinga ule asali. Walimu wasikilizwe vilio vyao ikiwepo mishahara, kupandishwa madaraja pamoja na posho za wale wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Jambo hili ni kero ya muda mrefu na linapunguza ari ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shule za bweni, uzoefu unaonesha wanafunzi wa shule za bweni ni dhahiri wanakuwa na mazingira rafiki ya kuwawezesha watoto wetu

kutumia muda mwingi kujisomea kuliko wale wa *day* ambao huondoka nyumbani alfajiri na kurejea usiku. Jambo hili si tu linawasababishia uchovu na kushindwa kujisomea, lakini pia kwa wasichana usalama wao ni mdogo wanapokuwa njiani. Naiomba Serikali iwaangalie wasichana wetu kwa jicho la karibu kwa kuwajengea shule za bweni za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya shule zetu; miundombinu ya shule zetu nyingi si rafiki kwa wasichana wetu kuhusiana na matundu ya vyoo ambavyo vitakuwa havina maji ya uhakika, haviwezi kuwa ni msaada kwa watoto wa kike wakati wa hedhi zao. Nusu ya watoto wa kike waliopo shulenii wanakabiliwa na changamoto ya kupata maambukizi ya *UTI*. Magonjwa haya ni hatari kwani yana tabia ya kujirejea lakini pia kupata magonjwa ya figo ambayo ni hatari zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifanye utafiti kuhusiana na magonjwa ya *UTI*. Halmashauri zijiwekee malengo mahsusii ya kujenga matundu ya vyoo na maji ya uhakika. Shule zisipewe vibali vya kufunguliwa kwanza bila ya kuwepo mfumo mzuri wa maji ya uhakika, viongozi husika wakishindwa kulisimamia hilo, basi wawajibishwe kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uwezekano wa uwepo wa nesi mwanamke katika shule za msingi angalau mara mbili kwa wiki ili wasichana wawe na fursa ya kupeleka malalamiko yao yanayohusu afya zao, lakini pia wapate ushauri unaohusu mabadiliko ya maumbile yao na nini wafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malezi; wazazi tuna wajibu wa kwanza wa kulea watoto wetu kimaadili kabla ya muda wa kwenda shule. Kambale mkunje angali mbichi, ukichelea mwana kulia mwisho utalia mwenyewe, inawezekana, timiza wajibu wako kwa faida ya Taifa. Ahsante.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze

na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Joyce Ndalichako na Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti yao ili tuijadili. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua Dkt. Ave Maria Semakafu kuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara hii, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuunga mkono hotuba ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na hasa ukurasa wa 29 wa kitabu chao. Serikali itoe tamko rasmi juu ya wanafunzi wa kike ambao wamekuwa wakifukuzwa shule kutohana na kupata ujauzito kurudishwa shulenii ili waendelee na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madeni ya walimu, niipongeze Serikali kwa kulipa madeni ya walimu kwa kuanza kulipa shilingi billion 33.1 sawa na asilimia mbili. Naomba Serikali iongeze kasi ya ulipaji madeni hayo.

Katika Mkoa wa Iringa, walimu wanaidai Serikali shilingi 1,238,841,517.00, lakini tangu wamehakikiwa hakuna hata Wilaya moja iliyolipwa kabisa. Naomba kujua utaratibu unaotumika au vigezo vinavyotumika kulipa haya madeni katika mikoa na Wilaya zetu. Inakatisha tamaa sana kuona mwalimu anafundisha bila ari na chama kinataka kuandaa maandamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu bure, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Niipongeze Serikali kwa programu hii, imeonesha kuwa kuna changamoto nyingi sana zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo, lakini bila kuanza tusingezibaini changamoto hizo. Lakini ni vema Serikali iwe na mkakati wa kuzishughulikia changamoto kwa wakati ili azma ya Serikali iweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuta Kodi ya Ujuzi (*SDL*) na uchangiaji wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*WCF*) katika vyuo vikuu binafsi, ukisoma ukurasa wa 33 katika kitabu cha Kamati, unazungumzia kwa kirefu kuhusu hilo, naomba

niunge mkono hoja. Hivyo vyuo havifanyi biashara bali vinatoa huduma kwa manufaa ya nchi yetu. Kuwepo kwa tozo hizi kunapelekea kuwa na changamoto ya kupanda kwa ada na kupungua kwa ajira ili vyuo viweze kujidesha, Serikali iliangalie upya jambo hili na kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za elimu zilizopo katika vyuo vyetu vya Iringa, bei za nyumba katika maeneo yanayozunguka vyuo vya Iringa ni kubwa mno, ni vema Serikali ingetoa bei elekezi. Mikopo bado inachelewa sana, hasa wanafunzi wa elimu ya vitendo (*field and research*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya watu wenye ulemavu, niipongeze Serikali kwa kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia lakini bado miundombinu katika shule nyingi si rafiki na watu wenye ulemavu kabisa. Mazingira ya vyoo vya shule nyingi bado si rafiki kwa watoto wa kike hasa wawapo kwenye siku zao. Uwiano uliopo kati ya idadi ya wanafunzi na idadi ya matundu ya vyoo bado si ya kuridhisha kwa viwango vya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali mbaya sana ya majengo ya shule; hali ya majengo ni mbaya sana, mfano katika Mkoa wetu wa Iringa shule nyingi tangu zijengwe hazijawahi kukarabatiwa, sera ipo vipi? Mtoto anasoma katika mazingira magumu sana, hakuna vioo, hakuna *floor*, hakuna *ceiling board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maktaba katika shule zetu, sera inasemaje kuhusiana na hili? Hali ya maktaba za shule za msingi na sekondari si nzuri, watoa huduma za maktaba (wakutubi) hawapati ajira kwenye maktaba za shule. Shule inapohamishwa inatakiwa iwe na maktaba lakini si shule zote zenye maktaba. Kama tusipozisimamia hizi maktaba hatutakuwa tumemtendea haki huyu mtoto tunayetaka kumjenga kielimu na kuwa na mazoea ya kujisomea ambayo ingemsaidia hata akienda elimu ya juu kuwa na utaratibu wa kusoma.

MHE. DEVOTH A. M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mimba kwa watoto wa kike walio chini ya miaka 18 waliopo shulen, lazima Serikali ikubali kwa kuweka mkakati maalum wa kuwaendeleza watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa shulen. Kupata mimba hatukubaliani nako, si kitu kizuri, lakini sasa tuwalaani watoto wa kike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pamoja na kuja na sheria ya kifungo cha miaka 30, lakini bado watoto wanaendelea kupata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu kwa shule za msingi zinaonesha wanafunzi 251 wamepata mimba, takwimu hizo bado kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Kuwaondoa shule watoto kwa kupata mimba bila kuwa na mpango wa kuwaendeleza ni sawa na kuendelea kutengeneza Taifa la mbumbumbu. Tujue watoto wanaopata mimba ni dhahiri hawajapata uelewa wa masuala ya afya ya uzazi kwa maana ya kujua uzazi wa mpango, afya ya mama na mtoto, elimu ya kulea mtoto, umuhimu wa chanjo na kadhalika. Ni wakati wa Serikali kuweka mkakati wa mpango wa kuwarudisha shule watoto wa kike wanaopata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwiano wa walimu katika shule zilizopo mjini na vijiji haupo sawa. Ipo haja Serikali kuona jinsi ya kugawa walimu kwa uwiano ili kukidhi mahitaji ya walimu kwani shule nyingi vijiji zina upungufu wa walimu, hasa wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la mkanganyiko wa vitabu, kutohana na makosa makubwa yaliyopo kwenye vitabu na bado vinaendelea kutumika kuharibu watoto wetu, ni vizuri Serikali ikachukua hatua kuvikusanya vitabu vyote na kuviondoa kwenye shule na kuja na utaratibu wa haraka wa kutengeneza vitabu vingine visivyo kuwa na makosa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga hoja mkono mia kwa mia. Pia nashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Joyce Ndalichako kwa msaada mkubwa alionisaidia kwa shule ya sekondari ya Kirando kwa kunisaidia shilingi 138,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanafunzi waliopewa mimba kurudi shule baada ya kujifungua haikubaliki kabisa, kwa kuwa kwanza tunapinga mimba za utotoni wakati tunasema mtoto anayestahili kuolewa ni miaka 18. Je, unahitaji sasa mtoto aolewe au azae chini ya miaka 18? Tunajikanganya na kuna sheria, mtoto anyonye kwa miaka miwili, pia tutaongeza watoto wa mitaani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mtoto kama anaanza mapenzi angali mwanafunzi vipi achanganye masomo na mapenzi? Kwa hiyo, turuhusu hata watoto chini ya miaka 13 waolewe kwa kuwa hata akijifungua ataendelea na masomo. Tukiruhusu ni kuruhusu wanafunzi wazae na kupata UKIMWI. Naiomba Wizara ikatae kabisa suala la kuruhusu mwanafunzi aliyepewa mimba kurudi darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiruhusu wanafunzi wanaopata mimba warudi mashulenii tutafungulia kwa walimu wasio kuwa waaminifu kufanya mapenzi na wanafunzi na kuwasaidia kimasomo kwa mapatano ya kuishi nao kimapenzi. Mimi sikubaliani na kufanya zinaa kabla ya ndoa na kuongeza watoto wasio kuwa na baba zao na kuongeza mzigo kwa Taifa letu.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Lushoto ni Wilaya yenye wakazi zaidi ya 600,000 na Wilaya yenye majimbo matatu ya uchaguzi. Hata hivyo Wilaya ile haina Chuo cha VETA tangu nchi hii ipate uhuru. Pamoja na hayo kuna vijana wengi sana ambaao wanamaliza elimu ya msingi na sekondari lakini vijana hawa wanakimbilia mijini kwa sababu hawajaandaliwa juu ya suala zima la kupata stadi za maisha. Hivyo basi, niiombe Serikali yangu tukufu kuanzisha Chuo cha VETA haraka iwezekanavyo katika Wilaya ya Lushoto ili

kuwanusuru vijana wetu na kutokukimbilia mijini. Pamoja na hayo Lushoto kuna majengo ambayo yapo tayari kwani kuna karakana ya seremala na jengo kubwa la gereji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali yangu iwawezeshe hawa wakaguzi wetu wa elimu Wilayani. Watu hawa wanapata taabu sana kwa kuwa hawapati bajeti yoyote hivyo kushindwa kufanya kazi zao za kutembelea shule na hii pia inachangia kushuka sana kwa elimu. Kwa mfano, Wilaya ya Lushoto ni ya milima na mabonde, kwa hiyo, Wilaya ile inahitaji miundombinu ya magari pamoja na mafungu ya rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya na Jimbo la Lushoto kuna shule za msingi zaidi ya 90 na seondari 35 lakini shule hizi zinakabiliwa na changamoto za walimu hasa wa masomo ya sayansi pamoja na nyumba za walimu. Pamoja na hayo walimu wetu watengenezewe mazingira mazuri pamoja na kuwapa motisha pale wanapofanya vizuri, lakini pia Serikali iboreshe miundombinu ya shule zetu kwani shule zilizo nyingi zinahitaji kukarabatiwa pamoja na kujenga matundu ya vyoo yaliyojaa, na yaliyobomoka yafanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haya maboma yanayojengwa kwa nguvu za wananchi, niiombe Serikali yangu ipeleke nguvu ya kumalizia majengo yake, pamoja na hizi maabara nydingia ambazo zimesimama kwa sababu wananchi wamejenga mpaka mtambaa wa panya yaani (kwenye lenter) na mengine yamepigwa mpaka na bati. Niombe Serikali yangu sasa imalizie maabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali ipeleke vitabu vya kiada na ziada kwa wakati kwani hii nayo ya kutokupeleka huduma hii kwa wakati kunasababisha kushuka kwa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu Tukufu, hili suala la chakula cha mchana ilichukue kwani wazazi walio wengi hawana uwezo na hii inasababisha

wanafunzi hasa kwa wale ambao wazazi wao hawajachangia, hujisikia vibaya na kuathirika kisaikolojia, na kumsababisha mwanafunzi kutozingatia masomo anayofundishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Kwanza kabisa nianze kuzungumzia changamoto za elimu kwenye jimbo langu la Tarime Mjini. Licha ya Tarime kuwa mjini lakini tuna shule moja ya kidato cha tano na sita (*A-Level*) ambayo ipo tangu miaka ya 1960, na shule hii ni ya wavulana tu. Hivyo tunaomba ombi letu ambalo limekuwa ni la muda mrefu lipatiwe ufumbuzi kwa kupandisha shule za Nyamisangura na Mogabiri kuwa na *A-Level* kwa kuwa miundombinu yake inakidhi vigezo na pia tuna walimu wa kutosha wa kufundisha masomo ya *A-Level*. Tunaomba Serikali ione umuhimu wa kuanzisha hizi shule ili kutoa fursa. Kuna watoto wetu wa kike ambao humaliza na kukosa fursa za masomo ya *A-Level*. Limekuwa ni ombi la muda mrefu tunaomba lifanyiwe kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Halmashauri ya Mji wa Tarime tuna changamoto za shule za msingi, kitu ambacho kinapelekea uhafifu na ubora wa elimu kwa sababu ya mazingira mabaya ya kufundishia na kujifunzia. Kumekuwa na uhaba mkubwa wa madarasa licha ya juhudzi za wananchi pamoja na mimi Mbunge wao ambapo nimeweza kujenga maboma kadhaa, lakini Serikali inashindwa kuweza kukamilisha majengo yake ili yaweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu inaelekeza kuwa na *ratio* ya wanafunzi 45 kwa darasa, lakini jimboni kwangu uwiano wa mwanafunzi kwa darasa ni darasa moja kwa wanafunzi 120 au 150 au 200. Hii haikubaliki na ni aibu kwa nchi yetu kwani ni dhahiri hapo kutakuwa hakuna mawasiliano kati ya mwalimu na mwanafunzi.

Naomba sana Serikali ilete fedha ili kuweza kumalizia maboma na kupunguza adha ya madarasa jimboni kwangu na hivyo kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kuhusiana na uhaba wa nyumba za walimu ambapo walimu wanapanga nyumba mbali na shule zao kitu ambacho kinafifisha ufundishaji kwani walimu wanachelewa kurudi au kuja shulenii hasa kipindi cha mvua. Hii ni aibu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema walimu wawe na nyumba shulenii. Naomba Serikali ilekeze kwenye nyumba za walimu ili kuweza kutoa ufanisi kwenye kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika jimbo langu kuna uhaba wa ofisi za walimu ambapo inapelekea walimu kukaa nje, chini ya miti hasa shule za Sabasaba, Azimio pamoja na Mapinduzi. Wengine kugeuza madarasa kuwa ofisi huku wakiwa hawana samani au makabati ya kuhifadhi vitabu. Kwa kweli hali ni mbaya sana, tunaomba Serikali ione haja ya kuboresha mazingira ya walimu ya kuandaliwa, kufundishia na kuishi. Hizi zitatoa motisha kwani walimu wana matatizo mengi sana kama vile madeni, kutokupandishwa madaraja, malimbikizo ya fedha za likizo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusiana na mahitaji au vifaa vya kufundishia. Kuna uhaba mkubwa sana wa vitabu kwenye jimbo langu, yaani uwiano wa kitabu ni 1:100, hii inaleta ugumu sana kwa mwanafunzi kuelewa. Inatakiwa kuwa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja, lakini sasa ni kitabu kimoja kwa wanafunzi 100 au 150; hii ni mbaya sana. Sasa cha kusikitisha ni juu ya vitabu vilivyogawiwa hivi karibuni kwa darasa la pili na la tatu, takribani 13,680,981 hivi vitabu vina makosa. Tunaenda kujenga Taifa la wajinga, maana mtoto huamini alichofundishwa au kusoma kwenye kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ione umuhimu wa kuweka nishati ya umeme kwenye shule zote ili kurahisisha ufundishaji na kutoa fursa ya wanafunzi kujisomea.

Pia tuweze kuboresha miundombinu ya vyoo kwenye shule zetu kwa ili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kupunguza magonjwa kwa walimu na wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni juu ya elimu bure ambayo kwa kiasi kikubwa hajatoa nafuu kwa mwananchi na zaidi *ime-affect*, maana wazazi wamegoma kutoa michango ya chakula, hata wengine kwenye ujenzi. Lakini pia bado wazazi wanaochangishwa fedha za kulipa walimu wa sayansi wa kujitolea michango ni mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie Kitaifa juu ya nini kifanyike ili kuboresha elimu ya Tanzania na kujenga Taifa lenye watu walioelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuomba Serikali ilippe madeni yote ambayo walimu wanadai, fedha za likizo, kupandishwa madaraja na stahili zote ikiwepo kuongezewa mishahara. Hii itatoa motisha na hamasa kwa walimu wetu na hivyo kuwa na ufundishaji bora na hivyo kuwa na elimu bora kwa wanafunzi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali ione umuhimu wa kuhakikisha makundi mawili, kwa maana ya wale wasiojiweza pamoja na watoto wa kike wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni makundi muhimu sana ambayo yamekuwa *sidelined*. Vilevile tuwe na uwajibikaji kwenye elimu ya watoto wetu na hii ni kwa wadau wote maana ya wazazi na walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Serikali iwekeze kwenye majengo. Kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri anaonyesha ni madarasa 2,000 tu yatajengwa katika madarasa 158,674. Hii inaonesha dhahiri Serikali bado hajadhamiria kuondoa tatizo la msongamano mashulenii kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya madarasa kwa sababu kwa *speed* hii itachukua miaka 79 kuweza kutatua

tatizo la madarasa/msongamano. Pamoja na upungufu wa matundu ya vyoo 200,000 (*Best 2016*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba vifaa vya maabara jimboni kwangu maana majengo mengi yamekamilika lakini hatuna vifaa na wataalamu wa maabara hadi majengo yanageuzwa kuwa madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mungu kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya nchi yetu tuna changamoto kubwa ya mimba za utotoni zinazopelekea watoto wa kike kuacha shule. Suala hili ni vyema Serikali ikachukua hatua kwa kuhakikisha elimu ya afya ya uzazi inatolewa mashuleneni ili watoto waweze kutambua mabadiliko ya miili yao na kuwawezesha watoto kufanya maamuzi sahihi. Serikali ihakikishe kuwa *clubs* za wasichana zinaundwa mashuleneni na kila shule iwe na *matron* au mwalimu wa kike atakayewajibika kusimamia *clubs* hizo na utoaji wa elimu ya afya ya uzazi (*sexual/reproductive health*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la utoro mashuleneni ambapo watoto wa kike wengi wanakuwa watoro kutokana na suala la *menstruation period* ambapo mtoto wa kike anaingia kwenye siku zake kwa siku tatu hadi nne ambapo kwa mwaka hufanya siku 48. Kama mtoto hatapata *sanitary pads*, atashindwa kwenda darasani na hivyo kuathiri ufaulu wake darasani au kupelekeea watoto wa kike kuacha shule kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe ruzuku ya *sanitary pads* kwa watoto wa shule ambapo watoto watapata *sanitary pads* (taulo za kujihifadhi) kwa bei rafiki ya shilingi 500 kwa pakiti badala ya shilingi 3000 hadi 4000 ya bei ya *sanitary pads* kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze pesa za mkopo wa wasichana vyuoni ambapo waongezewe shilingi 40,000 kwa *semister* au shilingi 80,000. Ongezeko hili litasaidia wasichana kumudu mahitaji yao ya *pads*. Pendeleko la shilingi 40,000 na shilingi 80,000 linatokana na bei ya *sanitary pads* kwa sasa.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu madai ya mtumishi aitwaye Ndugu Charles Kanyika. Naomba kuleta suala hili kwa maandishi kama ambavyo tayari nimewasilisha kwa Mheshimiwa Waziri. Mtumishi huyu anatarajia kustaa fu tarehe 15/06/2017 mpaka sasa hajapelekewa michango yake PSPF kwa miezi 18 suala ambalo litaathiri mafao yake. Nimeambatanisha maelekezo yake baada ya jithada zake kuomba ufumbuzi wa suala hili kutofanikiwa. Pamoja na kuwa huyu ni mtumishi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, ajira yake toka awali kwa mtiririko wa barua zake, mwajiri ni Wizaraya Elimu, naomba tumsaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu, hii dhana ya kwamba mwanafunzi aliyesoma *O-level* mpaka *A-level* katika shule zinazoitwa za bei mbaya kwa hiyo hastahilli mkopo kwa kigezo kuwa wazazi/walezi wana uwezo wa kulipia sio sahihi. Wapo watoto ambao wamesomeshwa na wafadhili baada ya *A-level* wafadhili sera zao au uwezo hauwapi nafasi ya kuwalipia elimu ya juu. Naomba wanafunzi wa aina hiyo watizamwe. Katika mchango wangu huu nimeambatanisha maombi kutoka kwa Padri Stephen wa *Selesian of Don Bosco* ambao watoto waliowafadhili wamekosa mikopo. Naomba ikiwa wana sifa Bodi ione uwezekano wa kuwasaidia. Nimeambatanisha barua pepe ambayo Padri Stephen aliniandikia na barua yangu kwa Waziri ambayo nakala nitaikabidhi Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NACTE vs St. Bakhita*. Kumekuwa na mkanganyiko wa namba za usajili ambazo wanafunzi wa *St. Bakhita* ambacho ni Chuo cha Uuguzi, wamepewa namba mbili tofauti na hawajui ipi ni namba yao ya usajili. Kila wanafunzi wanapohojii wanapokea vitisho

kiasi cha hata kupewa *supplementary* au *discontinuation*. Naomba *NACTE* itizame suala hili ili wanafunzi wawe na amani, pia nimemjulisha Mheshimiwa Waziri suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NACTE* kuingiliwa na Serikali kuliko kawaida, kwa mfano, Kurugenzi ya Mafunzo ya Wizara ya Afya ni kama iko juu ya *NACTE* naona kuna namna ya kudhoofisha *NACTE*. Nashauri *NACTE* ipewe nafasi ya kufanya kazi kwa mazingira bora ya ku-regulate vyuo vya kati. Aidha, ijengewe uwezo wa rasilimali watu na nyenzo ili ifanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *NACTE* ijitazame hasa katika kukagua vyuo, unakuta watoto wanasoma, wanamaliza vyuo, wakienda kwenye ajira ghafla wanaambiwa chuo alichosoma hakijasajiliwa na cha kusikitisha chuo kipo Dar es Salaam. Hili halikubaliki, ni uzembe wa hali ya juu. Pili, tozo mbalimbali wanazolipisha vyuo binafsi zimegeuka mzigo kwa wazazi. Ni kweli lazima kuwepo na tozo hizo ili kuiwezesha *NACTE* itekeleze majukumu yake ipasavyo lakini ziwe *fair and affordable* maana kinyume chake ni kuwabebesha mzigo kwa wazazi na walezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndoto ya uchumi wa viwanda bila kuweka nguvu kwenye elimu ya ufundi ni ngumu. Kwa ilivyo sasa Wizara ijikite (*it has to take lead*) kuhakikisha kuwa tunahuisha elimu ya ufundi katika maana halisi na sio kwenye maneno ya makaratsi. Tunahitaji *mat-technician*, *ma-artisan* kuliko hata *graduates*. Tunazungumzia uchumi wa mafuta na gesi lakini hata *focus* iko kwenye *Post-graduate level (masters)* na kuendelea. Nashauri sana, hata hii *VETA* isiwe bora *VETA* bali iwe na michepuo kulingana na mazingira na mahitaji ya maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo kwa kada za afya ngazi za chini. Naamini kama Taifa kila kada ina umuhimu wake lakini uzito na mahitaji yako tofauti. Nimelisemea hili katika mchango wangu wa Wizara ya Afya. Mahitaji ya kada za afya kuanzia *Labaratory Technicians*, Wauguzi, Maafisa Afya ni kada ambazo huko vijiji

wanafanya kazi kama madaktari na ni tumaini kubwa la wananchi. Hata hivyo, gharama za ada kwa vyuo vya uuguzi ni wastani wa shilingi milioni 3.5 kwa mwaka. Kwa kuwa vyuo vya Serikali havina uwezo mkubwa wa kudahili (kwa takwimu uwezo ni *around* 5,000 vyuo vyote kati ya maombi 13,000), nashauri Serikali ifikirie uwezekano wa kutoa mikopo kwa kada hizo. Kwa mfano, Peramiho wanamsaidia mwanafunzi kumlipia 50% ya ada na akimaliza anafanya kazi mwaka mmoja huku akikatwa sehemu ya mshahara kufidia mikopo/ile 50% ya ada. Tunaweza kuwa na utaratibu kama huo kusaidia kuongeza idadi ya watumishi wa kada ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya walimu, ni kweli kuwa Wizara hii ina *deal* na sera, lakini imekuwa kama kukwepa majukumu, kila ukimzungumzia mwalimu utaambiwa mara ni suala la TAMISEMI au Utumishi na kadhalika. Mwallimu ni dereva, hata kama gari ni *new model*, ni Benz, Vogue na kadhalika kama dereva yuko *demoralized* hasa katika *welfare*, gari haliwezi kufika. Walimu wamegeuka kama *second citizen*, Maafisa Utumishi kauli zao kwa walimu wanapofutilia haki zao ni vitisho mwanzo mwisho. Walimu wakitumika kwenye kazi za mitihani, vitambulisho, kura hawalipwi ipasavyo eti mtu anadanganywa na chai na keki kisha anapewa shillingi 10,000, *is totally unfair*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi ni mdau muhimu katika elimu, kumeanza kujengeka dhana kama *private sector* ni mshindani wa *public sector* katika elimu kuanzia utoaji wa miongozo, vitabu na usimamizi. Kwa mfano, *public schools* zimepewa vitabu lakini *private school* siyo wapewe bure lakini vipatikane sokoni. Tulihimiza watu wajenge shule na vyuo vikuu, leo hii kauli zetu kama viongozi *is like* nani aliwaambia muwekeze kwenye elimu. Cha muhimu uwepo usimamizi bora, tuiione *private sector* kama ni *partner* kwenye suala la elimu na sio washindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Tanzania Institute of Education*, wengi wamesema kuhusu suala hili, taasisi hii ama iongezewe nguvu kiutendaji ama kuwepo chombo cha ku-regulate maana *as of now* ni mchapaji, muidhinishaji na

msambazaji jambo ambalo siyo sawa kitaalam. Pia makosa kwenye vitabu yamekithiri na vitabu havifiki kwa wakati, kimsingi wamezidiwa. Nashauri wajengewe uwezo *both* kitaaluma na nyenzo. Vilevile kama tutarejea kurudisha Bodi ya *EMAC* na sekta binafsi, tuongeze umakini kwenye usimamizi. Katika uchumi wa soko ni vizuri tujikite kwenye udhibiti kuliko kuhodhi suala la vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye matokeo ya darasa la saba Mafinga Mjini pamoja na kuwa ni Halmashauri mpya tumekuwa nafasi ya nne kitaifa. Idara ya Ukaguzi hawana magari wala ofisi na vitendea kazi. Nafahamu jibu litakuwa hili ni suala la TAMISEMI lakini naamini ukaguzi uko Wizara ya Elimu, kwa hiyo, naomba ipatiwe gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na usumbufu wa michango ya chakula cha mchana, nashauri Halmashauri za mjini kama ilivyo *Mafinga Town Council* pawepo na utaratibu wa shule za msingi kusoma mpaka saa nane mchana siyo kama ilivyo sasa ambapo ama watoto wanarudia mchana au wazazi wanaombwa michango ya chakula. Kwa hali ilivyo na kwa mjini walimu wanatoka Kitongoji A mpaka B au C, sasa kwenda na kurudi ni gharama. Nashauri mliangalie kitaalam na kitaaluma ikifaa shule za mjini waishie saa nane mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi ni moyo wa elimu. Ukaguzi ni kama *CAG* kwa Serikali lakini *level* ya uhuru (*independent*)iko chini. Ukaguzi hii ya sasa inaikagua Serikali na walimu, je, sio muda muafaka sasa kuifanya iwe *agency*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukufahamisha kuwa shule ya msingi ya mahitaji maalum Makalala ipo katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga na si katika Halmashauri ya Mufindi kama ilivyo kwenye kitabu Ukurasa wa 272 kuhusu nukta nundu, ukurasa wa 296 kuhusu usambazaji wa vifaa maalum. Hoja yangu, kwa kuitaja *Mufindi DC* badala ya *Mafinga TC* ina mkangayiko, hili limejitokeza kwenye maeneo mengi, hivyo kuchelewesha utekelezaji, kwa mfano kiutawala (*administratively*) vifaa hivyo vikifika *Mufindi DC* kuwe na

taratibu za kuandikiana kwenda *Mafinga TC* ambako ipo shule ya mahitaji maalum Makalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi/ushauri, naomba kwenye taarifa zenu muitambue shule ya mahitaji maalumu ya Makalala kwamba ipo kwenye Halmashauri ya Mji wa Mafinga na si Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Ninaelewa kwa nini watu wengi wanachanganya, ni kwa sababu awali ilikuwa Halmashauri moja kabla ya kugawanywa Julai, 2017 na kupata Mafinga na Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma anaye rehemu, muumba mbingu na ardhi na viliyomo. Aldha, nakushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa uongozi wako madhubuti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ina majina mengi iliopewa kwa sababu ya utukufu na ubora wake na kwamba aliye nayo huambiwa kaelimika. Elimu ni ufunguo wa maisha, elimu ni maisha na majina mengi mengineyo kuhusu elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi, elimu hasa ni ile inayomkomboa mtu katika kusimamia majukumu yake na ya Kitaifa. Taifa lolote duniani haliwezi kuendelea bila ya mfumo mzuri wa elimu na mfumo bora wa elimu duniani ni ule unaozingatia mambo muhimu kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu imsaidie mlengwa mwenyewe na Taifa lake kwa ujumla wake. Pia elimu imuwezeshe msomi huyu kuweza kujitegemea na aondokane na kuwa tegemezi. Pia imsadie kuijua dunia yake anayoishi hususan katika dunia hii ya utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa kwetu Tanzania mfumo wetu wa elimu ni tofauti kidogo na matakwa ya mfumo bora wa elimu. Katiba yetu inataja kwamba kupata elimu ni haki ya kila Mtanzania ya msingi kabisa, lakini elimu inayotolewa hapa haikidhi haja na matakwa ya mfumo bora

wa elimu. Mfumo na mitaala yetu hajengi katika kutoa elimu bora (*quality education*) yaani ya muhitimu kuweza kujitegemea kutokana na elimu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa mfumo mzuri wa elimu ni pamoja na kuongezea bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kukidhi haja zote za elimu. India ni nchi inayoendelea kama Tanzania lakini bajeti yao katika elimu ni zaidi ya asilimia kumi, jambo ambalo limeifanya India kufanikiwa na kuwa miongoni mwa nchi bora duniani kwa kuzalisha na kuuza wataalamu mabingwa nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kutokana na uwekezaji mzuri juu ya elimu nchini India. Takwimu zinaonesha katika kampuni kubwa mashuhuri sana duniani iliyoko Marekani ya *Microsoft* ya tajiri mkubwa duniani, Bill Gates ina wafanyakazi zaldi ya asilimia kumi kutoka India, madaktari bingwa wengi walioko Marekani ni Wahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuiga jambo zuri si dhambi, wenzetu wamefanikiwa baada ya kuona umuhimu wa kuiongezea na kuikuza Wizara ya Elimu, hivyo naishauri Serikali itenye na kutoa pesa za kutosha kwa elimu ya ngazi zote, vyuo vya ufundi, kilimo na nyanja zote na sisi tuzalishé na kuuza wataalamu nchi za nje badala ya kuuza watumishi wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yetu inayotolewa zaidi inapelekea kuongeza idadi ya wahitimu katika kila ngazi. Kwa mfano, idadi ya wahitimu wanaomaliza shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu inaongezeka kila mwaka. Lakini idadi yote hii inayoongezeka kila mwaka ni tegemezi, hawana uwezo wa kujiajiri wenyewe, idadi kubwa ni lazima wapewe ajira Serikalini vinginevyo wahitimu hawa ndio hubakia wakizagaa tu mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi kwa Serikali, hatujachelewa bado, Serikali itilie maanani suala la mfumo bora wa elimu ili elimu itolewayo iwe ya manufaa zaidi ili utegemezi juu ya ajira kutoka Serikalini ipungue sana. Ikiwa

Serikali itaboresha Vyuo vya Ufundı (*VETA*) na huduma kamilifu, ni imani yangu kwamba wahitimu wetu wataweza kujajiri wenyewe na kuondoa mrundikano wa wahitimu wanaosubiri kupata ajira.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia Sera za Elimu hapa nchini. Mheshimiwa Waziri nianze kwa kukuomba kukipatia fedha za maendeleo Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ili kiweze kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa lililoanza kujengwa miaka minne iliyopita. Mheshimiwa Waziri Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere zamani Kivukoni ni chuo kinachobeba historia kubwa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni chuo cha kwanza kujengwa na Watanzania wenyewe tena kabla ya kupata uhuru. Chuo kile kimesaidia sana kuwaandaa viongozi wa nchi jirani kama vile Jocob Zuma, Rais wa Afrika Kusini. Mheshimimiwa Waziri jambo lingine ni kuhusu kuzisimamia na kuziangalia kwa karibu mno shule binafsi. Utaratibu wa shule binafsi ni mzuri sana tena sana, umesaidia kwa kiwango kikubwa mno kupungua kwa watoto waliokuwa wanakwenda nchi jirani kutafuta elimu bora. Hivyo umuhimu wake ni mkubwa mno, lakini kuna haja ya kuziangalia mara mbili zaidi hususani katika mambo muhimu mawili; kwanza ni kuhusu suala la ada kuwa kubwa mno na pili, huduma ya chakula kinachotolewa shulenii; kwa nini shule nydingi za binafsi hususani za Dar es Salaam hazitoi chakula kwa wanafunzi hasa zile shule za kutwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa watoto wadogo kuchukua pesa kwa wazazi wao ili wanunue chakula si mzuri hata kidogo na unapelekea watoto wetu kula vyakula visivyoeleweka, lakini pia ni chanzo cha kuwafundisha watoto tabia mbaya ya kupenda pesa wangali wadogo. Mheshimiwa Waziri naomba Wizara yako itoe maelekezo kwa shule zote binafsi zile za kutwa kuhakikisha zinawapatia chakula watoto wadogo wawapo

shuleni badala ya kuwaambia wazazi watoe pesa kuwapatia watoto wakanunue wenyewe chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uchache wa vyuo vya elimu ya juu na ufundi katika Mkao wetu wa Lindi. Mkao wetu wa Lindi una vyuo viwili tu ambavyo ni *VETA* Lindi na Chuo cha Utabibu. Naomba Serikali ilete vyuo zaidi Lindi kwani ardhi ya kujenga vyuo ipo na usafiri hivi sasa umeimarika hivyo kuharakisha mawasiliano. Nashukuru sana.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hotuba ya Kambi ya Upinzani na ile ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu huko vijiji zina matatizo mengi. Hakuna mabweni kwa ajili ya wanafunzi wala walimu wa kutosha. Watoto wa kike wanapangiwa vyumba vya kulala kwa kukosa mabweni, huko wanarubuniwa na kushawishiwa kwa kuwa hukosa pia fedha za kujikimu kwani wazazi wakati mwingine hawawapi kutokana na umaskini walio nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kike huweza kubakwa na kupata mimba, hivyo ninashauri Serikali ione namna ambavyo mtoto huyu anayepata mimba atakavyowenza kupata elimu baada ya kujifungua. Imekuwa kama adhabu kwa sababu tu ya kuwa ni wa jinsi ya kike kwani kama kijana aliyempa ujauzito huendelea na masomo hata kama sheria ipo hatujaona utekelezaji wake. Tunaomba Wizara ione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *VETA* tunaomba lipewe kipaumbele pamoja na *FDCs* ili wale watakaopewa kipaumbele kwa sehemu hizo wapate mafunzo na kuweza kujiajiri pindi watakacomaliza na hasa kupunguza wimbi la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejeee katika Mkao wa Iringa. Wazazi wameweza kujenga ama kuhamasisha ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana hasa shule ya sekondari

Lyandembela Ifunda Mkao wa Iringa na sekondari ya Mseke. Tunaomba Wizara iweze kushirikiana na TAMISEMI kuweza kusaidia katika umalizajili wa majengo haya pamoja na kugaiwa walimu wa masomo ya sayansi, walimu watakaokuwa walezi wa wanafunzi kwa ajili ya kufundisha unasihi. Mheshimiwa Waziri utakapohitimisha uweze kutueleza mkakati wa kuwa na walimu wa ushauri nasihi mashulenii hasa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuipongeza Wizara katika usimamizi wa elimu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyofanya. Vilevile nimpongeze Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu umejikita zaidi katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi (*VETA*). Katika kitabu cha bajeti cha mwaka 2017/2018 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (*VETA*) imepanga kutimiza malengo yafuatayo; itaendelea kufuatilia ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya mikoa mipya ya Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa. Maelezo yanapatikana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sera ya Taifa inasema kila Mkao na kila Wilaya kuwepo na Chuo cha *VETA*, nikiangalia katika Mkao wa Geita wenye Wilaya tano hakuna kabisa Chuo cha *VETA* katika Wilaya zote na katika Mkao. Wananchi wa Mkao wa Geita tunayo mahitaji makubwa sana ya elimu ya ufundi stadi. Watoto wengi sana wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari ambao hawaendelei na masomo ya ngazi za juu hawana ujuzi wa kuwawezesha kujiendeleza katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tukiwa na vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya itasaidia kuwawezesha vijana hawa kuwa na ujuzi. Vilevile Serikali ya Awamu ya Tano imekusudia kuwa na Tanzania ya viwanda. Hivyo tunahitaji vijana wawe

na ujuzi ili tuweze kufikia azma ya Tanzania ya viwanda. Kwa melezo haya ningependa kujua na kupata maelezo ya kina ni lini ujenzi wa Chuo cha VETA Mkoa wa Geita utaanza rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewiwa kuuliza kutokana na maelezo kwenye bajeti kwamba Serikali itandelea kufuatilia ujenzi, lakini haielezi bayana juu ya kuanza kwa ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Kwa dhati nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na msaidizi wake Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Taifa letu. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoiendea Tanzania ya viwanda ambayo itaongeza ajira kwa vijana wa Kitanzania, ajira hizi zitakuwa za vijana ikiwa tu wana ujuzi unaohitajika katika viwanda hivyo. Uwezo wa nchi yetu kwa maana ya Serikali kuanzisha vyuo vya ufundi hadi tukidhi mahitaji ya kila jimbo ama Wilaya kuwa na Chuo cha VETA kwa sasa ni kama miujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha azma ya kuwa na vyuo vya kutosheleza kwa ajili ya vijana wetu wote naomba nitoe ushauri kwamba kila Halmashauri katika shule zake za sekondari ijenge karakana ya fani moja ya ufundi. Hii itatuwezesha kufanikiwa kwa haraka na kuwezesha vijana wote watakapokuwa wanahitimu kidato cha nne watakuwa wana ujuzi. Kwa mfano, Azania sekondari (umeme), Kisutu sekondari (upishi/hoteli), Malangali sekondari (ujenzi) na Mbeya Day(useremala). Kwa mfano, huu tutawezesha vijana wote kuwa na ujuzi wa kuwawezesha kuajiriwa na kujajiri na kuwezesha kusukuma maendeleo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu juu ya kukithiri wa masuala ya ngono katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyochangia kwenye mchango wangu wa maneno kuwa ni kweli tulipofika leo masuala ya ngono yameonekana yanahusika moja kwa moja katika kupandisha alama ya ufaulu na imefanya wanafunzi wenyewe uwezo mdogo kuonekana kuwa vinara kwenye ngazi ya ufaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Serikali kutokana na mchango wangu juu ya ukithiri wa ngono vyuo vikuu. Ombi langu kwa Serikali ni kwamba kama ilivyofanya kwenye wasilisho la *Miscellaneous Amendement* na adhabu zake kwa yejote atakayempa mimba mwanafunzi aliyejukwepo masomoni ama kumuoja mwanafunzi basi adhabu yake iwe ni miaka 30 jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa unyenyekevu mkubwa Wizara ya Elimu ituletee muswada wa sheria kwa walimu wote vyuo vikuu watakaobainika kuwa na mahusiano na wanafunzi basi adhabu ya kwanza iwe ni kusitisha ajira na kufungiwa miaka kadhaa bila kuajirika mahali kokote sambamba na adhabu ya kichapo cha hadharani ili kukomesha kabisa tatizo hili. Ni ushauri wangu adhabu pia itoe *option* ya kifungo jela.

Pamoja na adhabu niliyopendekeza pia ni rai yangu kwa Bunge lako Tukufu, Ofisi ya Spika iridhie ombi langu la uwepo wa *special register book* itakayobainisha usajili wa makosa ya ubakaji, ulawiti, ndoa za utotonu/wanafunzi na hata watuhumiwa wote vyuo vikuu waliobainika kuwa na mahusiano na wanafunzi vyuo vikuu ili iwe rahisi kwa sisi Wabunge kufanya *follow up* ya makaosa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango juu ya uandaaji wa rasilimali watu kwa ajili ya usafiri wa anga ili kuweza

kupata tija kamili kulingana na uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuoanisha na kuendeleza Shirika la ATCL; pamoja na mchango huu pia napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako pamoja Mheshimiwa Mbarawa kwani baada ya juhudu zangu za kuonana na uongozi wa wanafunzi *NIT* sambamba na kikao cha tarehe 30/01/2017 na Mkurugenzi Mtendaji Shirika la ATCL nilibaini changamoto kubwa inayowakabili wanafunzi wa *NIT* hususani vijana wanaochukua mchepuo wa *Aircraft Maintenance Engineering*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi tajwa wana changamoto ya ada kubwa isiyohimili kwa wazazi walio wengi ambao wengi wao wameonekana kuwa na uchumi mdogo usiohimili ukubwa na uzito wa ada iliyopendekezwa na *NIT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Rwanda katika ku-promote expertiseya masuala ya usafiri wa anga walianza kwa kuandaa rasilimali watu kutoka katika nchi yao. Ada kwa masomo ya *Engineering* ni kiasi cha shilingi 40,000,000 na masomo ya urubaini ada (*direct fee*) ni kiasi cha shilingi 80,000,000 na katika kukabiliwa na changamoto ya uandaaji wa rasilimali watu kwa ajili ya usafiri wa anga, nchi ya Rwanda iligharamia masomo ya wanafunzi wa fani ya usafiri wa anga kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, kwa nini nchi yetu tunapata vigugumizi katika kukabiliana na kiasi cha ada ya shilingi milioni kumi kwa masomo yanayopatikana ndani ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hawa wanahitajika kuanza *practical training this June* lakini hata ndege ya mafunzo hakuna. Katika mazungumzo yangu na Mheshimiwa Profesa Mbarawa hivi majuzi nilielezwa Chuo cha *NIT* pamoja na Shirika la ATCL wamejipanga kukodi ndege za mashirika binafsi ili wanafunzi waweze kufanya *practical training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumenunua ndege mbili, *focus* yetu ni kuwa na ndege sita, sasa kwa nini mafunzo haya ya *practical training NIT* yasipewe kipaumbele? Kwani kufika kukodi ndege kwa ajili ya *practical training* na ilihali tunayo ndege ya Shirika la ATCLipo Mwanza, ambayo inahitaji matengenezo kidogo na badala yake tukodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoteza matumaini kwani wakati Mheshimiwa Rais anapambana ili kutujengea utamaduni wa kuondokana na matumizi yasiyo na umuhimu na kubana rasilimali fedha ya Taifa, lakin baadhi ya Taasisi bado tunaona Serikali ina fedha ya kupoteza kwa kufika kukodi ndege za mashirika binafsi kwa makusudi ya kufanikisha *practical training (PT)* yaani mafunzo kwa vitengo kwa wanafunzi wetu wa *NIT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba huwezi kuandaa *engineerwa* masuala ya ndege bila kumpa mwanafunzi elimu ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kama ifuatavyo:-

(i) Ndege ya Shirika la ATCL ilioegeshwa (*park*) Mwanza ipatiwe fedha na Wizara ya Fedha chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na chini ya usimamizi wa karibu wa Wizara ya Elimu ili kwa pamoja tumsaidie Mheshimiwa Rais katika kuimarisha usafiri wa anga ili kwa pamoja tuweze kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

(ii) Ni ushauri wangu Serikali kupitia Wizara ya Elimu iweze ku-*revive Civil Aviation Training Fund* ili kwa pamoja tuweze kuifikisha elimu stahiki kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa furaha na imani kubwa naomba kuunga mkono hoja wasilisho la Bajeti Wizara ya Elimu kwa asilima mia moja.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Wizara hii hasa eneo la ubora

wa zana za ufundishaji hasa vitabu nya kiada. Tangu Serikali ilipovunja Bodi ya *EMAC* uhakika wa vitabu umekuwa dhaifu sana na kusababisha upotoshaji mkubwa kwenye taaluma, hivyo kuchochea Taifa kudondokea katika umbumbumbu, ujinga na kukosa maarifa kwa watoto wetu. Vitabu viliwyopo sasa ni ushahidi wa dhahiri kuwa uwepo wa *EMAC* usingeweza kupitisha makosa haya. Pia dhamira ya kuirejesha *EMAC* iendane na suala zima la kuihusisha sekta binafsi ifanye kazi hiyo na Serikali ibaki kuwa mthibitishaji ili hata makosa kama haya yakijitokeza yasiathiri moja kwa moja Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kukuza uwekezaji katika viwanda. Serikali inapoamua kuchapa vitabu yenye sio lengo baya, lakini inakinzana na sera ya viwanda. Aidha, uwepo wa sekta binafsi katika tasnia ya uchapishaji itasaidia Serikali kuyaona mambo kwa jicho la mbali na jicho pana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke ushahidi wa vitabu vifuatavyo kuonyesha makosa ya dhahiri na ya wazi katika uchapishaji kuonyesha udhaifu mkubwa wa Taasisi ya Elimu kusimamia tasnia hii ya ukuzaji maarifa na utoaji elimu kwa vijana wetu.

(i) *English For Secondary Schools, Form Four – ISBN 978-9976-61-460-2*

(ii) *Geography for Secondary Schools, Form Three - TIE of 2016 –ISBN 978-9976-61-479-4*

(iii) *I learn English Language, Standard Three – ISBN 978-996-61-545-6.* (Vipo ikiwa ni ushahidi wa dhahiri).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yote yenye makosa yameainishwa na kuwekewe alama maalum kwa (*highlighter*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi nzuri na hotuba iliyosheheni utaalami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule kongwe zenyе historia kubwa hapa nchini ni pamoja na *Tabora Girls* ambayo imetoa viongozi wengi lakini ina hali mbaya hasa kukosa uzio. Pamoja na hayo, watu wamevamia na kujenga kwenye eneo la shule. Hivyo, niiombe Serikali inapotoa fedha za ukarabati iangalie shule hiyo. Bwalo la chakula kwa wanafunzi hao ni la muda mrefu na miundombinu yake haifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule kongwe nyngine ni *Tabora Boys* na Milambo. Shule hizi ni muhimu sana katika historia ya nchi hii. Ni shule zenyе kumbukumbu na historia kubwa ya Baba wa Taifa, lakini hazina uzio, majengo ni machakavu sana pia hata miundombinu ya maji ni hatari kwa afya zao na matundu ya vyoo ni machakavu. Nashauri pamoja na uhaba wa fedha ni vema wakaanza ukarabati huo kwani wanafunzi wanateseka sana. Ningemba sana mchango wangu uangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya walimu naomba yazingatiwe na yalipwe kwa wakati. Vilevile ukarabati wa shule ni vema uende sambamba na ukarabati wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya wazabuni kutolipwa madai yao. Wazabuni hawa wanaolisha shule wanadai fedha nyngi na kusitisha huduma kimya kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Waziri na Naibu Waziri, kwa jitihada kubwa wanazochukua katika kuinua elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia hotuba ya Wizara hii katika maneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, shule ya kidato cha tano. Naipongeza sana Serikali kwa kutoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Hatua hii ni ya kupongezwa sana kwa sababu imetoa fursa kwa Watanzania wengi sasa kupata elimu bila kujali idadi, uwezo au rangi. Hata hivyo, kuna tatizo katika baadhi ya maeneo mbalimbali nchini kutokuwa na shule za kidato cha tano mfano ni Wilaya ya Kilindi. Naomba hoja yangu ipate majibu, hivi ni kweli hatuna hata shule moja katika hizi zilizopo Kilindi ambazo tunaweza kuzipandisha ziwe za kidato cha tano? Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu *VETA*. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wilaya ya Kilindi ilikuwa ni miongoni mwa Wilaya chache ambazo zilitengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*. Wilaya tayari ilikwishatenga eneo kwa ajili ya ujenzi na ikumbukwe toka mwaka 2014 Wizara ilitamka itajenga chuo. Hivi ni hatua zippi zimefikiwa au kuna tatizo gani hasa?

Vyuo vya *VETA* vinatoa fursa kwa wananchi hususan vijana wetu ambao hawajabahatika kuendelea na kidato cha kwanza kupata fursa ya kupata ujuzi mbalimbali. Kilindi hatuna *FDC*, Chuo cha *VETA* ni hitaji muhimu kwa Wana-Kilindi, vijana wetu wa Kilindi wanahitaji la chuo hiki. Naomba Wizara iliangularie suala hili kwa jicho la ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uhaba wa walimu hasa wa sayansi. Tatizo la walimu ni changamoto kubwa sana, shule nyingi zina walimu wachache kuanzia shule za msingi hadi sekondari. Katika Jimbo langu la Kilindi tuna tatizo la walimu wa masomo ya sayansi. Nipongeze Wizara kwa kutupatia walimu sita wa shule za Serikali, lakini bado uhitaji ni mkubwa sana. Naiomba Wizara itupatie walimu wa kutosha. Ili dhana ya Serikali yetu kwenda kwenye nchi ya viwanda ifanikiwe ni lazima Serikali isomeshe walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ili tuondokane na tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi, Wizara ione namna ya kupunguza gharama za masomo katika vyuo vyetu ili kuwapa wazazi motisha. Vilevile ajira za walimu wa sayansi zipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu uwiano wa ugawaji wa walimu. Bado kuna tatizo la uwiano wa ugawaji na upangaji wa walimu katika nchi yetu. Kwa mujibu wa Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance Auditing*) iliyofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti wa Serikali (*CAG*) kuna tatizo kubwa katika eneo hili. Kuna baadhi ya mikoa mwalimu mmoja anafundisha watoto 26 wakati Mikoa mingine mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 46, hili ni tatizo kubwa, hali hii inadumaza maendeleo ya elimu. Niiombe Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na TAMISEMI, ipitie upya mgawanyo huu ili kuleta usawa wa maendeleo nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuamua kujenga hosteli pamoja na maktaba, yote haya yamefanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ujenzi wa mabweni utapunguza usumbufu na kuleta utulivu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na wataalam wote wa Wizara hii kwa juhudini kubwa wanayoifanya ya kuleta mabadiliko kwenye Wizara hii muhimu na kuinua ubora wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleza Bunge kuwa wataboresha shule za umma kuanzia miundombinu, vitendea kazi, walimu na kadhalika ili ziweze kutoa elimu bora na kurejesha heshima ya shule za sekondari. Kwa muda wa mwaka unaoishia Juni, 2017 ni shule ngapi zimeboreshwa na jukumu hilo limefikia wapi kwa jumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha vikao na

wadau wa shule binafsi ili kuweka *standards* za ada za shule za *private* ambazo ni kubwa mno na kila shule inatoa ada kwa utaratibu wake na hakuna *control* yoyote. Zipo shule zinatoza ada shilingi milioni tatu kwa mwanafunzi kwa mwaka bado kuna *bus fee* na michango mingine. Serikali ituletee hapa Bungeni taarifa ya vile vikao vimefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa sana la upungufu wa miundombinu kwenye shule za msingi na sekondari. Watoto wanasoma zaidi ya 100 kwenye darasa moja, lakini wapo wanaosoma kwa *shift*, wanaingia saa 2.30 asubuhi wanatoka saa 6.30 mchana na wengine saa 7.00 mchana mpaka saa 10.00 jioni. Watoto hawapati muda wa kutosha kupata masomo na vipindi vyta michezo, dini na mazoezi. Hakuna nyumba za walimu, wengi wanakaa kwenye nyumba za udongo huko mitaani, wengine wanakaa walimu watatu mpaka wanne kwenye nyumba moja hata ule uhuru wa kibinadamu hakuna. Walimu wanakatishwa tamaa na mazingira wanayofanyia kazi na yale wanayofundishia. Serikali itueleze mpango wa muda mrefu kuhakikisha walimu wanafundisha kwa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iboreshe na kuimarisha Ofisi za Ukaguzi wa shule za msingi na shule za sekondari kwa kuwapa magari ya ukaguzi kila Wilaya kwa ajili ya Mkaguzi wa Shule ya Msingi na gari lingine kwa shule za sekondari; Halmashauri za Wilaya iweke mafuta kwenye magari hayo ili muda wote wawe *field* na motisha uwepo kwa walimu wote hasa wale walio kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka sheria ya kurejesha mikopo kwa elimu ya juu na kuweka asilimia 15 kila mwezi. Japokuwa ni sheria, lakini hii sheria inaumiza sana walimu ambaao mishahara yao ni midogo. Ni vema waangalie utaratibu wa kuwasaidia walimu walipe kwa asilimia 7 kwa muda mrefu, lakini waweze pia kumudu maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya walimu ni vilio na

ni kero ya muda mrefu. Natumaini uhakiki umeisha na wenye vyeti *fake* wametambuliwa. Kuna walimu wa Kaliua walijiriwa mwaka 2014 hawakulipwa mishahara kwa mwezi Mei na Juni, 2014 (miezi miwili) huku wamo walolipwa mishahara yao. Pia malimbikizo ya madai yasiyokuwa ya mishahara ni mengi sana hayajalipwa kwa miaka zaidi ya saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwepo kwa mkanganyiko wa ubora wa vitabu vitakavyotumiwa na wanafunzi hasa *primary school* na zile za mchepuo wa kiingereza na uwepo upungufu mkubwa kwenye vitabu hivi vyta shule za awali ambapo ndipo eneo watoto wanapata msingi wa elimu yao, Serikali itueleze mikakati iliyopo ya kuhakikisha vitabu vyote vinavyotumika mashulenii vimefanyiwa uhakiki na kuondoa changamoto iliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatuambia nini kuhusu uwepo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Vitabu (*TEA*) lakini wameshindwa kufanya kazi ya udhibiti wa elimu yetu hasa shule za msingi. Nashauri kuwepo na taasisi binafsi zinazotengeneza vitabu vyta shule na visisambazwe mashulenii kabla ya kupitiwa na kuhakikiwa na mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la adhabu kwa watoto wa shule ni jambo jema kwa lengo la kumrekebisha mtoto na kumweka kwenye njia nzuri. Serikali inajua kuwa walimu wanatoa adhabu kubwa sana kupita kiasi? Watoto wanavuliwa nguo zote mpaka za ndani, wanachapwa mpaka wanalazwa na wengine wanapoteza maisha. Serikali itoe tamko leo Bungeni la kupiga marufuku adhabu za aina hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Sokoine ni chuo pekee cha kilimo hapa nchini kinachotoa elimu ya juu kwa masuala ya kilimo, ufugaji wa kisasa, *nutrition*, misitu, mazingira, tafiti mbalimbali na fani nyngine. Serikali kwa miaka mingi haijabadilisha miundombinu ya chuo hiki pamoa na kwamba kila mwaka udahili unaongezeka na

wanafunzi ni wengi. Nini mpango wa Serikali kuboresha chuo hiki tunapoelekea kwenye uchumi wa viwanda ambapo tutafika huko kwa njia ya kilimo?

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya Kamati kwa kutoa maelekezo ya mahitaji ya elimu kitaifa pamoja na kuonesha utatuzi wa changamoto za elimu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii; ukimuelisha mwanamke utaokoa jamii. Hivyo basi, hatua za haraka zichukuliwe katika kuongeza bajeti ya miundombinu katika shule za bweni za wanawake; kuboresha upatikanaji wa maji ili yawe ya uhakika; usalama kwa mabweni yasio na *fence*; huduma za afya katika mabweni ya kike na uboreshaji wa chakula kwa mabweni ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa wananchi wa Katavi wamekuwa wakisubiri ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo. Tunataka majibu ya Serikali, ujenzi utaanza lini na tufahamishwe kama fedha zimetumika nje ya utaratibusi au zimeliwa au chuo kilihamisha? Tatizo hili kuendelea kukaliwa Kimya na Serikali na Halmashauri ambapo zaidi ya shilingi bilioni moja zimeliwa na chuo hakipo, inamaanisha kwamba Serikali ya CCM inalinda wezi au imehusika moja kwa moja kudhulumu Chuo cha Kilimo kwa Wana-Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kuwa na Chuo cha Kilimo Katavi ni kwamba kundi kubwa la wananchi wa Katavi ni wakulima na wafugaji hivyo kupitia chuo hiki wangepata elimu bila kutakiwa kusafiri kwenda mikoa ya mbali na kupunguza gharama hususani kuleta mapinduzi ya kilimo cha kisasa mkoani Katavi, uwekezaji, ajira na uchumi wa viwanda kupitia chuo chetu kilichoyeyuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchache wa vitabu Katavi, tunaomba viongezwe pamoja na shule za sekondari na shule za msingi. Pamoja na juhudhi za walimu Mkoa wa Katavi kufundisha wanafunzi katika mazingira magumu lakini

ufaulu wa wanafunzi shule za msingi tumekuwa na matokeo mazuri kimsingi. Naomba vitabu viongezwe kwani hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wasioona katika Wilaya ya Mlele mmetenga vitabu 6014, vitendea kazi kwa wanafunzi wasioona ni vichache mno viongezwe ili kuleta motisha. Fedha zilizotolewa kama motisha kwa Halmashauri P4R, shilingi 78,777,349 Mpanda, Nsimbo shilingi 102,473,308 na Mlele shilingi 80,688,319. Bado kuna uhitaji mkubwa, mbona mikoa mingine mmepeleka kiasi kikubwa cha fedha? Je, mmetumia kigezo gani katika mgawanyo huu kama sio ubaguzi huu wa keki ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vitabu vyatya sayansi na *biology*. Mkoa wa Katavi (mgawanyo Kiwilaya, Mpimbwe - 0, Mpanda - 0), nini kimetokea mpaka Wilaya za Katavi kukosa vitabu vyatya kidato cha tano na sita katika mchepuo wa sayansi? Hamuoni kwamba mnapunguza molari ya wanafunzi kusoma mchepuo ya sayansi vitabu? Kidato cha kwanza, jumla ya vitabu 6,030 Mkoa mzima na kidato cha tatu jumla ya vitabu 3,780. Ukiangalia wingi wa shule na uwiano wa vitabu hivyo inaonyesha kabisa hakuna dhamira ya dhati ya kusaidia ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari zetu za Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari ya wanawake za *Mpanda Girls* na Milala sekodari. Shule hizi hazina wigo (*fence*) kwa ajili ya usalama wa wanafunzi hawa. Je, ni lini Serikali itatenga bajeti itakayotekelezeka ili kunusuru wanafunzi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba majibu ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Katavi, ni lini utaanza na kama fedha zilitumika hovyo Serikali inawachukulia hatua gani wahusika? Vilevile naomba michango kwa wanafunzi ipunguzwe kwani ni changamoto kubwa kwa wazazi wenye hali duni kiuchumi.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwanza niunge mkono hoja ya Wizara ya Elimu. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa sekondari. Tuna tatizo kubwa sana kwani maeneo mengi yana upungufu wa majengo ya shule za sekondari. Pamoja na juhudhi kubwa inayofanywa na wananchi kwa kujitolea asilimia 20 bado Halmashauri zinashindwa kuwasaidia kumalizia majengo ya shule. Niombwe Wizara iangalie uwezekano wa kusaidia kuboresha majengo na kujenga shule mpya pale ambapo ni stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye Wilaya mpya ya Tanganyika tupatiwe msaada wa fedha za kumalizia shule za sekondari za Tongwe, Bulamata sekondari, Ilangu sekondari na Mazwe sekondari. Shule hizi zinahitaji msaada wa Serikali wa kuzifanya ukarabati na kuongeza madarasa na nyumba za walimu na kujenga maabara pamoja na vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na matatizo ya uchakavu wa majengo na ukosefu wa vyumba vya madarasa kwenye shule zetu za msingi, bado tuna tatizo kubwa la ukosefu wa walimu. Tunaomba Serikali iangalie umuhimu wa kuongeza walimu wa kufundisha kwenye mashule hizi hii ikiwa ni pamoja na kuongeza marupurupu ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya walimu, kuna malalamiko makubwa ya walimu kuidai Serikali stahili zao ikiwemo kutopandishwa vyeo, kutolipwa posho zao za likizo, nauli na posho za madaraka. Niombwe Mheshimiwa Waziri aje na majibu ya uhakika juu ya suala zima la madai ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vingi vya ufundi vina hali mbaya sana kwa kukosa vitendea kazi hasa vya kufundishia jambo ambalo linasababisha vishindwe kukidhi malengo ya kuanzishwa vyuo hivi. Niombwe Serikali iboreshe

Chuo cha *VETA* Mpanda kwani hakina vitendea kazi pamoja na walimu. Chuo hiki kinategemewa sana na wananchi wa Mkoa wa Katavi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawatachia Mawaziri kila kheri katika kusimamia sera, sheria na kanuni za sekta hii muhimu ya elimu. Nina mambo muhimu katika maeneo matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, uboreshwaji wa miundombinu katika Shule ya Wasichana ya Sekondari ya Sumve. Shule hii Serikali imeisahau kama vile ni *private secondary school*. Shule hii inachukua wanafunzi toka maeneo mbalimbali ya nchi yetu wa kidato cha tano, lakini haina walimu wa kutosha, vitanda, magodoro hayafanani na jina la shule na mengine mengi. Naomba shule hii Wizara iithamini kama ilivyokuwa zamani hasa ikizingatiwa kuwa ni shule ya wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wilaya ya Kwimba leo ni zaidi ya miaka kumi tumetenga eneo la kujenga Chuo cha *VETA* lakini Wizara imekuwa ikiahidi kila mwaka kuwa kitajengwa lakini imekuwa ni hadithi isiyioisha. Naomba katika bajeti hii nipate ufumbuzi wa ahadi ya siku nyingi ya Wizara ya ujenzi wa *VETA* Kwimba au niambiwe nitumie mbinu gani ili ujenzi huo uanzé. Chuo hicho kinahitajika sana, mimi kama Mbunge kwa zaidi ya miaka 20 nimekuwa nikiomba ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kwimba, nimekuwa nikitumia lugha ya kiungwana, naomba na Wizara nao wawe waungwana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, *FDC* Malya. Tunacho Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya ambacho ni kama Wizara imekitelekeza, kinaendeshwa isivyo au kama siyo cha Serikali. Chuo hiki nilipendekeza kama Serikali inaona imeshindwa kukihudumia kuititia Wizara ikifanye kiwe Chuo cha *VETA* kwani shughuli inazozifanya zinafanana na za Chuo

cha *VETA*. Huo ni ushauri wangu endapo Wizara haijajipanga kujenga chuo, miundombinu iliyopo Malya inajitosheleza, inachotakiwa ni uboreshaji, lipo eneo kubwa la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, hayo niliyoomba ya shule ya wasichana ya Sumve, *VETA* na *FDC* Malya yatazamwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, katika jimbo langu tunayo shule ya sekondari ya wasichana ya waliokosa fursa baada ya kupata mimba, kuishia kidato cha kwanza au cha pili inayojulikana kama *Arch Bishop Mayala* iliyosajiliwa. Mwaka jana Makamu wa Rais alipata nafasi ya kuitembelea ambapo alivutiwa sana na uamuzi huo wa kuanzisha shule hiyo. Nimuombe Mheshimiwa Waziri katika ratiba zake Mkoani Mwanza aitembelee shule hiyo ili ajionee mwenyewe na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, suala la ugawaji wa vitabu katika shule zetu za sekondari ni vizuri ukafuata uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu nyumba za walimu. Sehemu za vijijiini pamezidi kuwa na uhaba wa walimu, unakuta shule moja ina walimu wawili tu. Tatizo hili linatokana na kwamba unakuta mwalimu ametoka nyumbani kwake kwenye mahitaji yote anapangiwa shule za vijijiini anakuta hakuna nyumba za walimu hata zikiwepo ni nyumba zisizokuwa na mahitaji yote jambo linalopelekea walimu wengi kukata tamaa kwenda vijijiini sababu ya tatizo hilo. Nyumba za wakazi huwa mbali sana na shule. Je, Serikali ina mpango gani wa kupambana na changamoto hii ya uhaba wa makazi ya walimu? Sababu mwalimu asipopata makazi mazuri hatakuwa na morali ya kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni madai ya walimu. Suala hili limekuwa ni jambo la kawaida kwa walimu kutolipwa stahiki zao kwa wakati. Kila mara tumeshuhudia walimu wakienda kudai fedha zao hawalipwi na madeni kuzidi kuwa makubwa. Tatizo lipo kwa walimu walipo kazini na wakistaafu bado wananyanyaswa. Zaidi ya wastaafu 1,000 wanadai shilingi bilioni 138 ambazo ni mafao ya michango yao kwa *NSSFna PSPF*. Je, Serikali ina mikakati gani ya kutenga fedha kwa ajili ya wastaafu hawa?

Tatu, ni kuhusu wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito wakiwa bado masomoni. Pamoja na kutenda kosa hilo lakini mtoto wa kike anaadhibiwa kwa kutoendelea na masomo wakati unakuta pengine aliyempa ujauzito wapo shule moja na anaendelea na masomo. Ni vizuri Serikali iliangularie suala hili kwa kuwaruhusu kuja kuendelea na masomo yao baada ya kujifungua lakini kuwe na *special school* kwa ajili yao ili wenzao wasije wakawanyanyapaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni kuhusu vyeti vya kughushi. Zoezi hili limewaathiri wafanyakazi wengi hadi kupelekea wengine kupata mishtuko ya moyo. Ni vizuri zoezi hili lingepangwa kwa madaraja, kuna wale walioghushi cheti kabisa, lakini kuna wale wametumia cha ndugu yake aliyeshindwa kuendelea kutoka darasa la saba na akaendelea kusoma na kufauli mpaka akapata *Ph.D. Aidha*, mtu huyu unakuta amefanya kazi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kama naunga mkono kutumia vyeti *fake*, lakini naishi Serikali iwe na jicho la huruma kuwasamehe na kuwalipa mafao yao. Kama Serikali iliweza kuwasamehe mafisadi wa *EPA* iweje ishindwe kuwasamehe hawa? Kwa nini Serikali iliifumbia macho dhambi hii ya kutumia vyeti *fake* na wahusika walioajiri watu hawa wamewajibishwa vipi?

Nashauri kwa wale wanaolalamika wameonewa basi Serikali ifungue milango kwa watu hawa kwenda kulalamika na Serikali iwastaafishe kwa manufaa ya umma na walipwe posho zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na vyeti *fake* pia kuna elimu *fake*. Unakuta mtoto anaingia kidato cha kwanza hajui kusoma, kuandika wala kuhesabu. Kuna vitabu vya kufundishia vinachapwa na makosa tunategemea nini katika elimu ya watoto hawa?

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii katika haya yafuatayo:-

- (i) Katika mgawanyo wa vitabu vya *History, Geography* na *English Book One* kwa kidato cha kwanza, Halmashauri ya Mpimbwe haijapata vitabu hivyo.
- (ii) Madai na madaraja ya walimu yashughulikiwe kwa haraka sana.
- (iii) Walimu wasaidiwe vifaa vya kufundishia kama *computers*.
- (iv) Vitabu vya kidato cha sita, vitabu vya *English* ni vitano tu.
- (v) Suala la uhamisho kwa walimu ni vema likaangaliwa upya na ikiwezekana wapangiwe maeneo yao kwa manufaa ya familia zao.
- (vi) Fedha zilizotolewa kama motisha kwa Halmashauri katika Mpango wa *P4R*, Halmashauri ya Mpimbwe, Jimbo la Kavuu haijapata fedha hizo.
- (vii) Mtaala wa elimu uangaliwe upya ili uwezeshe jamii kuendana na mabadiliko ya maendeleo duniani.
- (viii) Nakumbusha maombi yangu maalum niliyopatia Mheshimiwa Waziri. Naomba tusaidiwe wananchi wa Jimbo la Kavuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoa na timu yake kwa kuwasilisha hotuba nzuri na yenye kukidhi mahitaji na matakwa halisi ya Watanzania. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayoisha kwa mwaka huu kwa kiwango kikubwa sana imejitahidi kutekelezwa kulingana na uwepo na upatikanaji wa fedha. Pamoja na yote, naomba niongelee elimu bure. Mpango huu umeleta faraja na matokeo chanya kwa mtoto na mzazi wa Tanzania kwani umesaidia kuwepo na ongezeko la watoto wengi kuanza masomo kwa idadi kubwa. Mpango huu uendelee kuboreshwa sambamba na miundombinu yake, vifaa vyta kufundishia, motisha na maslahi stahiki kwa walimu na wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa madarasa ya shule za msingi, napongeza sana Serikali kupitia Wizara hii kwa kusaidia ujenzi wa vyumba vyta madara ya shule ya msingi Nyamajashi – Lamadi na shule ya msingi Fogo Fogo - Kabita katika Wilaya ya Busega. Msaada huu umefanikisha kupatikana vyumba na vyoo stahiki kwa wanafunzi ambao kwa muda mrefu ilikuwa ni kero na hasa kwa kukosekana kwa miundombinu hii. Naiomba Wizara iendelee kuweka mikakati na kuboresha shule nyingi katika Wilaya ya Busega ambayo ina idadi kubwa sana ya wanafunzi na uhaba wa miundombinu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na namwomba msaada zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji *high school*. Wilaya ya Busega haina *high school*. Napongeza sana msaada wa Wizara kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuanzisha shule ya A-Leve/Busega ambayo ni Mkula sekondari. Hadi sasa maandalizi yanaendelea vizuri na niombe tu Wizara ihakikishe masomo kwa wanafunzi watakaochaguliwa yanaanza. Sambamba na shule ya sekondari Mkula, naomba mwaka ujao wa fedha pawepo na mpango wa kuanzisha shule mbili zaidi za *A-level* kwani idadi kubwa sana ya wanafunzi hawapati fursa ya kuendelea

na masomo kwa michepwo mbalimbali. Nashauri pawepo pia na shule maalum ya A-level kwa ajili ya watoto wa kike (wasichana) ambao wamekuwa wakiathiriwa na mila potofu na kunyimwa fursa ya kusoma.

Mheshimiwa Waziri, kuhusu Chuo cha VETA, tumetenga eneo kwa iliyokuwa kambi ya ujenzi wa barabara ya Nyanguge - Musoma ya Sogesca kwa ajili ya uanzishaji wa Chuo cha Mafunzo Stadi kwa Vijana (VETA). Tunaiomba Serikali kukubali kuanzisha chuo hiki kwa kuwa baadhi ya miundombinu ikiwemo karakana, mabweni na madarasa viro tayari likiwemo na bwalo la chakula. Hii ni bahati nzuri na mpango nafuu licha ya faida pia eneo hili liko kandokando ya Ziwa Victoria, hivyo suala la maji na umeme tayari viro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, naamini Mheshimiwa Waziri atanikubalia maombi yangu na kuonyesha utayari wa kuyatekeleza ikiwemo ya yeye mwenyewe kuja na kutembelea Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Elimu ni ufunguo wa maisha, kila mtu atahitaji elimu ili aondoe ujinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa walimu, kuna shule nyingi katika nchi hii na mikoa mbalimbali zina uhaba wa walimu hasa walimu wa sayansi. Tatizo hili ni kubwa na hasa shule za vijiji kwa sababu walimu wengi wanataka kufundisha mijini kutoekana na matatizo yaliyoko vijiji, mfano, nyumba za kuishi, umbali wa shule na hawana vipando na kukosekana kwa miundombinu ya barabara au mwali muwanamke kuwa mbali na mume wake au mume kupangiwa kusomesha mbali na mke wake. Tunaomba maslahi yaboreshwe angalau waweze kujikumu na maisha. Walimu hawa wana kazi kubwa, sisi humu Bungeni tusingefika kama si kazi ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwaangalie sana walimu wenyewe tabia mbaya wanaoharibu wanafunzi kwa kuwapa mimba au kumpasisha mwanafunzi kwa kufanya naye ngono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo walimu wanawapa wanafunzi adhabu kubwa kupita kiasi. Kama vile mtoto kupigwa mpaka kupoteza fahamu au kupata ulemavu na wengine mpaka kuwapoteza maisha na wengine kutoroka shule au kufungiwa chumbani. Walimu hao watakapobainika wachukuliwe hatua zinazostahiki ili iwe fundisho kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto waliopata mimba mashulenii ni wengi na wengi wao ni wale waliokuwa hawana uwezo kwa kudanganywa na wanaume kwa kupewa *chips* au matumizi madogo madogo. Kwa hiyo, naiomba Serikali watoto wakibeba mimba warudishwe shulenii ili waendelee na masomo. Naomba waige mfumo wa Zanzibar. Pia naomba shule ziwe na mabweni ili kuwapunguzia watoto wa kike tatizo la kubakwa na kupata mimba zisizotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Serikali ambazo hazina matundu ya vyoo vijengwe vyoo na miundombinu ya maji kwa sababu watoto wa kike wanapokuwa katika siku zao wengi wanakosa masomo na hii ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naomba kuwasilisha.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa Taifa lilioloelimika ni Taifa bora kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari; kumekuwa na ongezeko kubwa la watoto wa kike kupata mimba na hivyo kusababisha kukatisha masomo yao. Watoto hao wa kike wanapokatiza masomo yao wanakwenda kuwa walezi wa watoto hali ambayo inawafanya waingie kwenye

umaskini na wengine kujiingiza kwenye ukahaba ili waweze kumudu kulea watoto wao. Hata hivyo, watoto hawa wanaweza kuingia kwenye hatari ya kupata maambukizi ya VVU na hivyo kuacha familia zao zikiwa na huzuni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visababishi vingi vya watoto kuingia kwenye kupata ujauzito nitavitaja vichache ikiwemo hali ya umaskini inayowakabili wanafunzi, hivyo, watoto wa kike hudanganyika kwa urahisi, umbali mrefu wa kutoka kwenye makazi yao kuelekea shulenii, shughuli zinazowazunguka watoto hawa wa kike mfano kuchota maji, kuokota kuni na kadhalika. Nashauri Wizara ilete muswada wa kubadilisha Sheria ya Mtoto ili mtoto wa kike akipata mimba aweze kuendelea na masomo ili kuwasaidia watoto hawa. Hii iende sambamba na adhabu kali kwa mtu yejote anayempa mimba mtoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya elimu, kumekuwa na changamoto kubwa ya miundombinu ya elimu mfano vyumba vya madarasa, mabweni, matundu ya vyoo ambavyo haviendani na kasi ya ongezeko la idadi ya wanafunzi na miundombinu ya shule au elimu. Darasa moja wanafunzi zaidi ya 60 hii haileti afya ya elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwiano katika wanafunzi na walimu, hili limekuwa ni tatizo kubwa sana hasa shule za Serikali ukilinganisha na shule za binafsi. Naomba Serikali na Wizara ijifunze kutoka shule za binafsi itasaidia kuboresha shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la walimu wa kufundisha viziwi na walemau kwa ujumla, kumekuwa na tatizo kubwa la walimu wa walemau kwenye shule zetu hivyo kupelekea watu hawa kukosa huduma muhimu ya kupata elimu sambamba na shule za ufundi na *VETA*. Mfano, shule ya *Moshi Technical* ilikuwa ikipokea walemau wengi na walisoma pamoja na kupata elimu ya ufundi jambo ambalo limewasaidia sana ambao hawakuweza kuendelea na elimu ya juu wameweza kujitegemea kwa kujajiri.

Nashauri Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kuona namna ya kuboresha shule ambazo zinatoa mchanganyiko wa elimu ya ufundi na kawaida ili kusaidia vijana wetu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo ya elimu ya juu; suala la wanafunzi waliokopa kurudisha mkopo ni la muhimu sana. Wasiwasi wangu ni namna ya urudishaji wa mikopo kwa wale ambao hawako kwenye mfumo rasmi wa ajira. Naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha anipe ufanuzi wa jinsi gani waliochukuwa mikopo ambao hawako kwenye mfumo rasmi wa ajira watarudisha mikopo hiyo ili kusaidia wahitaji wengine wa mikopo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya Kiswahili kwa kufundishia. Nakubaliana na matumizi ya lugha ya Kiswahili lakini wasiwasi wangu ni kama tunaweza kutumia Kiswahili. Kama hatutaweza kuklitumia mpaka elimu ya juu itakuwa ni changamoto kubwa sana. Nasema hivi kwa sababu lugha tunayoitumia kwa elimu ya juu ni Kiingereza hivyo italeta mkanganyiko kwa watoto hasa lugha ya Kiingereza wanapofika elimu ya juu. Nashauri tutumie lugha zote mbili kwa manufaa ya kibiashara na uchumi wa nchi yetu na Afrika Mashariki.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Nashukuru kwa fursa ya kuchangia hotuba. Naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa uongozi wake na maamuzi ya haraka katika kushughulikia changamoto za sekta hii. Ninawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Profesa Joyce Ndalichako na Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* na Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Maoni ya Kamati na Kambi ya Upinzani na ya Waheshimiwa Wabunge wote waliota maoni mazuri yanayoletea kuboresha sekta hii kwa ajili ya kujenga uwezo wa Taifa hili, kumudu weledi na rasilimali watu ya kutosha, ushindani wa soko na kuboresha

kiwango cha elimu inayotolewa nchini. Naomba mchango wangu ufanyiwe kazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata elimu bora ni msingi wa maendeleo ya mtu binafsi na kijamii na kiuchumi popote pale duniani. Kwa upande wa Tanzania, naipongeza Serikali ya CCM kwa jitihada zake za mwaka hadi mwaka za kuungeza fursa ya elimu sawa kwa wote na utoaji wa elimu bora ya msingi, sekondari na ngazi ya elimu ya juu, hili ni jambo la msingi ili kufikia malengo makuu ya maendeleo endelevu. Isitoshe, jamii iliyoelimika vizuri ni kiini cha kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali kwa uwiano wa usawa na pia kustawisha utawala bora. Ijapokuwa Tanzania imepata maendeleo makubwa katika kutoa elimu ya msingi, bado kuna upungufu mkubwa katika suala la ubora wa elimu wanayopata watoto. Kukaa shuleni hadi kumaliza darasa la saba pia ni tatizo sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia elimu ya mtoto wa Kitanzania kama mkakati wa kujenga rasilimali watu yenye uwezo mkubwa wa kushindana katika soko la ajira na kufanya kazi kwa tija, tunaitaka Serikali izingatie yafuatayo na kuyafanya kazi:-

Moja, malezi ya mtoto miaka ya awali hadi kufikia miaka mitano. Malezi na makuzi ya mtoto yanahuisha pande zote za mambo yanayoweza kumfanya mtoto akue vizuri tangu umri mdogo, ujana hadi utu uzima. Kwa hiyo, masuala ya afya ya mtoto tangu akiwa tumboni, anapozaliwa hadi anapobalehe, utu uzima na uzee, elimu ya mtoto huyu tangu anapozaliwa hadi uzeeni ni muhimu. Ndiyo maana ni vizuri Serikali ikafanya kazi kama kitu kimoja ili kujenga misingi ya kumletea elimu mtoto mwenye afya njema kiakili na kimwili. Maendeleo ya mtoto kuitia ngazi zote hizi ndiyo msingi wa maendeleo mengine yote yanayofuata katika maisha ya mtu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu huduma za awali za mtoto kiafya, vituo vyat kulelela watoto na shule za awali ni sehemu muhimu ya maendeleo ya mtoto kiakili. Pia

inasaidia wazazi kupata nafasi ya kufanya shughuli nyingine za maendeleo ya familia. Vituo hivi vinawezesha watoto kuchanganyika na wenzao kwenye michezo mbalimbali na mafunzo mepesi yanayojenga uelewa, utambuzi na hata hisia zao juu ya masuala tofauti. Kipindi hiki ni muhimu kwa mtoto, kwani kinamtayarisha kwa shule rasmi na wanapokuwa tayari kwenda shule ukifika umri wa kwenda shule wanakuwa wachangamfu, wanakuwa rafiki zaidi na kujiamini zaidi. Wanakuwa na mahusiano mazuri na wenzao, ujuzi wa lugha na watakuwa na mawasiliano mazuri. Watoto walio tayari kwenda shule wana nafasi kubwa zaidi na kufanya vyema kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliwahi kueleza Bungeni kuwa mahitaji halisi ya madarasa ya awali ni 16,014 ambayo ni sawa na idadi ya shule za msingi zilizopo nchini kwa sasa. Shule zenyé madarasa ya awali ni 14,946 ambazo ni sawa na asilimia 93.33 ya mahitaji. Hivyo, shule za msingi 1,068 hazina madarasa ya awali. Tunapenda kufahamu sasa kama idadi hii imeongezeka?

Takwimu za Serikali zimeainisha idadi ya walimu wa shule za awali kiwilaya. Je, walimu hawa wanasomea kufundisha watoto hawa? Je, idadi yao inatosheleza mahitaji? Kama siyo, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatoa walimu wa kutosha kwa kila kijiji kuwa na shule ya awali? Naomba Serikali ije na mkakati wa shule za awali kila Wilaya kama ilivyo kwa zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa Serikali itoe motisha kwa sekta binafsi kuhakikisha kuwa kila sehemu ya kazi au kiwanda au shamba kubwa la kibiashara linakuwa na kituo cha kulea watoto na vilevile kuwe na ramani za jinsi vituo hivi vitajengwa ili kuzingatia usalama wa watoto na upatikanaji wa huduma muhimu kwa mtoto, yaani kusoma, kucheza, kula chakula bora, kupumzika na kujisaidia. Hii itawafanya wazazi hata wa vijijini kuwa na imani kwenda kuwaacha watoto kwenye vituo hivi ili wao wakaendelee na shughuli nyingine za maendeleo, watoto wapate fursa ya kujifunza na kucheza na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chakula na lishe bora shulen; ipo haja ya Wizara za Elimu, TAMISEMI, Maji na Fedha kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha huduma zote zinazoainishwa kwenye hotuba hii vinafanikiwa, ikiwa ni pamoja na kuanzisha mpango wa kuwalisha watoto shulen. Tunafahamu kuwa mpango huu uko katika hatua za awali na tayari baadhi ya shule zimeshaanza kupelekewa chakula kwa ajili ya kuwalisha watoto na kampeni za uhamasishaji kwa familia juu ya umuhimu wa lishe bora kwa watoto shulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa shule ambazo chakula kinatolewa, basi kiandaliwe vizuri na kiwe na lishe bora na kiandaliwe katika mazingira yanayoridhisha ili kuwaweka watoto katika hali ya afya njema. Tuna wajasiriamali wengi wanaotengeneza majiko mazuri yanayofaa kutumika kwenye taasisi mbalimbali wapewe *tender* za kutengeneza majiko kwa ajili ya shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla watoto wanataka kuona mabadiliko na maboresho kwenye maeneo ya lishe ya mama na mtoto na watoto wote kwa ujumla kwa kuhakikisha kuwa uhakika wa chakula unakuwepo, kuendeleza tabia ya mazoea ya kula chakula chenye lishe bora na kuelimisha watoa huduma kuhusu tabia ya kula chakula chenye lishe bora na kuelimisha watoa huduma kuhusu tabia ya kula chakula chenye virutubisho vyote vinavyohitajika mwilini na njia bora za kuandaa chakula chenye lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mapendekezo yafuatayo ili kulinda haki za watoto na kufanikisha eneo la pili mionganoni mwa maeneo kumi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa Serikali na misaada mbalimbali, Wizara zinazohusika na masuala ya lishe kama vile Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu zitenge rasilimali na fedha za kutosha ili kuboresha lishe shulen na katika familia. Pia Wizara hizi zihakikishe kuwa sheria husika zinatungwa na taratibu na viwango vinawekwa ili

kuhakikisha upatikanaji wa vyakula vilivyo sindikwa na vyenye lishe bora vinapati kana na kusambazwa kwa wingi nchini na kuwafikia walaji ili kuwakinga watoto na magonjwa kama yale ya utapiamlo na unyafuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mheshimiwa Rais akutane pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ili kujadili mikakati itakayofanikisha suala zima la kuratibu upatikanaji wa lishe bora katika jamii zetu. Serikali iwajibike kuanzisha programu mahususi za kusaidia familia moja moja kupata uhakika wa chakula na hivyo kufanikisha tabia ya kula chakula chenye lishe bora (kwa mfano kampeni ya nchi ya Rwanda ya kugawa ng'ombe mmoja kwa familia moja ambapo kila familia maskini hupewa ng'ombe mmoja wa maziwa kwa ajili ya lishe bora ya watoto).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuamsha na kuendeleza ufahamu kuhusu lishe bora kwa watoto; watoaji huduma, wazazi na jamii kwa ujumla, inapaswa kuelimishwa kuhusu uhakika wa chakula na masuala ya lishe kwa watoto kama vile njia bora za kutumia rasilimali chache zilizopo, uandaaji na ulaji wa chakula chenye virutubisho vya kutosha na utaratibu mzuri wa kulisha watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee lishe kama sehemu ya huduma ya afya. Zahanati na vituo vya afya viwe vinatoa taarifa na elimu kuhusu lishe bora kwa watoto na wajawazito na hata kwa wanawake wenyewe watoto wachanga pamoja na kutoa tiba ya kutosha na yenye kukidhi mahitaji ya watoto wachanga wanaosumbuliwa na magonjwa yanayotokana na lishe duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu katika kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwa wote; iko haja ya kuweka utaratibu au programu za kudhibiti bei za vyakula ili kupunguza uwezekano wa kupandishwa kwa bei hizo kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kupanua wigo wa

programu za chakula kwa watoto shulenii kwa kuongeza fedha na rasilimali nyingine husika ili kuongeza idadi ya shule zenye kutoa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya usafi na usalama shulenii yako kwenye hali mbaya, ya chini kabisa, tofauti na miongozo iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Ufundii, licha ya juhudii za Serikali za kuongeza vyumba vya madarasa pamoja na idadi ya shule za msingi, inaelekeea mkazo mdogo sana umewekwa kwenye vyoo. Bado vyoo visafi na vyenye usalama kiafya ni muhimu kwa kujenga mazingira rafiki ya kufaa kwa kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za Serikali Tanzania za elimu ya msingi zinahitaji miundombini bora na ya kukidhi mahitaji ili kuboresha mazingira na uwiano mzuri wa idadi ya wanafunzi na matundu ya vyoo yaliyopo shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya vyoo; shule zilazimike kuweka kipaumbele kukarabati miundombini na kuboresha usafi wa vyoo na matundu ya vyoo yaliyopo shulenii ili kuepukana na maambukizi ya magonjwa. Pia kuweka mifumo mizuri ya kumudu takataka zinazozalishwa shulenii ili kuepukana na uchafuzi wa mazingira na kufurika kwa vyoo. Ukosefu wa huduma ya maji shulenii mara nyingi husababisha watoto kuwa watoro shulenii na maji machafu husababisha kuenea kwa magonjwa. Kwa hiyo, inapendekezwa kuhakikisha kwamba maji safi na yanayofaa kwa kunywa yanapatikana kwenye shule zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiwango cha usafi wa mazingira na afya shulenii; shule zote lazima zikaguliwe na kuwajibika kwa lolote lile linalohusika na mazingira machafu na hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina wajibu wa kusaidia shule aidha kwa kutenga fedha au kuzipatia rasilimali nyingine ili kutatua tatizo la mazingira machafu na hatarishi hasa kwa shule za Serikali zilizoko vijijini ambazo zinategemea mgao wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi pia zinakabiliwa na ukosefu wa maji safi na salama ya kunywa pamoja na viwanja nya michezo. Matundu ya vyoo na vyoo, upungufu uliopo ni kwenye kubuni michoro, kujenga na kutunza vyoo vilivyopo shulenii. Tunasisitiza kuwa vyoo vilivyopo havifai na ni vichafu kwa matumizi ya watoto. Isitoshe, kuna upungufu wa vyoo na matundu ya vyoo unaosababisha mistari mirefu ya watoto katika kutumia huduma hiyo na kuwachukulia muda wa kuwa darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi wanazopata watoto ni kutokana na umbali wa vyanzo nya maji kutoka majumbani mwao. Umbali mrefu unaathiri jukumu la kusoma na mara nyingi wanachelewa au kutokwenda kabisa shulenii kutokana na uchovu. Zaidi ya hayo, suala la usalama wakiwa wanaenda kuchota maji kwa kuzingatia kuwa njia ya vichochoro wanavyopitia siyo salama kwa watoto hasa wasichana ambao huwa na hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhaba wa maji; kaya na jamii nyingi zina upungufu wa huduma ya maji na zina mfumo mbovu wa usambazaji wa maji kama vile mabomba yaliyovunjika, hivyo hulazimisha kaya kununua maji kwa bei ghali kutoka kwa wachuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukosefu wa usawa wa jinsia; wasichana mara nyingi wanatumwa kwenda kuchota maji na wanalazimika kutembea masafa marefu kutafuta maji hayo, wakati wavulana wanaruhusiwa kwenda shule. Jukumu hili la kutafuta maji mara nyingi huwaweka wasichana kwenye hatari ya kunyanyaswa na kudhalilishwa kijinsia na hata kubakwa na watu wasiowajua wakati wakiwa njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza uwekezaji kwenye elimu ya awali kwenye maeneo yafuatayo; moja, makuzi ya awali ya maendeleo kiakili ya watoto. Nashauri wazazi/walezi na Wizara husika kubuni na kutekeleza shughuli mbalimbali zinazowawezesha watoto kukua kimaumbile na kiakili kwa kuanzisha shule za ziada za awali na kuwahusisha

watoto kwenye shughuli za kuchangamsha akili, kutambua na kukuza vipaji na kukuza lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya mama na mtoto baada ya uzazi inahitaji kuboreshwa hasa kwa kupima, kinga na tiba kwa magonjwa sugu ya watoto na kupanua wigo wa huduma ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata chanjo na kinga kwa magonjwa mbalimbali. Utengaji wa bajeti ya kuwekeza kwenye miradi na mipango ya malezi na makuzi kwa watoto pamoja na ile inayosimamiwa na Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ili kuongeza msisitizo na mwonekano Kitaifa na kikanda wa suala hili la makuzi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu ubora wa elimu; ufundishaji shulenii bado si wa kuridhisha nchini kote. Kuna changamoto katika mtaala iliyopo pamoja na mbinu za ufundishaji ambazo hazina mwelekeo mzuri utakaowajenga watoto kupata ujuzi wa kutosha wa kuchambua mambo na kuwa wabunifu na uthubutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa walimu; mgawanyo wa walimu waliopo hauridhishi na husababisha shule nydingine kuwa na upungufu mkubwa zaidi. Isitoshe, pamoja na kwamba walimu wapo, mara nydingi wanakosa motisha na ari ya kufundisha na matokeo yake ni kutokufanya vizuri kwa watoto kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wenye ulemavu na wasichana hawapati elimu sawa na watoto wengine kutokana na mila na desturi ambazo zinawabagua. Vilevile makundi haya mawili hayathaminiwi na jamii zao ambazo huwapatia wavulana kipaumbele. Hali duni ya miundombinu shulenii/vifaa; shule zilizo nydingi hazipati mgao wa kutosha wa rasilimali na zimejengwa vibaya, hivyo kuyafanya mazingira ya kufundishia na kusoma kuzorotesha ufanisi katika kutoa elimu bora. Pamoja na hayo, shule nydingi hazina vyumba vya madarasa vya kutosha au vifaa vya kutosha kufundishia (karatasi, vitabu na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine kubwa inayosababisha mahudhurio hafifu ya watoto shulenii umbali mrefu wanaohitajika kutembea kwenda shule. Zaidi ya hayo, njia nyingine wanazopitia ni hatarishi hasa kwa wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuna umuhimu wa Serikali kufanya maboresho katika sekta ya elimu kwa kuwa na walimu bora wenye ujuzi na ari ya kufundisha ili kuleta ufanisi. Uwekezaji zaidi uongezwe katika kuboresha elimu iliyotolewa shulenii hasa kwenye shule za Serikali na zile zilizoko vijiji ambazo zimesahaulika kupita kiasi. Mafunzo zaidi kwa walimu yapewe kipaumbele na kuongeza vifaa shulenii kama vile vitabu, karatasi, kwa shule zote na siyo tu zile za watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni utoaji elimu bure kwa wote. Mazingira ya shule yaboreshwe ili kuvutia na kuwa toshelezi na rafiki kwa watoto wote ikiwa ni pamoja na wasichana na wale wenye ulemavu ili kukwepa ubaguzi na maendeleo hafifu shulenii.

Kuhusu ukaribu wa shule na huduma ya usafiri; wakati wa kuchagua sehemu za kujenga shule mpya, umbali watakaotembea watoto kwenda shule na ukaribu na shule vizingatiwe. Pamoja na hayo, njia za kwenda shule lazima zichaguliwe vizuri na kuchunguzwa ili kuwalinda watoto dhidi ya watu wenye nia mbaya na hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuzuia mimba za utotoni, fursa ya kupata huduma za afya ya uzazi; juhudii zifanyike kutoa fursa zaidi kuwawezesha wasichana kupata huduma za afya ya uzazi katika maeneo yao wanapoishi na katika vituo vya afya/kliniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kuhusu mimba za utotoni shulenii, elimu ya afya ya uzazi isiishie tu katika ngazi ya shule za sekondari bali ipelekwe pia katika shule za msingi na katika Vituo vya Maendeleo ya Jamii ili kuwafikia wasichana ambao wako nje ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria na sera kuhusu suala la ngono kwa watoto hazitekelezwi ipasavyo wala kufuatiliwa kwa karibu ndani ya jamii nyingi. Juhudi zaidi zinahitajika kwa vyombo na watu wanaohusika na usimamizi wa sheria kuwajibika kufuatialia kwa makini na kupeleka Mahakamani kesi za kubaka, ngono za kulazimishwa na za kulipia kwa watoto na kuhakikisha wavunjaji wa sheria au wakosaji wanaadhibiwa vikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu wa usafiri wa wanafunzi, shule lazima ziwekeze katika mfumo na utaratibu mzuri wa usafiri kwa watoto badala ya kutegemea usafiri wa umma ambao huwaweka wasichana katika hatari ya kudhalilishwa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto waathirika wa mimba za utotoni na elimu; wasichana wanaoacha shule kwa sababu ya ujauzito waruhusiwe kurudi shulenii kumalizia masomo baada ya kujifungua. Shule lazima ziwhamasishe hawa wazazi ili watoto warudi shulenii na kuepuka kuwafukuza kwa kisingizio tu cha hali yao ya ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukomesha ndoa za Utotoni. Tunaamini kuwa mimba za utotoni ni chanzo kikubwa cha ndoa za utotoni na tunasisitiza na kuhimiza kuelimisha jamii kuhusu hatari na madhara ya matokeo ya mimba za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatili dhidi ya watoto ni kitendo cha kuvunja haki za binadamu na tatizo la kijamii na kiafya lenye madhara makubwa. Ukatili unaondoa nguvu ya misingi mikubwa ya malezi ya watoto ambayo watoto wanahitaji ili kukua na afya na maisha yenye tija na pia ukatili unakiuka haki za msingi za watoto kupata ulinzi. Matatizo mengi yanayowakumba watoto humu Tanzania ikijumuisha kazi zinazowanyonya watoto, kuwasafirisha watoto kwenda kufanya kazi hatarishi za kuuza miili yao na ukatili wa kijinsia yanaathiri vijana zaidi ya watoto wadogo. Mara nyingi asasi zile zile na hata watu binafsi ambao wanategemewa kuwalinda watoto kama vile walimu, polisi, familia zenyewe

zimetajwa kuwa zinahusika kuendeleza ukatili dhidi ya watoto na udhalilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla watoto wanahitaji ulinzi dhidi ya ukatili na aina nyingine za unyanyasaji. Sheria kuhusu kazi ngumu kwa watoto na adhabu kali za wakosaji ambao wanakiuka na kuwafanya watoto ukatili yashughulikiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo katika kulinda haki ya mtoto na kufanikisha utekelezaji wa eneo la tisa la uwekezaji:-

Moja, Sheria za Ajira ya Watoto na Sera. Serikali za Mitaa na wadau wengine wakuu lazima wawajibike katika kusimamia utekelezaji wa juhudzi za kulinda haki za watoto. Serikali za Mitaa pia lazima kuongeza uelewa na kujilmarisha ili kumudu kwa ufanisi kusimamia kazi ya utetezi na ulinzi wa haki za watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; nashauri Serikali kuandaa mfumo wa ufuutiliaji wa ulinzi wa haki za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi hasa wale wanaoishi mitaani. Hii itasaidia wanajamii na viongozi wa Serikali za Mitaa kuchukua hatua za kupima maendeleo yaliyofikiwa katika kukomesha ukatili na udhalilishaji wa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makazi ya muda au makazi salama; watoto pia walipendekeza kuanzishwa makazi au vituo vya muda vya kutosha kulelea watoto wanaoishi mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa sheria; kutokana na ongezeko la ukatili kwa watoto, ajira za watoto na unyonyaji, watoto walipendekeza kusambaza sehemu zote nchini nakala ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wenye ulemavu; nchini Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine

zinazoendelea na pamoja na kuwepo kwa sheria nzuri zinazolinda watoto, watoto wenyе ulemavu, wanapata taabu sana wanapajaribu kuchukua fursa za kupata huduma mbalimbali kama vile huduma za afya, elimu na huduma nyinginezo wanazopata watoto wengine. Uelewa mdogo kuhusu ulemavu na fikra potofu za jamii kuhusu ulemavu na watu wenyе ulemavu ni miongoni mwa vipingamizi ambavyo vinasababisha kupoteza fursa ya kuleta usawa miongoni mwa watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ulemavu, kimsingi kuna haki ya msingi ya maisha na hali za watoto wenyе ulemavu kuboreshwa hasa kwenye sera za shule na miundombinu na kujenga mazingira rafiki shulenı ambayo hayatakuwa tena na ubaguzi wala unyanyapaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu rafiki shulenı pamoja na majengo na madarasa ni muhimu yajengwe kwa kuzingatia kuweka sehemu maalum za kupita, alama maalum, vyoo maalum na aina nyinginezo za ujenzi unaokidhi mahitaji ya watoto wenyе ulemavu wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria na sera zinazowalenga watoto wenyе ulemavu lazima zisambazwe kwa watu wengi ili zifahamike na kufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matengo ya Bajeti na rasilimali zaidi lazima zitengwe kwa ajili ya watoto wenyе ulemavu ili kufanikisha utetezi na ulinzi wa haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri Serikali iongeze uelewa wa jamii kwani wale wenyе ulemavu wa mtindio wa ubongo mara nyingi wanaeleweka vibaya na chanzo cha matatizo yao kubahatishwa tu (kwa mfano kudhaniwa kuwa wamerogwa) na hivyo jamii inahitaji elimu ya ufahamu ili kubainisha, kutofautisha na kuelewa aina mbalimbali za ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa watoto

wenye ulemavu shulenii; jamii husika na shule ziwajibike kuhakikisha kuwa watoto wote wenye ulemavu wanaandikishwa shulenii na kushiriki katika ngazi zote muhimu za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaomba maoni haya yaingizwe kwenye mipango ya Wizara ili kidogo kidogo yaanze kufanyiwa kazi na mpaka mwaka 2020 tutakuwa tumepeiga hatua kubwa. Mungu awatie nguvu Waheshimiwa Mawaziri wote wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuimarisha elimu na ushiriki wa wazazi na jamii. Wazazi na jamii kwa ujumla ni wadau muhimu sana katika kusimamia suala la upatikanaji wa elimu bora. Ni vizuri tuwape fursa ya kutoa michango yao ya kimawazo.

Vilevile wazazi na jamii wanatakiwa waelewe majukumu yao kwa ufasaha juu ya mchango wao kwenye elimu, kwa mfano kuchangia chakula shulenii, ujenzi na kadhalika. Wanafunzi wana haki zao za msingi wanapokuwa shulenii ikiwa ni pamoja na haki ya kulindwa, haki ya kupata elimu bora, kutobaguliwa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naiomba Serikali ijenge mabweni katika shule. Hii itasaidia wanafunzi wa kike kutobakwa njiani wanapokuwa wanaenda shule. Wakati umefika Tanzania kuwa na bodi maalum ya kusimamia sera za elimu. Kuna baadhi ya wazazi wanawashawishi watoto wao wasifanye vizuri kwenye mitihani ili *wa-fail* wapate kuolewa au wanakuwa hawana uwezo wa kuwasomesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iongeze bajeti ili kuboresha elimu. Pia Serikali ihakikishe kwamba wanafunzi wanapata chakula bora shulenii. Hii inawapa vishawishi watoto kwenda shule na kuwa na akili kwa sababu wanakula chakula bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ijenge madarasa ya kutosha; lakini pia katika shule zetu kuna upungufu wa vyoo vya wanafunzi na baadhi ya shule kukosa walimu wa kike. Je, ni lini Serikali itaboresha na kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora katika Shule za Umma ambazo ndizo zinazowahudumia wanafunzi wengi katika Taifa hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya walimu wanaofundisha katika shule za pembezonii wanaishi katika mazingira magumu. Hawana miundombinu, hawana makazi mazuri kwa ajili ya kuishi na miundombinu ambayo siyo rafiki kwao. Kwa sasa fani ya ualimu siyo wito ni ajira kama ajira nyingine. Ni vizuri kuajiri walimu wenyewe sifa ya ualimu wenyewe weledi. Siyo ualimu kwa ajili ya mshahara. Vilevile kuna upungufu wa ofisi za walimu. Baadhi ya walimu kukosekana mafunzo shulenii (kazini) lakini pia kutopandishwa madaraja; walimu kutolipwa kwa wakati, stahiki zao, (walimu wanaohamishwa, kustaafu, pesa ya usafiri).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo ya elimu ya juu (vyuo vikuu); Serikali inapaswa kutekeleza kwa vitendo mkataba wa utoaji nafasi sawa ya elimu kwa wote. Serikali inatakiwa kuhakikisha kuwa elimu inakuwa 6% ya pato la ndani. Tanzania hajjaweze kufikia lengo hilo kwa miaka mitatu mfululizo ambapo bajeti yetu ya elimu ni 17%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba bajeti iongezeke ili kumudu gharama za udhamini wa wanafunzi wote nchini wenyewe sifa ya kudahiliwa katika vyuo vikuu. Kwa kuwa elimu ni haki ya msingi ya kikatiba ni vyema Serikali iache sera ya kibaguzi ya kuhusisha wazazi kuchangia elimu ya juu ambayo mpaka sasa imekuza tabaka la wasionacho na wenyewe nacho kwa ubashiri unaofanywa na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utambuzi wa wanafunzi wenyewe sifa ya kupata mikopo, kwa mfano; takwimu za mwaka 2015/2016 ni wanafunzi 21,500 ambayo ni asilimia 24 tu katika wanafunzi wote 88,000 wenyewe uhitaji wa mikopo walidhaminiwa mikopo. Wanafunzi asilimia 76

hawakudhaminiwa mikopo. Serikali inapaswa kutekeleza kwa vitendo utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu bila ubaguzi wowote, kwani kila mtu ana haki ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile robo tatu ya wanafunzi wahitaji wanakosa mikopo na siyo kwa sababu hawana sifa ni kwa sababu ya usiri uliopo Bodi ya Mikopo. Naiomba Serikali kuitia Bodi ya Mikopo kuweka utaratibu endelevu wa kukusanya fedha za mikopo kwa wanufalka waliodhaminiwa mikopo ili kuongeza wigo wa kuwadhamini wanafunzi wa vyuo vikuu nchini na siyo kukusanya fedha kwa nguvu na kinyume cha sheria kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepandisha makato kutoka asilimia nane hadi 15 ili kuharakisha makusanyo ya mikopo kinyume na utaratibu na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kodi kwenye shule binafsi, Serikali ipunguze kodi kwenye shule za *private* kwa sababu shule hizi zinasaidia Serikali. Vilevile shule hizi za *private* zifanyiwe ukaguzi mara kwa mara kwani kuna baadhi ya shule zinakiuka maadili (hazipo kwenye viwango) na Serikali ihakikishe wanafunzi wa shule za *private* wanapewa mlo ulio kamili, kwani wazazi wanakuwa wanalipa ada nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu ya watu wazima bado ni tatizo. Watanzania wengi ambaao wanaishi pembezoni hawana elimu. Waelimishwe kuhusu suala la elimu na faida zake. Watu wazima wakipatiwa elimu itasaidia kupunguza umaskini na ujinga katika nchi yetu. Ni vizuri Serikali irudishe mfumo kama wa zamani. Jioni watu wazima wapatiwe elimu kama ilivyokuwa kipindi cha nyuma wanafunzi wakitoka shule jioni wanaenda kusoma watu wazima.

MHE. ELIAS J. KWANDIKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha VETA Ushetu, nchi yetu imekuja na dhamira ya kuifanya Tanzania iwe nchi ya uchumi wa katni na nchi ya viwanda. Hii itafanya wananchi kupunguza hali ya umaskini. Pia kufanikiwa ajenda hii, jitihada zifanyike ila siyo tu kutoa ajira hususan kwa vijana bali ni kuhakikisha nguvu kazi inatumika kwenye uzalishaji. Hivyo kunahitaji vijana wetu wawe na *skills* za kutosha kutoa mchango wao muhimu kwa ukuaji wa uchumi. Hivyo tunaomba Serikali yetu itujengee Chuo cha VETA katika Halmashauri ya Ushetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushetu inazo fursa za kutosha kufanya chuo hicho kilete tija kwa kuwa eneo hili ni kiungo kwa vile tunapakana na mikoa mitatu ya Geita, Kigoma, Tabora pamoja na Shinyanga yenyewe. Ni rahisi wananchi wa mikoa hii kufika Ushetu.

Pili, Ushetu kunapatikana rasilimali za kutosha za mazao ya misitu, mazao ya kilimo na kadhalika.

Tatu, Ushetu kunapatikana ardhi ya kutosha ambayo haina gharama. Wananchi wake wanao ushirikiano na wanajituma na wanapenda sana maendeleo.

Mhehimiwa Spika, namalizia kwa kusema tunomba sana Chuo cha VETA haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kuwarudisha watoto wajawazito waliojifugua shuleni; turejee mifumo ya elimu duniani yaani *formal education* na *non-formal education*. Fursa ya elimu kwa waliopata ujauzito ipo kupitia *non-formal*. Serikali iimarishe *non formal system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lugha ya kufundishia; Sera ya Lugha ya Kufundishia inakinzana na ukuzaji wa fikra za kibunifu na kujiamini. Kiswahili kama lugha ya kwanza

kwa walio wengi ndiyo lugha sahihi ya kufundishia. Kiingereza na lugha nyingine zibaki kuwa masomo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuta ujinga au kuongeza idadi ya wanaojuu kusoma na kuandika, Serikali izingatie umuhimu wa kuwa na Taifa lilioelimika kwa kuwatazama wasio na fursa ya kujunga na *formal education*. Inakadiriwa watu milioni sita hawajui kusoma na kuandika. Hii ni hatari kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya mitaala, kuna umuhimu wa kuimarisha dhana ya uzalendo ndani ya somo la uraia. Watoto au Watanzania wajifunze kuwa kuzaliwa Mtanzania ni jambo bora zaidi kuliko kuzaliwa mahali popote pale duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wajifunze falsafa hususan kipengele cha namna ya kufikiri (*systemic and systematic thinking*)*logical reasoning* na kadhalika.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa kutoa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari ('O' level).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu idadi kubwa ya kujunga na shule za msingi; watoto wameongezeka kwa idadi kubwa sana. Hii imepelekea pia ongezeko la watoto wa sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali na Waheshimiwa Wabunge kwa kununua madawati kwa shule za msingi. Sasa watoto wetu wanasoma vizuri wakiwa wanakaa kwenye madawati. Pongezi kwa kujenga maabara kwa shule za sekondari; pongezi kwa Serikali kwa kuongeza mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Serikali:-

(a) Serikali iongeze kujenga *hostel*/kwa ajili ya watoto wa shule za sekondari ili kupunguza umbali kwa watoto;

- (b) Kuongeza idadi ya walimu hasa walimu wa masomo ya sayansi kwa shule za sekondari;
- (c) Kuongeza nyumba za walimu;
- (d) Kuongeza kujenga madarasa na ofisi kwa ajili ya walimu wetu;
- (e) Posho iwepo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari;
- (f) Kuongeza mishahara kwa walimu wote wa shule za msingi na sekondari; na
- (g) Kuboresha mazingira ya walimu, kwa mfano, nyumba kuwekewa umeme, maji yawepo shulenii, vifaa vya kufundishia viwepo, usafiri wa shule uwepo kwa kila shule ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu kwa umuhimu wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima kufika siku ya leo. Vilevile nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kupunguza changamoto za madawati nchini na kutoa elimu bila malipo ya ada toka shule ya chekechea mpaka shule za upili kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya utangulizi huu nianze kutoa mchango wangu na ushauri kwa Serikali. Halmashauri ya Morogoro ina ukubwa zaidi ya kilometra za mraba 11,700 na umbali zaidi ya kilometra 180 toka Morogoro Mjini na shule ya kwanza ya sekondari ilijengwa mwaka 2000 na nyiningine wakati wa ujenzi wa shule ya kata mwaka 2006 lakini hatuna shule ya fani hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Morogoro ina changamoto nyingi hasa ya miundombinu na uwezo mdogo wa mapato. Ili kukabiliana na changamoto hizo naiomba Serikali Kuu itusaidie katika ujenzi wa shule ya kidato cha tano na sita katika shule ya kata ya Mkuyuni, Ngerengere ama Nelson Mandela ambazo ni makao makuu ya tarafa za Mkuyuni, Ngerengere na Mikese kama zilivyofuatana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kudhibiti utoro na mimba za utotoni; kutokana na takwimu za *BEST 2016* za utafiti wa kufahamu sababu mbalimbali za wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kuacha shule mwaka 2015 ni vifo, mimba na utoro. Kutokana na takwimu hizo, mchanganuo wake ni kama ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujauzito ni 3,637; utoro, 139,866 na vifo ni 3,917. Kutokana na takwimu hizo, utoro ni chanzo kikubwa cha watoto kuacha shule, ni zaidi ya 94% kuliko hata ujauzito. Katika hawa wapo watoto wa kiume na wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kuja na mkakati maalum kama ule wa ujenzi wa shule za kata na wa utengenezaji madawati nchi nzima, kumaliza ujenzi wa mabweni katika shule zote za kata ndani ya miaka miwili ili kukabiliana na tatizo la utoro na mimba za utotoni; kwa watoto kuishi shuleneni chini ya uangalizi wa walimu na waangalizi wao wawapo mashuleneni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe mwongozo shule zote za kata kujenga mabweni katika shule za kata kwa kutenga fedha katika bajeti zao na kushirikiana na wadau wa maendeleo na wananchi wa sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Halmashauri wapewe mwongozo na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika kusaidiana na wadau kumaliza tatizo hili la utoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nataka kutoa ushauri pia katika ujenzi wa maktaba katika kila Wilaya na Tarafa nchini ili kukabiliana na changamoto ya kushuka kwa ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Afrika ikiwemo Tanzania, tuna tatizo kubwa kama Bara na kama nchi kwamba watu wengi hawapendi kusoma na kujifunza ili kupata uelewa na maarifa mbalimbali kutakakowezesha watoto kufanya vyema katika mitihani na pia mtu wa kawaida kupata uelewa wa kukabiliana na mambo ya kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wenzetu wa mataifa ya nje wanatuambia ukitaka kumficha kitu Mwafrika weka vitu katika maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata vijana na wanafunzi wengi wanasona kwa ajili ya kufaulu mitihani na siyo kupata uelewa na ufahamu wa somo ama kwa kutopenda kusoma au kukosekana kwa miundombinu ya kujisomea na hata shule zetu zinakosa kuwapa mazoezi na mitihani ya mara kwa mara wanafunzi kwa kukosa miundombinu ya vifaa vya kuandalia mitihani hiyo mingi kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ili kuinua elimu yetu na kujenga utamaduni kwa watoto kupenda kujisomea tangu wakiwa wadogo. Kwa kuzingatia uwezo mdogo wa Serikali wa kujenga maktaba katika kila kata; na kwa kuwa hakuna vitendea kazi vya kuandaa mitihani ya majaribio katika shule nydingi za umma; hivyo basi, naishauri Serikali yangu kuja na mkakati wa kujenga maktaba katika kila Wilaya na Tarafa ili zitumike kwa kujisomea. Hii itawasaidia watoto wa shule za msingi na sekondari katika tarafa husika na jamii husika, pamoja kutumia majengo hayo kama kituo cha elimu, mafunzo na miundombinu ya kuandaa mitihani, kuichapisha na kupeleka katika shule ya eneo lake kutohana na mahitaji ya shule husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kujenga maktaba

na vituo vya elimu kwa jamii katika kila makao makuu ya tarafa, itasaidia sana kujenga utamaduni wa kujisomea kwa watoto wetu na jamii kwa ujumla, pia kupunguza gharama za kuandaa mitihani ya majaribio na ushindani kati ya shule kwa shule, kata kwa kata na tarafa kwa tarafa ili kuongeza uelewa na uwezo wa vijana wetu kuelewa masomo yao na kuijandaa vyema kushinda na kufaulu mitihani yao katika shule za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa matayarisho mazuri na ya kitaalam ya hotuba ya Wizara hii. Nawaombea Mungu awape uwezo na mashirikiano katika utendaji wa kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu ujenzi wa mabweni nchini. Napenda kupongeza Serikali yetu kwa juhudhi kubwa inayofanya katika ujenzi na ukarabati wa mabweni. Juzi tumeshuhudia Mheshimiwa Rais akizindua mabweni katika Chuo cha Dar es Salaam. Ushauri wangu katika suala hili ni kwamba mabweni yawe na miundombinu salama ili kuepuka madhara ambayo mara nyingi yamekuwa yakijitokeza. Pia mabweni yowe na milango zaidi ya mmoja ya kutoka na hata milango ya dharura. Vilevile mabweni yowe na vizimia moto ili kudhibiti madhara ya umeme unapoleta hitlifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu Chuo Kikuu cha Dodoma ni mionganoni wa vyuo bora katika nchi yetu. Chuo hiki kina eneo kubwa na sekta nyingi lakini bado inaonekana

kuwa wanafunzi wanaojiunga katika chuo hiki ni kidogo kutokana na ukubwa na uwezo wa chuo. Hii inatokana na mabweni ambayo hayaridhishi. Hivi sasa *competition* ya vyuo ni kubwa sana hapa nchini. Vyuo binafsi vinaonekana vina nafasi kubwa ya kupata wanafunzi wa kuijunga na vyuo vyao kuliko chuo chetu cha Dodoma kutokana na mabweni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, aniambie ni asilimia ngapi ya wanafunzi waliojiunga mpaka kufikia mwaka huu kutokana na mahitaji ya chuo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam. Taasisi hii ni taasisi inayofanya kazi zake vizuri na kwa ubora sana. Tunaiomba Wizara izidi kuboresha ili kufikia lengo liliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hii inajishughulisha pamoja na mambo mengine kutoa mafunzo katika ngazi tofauti kama vile ufundi sanifu na uhandisi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze sifa za kuijunga na mafunzo hayo ambayo hakuyaeleza katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ni hotuba nzuri, inatoa dira wapi tunaelekea katika kuinua kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, aiangalie sana Wilaya ya Wanging'ombe, Mkao wa Njombe. Wilaya hii kitaalam ndiyo inayongoza katika Mkao huu na iko katika nafasi nzuri sana kitaifa kwa miaka mitatu. Nakuomba uidhinishe tuanze kidatocha tano na sita kwenye shule tatu za Makoga, Wanike na Wanging'ombe na nitakushukuru sana zingeanza mwaka huu. Tayari madarasa na mabweni kwenye shule za Makoga, Wanike na Wanging'ombe yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wilaya ya Wanging'ombe ijengewe Chuo cha VETA. Lipo eneo Soliwaya limeshaandaliwa kwa ajili ya kujenga Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Wizara kwa msaada wa kuboresha miundombinu ya shule ya sekondari ya Usuka na shule za msingi za Dalami na Illembule. Naomba mpango huu uendelezwe mwaka huu katika shule ya sekondari ya Igosi na shule za msingi za Wanging'ombe, Palangawamu, Mtapa na Saja. Majengo hayo yamechoka sana kupita maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kuwapongeza na kuwatachia kila heri.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya elimu ni bajeti finyu sana ambayo halwezi kukidhi mahitaji ya elimu ya nchi hii. Angalau elimu ipangiwe asilimia tatu ya *GDP* kama nchi za wenzetu katika Afrika Mashariki ambapo huanzia asilimia nne hadi asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *re-entry policy*; watoto wa kike wanaojifungua wakiwa shulen i wawekewe sera ya kurudi kuendelea na masomo baada ya kujifungua, sera hii itasaidia watoto hawa kupata haki ya elimu (*right to education*). Aidha, itapunguza idadi ya wasio na elimu nzuri nchini na pia kupunguza idadi ya wasio na ajira nchini. Nchi nyingi zimefanikiwa katika hili, mfano ni nchi ya Zambia. Wapo Wabunge waliofanya utafiti juu ya hili na wadau wa nchi hii walifiki wanaobeba mimba warudi shulen i kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa elimu nchini; elimu bora hutolewa na walimu bora ambao wanalipwa vizuri na Serikali, wana mahali bora pa kuishi, wana madarasa ya kutosha na hakuna mlundikano wa wanafunzi darasani. Aidha, walimu walipwe stahili zao mapema kuondoa malalamiko ili wafanyakazi wakiwa na amani moyoni.

Aidha, miundombinu ya elimu kama uhaba wa walimu mashulenii, uhaba wa madarasa na madawati, uhaba wa vyoo, uhaba wa maji safi na salama na uhaba wa vitabu, chaki na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makato ya mishahara bila ridhaa, walimu wamekuwa wakikatwa mishahara yao bila ridhaa yao jambo ambalo ni kinyume cha Sheria za Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2013 makato hayo ni kama vile ya kwenye ujenzi mbalimbali wa majengo ya umma; kwa mfano, maabara, madarasa na kadhalika. Makato mengine ya *NIC* toka mishahara ya walimu wa Wilaya ya Kakonko wanaozidi 14 bila mikataba yoyote. Makato haya ni wizi wa mishahara ya walimu kwani hata kwenye *salary slip* makato hayo hayaonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kusimamisha kazi walimu kwa kigezo cha wanafunzi ku-fail. Hili halikubaliki kwani ni wahalalishaji tu. Aidha, wakuu hawa hufikia hatua ya kuwashusha vyeo Walimu Wakuu kwa kigezo cha wanafunzi ku-fail bila kujali miundombinu mashulenii.

Kuhusu kuundwa kwa *TSC* toka iliyokuwa *TSD* hakujaleta mabadiliko yaliyokusudiwa, mfano *TSC* ilitakiwa:-

- (i) Iwe ndio mwajiri/afunge mikataba na walimu;
- (ii) Ilipe mishahara;
- (iii) Ipandishe madaraja;
- (iv) Iadhibu walimu (nidhamu); na
- (v) Itoe barua ya kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake mwalimu amendelea kuhudumiwa na Wizara, Idara nyingi sana hivyo kuleta ugumu kwa walimu katika kuhudumiwa.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ndoa za utotoni, wazazi na Waheshimiwa Wabunge tunaomba tuwe kitu kimoja tuangalie namna gani tunaweza kumsaidia mtoto wa kike hasa wanaopata mimba wakiwa

masomoni, Serikali ione namna ya kuwasaidia watoto hawa wanaokuwa na matumaini ya kuendelea na masomo lakini masomo yao hukatishwa kwa kupata mimba bila kutegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanapata mimba? Wanapata mimba kutokana na kudanganywa na wanaume kwa kupewa vitu vidogo vidogo ambavyo huwafanya kujisahau wajibu wao na kuingia kwenye mtego huo bila kutegemea, wengine hutokana na umbali mrefu wa mahali ilipo shule. Ili kupunguza idadi hii kubwa ya watoto kupata mimba ni lazima Serikali ihakikishe wanajenga *hostel* za kutosha kwenye mashule, hii itasaidia sana kupunguza uharibifu kwa watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za mfumo wa elimu, kukosa falsafa ya elimu yetu, changamoto ya usawa wa elimu kuhusu mtoto wa kike na wasiojiweza, usimamizi mbovu wa elimu shuleni, utakuwa udhibiti ubora, uandaaji walimu, uwajibikaji mdogo kwenye elimu wadau wote, ubora hafifu ya ufundishaji, kukosa walimu bora wasio na hamasa hasa vifaa. Mazingira duni ya kujifunzia kama vile uduni katika miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za miundombinu; madarasa 146,106 hii ni kwa shule za msingi. Madarasa 12,568 kwa shule za sekondari hii ni kutokana na taarifa ya Kamati. Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/2018 ni kujenga madarasa 2000 tu ya shule za msingi na sekondari ilihali mahitaji ni takribani 158,674 kwa asilimia moja hadi mbili tu kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu motisha kwa walimu; kutokana na malimbikizo ya mishahara shilingi bilioni 200 kutokana na madeni hayo kunashusha sana moyo wa walimu hawa kufanyakazi kwa moyo wa kufundisha, kwa sababu mwalimu huyu akipata haki yake bila usumbufu itamfanya afanye kazi kwa bidii na moyo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali Serikali iwaonee

huruma watoto hawa wa maskini ambao wanarubuniwa na kuingia kwenye maisha ya ndoa ambazo hawajazikusudia. Naishauri Serikali ijitahidi sana kila shule iwe na hosteli za kutosha ili watoto wawe wanaenda kukaa shule hadi *semister* inaisha ndipo warudi nyumbani na wanapokuwa nyumbani mara nyingi watoto huwa chini ya uangalizi wa wazazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makosa ya vitabu; hadi sasa tayari vitabu 13,680,981 vya darasa la pili na tatu vimesambazwa mashulenii wakati vitabu vina makosa mengi sana. Kwa sababu vitabu takribani milioni sita vya darasa la kwanza vimechapishwa na vina makosa pia na vitabu hivi ni takribani ya milioni 18 ambavyo gharama yake takribani shilingi bilioni 108, hizi shilingi bilioni 108 ni fedha nyingi sana na Serikali haionii inalipa Taifa hasara maana fedha hizi zingeenda kujenga *hoste/kwenye* shule zetu, zingesaidia sana kupunguza tatizo la watoto wetu kupata shida ya kwenda shule na kurudi au fedha hizo zingeweza hata kujenga madarasa ya kutosha kwenye shule za nchi yetu.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Nawapongeza Mawaziri na watendaji kwa juhudii wanazochukua, ushauri kwa Serikali itoe fedha kwa wakati na za kutosha ili kupunguzia Wizara hii shida inayoendelea sasa hivi inayopelekea elimu kushuka.

Ninashauri juu ya ndoa za utotoni na mimba za utotoni, ninaiomba Serikali itoe elimu ya kutosha ili watoto wajue mabadiliko ya maumbile yao. Hivyo basi, naishauri Serikali kuridhia sheria ya watoto wanaopata mimba warejeshwe shulenii kwa masharti ambayo hayatafanya wanafunzi hao kurudia kosa hilo.

Pia ninaishauri Serikali iendelee kuandaa mazingira rafiki kwa watoto wa kike kupata elimu bila vikwazo vya kumrudisha nyuma. Nlishauri Serikali kuimarisha vyuo vya *FDC* nchini ambavyo vitasaidia kuelimisha vijana wetu na kujajiri

mfano, *FDC* Kibaha ina mapungufu mengi sana. Niishauri pia Serikali kukagua shule binafsi nyingine ni za ovyo hazina vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kulipa madai ya walimu ili kuwatia moyo, hivyo *BRN* kufikiwa kwani huwezi kupata matokeo makubwa bila kuwekeza kwa walimu. Mikopo ya elimu ya juu iangaliwe kwani hakuna haki na weledi kwa watoaji wanaotakiwa kupewa wanakosa na wasiostahili ndio wanapata, Serikali iangalie hilo.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2016/2017. Kumekuwa na ongezeko la watoto walioandikishwa kuanza shule, Serikali imebeba gharama kubwa za kumsomesha mtoto na kushirikiana na wazazi na walezi wa wanafunzi hawa kuititia programu ya elimu bila malipo. Bado changamoto zilizopo za upungufu wa madarasa kwa shule zote za sekondari na shule za msingi, upungufu wa nyumba za walimu kwa shule zote hizi za sekondari na shule za msingi,

Pia upungufu mkubwa wa matundu ya choo kwenye shule hizi za sekondari hasa zaidi kwenye shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upungufu wa walimu kwenye baadhi ya shule za sekondari na shule za msingi na upungufu wa vitabu vya kufundishia na vitabu vya wanafunzi haya ni mambo muhimu ambayo Serikali inayashughulikia kwa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limetokeza suala la watoto wa kike kupewa mimba mashulenii. Serikali inapaswa kuendelea kulikataza na kulisimamia suala hili kwa kuhakikisha wanaume wanaokatisha masomo ya wanafunzi hao wa kike kwa kuwapa mimba wanaadhibiwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Pia ni muhimu kwa Serikali na hususan Halmashauri za Mikoa na Wilaya kuhakikisha zinajenga *hostel* za kutosha kwa ajili ya wanafunzi wote wa kike na kuwakinga wanafunzi hao. *Hostel* hizi zitapunguza sana tatizo lilitopo la wanafunzi wasichana kupata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Morogoro Kusini kuna shule nyingi za sekondari ambazo zimejengwa kwa nguvu kubwa za wananchi lakini zina changamoto hizi za mimba. Tunaomba Wizara itoe fedha za kutosha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Vijiji ili tuondoe tatizo hili la aibu la wanafunzi wa kike kupewa mimba mashulenii. Mazingira ya wanafunzi hawa ni mabaya sana na yanasaababisha kupata mimba hizo. Tukiwezesha kujenga *hostel* za wanafunzi wa kike kwenye shule hizi, tutaondoa tatizo liliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo langu la Mororogo Kusini tunalo eneo tayari la kuanzisha shule za VETA. Bado naikumbusha Serikali iweze kutupa msaada tuweze kuanzisha chuo hicho kwa kipindi kijacho cha mwaka 2017/2018 - 2018/2019. Sambamba na hilo jimbo la Mororogoro Kusini imeziteua shule za sekondari Matombo na shule ya sekondari Misewesewe ya wasichana iliyopo kata ya Mngazi kuanzisha kidato cha tano (*form five*) kuanzia mwaka 2017/2018. Matayarisho yamekamilika kwa shule hizi hususan shule ya sekondari ya Matombo ili ianze kupokea wanafunzi wanaoingia kidato cha tano kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2017/2018. Nimepata taarifa kwamba kumekuwa na ucheleweshaji wa kuwezesha mpango huu kutokana na urasimu Wizarani. Naomba Wizara ihakikishe tunalikamilisha mapema ili wanafunzi waweze kupata elimu ya *form five* ndani ya Wilaya ya Morogoro Vijiji kuitia shule zetu hizo mbili zilizoteuliwa ambazo kwa kiasi kikubwa zimecheleweshwa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze sana Wizara kwa kazi kubwa inayofanywa ya kuinua elimu ya Tanzania, bado kuna kama kazi ya kufanya ambayo ninaamini kwa uwezo wenu mtaikabili na kuimaliza mapema. Naomba kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Buhombe ina

changamoto ya uwepo wa Chuo cha VETA, Wilaya hii ipo kwenye rasilimali nydingi zikiwemo misitu (mbao), madini, mifugo (ngoz) ambazo zinaweza kurahisisha kwa kiwango kikubwa ujifunzaji na upatikanaji wa ujenzi (*skills*) wa kutumia rasilimali hizi ili ziwe zenye faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yetu ina changamoto ya *high school*/kama nilivyokuja ofisini kwako, naomba sana Mheshimiwa Waziri, shule yetu ya sekondari ya Businda iongezewe mabweni na mabwalo, madarasa na maabara ili shule iwe *high school*. Kwa sasa hali tuliyonayo wanafunzi wetu wengi wanalazimika kusafiri umbali mrefu kufuata elimu ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa shule, idara ziimarishwe na ninaomba kushauri upatiwe rasilimali za kutosha kwa maana ya miundombinu, rasilimali fedha na watu, nashauri pia wakaguzi walipwe mishahara inayowapasa kama ilivyo kwa Wakuu wa Idara (LSS). Aidha, naomba idara hii, ifanywe kuwa wakala wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niungane na wengine katika kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri inayoendelea kuifanya. Nampongeza sana Mheshimiwa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya kwa hotuba nzuri ya Wizara hii, pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Rais wangu wa Awamu ya Tano Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa kuleta mfumo wa elimu bila malipo. Mfumo wa elimu bila malipo umewakomboa wengi hasa waishio vijijini na kuongeza idadi ya watoto kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Wizara

pamoja na kazi nyingi nzuri na mipango ya Wizara inayoendelea, waingie shule ya msingi ya Kipera ambayo ina watoto wasiopungua 70 wanapata elimu maalumu, ni watoto wenyewe ulemavu na mionganini mwao wapo watoto wenyewe ulemavu wa ngozi (*albinism*). Mazingira ya ulinzi wa watoto hawa siyo rafiki, shule ipo pembezoni kabisa, huduma ya maji hakuna, ulinzi hawana, watumishi ni wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako kwa kuipa fedha shule ya msingi ya Kalenga iliyoko Jimbo la Kalenga kiasi cha shilingi 241,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo. Shule hiyo kwa hali iliyokuwa ingeleta maafa kwa watoto wanaosoma pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri azipokee salaam toka kwa wananchi wa kijiji cha Kalenga mahali shule ilipo pamoja na vitongoji vyake. Wanatoa shukrani nyingi kwa kupelekewa pesa hizo na mimi kama mdau wa Kalenga nasema ahsante sana.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani iliyosomwa na Mheshimiwa Susan Lyimo, Waziri Kivuli wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira ya shule za kata kutokuwa na mabweni, pia umbali na kutokuwa na ulinzi wa wanafunzi hasa wa watoto wa kike huko vijijini tunakotoka, umaskini wa kipato wa wazazi hupelekea wazazi kuwapangia nyumba watoto karibu na shule au wanafunzi kusafiri umbali mrefu kwenda shulenii. Watoto wa kike hukumbana na vikwazo vingi kama ubakaji, ushawishi wa pesa za kujikimu kutokana na kuishiwa kabla mzazi hajampa matumizi, elimu ndogo ya uelewa na ukosefu wa walimu na kusababisha utoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naishauri Serikali ifuatilie na iwapo mtoto wa kike (mwanafunzi) akapata

mimba kwa sababu hizo au nyingine na kwa kuwa anatoka familia za maskini awekewe utaratibu wa kuendelea na masomo ili apambane na umaskini wa kipato. Pia naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Bunge kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya madarasa, walimu, vyoo, maji shulenii tete sana kupelekea kuperomoka kwa elimu. Hivyo, bajeti hii iangalie na kutatua kero hizo. Wananchi wamechangia kwa kujenga maboma ili Serikali imalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madeni ya walimu, kupanda madaraja walimu na posho ya mazingira magumu, navyo ni kero kubwa na kupelekea walimu kushusha morali ya kazi na kushuka kwa elimu hasa shule za vijiji kutokana na mazingira magumu. Serikali ione haja ya kuwezesha maslahi ya walimu ili kuinua elimu. Kitengo cha ukaguzi nacho kiwezeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kuwasilisha.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mungu kwa mapenzi yake ya kuniwezesha kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Wizara kwa jitihada zake nzuri katika kuiboresha elimu ya Kitanzania, pamoja na juhudii hizo bado kumekuwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vyoo vya kutosha na maji mashulenii. Mara nyingi unakuta watoto zaidi ya 70 wanatumia tundu moja la choo, hili halikubaliki na Serikali ihakikishe kuwa shule haipewi kibali kama haina matundu ya vyoo ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la maji mashulenii, shule zisipewe vibali vya kuanza kufanya kazi kama hazina miundombinu ya kuvuna maji. Bado maji ni muhimu sana katika afya ya watoto mashulenii hasa wa kike

pale wanapokuwa katika siku zao za hedhi, ambapo wengi wamekuwa wakikosa kwenda shule kwa hofu ya kukosa maji pale anapokuwa shule. Maji hayo bado yanachangia katika utoro wa wanafunzi wa kike katika maeneo ambayo hayana maji. Mara nyingi wasichana hawa wamekuwa wakitumika majumbani kutafuta maji hivyo wamejikuta wanaacha shule ama kukosa masomo baadhi ya shule.

Kuhusu utoro wa watoto wasichana mashulenii, unasababishwa pia na ukosefu wa hedhi salama kwa watoto hawa. Pia kwa sababu katika utoaji wa elimu bure vipo baadhi ya vifaa vinavyotolewa na Serikali bure vikiwemo vitabu, chaki hata *pen*, ni ombi langu sasa kwa Serikali kuanza kutoa taulo za kike mashulenii ili waweze kujihifadhi wanapokuwa katika siku zao za hedhi. Ni imani yangu kwamba kwa kufanya hivyo kilio cha ukosefu wa wasichana kukosa masomo kitapungua. Mfano mzuri, zipo nchi nyingine za Kiafrika ambazo tayari zimefanya hivyo na kupunguza changamoto hii kwa ukubwa. Nchi hizo ni kama Uganda, Kenya, Nigeria, Zimbabwe na nyinginezo ambazo zimekuwa zikitoa taulo za kike za kutumia zaidi ya mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ukosefu wa madawati, kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali katika suala zima la ukusanyaji wa madawati kwa ajili ya shule za Serikali, zoezi ambalo limepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya ukosefu wa madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na utaratibu wa madawati yanayoharibika kusubiri kupelekwa kwenye karakana ya Wilaya kwa ajili ya matengenezo. Ombi langu kwa Serikali ione umuhimu wa madawati haya kuwa yanatengenezwa na wafungwa ili kuepusha madawati hayo kukaa kwa muda mrefu, saa nyingine hata miezi mingi kabla ya kutengenezwa. Ila kwa wafungwa yanekuwa yanatengenezwa hapo hapo mashulenii kwani mara nyingi uharibifu wake huwa siyo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wanafunzi wanaopata mimba za utotoni warudishwe shulenii kwani wengi wao wanapata mimba wakiwa na umri mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo elimu ya juu; mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi wachache na wengi wenyewe uwezo kuachwa hasa watoto wa kike wanaochukua kozi ya Udaktari na *Engineering*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi vyuo ni vichache hasa Mkoa wa Mbeya, kwani nchi yetu inajinasibu kuingia katika uchumi wa viwanda na tuna wanafunzi wengi wanaishia elimu ya msingi na elimu hii ingesaidia kuwapa elimu vijana wetu.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa wanafunzi kupata elimu bure kuanzia chekechea mpaka kidato cha nne. Pili, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Napongeza Bodi ya Mikopo kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wengi. Kwa upande mwingine kuna wanafunzi ambao wamesoma kwa taabu ya kujilipia au kulipiwa na wazazi wao kwa kusuasua kwa madarasa ya chini, bahati nzuri wanafaulu mpaka Chuo Kikuu lakini kwa bahati mbaya hawapati mikopo kufuatana na vigezo vilivyowekwa. Wanafunzi wengine inabidi waache chuo, kwa sababu ya kukosa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwajali na kuwahurumia wanafunzi hawa wanaokosa masomo kwa sababu hawana fedha za kulipia, nashauri inapowezekana wanafunzi wote wapewe mikopo. Mikopo ni mikopo wapewe kwani mikopo hii watailipa hapo baadae. Mheshimiwa Waziri naomba tuwajali pia watoto hawa wahitaji wa elimu ya juu, hawawezi kulipia elimu yao. Serikali yangu siku iwaangalie wanafunzi hawa na wenyewe wapewe mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha kwa wanafunzi wanaofaulu alama za juu na hasa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi, jambo hili likifanyika kuanzia madarasa ya chini, naamini wanafunzi watajituma kusoma, kufaulu na baadaye kulijenga Taifa letu. Jambo hili pia lielekezwe kwa upande wa walimu. Walimu wanaofanya vizuri katika ufundishaji wapatiwe motisha, hii itawapatia moyo kazini mwao na moyo wa utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitabu nashauri iundwe Kamati ndogo ya kupitia vitabu hivi jambo hili litakuwa zuri, kusudi watoto wetu wapate elimu nzuri, kupitia vitabu viliuyoandikwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wanohitimu vyuo vya VETA ni pongezi kwa Serikali kwa kuwa na mpango wa kuwa na chuo cha VETA kila Wilaya kwa kuwa vyuo hivi vya VETA vinafundisha kwa vitendo, ni vema kila mtoto anapomaliza mafunzo haya aweze kusaidiwa zana ama vifaa vyta kuanzia kazi, angalau kidogo ili waweze kujajiri wenyewe, nashauri jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia elimu inayotolewa katika vyuo hivi iwe ya kuhitajika katika eneo husika ambapo chuo kipo. Kwa mfano, kwa wastani kila Wilaya hapa Tanzania hata mijini wananchi wengi hutegemea kilimo, kwa kupata kipato cha familia pamoja na kupata chakula chao, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba na kukushauri kuwa kila Chuo cha VETA kuwe na mkondo wa elimu ya kilimo, kwa sababu ya kuinua familia na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma shule hasa za sekondari zilikuwepo zinajulikana kuwa ni shule za kilimo lakini sasa hivi hakuna, nashauri utaratibu huu uanze tena ili kusudi wanafunzi baada ya kupata elimu ya sekondari na kama hakubahatika kwenda elimu ya juu, aweze kujitegemea kwa elimu ya kutosha ya vitendo watakayokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vkuhusu Vyuo vyatubu na Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) naishukuru na kuiomba Serikali kuzidi kuangalia vyuo hivi, kwani wanafunzi wanaomaliza katika vyuo hivi wataendelea kueneza elimu ya vitendo waliyoipata katika maeneo yao. Mheshimiwa Waziri nashauri mabweni yaendelee kujengwa na kuboreshwa katika vyuo hivi ili vyuo hivi watoto wengi waweze kudahiliwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri jambo hili aliangalie na kulipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuongelea walimu wa masomo ya sayansi. Naomba mikakati iongezeke ya kupata walimu wengi wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara haujafanya vizuri mitihani ya darasa la saba hata kidato cha pili. Moja kati ya sababu zilizotufikisha hapo ni uhaba wa walimu, Mkoa una upungufu wa walimu kwa asilimia 40. Baadhi ya shule za msingi zina walimu watatu wakati madarasa ni saba.

Je, watafundishaje? Tunaomba Wizara inapoajiri walimu izingatie kuwa Mkoa wa Mtwara una upungufu mkubwa hivyo wapewe walimu wengi ili walingane na mikoa mingine.

Suala la pili ni vuguvugu la kufuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika limepungua sana. Waratibu wa Elimu Kata zamani walikuwa wasaidizi wa EWW. Idadi ya wananchi wasiojua kusoma na kuandika inaongezeka mwaka hadi mwaka, Wizara ifufue na iweke mkakati wa kufufua EWW. Waratibu wa Elimu Kata hawana kazi nyingi wapewe jukumu la kusimamia EWW kama ilivyokuwa hapo zamani.

Tatu, hali ya taaluma katika shule za msingi na sekondari hairidhishi na hii inasababishwa na shule zetu kutokaguliwa, wakaguzi hawatoshi na hawana usafiri. Serikali iongeze idadi ya wakaguzi na wapewe usafiri wa

uhakika ili waweze kukagua shule zao zote. Naunga mkono suala la kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Waziri pamoja na Naibu Waziri, bila kuwasahau Katibu Mkuu na watendaji wote, naomba nitoe ushauri kidogo kuhusu suala ambalo ninaona; kuna utata na linatesa sana wazazi wa watoto wanaohitimu kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtihani wa Taifa wa kuhitimmo kidato cha nne hufanyika kila mwezi Oktoba ya mwaka, matokeo ya kidato cha nne hutoka kati ya Januari na Februari, lakini wanaopaswa kuendelea na masomo ya kidato cha tano wanasubiri hadi mwezi Julai. Hivyo, mtoto huyu ana miezi takribani nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika hii ni mateso sana kwa watoto kusubiri na wazazi kuwalinda watoto hawa ili wasije wakaingia kwenye kujifunza mambo yasiyofaa na kudumaza ari na moyo wa kusoma na uwezo unapungua. Hali hiyo, huwapelekea wale wenye uwezo kuwapeleka watoto wao *pre-form five* kitu ambacho kwa wasio na uwezo kinawanyanyapaa.

Ushauri wangu matokeo ya kidato cha nne yanatoka Januari ili kubaini waliofaulu, watoto wanaofaulu kuanzia alama “D” *one to three*, wapelekwe JKT kwa muda wanaosubiria kuanza kidato cha tano mwezi wa saba. Hivyo, kuanzia Februari hadi Juni. Wakishahitimmo watapata muda mdogo tu wa kukaa nyumbani na hivyo kuendelea na masomo vizuri. Hivyo itaondoa JKT ya kidato cha sita haitakuwa na haja ya kuwepo. Utaratibu wa kuwapata vijana kwenda kwenye Majeshi yetu unaotumika utabadilika na badala yake watapata walioenda JKT moja kwa moja. Mfano Jeshi la Polisi, Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kama utaratibu wa

kuwapeleka Jeshi la Kujenga Taifa litaonekana halifai, basi itafutwe namna yoyote kuhakikisha muda wa kuanza kidato cha tano unasogezwa ili waanzo Mei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. Waziri na timu yake hongereni sana kwa kazi. Ninayo mambo machache ya kuishauri Serikali na Wizara hii.

(a) Wazo la eti wasichana wanaopata mimba, warejeshwe shulenii dhahiri halina mashiko na halina msingi. Hatuwezi kuanza karne hii eti kuhamasisha watoto wa kike akipata mimba arejeshwe shulenii. Hii haikubaliki, haifai na kama Bunge tusishabikie jambo ambalo madhara yake ni makubwa sana. Tuendelee kupiga vita tabia ya zinaa mashulenii.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu vya kufundishia visivyo na ubora ambavyo vimeshasambazwa mashulenii kwa mamilioni:-

(i) Vitabu hivyo vyenye makosa viondolewe mashulenii haraka iwezekanavyo.

(ii) Waliohusika na ujinga huo wawajibishwe ikiwa ni pamoja na kuwastaafisha kazi zao hata ikibidi kuwafukuza. Ni jambo la aibu sana kwa Serikali yetu na kwa Chama chetu cha Mapinduzi.

(iii) Fedha na gharama iliyotumika kuchapisha vitabu hivyo ilipwe na wahusika haraka sana ikiwa ni pamoja kuwafilisi mali wanazomiliki ambazo zitakuwa zimepatikana kwa wizi na udanganyifu huo.

(iv) Walioviandika vitabu hivyo na makampuni yao wasipewe kazi hiyo tena. Wasipewe *tender* tena za kuandika na kuchapisha vitabu.

(c) Chuo cha *FDC* Kasulu; chuo hiki ni kikongwe sana na kimechakaa, kilijengwa mwaka 1974. Ninaomba sana chuo hiki kiwemo katika vile vyuo kumi vitakavyofanyiwa ukarabati, kama hotuba ya Waziri ilivyobainisha ukurasa wa 93 – 94. Mkoa wa Kigoma upo nyuma sana kielimu na hata kiufundi. Kigoma na hususani Kasulu tuna kila sababu ya chuo chetu kuongezewa ubora wake wa miundombinu.

(d) Kuhusu maktaba ya Wilaya ya Kasulu; ninaomba sana Wizara ya Elimu iangalie uwezekano wa kukamilisha jengo lenye ghorofa moja la maktaba ya Wilaya ya Kasulu ambalo lilanza kujengwa 2007 kwa nguvu za Mbunge wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Jengo hilo linahitaji vifaa vifuatavyo:-

(i) Finishing ya Ndani (milango, *ceilings, gates* na kadhalika).

(ii) Kuboresha mazingira ya nje ikiwemo kujenga uzio wa tofali ili kuimarisha eneo hilo.

(iii) Gharama ya takribani shilingi milioni 200 - 300 inaweza kabisa kukamilisha jengo hilo na likaanza kutumika. Wizara isaidie nguvu na juhudhi ambazo tayari Wilaya imefanya.

(e) Kusaidia kukamilisha maabara za sayansi zilizopo katika Mji wa Kasulu. Majengo ya maabara katika shule zetu nyingi za sekondari zipo katika hatua mbalimbali kuanzia asilimia 40 hadi 70 za ujenzi. Wizara kwa kutumia fursa mbalimbali kama vile *P4R Programs* na *Equip Tanzania Projects* inayotekelizwa katika Mkoa wa Kigoma. Ni vizuri juhudhi za pamoja kati ya Wizara na Halmashauri zetu tuwe na mpango wa kukamilisha maabara hizi, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa kazi, naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imefuta shule ya sekondari ya Milundikwa ikiwa na kidato cha kwanza hadi cha sita na kuua kabisa matarajio ya watoto katika ngazi zao mbalimbali walizokuwa wamefikia bila kuangalia *performance* nzuri sana ya shule hii. Ikiwa na miundombinu yenye thamani ya shilingi milioni 871. Naitaka Wizara inisaidie kurudisha miundombinu mbalimbali iliyokuwa imejengwa na wazazi ikiwemo madarasa, mabweni, maabara, vyoo, maji na mambo kadhaa ambayo sasa wanafunzi wameyakosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara itafute wadau mbalimbali kokote wanaoweza kupatikana ioneni kwa jicho la huruma, Mheshimiwa Waziri mpaka sasa sijaona mchango wa Wizara yako, kazi zinazoendelea kwa sasa ni kiduchu tu, bado kazi ni kubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni miundombinu ya elimu Wilayani Nkasi (Nkasi Kusini kwa upekee) ni hatari na pamoja na mchango huu, naomba kuambatanisha na hali ilivyo mbaya kwa takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi idadi ya watoto darasa la awali hadi darasa la saba ni watoto 80,604. Idadi ya walimu mahitaji ni 1,791; waliopo 1,089 na upungufu ni asilimia 39. Takwimu za vyumba vya madarasa mahitaji ni 1,791; vilivyopo 655; upungufu ni 1,136 ambao ni sawa na asilimia 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejenga maboma 273 vya vyumba vya madarasa ili kukabiliana na hilo tatizo, tunaomba tupanue kupunguza kero hiyo, kadhalika takwimu za nyumba za walimu, mahitaji 1,089 zilizopo ni 392 upungufu 697 upungufu asilimia 64. Wananchi tumejenga maboma mengi bado kupauliwa, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekondari; idadi ya shule ni 23 na 22 ni za Serikali moja tu ni ya binafsi. Jumla ya wanafunzi waliosajiliwa mwaka 2017 wanaume ni 1,345 na wanawake 1,174 jumla ni 2, 519. Idadi ya kutoka kidato cha

kwanza hadi cha sita wanaume ni 3,854 na wanawake ni 3,141 na jumla ni 6,995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wa sayansi waliopo kwa sasa ni 14 tu wanahitajika walimu 95 tusaidie. Takwimu za nyumba za walimu, mahitaji ni 366, zilizopo 89, upungufu 277, sawa na asilimia 75.6. Tuna maboma 36 tunaomba tusaidie kupaua. Maabara mahitaji ni 66 zilizopo ni tano upungufu 61. Kila sekondari kuna ujenzi wa maabara wameshindwa kumalizia tunaomba msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto wa kike kushindwa kumaliza shule kwa tatizo la mimba tulishughulikie kama Zanzibar, tusiwhakumu watoto wa kike mbona watoto wa kiume wanawapa mimba na wanaendelea na kusoma nani atamsaidia binti wetu asome? Pia walemavu wasaidiwe.

Jimbo la Nkasi Kusini linapakana na Ziwa Tanganyika kwa upande wa Magharibi ambapo kata zilizoko kando kando ya ziwa zina changamoto nyingi zikiwemo, mawasiliano ya simu (kata ya Kala).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya barabara ambazo siyo nzuri, nyumba za walimu na madarasa; mambo haya yote yamekuwa yakifanya watumishi wengi kutokupendelea kwenda kufanya kazi maeneo hayo. Hivyo ni eneo lenye uwiano wa walimu usiolingana na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huu, tunaomba kupata walimu zaidi hasa katika shule za maeneo haya, sekondari na msingi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vijiji visivyofikika kwa gari, mfano, Kijiji cha Kasanga - Kata ya Ninde; Kijiji cha Msamba - Kata ya Ninde; Kijiji cha Izinga - Kata ya Wampembe na Kijiji cha Mwinza - Kata ya Wampembe. Vijiji hivi pamoja na vingine hulazimika kwenda kufanya mitihani ya darasa la saba katika shule nyingine kwa sababu wasimamizi hawako tayari kwa usafiri wa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itafute ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kusidia wananchi katika jitihada zao za kilimo na kufungua barabara za maeneo ya wananchi hawa. Tusikubali jambo hili liendelee siku zote, tutafute suluhu kwani itawezekana pia watoto wanaosafirishwa majini mara kwa mara wakapata shida japo hatuombei jambo hilo; tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wamekuwa wakisafirishwa kwa makundi makubwa/idadi kubwa kwenda kufanya mitihani maeneo yanayoruhusiwa au basi, shule zote zipate fursa ya kufanya mitihani kwa kupata vyombo vyaa usafiri kwa usimamizi ili shule zote ziweze kufikika wakati wa mitihani, watoto wafanye mitihani kwa utulivu shulenii kwao walikozoea.

Maeneo ya pembezoni kama Jimbo langu naomba yapewe upendeleo kwa nyumba za walimu na madarasa ili kuwakomboa wananchi hawa ambaa wanatakiwa kushikwa mkono ili wasogee. Watoto yatima waruhusiwe kusomeshwa kama watakuwa wamefaulu vizuri, maana wengi wao wamekuwa wakirudi nyumbani kwa kukosa msaada zaidi au vinginevyo ianzishwe taasisi itakayoiangalia changamoto hii kwa umahiri mkubwa (yatima kusoma).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashukuru kupokea shilingi 259,000,000 Kasu sekondari ili kuendeleza miundombinu ya shule mpya kufuatia kufutwa kwa Mihudikwa sekondari na watoto kuhamishiwa Kasu.

Tunaomba Chuo cha Chala kiboreshwe kiwe VETA kamili ili wananchi wa Nkasi wapate ujuzi hasa wale wanaofuzu darasa la saba na sekondari pia. Ahsante.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kunipa uhai na nguvu za kuwepo mahali hapa na kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. Pia namshukuru Mungu kuweza kuchangia Wizara hii muhimu kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri zinazofanyika, kuisimamia vizuri Wizara hii muhimu hakika matunda yake yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi la kutoa elimu bure, kwa kweli imewapunguzia mzigo wazazi na matokeo yameonekana watoto wengi wanapelekwa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeza Wizara baada ya tetemeko lililoupata Mkoa wetu wa Kagera, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Kyerwa na kuahidi kusaidia miundombinu iliyoharibiwa na tetemeko, namshukuru sana Naibu Waziri kwa msaada huo mkubwa kwa wananchi Kyerwa ingawa bado tunaendelea kuomba msaada wa kusaidiwa miundombinu mingi Kyerwa imechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kyerwa miundombinu mingi ya shule zetu imechakaa sana, kitu kinachosababisha watoto wetu kusoma kwenye mazingira magumu sana. Mfano, shule ambayo namuomba sana Mheshimiwa Waziri kutusaidia kuboresha miundombinu ni shule za msingi Kaisho, Mabila, Murongo, Businde, Songambele, Nyakatuntu, Bugomora na Isigiro ambazo shule hizo zina upungufu wa vyumba vyaa madarasa ni 94 vyenye gharama ya shilingi 1,880,000,000. Kwa upande wa vyoo kwenye shule hizo ni mbaya sana mapungufu ni matundu ni 198 yenye thamani ya shilingi 217,800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekondari na kwenyewe hali ni mbaya tunaomba kusaidiwa na kuomba sana Waziri Mheshimiwa Ndalichako, naomba sana msaada wako maana sehemu kubwa wananchi ndiyo waliochangia kuweka hiyo miundombinu, ninaiomba kusaidiwa angalau ili kuunga mkono juhudzi za wananchi Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejitalidi

sana lakini mahitaji ni makubwa sana kitu kinachopelekea shule nydingine wanafunzi wanasomea nje. Mfano, shule ya msingi Maendeleo iko katika Kata ya Businde, walimu sita wako kwenye nyumba moja kitu ambacho kimesababisha kushindwa kuleta familia zao hasa wenza wao. Naiomba sana Wizara kuziangalia shule za namna hii jinsi ya kuzisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee shule za sekondari za kata, wananchi wamejitahidi maeneo mengi kujenga madarasa na maabara lakini zaidi ya asilimia 85 hazina vifaa vinavyotakiwa kwenye maabara, naiomba sana Wizara kuzipatia vifaa hizo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kyerwa hatuna Chuo cha Ufundu, niiombe sana Serikali inapoangalia maeneo ambayo hawana vyuo vya ufulu naombwa Kyerwa tuangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango yangu naweza nikawa nimeongelea masuala yanayohusu Wizara ya TAMISEMI, lakini Wizara ya Elimu ndiye bosi wa elimu nchini. Miundombinu ikiwa mizuri, maabara zikiwa na vifaa vinavyotakiwa, tukapata walimu wa sayansi, elimu itakuwa nzuri na Wizara ya Elimu itakuwa imefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa motisha wanayopewa walimu, lakini bado walimu wanadai stahiki zao, niombe sana walimu wanaodai walipwe ili waweze kutulia na kuwafundisha watoto wetu bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee utaratibu wa Chuo Kikuu Huria ambao ulikuwa unawapa nafasi wale ambao hawakufanikiwa kufaulu kidato cha nne kwenda kidato cha sita, utaratibu wa kusoma *foundation* mwaka mmoja halafu mtu akifafulu anaenda kusoma digiri. Hili jambo limewasaidia wengi wakiwemo wanasiasa ambao wengi wao humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri suala hili liruhusiwe lakini lisiwe vyuo vyote ila Chuo

Kikuu Huria kiendelee kutoa elimu hii ambayo wengi leo hii chuo hiki kimepata Profesa, Madaktari na wengine wengi wamepitia chuo hiki. Wako Wabunge wengi ambao wanataka kujiendeze lakini kwa zio la Mheshimiwa Waziri tumeshindwa. Ninakuomba Waziri uliangalie ili kutusaidia wanasiasia tuijiendeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo narudia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika tunawaombea kwa Mungu awape hekima katika kutimiza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa uamuzi wake wa kuitangaza elimu kuwa bure na tumeshuhudia wingi wa wanafunzi wakitumia fursa hiyo. Mwenyenzi Mungu atakulipa kwa upendo wako kwa Watanzania na kujali utu na kutoa haki ya elimu kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ongezeko la wanafunzi mashulenii limekuwa kubwa, nashauri Wizara kuwa na programu maalum ya ajira kwa walimu kwa mkataba kwa kuwatumia walimu wastaifu kwa muda mfupi na wa kati, ili kuijandaa na ajira mpya kwa wale walimu watakaomiliza mafunzo, kuwezesha kuziba pengo la ukosefu wa walimu kutohana na wingi wa wanafunzi.

Kuhusu ujauzito kwa wanafunzi wa kike, tunaiomba Wizara kukamilisha mchakato wa sheria ya kuendelea na masomo kwa wanafunzi wanaopata mimba mara tu akishajifungua. Utafiti unaonesha kwamba wale waliopata mimba mara baada ya kujifungua, wakakubali kurudi shule kwa hiari wamefanya vizuri katika masomo yao na wamefaulu na kuendelea na masomo ya juu. Mifano hiyo ya

wanafunzi hao iko Zanzibar ambapo tayari tumepitisha sheria ya watoto wa kike wapatapo mimba shulenii kurudi shule mara baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo elimu zaidi itolewe kwa wanafunzi wote kujitambua kutokana na mabadiliko ya miili yao ili wawe na ufahamu wa jinsi ya kujilinda na unyanyasaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi sahihi ya lugha ya kiswahili, je, Wizara ina mipango gani wa lugha ya kiswahili kuikuza na kuzungumzwa kwa usahihi hasa ukizingatia kuwa lugha hii sasa inazungumzwa na nchi nyingi za Afrika na Tanzania ndiyo lugha yetu. Hadi sasa Tanzania imetoe wataalam wangapi wa lugha ya kiswahili kufundisha nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.
Ahsante.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, Wizara ya Elimu na viongozi wote wa Wizara ya Elimu kwa juhudii kubwa za kuendeleza elimu nchini kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na waliopendekeza watoto wa kike wanapopata ujauzito wakiwa bado wanafunzi waruhusiwe kurejea shulenii baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya watu wazima iimashwe zaidi ili kuwasaidia wale vijana walioacha shule mapema na waliokosa kwenda shule kwa sababu mbalimbali zikiwemo umaskini wa familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundu ipewe nguvu na shule za ufundu zipatiwe vifaa vyta kisasa ili wanafunzi wanapomaliza waweze kujajiri, pia waweze kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawatakia kazi njema.

MWENYEKITI: Ahsante, ataanza Mheshimiwa Simbachawene, ajiandae Mheshimiwa Ashatu. Mheshimiwa Ashatu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Elimu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhakikisha elimu yetu inakuwa bora na inaweza kwenda mbele.

Ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais wetu kwa kuleta elimu bure kwa vitendo na sasa tunaona watoto wote wa Tanzania walioko mijini na vijijini waliokuwa wamekosa nafasi sasa wanaweza kuipata elimu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie *point* chache ambazo ziliongelewa; kwanza ilikuwa ni kwamba Kamati iliomba Serikai iongeze bajeti ya Wizara ya Elimu hadi kufikia asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hili naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba tulipoanza mwanzo tulianza Wizara ya Afya tukasema ipewe asilimia 15, leo tunasema Wizara ya Elimu ipewe asilimia 10 na tutakuja Wizara ya Kilimo tutasema kutokana na mikataba mbalimbali ipewe asilimia 10. Tukijumlisha hizi asilimia tunapata asilimia 35 ya bajeti nzima inakwenda kwa Wizara tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai kwamba tumeingia mikataba hii, lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba tuiamini Serikali yetu, dhamira yake ni ya dhati, tunapotoa bajeti *cealing* tunaangalia vipaumbele vya Serikali yetu kwa pamoja, kila mmoja apate ili tuweze kuhakikisha kwamba tunaweza kufikisha maendeleo katika sekta zote ndani ya jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, tukichukulia mwaka 2015/2016 bajeti ya sekta ya elimu ilikuwa shilingi bilioni 3870; mwaka 2016/2017 bajeti ya elimu ilipanda na kufika shilingi bilioni 4570 ambayo ni ongezeko la asilimia 22. Kwa hiyo, Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha elimu yetu inapata bajeti ya kutosha na hii inaoneshwa na hizi jitihada ambazo zimekuwa zikiendelea. Tunafahamu umuhimu wa elimu katika maendeleo ya Taifa letu na wananchi wetu kwa ujumla na Serikali yetu ni sikivu, itakuwa inaongeza bajeti ya Wizara ya Elimu pindi uchumi wa Taifa letu unapoimarika na pato la Taifa letu linapokuwa limekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili napenda niseme Kamati yetu pia illipendekeza kwamba longezwe bajeti katika Bodi ya Mikopo. Naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kama nilivyosema mwanzo, azma ya Serikali ni kuhakikisha elimu yetu inakaa vizuri, watoto wetu wanapata elimu tena elimu ambayo ni nzuri, elimu ambayo wananchi wetu wataweza kuifurahia matunda yake. Katika hili naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba pia katika Bodi ya Mikopo tunafahamu mwaka huu tumeleta bajeti kama ilivyokuwa mwaka jana ya shilingi bilioni 427.55, lakini tuisahau kwamba Bunge letu hili lilipitisha mwaka jana kwamba Wizara yetu ya Elimu pamoja na Wizara ya Fedha tuhakikishe kwamba tunakusanya mikopo ile ambayo walikopeshwa wanafunzi wetu na sasa wapo makazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwezi mmoja sasa tuna uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 13 na pesa zote hizi zinazokusanywa tukizidisha kwa mwaka mzima ni zaidi ya shilingi bilioni 150. Serikali yetu kwa kujua umuhimu wa elimu, pesa zote hizi tumesema ziwe ni *Revolving Fund* waendelee kukopeshwa wanafunzi wetu wa elimu ya juu. Kwa hiyo, tutaona kwa mwaka mmoja Serikali yetu imeongeza shilingi bilioni 150 kwa Bodi ya Mikopo. Hiki ni kiwango kikubwa na tunayo imani kuwa wanafunzi wetu watazweza

kukopeshwa mikopo hii na wataweza kupata elimu kuendelea kuonesha ithibati ya Serikali yetu katika kufikisha elimu iliyo sahihi na kila mwananchi ambaye ana *qualify* kupata mikopo hii aweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kulisemea jambo moja ambalo limesemwa ni kodi nyingi zilizopo katika sekta ya elimu. Tumewaona wenzetu ambao wana shule binafsi wakilisemea kwa kiwango kikubwa. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba, kodi hizi zilipitishwa na Bunge lako Tukufu. Tukiangalia Sheria ya Kodi ya Mapato, imeletwa hapa tumeipitisha na inatambua kabisa kwa wale ambao hawafanyi elimu kama ni biashara wanapewa msamaha wa kodi nyingi ambazo ziko ndani ya sheria hii, lakini kwa mtu ambaye anafanya biashara ya elimu, anatoa huduma sawa, lakini anatengeneza faida, hivi kweli Waheshimiwa Wabunge tunaweza kuliachia hilli kwamba tuwasemehe tu, tuangalie vizuri, tulipitisha sheria hii wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapa mfano mmoja, hakuna asiyetambua ada zinazotozwa na *International School of Tanganyika*, lakini katika shule zilizokuwa zikipata msamaha wa kodi ni shule hii. Hivi ndani ya shule hii, kuna mtoto wa maskini nani anayeweza kusoma katika shule hii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufikirie kwa mapana tunahitaji kuongeza bajeti yetu ya Wizara ya Elimu, hapo hapo tunataka tupunguze vyanzo vya mapato. Tuwe makini katika mapendekezo yetu tunayoyaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya ninakushukuru kwa kunipatia nafasi kusema haya machache. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Simbachawene, ajiandae Mheshimiwa Mwigulu na ajiandae Mheshimiwa Angellah Kairuki.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninashukuru kwa michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge ambayo katika kuchangia wamegusa maeneo ambayo na sisi Wizara ya TAMISEMI ndio ambayo tunayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo nataka nitoe ufanuzi kama sehemu ya mchango, ni suala la elimu bila malipo. Elimu bila malipo imesemwa sana na wachangiaji wengi na kwa namna ilivyokuwa inasemwa ni kama vile elimu bila malipo ni programu maalum ambayo imewekwa, ina fedha zake na kwamba sasa suala la utoaji wa elimu nchini hakuna mpango mwagine wowote ni elimu bila malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili siyo sawa sawa lakini elimu bila malipo dhana na falsafa yake ilikuwa ni kujaribu kuondoa gharama za mapema hasa kwa wazazi na hasa wale wazazi wasiokuwa na uwezo kutakiwa kuchangia michango mingi sana ili watoto wao waweze kupata elimu. Jambo hili lilikuwa baya zaidi pale ambapo linawaweka kwenye jukumu la kwanza kabisa wale watoto wanaoandikishwa darasa la awali na darasa la kwanza, wazazi wao walipaswa kulipa kulingana na mpango uliowekwa na shule kiasi cha kuanzia shilingi 10,000 hadi shilingi 100,000. Sasa jambo hili liliwafanya wazazi wengi sana washindwe kuwaandikisha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuonesha tu namna ambavyo ongezeko la wanafunzi limekuwa kubwa kutokana na kuondolewa kwa gharama hizo ambazo sasa Serikali inazilipa, utaona kwa mfano kwa mwaka 2014 uandikishaji wa wanafunzi wa awali na darasa la kwanza ulikuwa kwa jumla yao walikuwa 915,000. Mwaka 2015 tulipoanza kuchukua gharama hii Serikali na kuzuia wazazi kutoa pesa hii ili wawaandikishe watoto, uandikishaji wa darasa la kwanza na awali walifika jumla ya 2,200,637. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 waliongezeka zaidi watoto kwa sababu wazazi wameondolewa ule mzigo na udahili wa watoto wa darasa la kwanza na darasa la awali ulifika 2,909,894. Kwa mwaka 2017 umeongezeka zaidi kwa maana ya kwamba sasa wazazi wameshaona kwamba Serikali imewapokea huu mzigo wa kulipa zile gharama za awali, udahili wa darasa la awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2017 hadi Machi juzi tulivofunga usajili, tumeandikisha watoto 3,188,149. Kwa upande huu kwamba sasa tunampatia kila mtoto wa Tanzania elimu sasa hili tumefanikiwa, kinachobakia ni changamoto ya kuboresha tu kutoa elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge waliosema kwamba hii elimu bure imesaidia na ninawapongeza sana Wabunge wanaoliona hilo. Kitendo cha Serikali kupokea mzigo huu ikiwa ni pamoja na kulipa ada kwa wanafunzi wa Sekondari, kulipa ada wale waliokuwa wanasoma shule za bweni walikuwa wanatakiwa kulipa ada shilingi 70,000 na wale wa kutwa walitakiwa kulipa ada shilingi 40,00 Serikali inazilipa hizi fedha siyo tena zinalipwa na wazazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na gharama za mitihani wa kidato cha pili ilikuwa ni shilingi 10,000 na mitihani mingine ya Taifa ya *form four* ilikuwa ni shilingi 50,000 gharama hizi pia Serikali imezichukua. Kwa hiyo, utaona wazazi wamepata nafuu kubwa sana pia wanafunzi wengi sasa hawafukuzwi shulenii kwa ajili ya kwenda kufuata michango hii na hawazuiliwi vyeti vyao na Baraza la Mitihani kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inagharimia kwa kutoa shilingi 10,000 kwa mtoto wa shule ya msingi na shilingi 25,000 kwa mtoto wa shule ya sekondari kwa ajili ya uendeshaji wa shule ambazo fedha hizi zinapelekwa moja kwa moja shulenii. Jambo hili limewapa faraja sana wazazi na kuondoa mzigo kwao, kwa hiyo wazazi wamebakia tu na jukumu la kuhakikisha kwamba watoto wao wanakuwa na sare na vitu vinavyowasaidia ili kujifunza ikiwa ni pamoja

na madaftari, kalamu na vitu vingine vidogo vidogo pamoja na nauli kwa wale wanaokwenda shuleni na kurudi, lakini na kuhakikisha kwamba watoto wao wanakula wale ambaao hawakai shule za bweni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inatoa hela ya chakula kwa ajili ya wanafunzi walio bweni. Kwa mwezi Serikali inatumia kiasi cha shilingi bilioni 20.8 kwa kila mwezi kwa ajili ya kugharamia gharama ambayo ingepaswa kulipwa na wazazi au walezi wa wanafunzi hawa. Mafanikio haya ni makubwa sana na hii nirudie kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ambaao tunafahamu kwamba bado tunalo jukumu kubwa ikiwa ni pamoja na majukumu mengine yanayohusiana na kuwasaidia watoto wetu ili waweze kupata elimu nzuri. Siyo kweli kwamba kwa sababu elimu bila malipo basi gharama zote Serikali imechukua na kila kitu ni Serikali hapana, hakuna programu hiyo, hatujawahi kupitisha mpango huo hapa, lakini jambo hili ilikuwa ni kuwapunguzia mzigo wazazi na walezi wa watoto ili waweze kupata haki yao ya elimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafanikio haya sasa tunapata tatizo jingine na ambalo nalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi nalo ni suala la miundombinu katika utoaji wa elimu. Tuna upungufu mkubwa sana sasa wa madarasa na tuna upungufu mkubwa sana wa nyumba za walimu na tunao upungufu bado wa matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwashule za msingi upungufu wa madarasa ni 119,275 na kwa sekondari upungufu wa madarasa ni 7,458 na kwa nyumba za walimu kwa shule za msingi upungufu ni nyumba 182,899 na kwa sekondari ni nyumba 69,811. Hali kadhalika tuna upungufu wa matundu kwa shule za msingi na sekondari ya vyoo. Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine nchini, kuhakikisha kwamba tunaendelea kusaidiana na Serikali kama tulivyofanya siku za nyuma kwa kushiriki katika miradi iliyopangwa katika maeneo yetu kwa kushirikiana na wananchi ili tuweze kuisaidia Serikali kupunguza kazi hii/mzigo

huu ambao uko mbele yetu. Hata hivyo, Serikali tunapanga bajeti kwa mfano kwa mwaka unaoisha tulipanga karibu kiasi cha shilingi bilioni 59 kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kutoa rai na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na kuwaomba wananchi wote wa Tanzania, nchi yetu inafuata siasa ya ujamaa na kujitigemea, kila mmoja analo jukumu la kuhakikisha kwamba anashiriki katika kujenga nchi yetu. Sote tunajua, miundombinu ya elimu inatusaidia siyo tu Taifa kupata wanafunzi na wananchi walioelimika pia wazazi wanafanya uwekezaji kwa sababu watoto hawa ni wa kwao. Kwa hiyo, tushirikiane na Serikali kwa sababu bado mzigo huu ni mkubwa na Serikali peke yake haiwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ambao wanaojitolea kwa namna moja au nytingine na wadau wengine wote nawashukuru, tuendelee kushirikiana ili kupambana na upungufu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja mkono. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwigulu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza niunge mkono hoja na niwapongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingi ambavyo Waheshimiwa Wabunge wanavisema ndiyo vitu ambavyo Profesa na Injinia huyu wanahangaikia kila leo, katika kazi waliyotumwa na Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanarekebisha baadhi ya maeneo ambayo kama Watanzania tunayaona yakiwa na kasolo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu baadhi ya mambo yaliyogusa Wizara yangu niongelee moja, Mheshimiwa Mahawe pamoja na Wabunge wengine waliongelea jambo liliolhusu masuala ya usafiri hasa wakigusia usafiri wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema wakati wa bajeti yangu nitoe pole kwa familia pamoja na Watanzania wote tuliookubwa na tatizo hilo. Sasa nitoe maelekezo kwamba baada ya jambo hili kutokea, askari wetu wasifanye kwa zimamoto jambo hili.

Katika wiki mbili hizi ambazo shule nyingi zinaelekeea likizo, wawaandalie vitu vinavyotakiwa kuwa kwenye magari yanayobeba wanafunzi. Wawaandalie masharti yanayotakiwa kuwa kwenye magari na shule zitakapofungwa wamilliki wote wa magari hayo, pamoja na wamiliki wa shule wanaotumia magari hayo waweze kufanya kazi mambo hayo na kabla ya shule kufunguliwa watoe taarifa ni namna gani wametekeleza masuala hayo ambayo yatakuwa yameainishwa yanayohitajika katika shule hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishughulikia tunayemkamata peke yake, yule ambaye tutakuwa hatujaweza kumkamata ataendelea kuwa na gari bovu na tutamtambua siku ambapo litakuwa Limeshaleta matatizo, hiki ndicho kilichojitokeza katika siku hizi zilizopita.

Kwa hiyo, Idara zinazoshughulikia masuala ya usafiri likiweipo hili la mashulen i pamoja na maeneo mengine yanayobeba abiria, wabainishe vitu ambavyo vinatakiwa, wawapatie wamiliki na kwa shule wiki hizi mbili, zinatosha kuwaandalia masharti hayo. Kipindi cha likizo kinatosha kwa wamiliki wa magari pamoja na wamiliki wa shule kutimiza masharti hayo, lakini shule zitakapofunguliwa watoe taarifa, ukaguzi ufanyike na masharti kwa wanafunzi wanaosafiri mwendo mrefu lazima magari yale yawe yamepitishwa kwamba yanaweza yakabeba abiria kama ambavyo tunafanya kwa mabasi. Tusikamate moja moja kwa rejareja

halafu tukaacha wale ambao hatukuweza kuwaona ama kuwakamata na tukaacha kuwapa masharti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lililosemwa kwa kirefu ni hili jambo la mimba kwa wanafunzi/mimba za utotoni. Waheshimiwa Wabunge, niwaombe kwenye jambo hili tuelewane vizuri na niwaombe tusikilizane vizuri. Moja sisi ni viongozi, na siyo tu viongozi, tena watunga sheria, ni lazima jambo hili tulibebe kwa upana wake, tusilibebe kwa kipengele kimoja kimoja ambapo tutajikuta tunatunga sheria zinazokinzana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, siku tulipokuwa tunapitisha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, mjadala mzito ilikuwa kuhakikisha tunatimiza sheria inayotaka ndoa zifanyike baada ya miaka 18 na kuendelea. Bunge hili na Wabunge hawa pia, Bunge ni Taasisi tulitunga sheria inayosema mtu akibaka ama akampa mimba mwanafunzi anatakiwa kufungwa miaka isiyopungua 30. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tukisema hilo ni kosa, lakini leo hii tukichukua kipengele kimoja kimoja tena kwa kutumia kigezo cha huruma, tukahalalisha makosa hayo kuna sheria zingine tutashindwa kuzitunga na tutashindwa kuzitekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tu jambo ambapo huwa likitokea baya, tunatafuta namna ya kulihalilisha, watu wakipata njaa hatuhangaika kujiuliza kwa nini watu wanapata njaa, tunataka wapewe chakula kama vile kitashuka toka mbinguni. Watoto waki-*fail* sana mtihani hatuhangaiki kwa nini wana-*fail* tunabadilisha *fail* grade ili wafaulu vilevile, leo hii watoto wengi wakipata mimba hatuhangaiki ku-*protect* kwa nini wanapata mimba, kwa nini tuzuie wasipate mimba utotoni, tunahangaika kutaka kunahalisha wapate mimba. Hatuwenzi tukaipa dhambi jina zuri na baadae tukaitukuza, dhambi ni dhambi itabakia kuwa dhambi, hatuwezi tukaipa jina zuri na hatimaye tukaitukuza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi atakaye mpa mimba mwanafunzi tutamkamata, atafika kwenye mikono ya sheria na mzazi atakayeshabikia mwanafunzi kupewa mimba na yeye atakuwa ameshiriki kwenye uovu wa aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto mdogo aliyeko shulenii atakayeruhusu masuala ya kupata mimba ajue anakiuka maadili ya elimu, anakiuka maadili ya mila, anakiuka maadili ya imani na anakiuka maadili ya kisheria za nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mimi najua vizuri Tanzania hii, kuna watu wanajua Tanzania hii kwa vipande vipande. Kwa mfano, katika nchi yetu hata ukiruhusu watoto kurudi shulenii wanaopata mimba, watoto wa Kilimanjaro uwezekano wa kuwepo wanaopata mimba ni mdogo sana. Kwa sababu Kilimanjaro *level yake civililazition, level yake ya sensitization* ya elimu ilishafika juu...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango chake ni kikubwa, lakini leo hii ukiruhusu watoto kupata mimba na kuendelea na shule, halafu ulishaondoa viboko mashulenii, ulishaondoa adhabu mashulenii, huku Bara kwetu wanapomaliza mtihani wa kidato cha nne nusu yao ama wote wa kike watakuwa walishaolewa wana mimba wanasuburi wazae warudi mashulenii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme moja kubwa la ngazi ya watunga sheria kama Wabunge, tuangalie, tusichukue sheria moja tuangalie kwa ukubwa wake. Jimboni kwangu hivi nilivyoongea siyo kwamba natukuza watoto kupata mimba, lakini kama Kiongozi nimefanya hamasa Umoja wa Vijana wa CCM wote wafyatue tofali, nimetoa Mfuko wa Jimbo nikapeleka *cement*, nimepeleka nondo, nikatafuta na wadau tumeanzisha ujenzi wa *hoste/kwa shule*

zote 20 za kata kwenye Jimbo letu, ili kuwatengenezea watoto mazingira yatakayowaondoa kwenye mazingira ya kupata mimba.

Hatuwezi viongozi leo hii tukasema kwa sababu wanapata mimba basi turuhusu waendelee kupata mimba halafu waendelee na shule. Utaratibu gani huu wa nchi gani hii ambao watu wanarahisisha mambo kwa namna hiyo? Hatuwezi tukaruhusu vitu vya aina hiyo, halafu leo hii tukiruhusu aliyepewa mimba akaonekana hana kosa kwa neno lolote zuri tutakaloliweka, yule tunayemshtaki tunamshtaki kwa kosa gani? (*Makofi*)

Mambo makubwa matatu ninayoyasisitiza, moja Wabunge ni watunga sheria, tuangalie sheria hizi zinazokizana kwa mapana yake. Pili, tusiangalie sana suala la mimba hata tukaacha vigezo vingine, manaa yake tunaongelea mimba kama vile mimba inaweza ikaingia halafu mtoto asipate UKIMWI. Tunawasisitizia watoto wakafanye mambo hayo kama vile watapata mimba waendelee na shule, kama vile mimba itaingia halafu asipate UKIMWI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge na Watanzania ni vema tukaweka uzito kwenye suala la maadili, kwenye suala la malezi, tukaweka na mazingira bora ya watoto kukaa bila kupata mimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati naenda kuanza *form one* baba yangu aliniambia ukipata mjukuu mjini usimuache kule, lakini mama yangu akaniambia unavyoenda kule mjini uwe makini kuna UKIMWI kuna mtu tumemzika juzi. Hata kwenda *discosikuenda nikidhania* wote wanaocheza *discowana* UKIMWI, lazima tuwasisitizie watoto wetu madhara ya matatizo wanayoweza kuyapata wakifanya ngono katika umri mdogo na siyo kuwaambia fanyeni ngono mtarudi muendelee na masomo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo Serikali imeendelea kuweka mazingira ambao yanawa... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ahsante, unachukua muda wa Waziri mwenzion sasa. Mheshimiwa Kairuki dakika tano.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme naunga mkono hoja hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapende kipekee kumpongeza sana Mheshimiwa dada yangu, Profesa Ndlichako pamoja na Mheshimiwa Injinia Manyanya, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na utendaji mzima wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya katika usimamizi wa sekta yetu ya elimu, hongereni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kutoa ufanuzi katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa na tunashukuru sana kwa hoja hizo; la kwanza ni kuhusiana na ulipaji wa madai ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo madai ya malimbikizo ya mishahara vilevile yapo madeni ambayo yanahusiana na masuala mengine kama uhamisho, nauli na mengineyo ambayo siyo ya mishahara. Ukiangalia katika mwaka 2015/2016, tuliliwa walimu 18,702 malimbikizo ya mishahara ya zaidi ya shilingi bilioni 13.9.

Vilevile katika mwaka huu wa fedha katika kipindi cha Julai mpaka sasa tulipofikia, tumeweza kulipa madai ya walimu 12,037 yenye jumla ya takribani shilingi bilioni 12.6, vilevile tunaendelea kuhakiki madai yao, pia tumeendelea kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia tumeendelea kuhakiki madai ya malimbikizo ya walimu 8,155 yenye jumla ya shilingi bilioni 9.7.

Ninashukuru sana kwa Wizara ya Elimu kupitia mradi wa *P for R* wameweza kulipa zaidi ya shilingi bilioni 10.5 na Serikali tumeshalipa zaidi ya shilingi bilioni 42.3 kwa watumishi mbalimbali ambao wana madai yasiyokuwa ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo mengine ya malimbikizo tunaendelea kuyafanya wakati wowote uhakiki utakapokamiliika basi yataweza kulipwa. Kulikuwa kuna hoja kwamba wako ambao walipandishwa cheo au vyeo lakini walikuwa hawajarekebishiwa mishahara yao na Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii walitaka kufahamu ni kwa nini suala hili limejitokeza. Kama Wabunge watakumbuka tulipotoa uamuzi wa kuahirisha ajira mpya tarehe 13 Juni, masuala yote haya ya kimaendeleo ya kiutumishi nayo pia yalismama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapoingia katika mwaka ujao wa fedha, watumishi ambao walikuwa wanastahili kupata vyeo vyao wataweza kurekebishiwa na kupata vyeo sahihi nya kimuundo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge katika suala zima la upandishwaji wa vyeo, katika mwaka ujao wa fedha 2017/2018, tumetenga au tumekasimiwa kupandisha vyeo watumishi wa umma 193,166, kwa hiyo tunaamini tutakuwa tuko vizuri na wote wanaostahili kupata vyeo vyao kwa mujibu wa sifa zinazohitajika na vigezo basi wataweza kupandishwa vyeo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya hospitali ya Mloganzila kwamba inashindwa kufaya kazi kutokana na upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba tumeshapeleka watumishi 50 na katika ajira mpya ambazo tumetoa kibali cha Wizara ya Afya na TAMISEMI 258 tumewapelekea tena watumishi wengine kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo walikuwa na nafasi wazi 213, kitu ambapo tunachokifanya sasa tumewapa kibali na kuwahamisha kutoka kwa watumishi wengine walioko ndani ya Serikali na tayari kati ya idadi hiyo 213, watumishi 109 wamesharipoti na tunasubiri hao 104 wengine tunaendelea kujaza nafasi zao kwa njia ya uhamisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea pia na tunatarajia kabla hatujamaliza mwaka huu wa fedha, tutatoa pia kibali cha ajira mpya kwa Mloganzila 105 mpaka tutakapomaliza mwaka huu wa fedha mwezi Juni, watakuwa wamepata watumishi wapya 378 na tutaendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka kuhakikisha kwamba wanapata lkama ambayo wanaweza wakafanya nayo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya upungufu wa walimu pamoja na wataalam wa maabara. Tayari tulishatoa kibali na tumeanza na Walimu wa Sayansi 4,129 na tayari ofisi ya TAMISEMI imeshawapangia vituo wameshaanza kazi. Vilevile tumetoa kibali cha Wataalam wa Maabara 219 na tayari 137 hadi sasa wameshapatikana na tutaendelea kufanya hivyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana

Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, pia nitumie nafasi hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na viongozi wote wa Bunge kwa ujumla kwa jinsi ambavyo mnaliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kusimamia vizuri Serikali kwa niaba ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka 2016/2017 sikufanikiwa kuchangia bajeti kutokana na kifo cha mama yangu mzazi, hivyo basi naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kunitfea katika nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namshukuru Makamu wetu wa Rais, Rais wa Zanzibar pamoja na Waziri wetu Mkuu kwa jinsi ambavyo wananiongoza na kunipa maelekezo na ushauri mbalimbali katika kutimiza wajibu wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako kwa ushauri na mwongozo wake kwangu, ambao umekuwa ukiniongezea ufanisi katika utendaji wangu wa kila siku. Nimekuwa nikijipambanua siku zote kama silaha ya msaada kumbe yeye ni rada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake chini ya uongozi wa Dkt. Leonard Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu Profesa Simon Msanjila na Dkt. Avemaria Semakafu kwa ushirikiano wanaonipa na kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru familia yangu na vilevile nimkumbuke mama yangu mzazi kipenzi Bi Xavelia Mbele pamoja na Marehemu wote waliotangulia wakiwemo wale watoto wa Arusha, ndugu na marafiki wote tunawaombea wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea nawaona wapiga kura wangu wa Jimbo la Nyasa wakitabasamu miyoni mwao kuwa walinchagua Mbunge sahihi, mimi ni mtumishi wao, kwani wao ni bora zaidi, nawapenda sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo, na hivyo naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekitti, nikianzia na *D/T* suala la kupeleka wakaguzi maalum kutokana na kuchelewa kwa ujenzi, lakini pia matumizi makubwa ya fedha. Kimsingi tayari barua ilishaandikwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani yenye Kumbukumbu Na. PL/AC.19/119/01 ili afanye ukaguzi maalum wa mradi huo. Taarifa itakapokamilika itawasilishwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Vilevile napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mradi huo sasa umeendelea vizuri na umefikia asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja ya kutaka kufahamu sifa za kuijunga na Taasisi ya Teknolojia - *D/T*. Kimsingi hapa nitatamka tu sifa za msingi, lakini ni vyema mkawasiliana na chuo au kupitia tovuti yao kuweza kupata taarifa kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kuna ngazi mbili, ngazi ya kwanza ni ya *diploma* ya kawaida ambayo muombaji anatakiwa awe na sifa za kidato cha nne na awe amefaulu angalau *pass* nne kuanzia "C" na vilevile kwa upande wa *degree* awe na *diploma* ya kawaida na *GPA* ya tatu au awe na cheti cha kidato cha sita na awe ana *point* angalau nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na dhana kutoka mionganini mwetu ambayo kuitia michango nimeweza kufahamu kwamba kuna hisia kwamba vyuo vya ufundi sasa hivi vimepungukiwa na viwango tofauti na ilivyokuwa awali. Nipende tu kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba hali ya sasa ni kwamba vyuo hivyo vimeboreshwa zaidi kwa kuweka ngazi mbaalimbali zinazowezesha unyumbu katiaka utoaji kozi hizo. Kwa hali ya mwanzo ilikuwa ni kama unasoma kwa mfano kozi ya ufundi sanifu ilikuwa ni lazima uhakikishe unamaliza kozi nzima na ukikatisha ulikuwa hupati cheti kabisa. Sasa hivi mfumo unakuwezesha kusoma hatua kwa hatua na kila ngazi unayoifikia unapata cheti ambacho kinakuwezesha kufanya kazi zako na pia kuweza kurudi pale inapohitajika kurudi chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *VETA*, hilo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana juu ya mahitaji ya *VETA*. Tatizo kubwa ni upatikanaji wa fedha. Niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao maeneo yao yana majengo na yana ardhi za kuweza kutupa ili kuendeleza tunaomba basi mkamilishe upatikanaji wa hati, ili maeneo hayo yanapoletwa kwetu yasiwe na mgongano. Kwa misingi hiyo napenda kuwapongeza Wabunge ambao wameisha chukua hatua kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mbunge wa Busokelo ambaye alifuatilia na akafuatilia hati kwa Mheshimiwa Mwandosya na hivi sasa chuo cha *VETA* kimeishakamilishwa na wanafunzi wanasoma. Lakini pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wanajituma katika kuchangia katika suala la elimu, wapo wengi. Nafahamu kuna ambao wamechangia uboreshaji wa shule kama Loleza, Mheshimiwa Mbene kwenye eneo lako na wengine wengi naomba tuendelee kushikamana katika hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuendelea kuwa na *VETA* katika kila Wilaya, lakini kwa sasa tutazingatia kuimarisha *VETA* zilizopo kwa kuziongezea

mabweni, walimu pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia, lakini vilevile kuhakikisha kuwa tunaimarisha vyuo vingine kama *FDC* ili viweze kuchukua wanafunzi na kukidhi mahitaji yanayoendana na hali ya sasa. Kwa upande wa *FDC* ni kwamba *FDC* nyingi yaani vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinaonekana kuwa na hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafanya mukutano tayari na wakufunzi wa vyuo hivyo, tuna vyuo jumla 55, na mwaka huu tumeshatenga shilingi bilioni 12 kwa ajili ya kuanza ukarabati katika vyuo hivyo, lakini pia kufuatilia mitaala itakayowezesha kufanya kozi zitakazosaidia wananchi kwa ujumla kwa mahitaji ya soko hasa katika kwenda katika uchumi wa viwanda, vilevile kuzingatia makundi mbalimbali ikiwemo watoto wa kike ambao hawakupata fursa ya kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *COSTECH*. *COSTECH*imekuwa ikiendelea kutengewa fedha, kwa mfano kwa mwaka huu 2016 ilipata shilingi bilioni 45.26 katika fedha hizo kuna ambazo zimetekeleza miradi ya upande wa pili wa nchi (Zanzibar). Kwa mfano *SUZA* katika mradi wa vifaranga vya kaa, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Mpunga na Viazzi Kizimbani, Mwani kwenye *Institute of Marine Sciences*. Pia kwa upande wa Bara kuna taasisi kama *TIRDO* na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali itaendelea kutenga fedha na kuhakikisha kuwa mfuko huo wa *COSTECH* unatumika vizuri, ambao tunaita *MTUSATE* na kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuleta matokeo ambayo yanatarajiwa hasa katika kuongeza thamani ya mazao yetu pamoja na fursa tulizonazo nchini. Vilevile tumeendelea kuongeza nguvu na jitihada katika kituo chetu cha *TEHAMA* na kiatamizi ambacho kinahusika na masuala ya kuibua vipaji mbalimbali vya vijana wetu ambavyo viko pale katika Ofisi za *COSTECH* - Kijitonyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la walimu wa masuala ya sayansi. Nipende tu kukufahamisha kwamba ni

kweli tuna upungufu katika eneo hilo, lakini hata hivyo Serikali imeisha jitahidi kwa mwaka huu, imeweza kuajiri walimu wa sayansi na hisabati 4,129 na baada ya uhakiki wa vyeti nya walimu 3,081 basi ajira hizo zitaendelea tena. Nipende tu kusema kwamba Serikali imekuwa ikiendelea na jithada hizo ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wetu wanapata elimu inayostahili kwa kupewa walimu wenyе sifa pamoja na vifaa nya kufundishia na kujifunzia kama vifaa nya maabara.

Vilevile kwa upande wa mafundi sanifu wa maabara Serikali kwa kushirikiana na vyuo nya ualimu kwa kushirikiana na *TCU* na *NACTE* wataandaa mitaala na kuanza mafunzo kwa ajili ya kuongeza wataalam wa maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala linalohusu ya tatizo la ujinga katika nchi yetu. Kama ambavyo nimejibu swalii la msingi namba 152 la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga tarehe 5 Mei, 2017, ni kweli tuna watu wasiojua kusoma na kuandika yaani vijana na watu wazima asilimia 22.4 kwa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Zipo jithada mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo hilo kuititia *MUKEJA*, lakini pia kuititia Mpango wa Ndiyo Ninaweza, kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na vilevile kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanaotakiwa kuanza shule wanakwenda shule ili kupunguza ongezeko la watu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuititia Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba watoto wote wanaotakiwa kwenda shule wanakwenda kuanzia elimu ya awali na hivi tumeanzisha hata shule shikizi pamoja na kuongeza idadi ya walimu wa elimu ya awali na hivyo kuwezesha kupata wanafunzi wengi zaidi katika eneo hilo. Tunatarajia ifikapo mwaka 2022 wakati wa sensa ijayo Taifa letu liwe limepunguza ujinga na kufikia angalau asilimia si zaidi ya 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya lugha ya alama. Tayari Wizara imeshaanza jithada za kutengeneza vitabu kwa ajili ya kufundisha lugha ya alama. Tunategemea

hali hiyo itawezesha wanafunzi na wazazi wao kupata mawasiliano ya kira hisi lakini pia hata sisi wenyewe kuifahama lugha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna jambo ambalo limejitokeza leo na katika siku hizi za karibuni, niombi kuungana na Mheshimiwa Waziri wangu kwa masikitiko makubwa juu ya mapungufu yaliyojitokeza katika uchapishaji wa vitabu. Hivyo tunawaomba radhi kwa niaba ya wananchi kwa mapungufu hayo. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri wangu atalizungumzia suala hili kwa kina zaidi. Nomba radhi kwa niaba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya nizidi tu kusema kwamba tumedhamiria kama Wizara kuona kwamba elimu inaendelea kutolewa ikiwa bora na kila aina ya tatizo tutajitahidi kadri inavyowezekana kulifanyia kazi na kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanapata fursa ya kusoma vizuri na kupata ajira katika soko linaloendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuunga hoja tena. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama tena mbele yako ili niweze kutoa ufanuzi wa hoja ambayo niliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tarehe 13 Mei, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekito, Waheshimiwa Wabunge wametoa hoja mbalimbali, wakati wakijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba na wajumbe wake kwa kuchambua na kujadili kwa kina bajeti ya Wizara yangu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kuwasilisha vyema Maoni ya Kamati hapa mbele ya Bunge lako Tukufu. Niseme kwamba Wizara yangu imepokea maoni na ushauri ambao umetolewa na Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Naibu Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, na niseme kwamba ushauri ambao wameutoa utazingatiwa na Wizara yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii, kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni mazuri na kwa michango yao ambayo wameitoa katika sekta ya elimu lakini pia ambayo waliitua wakati wakijadili hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo jumla ya Wabunge 85 walichangia kuhusu sekta ya elimu. Katika hoja hii ambayo nimeiwasilisha tarehe 13 Mei; jumla ya Wabunge 53 walichangia hoja kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge 57 walichangia kwa maandishi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa wote kwa michango yao mizuri ambayo hakika itachangia kuimarisha sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala ulikuwa umeletwa kwa hisia na umekuwa ni mjadala ambao umeibua mambo mengi, lakini niseme tu kwamba Wizara yangu inapenda kuhakikisha kabisa Bunge lako Tukufu kwamba ushauri wote ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao unalenga kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu iliyo bora inayoendana na mahitaji ya sasa, Serikali itauchukulia ushauri wao kwa uzito wa hali ya juu na itafanya kazi mapendekezo yote na maoni ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa wakiwa na lengo la kuhakikisha kwamba azma ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi

wa viwanda inaweza kutekelezwa; na wakitambua kwamba elimu ndio nguzo pekee ya kutufikisha hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imejipanga kutoa ufanuzi wa hoja zilizotolewa na kwa kweli kutokana na umuhimu na michango mizuri ya Waheshimiwa Wabunge ningetamani kila ambaye alisimama hapa kuongea au aliyechangia kwa maandishi niweze kumpa fafanuzi. Hata hivyo kutokana na muda nilio nao sitawezza kutoa fafanuzi wa hoja zote. Naomba Waheshimiwa Wabunge mkubali kwamba nitatoa fafanuzi kwa yale ambayo nitawezza kujaliwa kulingana na muda, lakini ninawahakikishia kwamba hoja zenu zote ambazo mmezitoa nitawapa ufanuzi kwa maandishi na nitaziwasilisha kwenu kabla hatujamaliza kikao hiki cha Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa na kwa sababu ya muda na kwa sababu pia siwezi kuwataja Waheshimiwa wote basi nitataja tu hoja bila kueleza nani ameisema, lakini nitakapotoa katika maandishi nitawatambua wote ambao wamezitoa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la elimu maalum. Suala la elimu maalum limezungumzwa kwa hisia kali sana kuhusu changamoto ambazo watoto wetu wa Kitanzania ambao wana mahitaji maalum wamekuwa wakizipata katika jitihada zao za kupata haki yao ya msingi ya elimu. Kwa kweli mambo mengi yamezungumzwa kuhusiana na mazingira ambayo si rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kuhusiana na vifaa vyao vyaa kujifunzia na changamoto nyingine ambazo wanazipata ambapo wengine wanalazimika kukaa shulenii hata hawaendi likizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kama kuna kitu ambacho Wizara yangu inaipa kipaumbele ni hawa watoto wenye mahitaji maalum. Kwa kweli wakati hoja hizo zilipokuwa zinawasilishwa ziligusa sana hisia yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema kwamba suala la watoto wenyewe mahitaji maalum ni kipaumbele katika Serikali ya Awamu ya Tano, na niseme kwamba kwa kuzingatia uzito wa hoja ambazo zimetolewa hata katika vitabu kama kuna mambo ambayo tunaweza tukayafanya tutajitazama upya hata kama ni kufanya *re-allocation* lakini kwa kweli tutahakikisha kwamba tunaweka kasi ya nguvu ya kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ambazo zinawakabili wanafunzi wenyewe mahitaji maalum.

Kwa hiyo, niseme kwamba yote mliyoyazungumza kuhusu wanafunzi wenyewe mahitaji maalum Waheshimiwa Wabunge nimeyapokea na ninawaahidi kwa moyo mkunjufu nitayaafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa na ninaona katika michango ya maandishi Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza ni kuhusiana na suala la ukarabati wa shule kongwe. Kumekuwa na michango mingi ambayo wanaiuliza kwamba mbona hapa hakuna na mpaka nimeulizwa kwamba Waziri hukumbuki ulikotoka, hata shule yako ya *Tabora Girls* haipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi kwamba shule hizi kongwe zinakarabatiwa zote, na tulizo hesabu kwa vigezo ambavyo tulitumia ni zile shule ambazo zimeanza miaka ya zamani miaka ya 60 kwenda mbele, yaani kati ya 60 na 70 ambazo zilikuwa ni shule za Kitaifa. Tunazifahamu shule kama Malangali, Ungwe, *Tabora Girls*, *Tabora Boys*, Kwiro kwa hiyo niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba zote zitakarabatiwa; na kuna mpango wa ukarabati ambao nimewasilisha karatasi kwenu ukionyesha kila shule iko katika mpango gani. Shule ya *Tabora Girls*, *Tabora Boys* zipo katika awamu ya kwanza na zinafadhiliwa na TEA kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge muondoe wasiwasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeulizwa sana hasa katika michango ya maandishi, ni kuhusu vigezo vya kuanzisha kidato cha tano. Waheshimiwa

Wabunge ni kwamba Wizara yangu itagawa kwa sababu ya muda mwongozo ambao mnapaswa kuzingatia katika kuanzisha kidato cha tano. Naahidi kwamba mpaka wiki ijayo nitawapa muongozo kwa utaratibu ambao mnatakiwa muufuate. Hata hivyo Waheshimiwa Wabunge ningependa kuwaambia kwamba shule zote za *A-Level*/ni shule za kitaifa. Ipo dhana kwamba ukibadilisha shule ikawa ya *A-Level*/basi watakaochaguliwa watakuwa ni wale ambao wanatoka katika jumuiya yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iko tayari na itafurahi kupokea maombi na itayafanya kazi. Hata hivyo tutambue kwamba tunapozibadilisha kuwa shule za *A-Level* zinakuwa ni shule za kitaifa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sina haja ya kuusoma muongozo hapa kwa sababu ya muda lakini ninawahakikisha kwamba wote nitawagawia ili muweze kuufahamu na muweze kutekeleza jukumu lenu la msingi la kuhakikisha kwamba mnapeleka elimu si tu elimu ya sekondari ya chini lakini hata na *A-Level* ziweze kuwa nyingi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumziwa na wachangiaji wengi ni suala la ukaguzi wa shule. Wachangiaji wameonyesha kutoridhishwa, kutofurahishwa na mazingira ya ukaguzi shule ambayo yako katika maeneo yetu. Waheshimiwa Wabunge na mimi nikiri kwamba kweli Idara yetu ya Ukaguzi inakabiliwa na changamoto, na ndio maana katika bajeti hii Wizara yangu imetenga fedha hata za kuwawezesha kupata ofisi, kwa sababu wengi wanakaa katika sehemu za kupanga, na sote tunafahamu mambo ya kupanga yana adha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Wizara yangu itaendelea kuimaridha mazingira ya wakaguzi wa shule kwa kutambua kwamba wathibiti wa ubora wa shule, wana mchango wa pekee, wao ndilo jicho letu la kutuambia kitu gani kitaendelea katika sekta ya elimu. Kama Wizara lazima tutahakikisha kwamba tunawapa vitendea kazi, tunawapa mazingira mazuri ya kufanya kazi ili waweze kutuangalizia vizuri elimu yetu katika ngazi zote kwa sababu wao wako

katika sehemu zote kuanzia huko kwenye vijiji mpaka kwenye ngazi ya Taifa; wanaweza wakaona kwa urahisi kama tutawezesha vizuri. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge napokea ushauri wenu na Serikali itaendelea kufanya kazi suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusiana na suala la makato ya asilimia 15 kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu. Niseme kwamba suala hili kuna kesi ambayo imefunguliwa mahakamani *miscellaneous case course* namba 6/2017, kwa hiyo kwa mujibu wa kanuni ya 64(1)(c) cha kanuni za kudumu za Bunge sitawenza kutolea ufanuzi suala hili kwa sababu kifungu hiki kinazuia kujadili mambo ambayo yako mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hoja na mapendekezo ambayo yametolewa na yamekuwa yakitolewa pia hata na Kamati yetu ya kuweza kupitia na kuangalia upya mfumo wetu wa elimu kwa lengo la kuweka misingi imara ili Taifa liweze kupata kasi ya maendeleo hasa sasa hivi ambapo tunatekeleza sera ya viwanda katika awamu hii ya tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali imekuwa ikifanya mapitio ya mfumo wake wa elimu na itaendelea kufanya mapitio ya mfumo wake wa elimu. Hata hivyo kwa kuzingatia kwamba suala hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara mimi ninaomba kwa dhati kabisa, kama kuna maeneo, kama kuna hadidu za rejea ambazo inaonekana ni vema Serikali ikazingatia inapokuwa inafanya mapitio, Wizara yangu iko tayari kupokea. Kama nilivyosema tutaendelea kufanya mapitio kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu iliyo bora. Kwa hiyo, maoni yoyote, ushauri wowote ambao unalenga kumpatia mtoto wa Kitanzania elimu iliyo bora Wizara yangu itaupokea kwa mikono miwili kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa pia suala la uhaba wa wahadhili katika vyuo vyetu vyaa elimu ya juu.

Mimi nikiri kwamba hiyo ni changamoto ambayo ipo na Serikali imekua ikitatua changamoto hiyo kwa kutafuta ufadhilli kutoka kwenye nchi mbalimbali kwa sababu kumekuwa na baadhi ya nchi ambazo waekuwa wakitoa *scholarship* kama vile China, Uingereza, Misri, kuna wanaosoma Ujerumanii kupitia *DAAD scholarship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema *charity begins at home*, katika bajeti hii ambayo Waheshimiwa Wabunge ninaomba sana mnipitishie tumetenga kiasi cha shilingi bilioni nane za kwetu wenye kwa ajili ya kuongezea nguvu ambayo wahadhili wetu walikuwa wakifundisha watoka nje zaidi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba mniunge mkono ili tuendelee kutatua hiyo changamoto ya uhaba wa walimu katika vyuo vyetu vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilmezungumziwa suala la hospitali yetu ya kisasa ya Mloganzila. Kwanza nipokee pongezi za dhati ambapo Waheshimiwa Wabunge wengi wamepongeza kwa hospitali ya kisasa na yenye vifaa tiba vya kisasa. Serikali imepokea pongezi zenu na tunawashukuru sana. Waheshiniwa Wabunge niwahakikishie kwamba kama mnavyoona hiyo ni hospitali ya kisasa imejengwa kwa gharama kubwa na dhamira ya Serikali ya kuanzisha hiyo hospitali iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi amenisaidia kutoa ufanuzi kuhusu ajira za watumishi na Kamati ya Bunge ilisema kwemba nilikuwa nimeahidi nilipokutana nao tarehe 27 Machi, kwamba Serikali itatoa kiasi cha shilingi bilioni tano. Nafurahi kulialifu Bunge lako Tukufu tayari Serikali imekwisha ipatia hospitali ile ya Mloganzila shilingi bilioni tano ili kuiwezesha hospitali hiyo kukamilisha maandalizi muhimu ili tuweze kuifungua rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaamini kwamba ndani ya muda mfupi nitakuja na habari njema na nitawakaribisha Waheshimiwa Wabunge tutakapokuwa tunazindua rasmi huduma katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeongelewa nalo ntaliongea kwa kifupi kwa sababu ya muda ni suala la wamiliki wa shule binafsi na kwa maoni yangu na kwa michango ambayo imekuwa ikisemwa kama kumekuwa na dhana kama vile sasa wamekuwa ni watu ambao hawakubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Waziri mwenye dhamana ya elimu naomba niwatoe wasiwasi na niwahakikishie kabisa kwamba Serikali bado inatambua na kuthamini mchango unaotolewa na sekta binafsi katika sekta ya elimu. Hivyo basi niombe hata Waswahili wanasesma vikombe viwili vikaa pamoja havikosi kugongana. kama kuna mambo ni changamoto za kawaida, mimi sioni kama kuna jambo ambalo mkikaa mkiwa na dhamira, kwa sababu cha kwanza ni dhamira na kukiwa na dhamira hakuna jambo ambalo linashindikana.

Kwa hiyo, naomba sana hizi changamoto ambazo zimezungumzwa nadhani hapa hatuwezi kuzimaliza, lakini niwaambie wamiliki wa shule binafsi tuko pamoja na ninyi na mimi nitaomba tuwe na kikao ili tuweze kukaa kwa pamoja tuangalie kwa kina na tupate ufumbuzi wa moja kwa moja kwa sababu haipendezi kila siku jambo linakuwa linasemwa hilo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye suala ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge na limezungumzwa kwa hisia kubwa sana; suala la wasichana ambao wanapata ujauzito wanapokuwa shulen. Nimesimama hapa nikiwa kama mama, kama mzazi na kama Waziri mwenye dhamana ya elimu. Hili suala ukitazama michango ambayo imetolewa ni suala ambalo kwa kweli inabidi tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwanza inasikitika sana inapoona watoto wa kike wanakatisha ndoto zao za elimu kutokana na sababu yoyote ile ikiwemo ya mimba. Ninafahamu kwamba mimba kabla ya ndoa inaathiri sana hata kisaikolojia kwa sababu unakuwa kama vile hata

ukubaliki na kadhalika. Kwa hiyo, kunakuwa na madhara makubwa ambayo yanakuwa yanajitokeza. Pamoja na tatizo kubwa la mimba za utotoni kwa watoto wa shule ambao wanakuwa wanakosa fursa ya kuendelea lakini lipo tatizo pia kubwa la utoro shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningeomba nitoe takwimu, ukiangalia takwimu za kitabu cha elimu *Basic Education Statistics* cha mwaka 2016, ambacho nitaomba Waheshimiwa Wabunge wote wapatiwe nakala mapema iwezekanavyo. Takwimu zinatuonesha kwamba katika mwaka 2015 wanafunzi wa kike ambao waliacha shule ya msingi kwa ajili ya ujauzito walikuwa 251, na watoto wa kike walioacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito walikuwa 37,658. Ukienda kwa watoto wa kiume walioacha shule kwa utoro ni 44,930.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, tatizo la mimba ni kweli ni tatizo kubwa na linawatesa hata watoto wetu kisaikolojia, lakini naomba niseme kwamba tatizo la utoro ni kubwa zaidi kuliko hata la mimba. Tunapoteza wanafunzi wa kike peke yake 37,658, na hawa ni wa msingi peke yake, ukienda sekondari watoto wa kike walioacha shule kwa utoro walikuwa 26,069 na watoto wa kiume walikuwa 31,209. Ukijumlisha wote wa msingi na wa sekondari jumla yao walioacha shule kwa utoro ilikuwa ni 139,886 na walioacha shule kwa mimba walikuwa 3,637. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, kama ninavyosema Serikali yetu imesaini makubaliano ya kutekeleza mpango wa maendeleo endelevu mwaka 2030 ambapo tunawajibika kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wanaenda shule mpaka sekondari. Kama Waziri mwenye dhamana ninatambua hivyo na ninapoona kwamba unakuwa na wanafunzi 139,000 ambao hawaendi shule kwa sababu ya utoro, Waheshimiwa Wabunge ninaomba sote tuungane kwa kuhakikisha kwamba kwanza tunashughulikia tatizo la utoro shulenii. Kwa sababu tatizo la utoro shulenii ndilo ambalo linapoteza vijana wengi zaidi kuliko hata mimba. Tukianza

na tatizo la utoro tutakuwa tumeokoa vijana wengi zaidi.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie suala la wanafunzi ambao wanapata mimba shulenii. Nchi yetu inaongozwa kwa sheria, kanuni na taratibu na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge sisi wenyewe ndio ambao tunatunga sheria. Ninashukuru sana watu ambao wamegusia sheria ambayo Bunge hili lilipitisha mwaka 2016, ambayo ilifanya marekebisho ya Sheria ya Elimu na kuweka kifungu ambacho kinatoa adhabu kwa mtu yoyote ambaye anatoa ujauzito kwa mtoto wa kike akafungwe jela miaka 30. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba sambamba na kuzungumzia na mimba shulenii naomba nillifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba zipo sababu nydingine ambazo zinapelekea pia wanafunzi kukosa haki yao ya msingi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika Sheria ya Elimu Sura ya 353 (61)(o) kinatoa utaratibu wa kuandaa kanuni za kuainisha vigezo vitakavyotumika kufukuza mwanafunzi shulenii kutokana na masuala mbalimbali. Kanuni ya nne ya elimu ya mwaka 214 inatoa mwogozo kuhusu mambo ambayo yanaweza yakasababisha mwanafunzi akafukuzwa shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niyasome kwa ridhaa yako, kwanza, utovu wa nidhamu wa makusudi unaojirudiarudia na unaohatarisha nidhamu ya wanafunzi shulenii au kuharibu hadhi ya shule kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, kufanya makosa ya jinai kama vile wizi, kuharibu mali za umma na mali za shule; tatu, uasherati; ya nne dawa za kulevyia; ya tano kosa lolote jingine ambalo litaenda kinyume na maadili bila kujali kama aliwahi kutumikia kosa hilo au hapana. Nchi yetu imekuwa ikiwajengea vijana malezi ambayo yanazingatia maadili na utamaduni wa kitanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua *feelings* ambazo zimeonyeshwa katika hili suala na kama ninavyosema mimi linanigusa moja kwa moja kwa sababu sitakiwi kumwacha mtoto hata mmoja katika sekta ya elimu, awe mtoto wa kike au awe mtoto wa kiume ni jukumu langu kuhakikisha kwamba anapata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hayo niliyoyaeleza na kwa kuzingatia kwamba pia zipo sababu nyingine ambazo zinasababisha mtu kufukuzwa shule; kutokana na hii sheria mwanafunzi anapobainika anabusiana shulenii anafukuzwa shule, kitendo cha kubusiana tu. Kwa hiyo, ninachotaka kusema kwa nini ninayasema haya yote, niseme nimepokea hoja na hisia za Wabunge wote, lakini kwa kuzingatia haya ambayo ninaelekeza ambayo ninaeleza ninaona pia bado upo umuhimu wa kuliangalia hili jambo kwa mapana yake. Kama tunaangalia basi tuangalie vipengele vyote vinavyosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule na kadhalika lakini pia tuzingatie mila na desturi na vitu vingine ambavyo vinatunza kama kielelezo cha maadili ya utu wa Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza na mimi hili linanitia hasira sana, ni suala la vitabu kuwa na makosa. Mheshimiwa Naibu Waziri wangu ameomba hapa msamaha lakini mimi siwezi kuomba msamaha kwa ajili ya uzembe wa watu, ila nasema nitawawajibisha, siwezi kuomba msamaha kwa ajili ya uzembe wa watu ambao wanalipwa mshahara kwa kodi za Watanzania kufanya kazi yao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kama nilivyozungumza katika hotuba yangu, nilipokea taarifa kuhusu hivyo vitabu na nikiri kwamba sijapata muda binafsi wa kuiangalia; lakini kile kitabu cha kiingereza darasa la tatu binafsi nilikiangalia, ni aibu nilikiangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwamba kitabu cha darasa la tatu cha kiingereza watu walioandika ni aibu, watu wanaaoajiriwa Taasisi ya Elimu kigezo cha chini kabisa cha

elimu ili mtu aweze kuwa Mkuza Mitaala ni *degree*. Hivi mtu ambaye amesoma mpaka akapata *degree*, na elimu yetu sekondari ni kwa kiingereza, hata kama amepita diploma akaenda mpaka akapata *degree* kwa kiingereza, kiingereza cha namna ilie, hili jambo haliwezi kukubalika hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba wote tunafahamu makali ya Serikali ya Awamu ya Tano, kama tumethhubutu watumishi wasiokuwa na vyeti 9,900 kwa mkupuo wakaondoka, hawa wanaotaka kuhujumu elimu yetu ni nani? Hili ni jambo ambalo Serikali inalichukulia kwa uzito wa hali ya juu sana na kila mmoja ambaye amehusika na kadhia hii kila mtu atabeba msalaba wake mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo sema tayari kuna kamati ambayo imeundwa na Wizara yangu ya kuchambua; kwa sababu nimesema kwamba binafsi nimeona kitabu kimoja na kama Waziri mwenye dhamana siwezi kufanya maamuzi bila kuwa na taarifa inayochambua vitabu vyote tayari wataalam wapo kazini wanachambua kitabu kimoja baada ya kingine ili tuweze kubaini ukubwa wa tatito hili na hivyo basi Serikali iweze kuchukua hatua stahiki.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge katika suala hili la vitabu ni kwamba binafsi naungana na ninyi na hata kama mnaweza mkatusaidia kutuonyesha makosa ambayo ninyi mmeyabaini zaidi, Serikali itafanya kazi kwa sababu hatuwezi kucheza na elimu yetu na vitabu ndio chanzo cha maarifa kwa watoto wetu hatuwezi ku-afford kama Serikali tukawa na vitabu ambavyo vina makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umeshanipigia kengele na nisingependa uknipigia kengele ya mwisho, lakini labda tu nizumgumzie jambo moja la mwisho kuhusiana na mabweni ya chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya yameainishwa na ndugu yangu msemaji kambi ya upinzani kuhusiana na ghamama za ujenzi na kwamba hata katika mchango wake wa maandishi amekuwa na wasiwasi kwamba hivi shilingi bilioni 10 zinaweza zikajenga majengo yale yanayoonekana. Niseme kwamba Serikali imetumia *force account* ambayo ni utaratibu ambao uliidhinishwa na Bunge lenyewe ambao unawezesha vifaa kununuliwa moja kwa moja na kazi ikasimamiwa na wakala au Taasisi ya Serikali.

Majengo yamejengwa na Wakala wa Majengo Tanzania, na niseme kwamba Wizara yangu imelipa kiasi cha shilingi bilioni 10 kwa ajili ya majengo na mimi nilikuwa nategemea kwamba mngetupongeza kwamba tumeweza kujenga mabweni kwa bei ambayo ni ya nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala la kwamba hizi fedha hazikupitishwa na Bunge naomba niweke sawa. Ahadi ya kujenga mabweni aliitoa Mheshimiwa Rais wetu tarehe 4/06/2016 alipokuwa Chuo Kikuu cha Dar essalaam na alipokuwa ametoa hata mkiangalia katika vitabu vyenu vya *volume estimates* mtaona kwamba katika mwaka huu wa fedha kulikuwa na shilingi bilioni tano, ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya Chuo Kikuu kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa chuo kikuu cha Dar e salaam. Mara baada ya ahadi hiyo hicho kiasi cha shilingi bilioni tano za mwaka wa fedha 2015/2016 zilipelekwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ukiangalia hata katika vitabu utaona kwamba walikuwa wametengewa shilingi bilioni tisa ambapo tayari bilioni tano zilitolewa kwa ajili ya mabweni na bilioni nne nyingine zitakuwa kwa ajili ya ukarabati kwa sababu mwaka wa fedha haujaisha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie kwamba hakuna kitu ambacho kimekiukwa, na niombe tu kwamba tumpongeze Rais wetu kwa uamuzi mzuri na kweli ametatua tatizo kubwa kwa wanafunzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya ufanuzi wa hoja ambazo nimeweza kuzifanua kutokana na muda, kama nilivyosema hapo awali naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja zenu zote ambazo mmezitoa tutawapa ufanuzi kwa maandishi kabla hatujaondoka katika kikao hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na baada ya maelezo hayo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wote tunapoenda sasa kwenye kupitia mafungu ili kupitisha bajeti yangu naomba wote kwa umaja wenu mniunge mkono ili niweze kuendelea kutumikia katika sekta hii ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, Katibu.

NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 46 - Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia

Kif. 1001 – *Administration and HR Management.....* Sh. 8,936,885,000/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa nimemeshapata majina kwa mujibu wa Kanuni zetu. Ninaye Mheshimiwa Ester Mmasi, tunaye Mheshimiwa Phillipo Mulugo, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Doto Biteko pamoja na Mheshimiwa Peter Serukamba; nitawaita wengine baadaye.

Kwa upande wa CUFyuko Mheshimiwa Ally Saleh, kwa upande wa CHADEMA yuko Mheshimiwa Susan Lyimo,

Mheshimiwa Upendo Peneza na upande wa *NCCR Mageuzi* yuko Mheshimiwa James Mbatia. Tunaanza na Mheshimiwa Ester Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa masikitiko makubwa kutokana na haya tuliyoyaona kwa masuala mazima ya uchapishaji wa vitabu vya kiada kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi, hiki ni kitabu cha darasa la tatu ambacho Mheshimiwa Waziri alikuwa anaki-*quote* pale. Ukiangalia maudhui ya picha lakini pia na *title* haviendani. *Title* tunaambiwa *I Learn English language*, ukiangalia maudhui ya picha huwezi kuwa na *title* kama hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi vina makosa ya kimaudhui yasiyovumilika, vina makosa ya kiuchapaji yasiyovumilika, vina makosa ya kimantiki yasiyovumilika. Lakini si hivyo tu vitabu hivi vimetumia pesa, kodi ya wavya jasho wa Taifa hili shilingi bilioni 108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Hansard* zimeandika na sisi Wabunge tulipitisha hapa kwenye *miscellaneous amendment* juu ya uanzishwaji wa Idara ya Mahakama ya Kifisadi na tukaazimia ubadhilifu wa kuanzia shilingi bilioni moja mtu huyu aende kwenye Mahakama ya Kifisadi. Leo tuna shilingi bilioni 108 ikiwa na picha nzima ya masuala ya ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura hii tulioletewa hapa mbele na tulijojadili yote kwa ujumla wetu, tunaona huu ni uhaini kwa sababu uhaini si tu kutumia Jeshi kuangusha Serikali, uhaini ni pamoja na kutumia udhaifu wa elimu katika kuangusha Taifa na Serikali kwa ujumla. (*Makkofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri asimame na aje aueleze umma wa Watanzania, uwaeleze wavya jasho wa Taifa hili ambao waliridhia kukatwa kodi na kuweza kuchangia maendeleo ya taaluma yetu. Mheshimiwa Waziri, tunaomba utakapokuja hapo uwaeleze umma wa Watanzania ni kwanini mpaka leo watu hawa hawajasitishiwa ukomo wa ajira zao, namba moja.

Lakini pili, kutokana na makosa yasiyovumilika kimantiki kwa nini Kitengo cha *EMAC* kisitoke *Institute of Education* kikarudi chini ya Wizara yako ili uwe na jicho la moja kwa moja katika kusimamia *quality education* kwenye muktadha huu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, sisi tuliopitisha hapa uanzishwaji wa Idara ya Mahakama ya Kifisadi tunahoji leo, ni kwa nini watu hawa wasiwe nao wa kwanza ama wa pili katika kuingia kwenye Mahakama hii ya Kifisadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba Waziri atupe majibu ya kina, majibu ambayo yatakonga mioyo yetu, majibu ambayo yatafuta machozi ya Taifa hili vinginevyo nitashika shilingi.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza katika hitimisho la suala hili, ni kwamba hili suala la vitabu ambavyo hata anachokishika na mimi ninacho hapa ni kwamba kuna Kamati ya Wataalam ambayo inapitia kitabu kwa kitabu ili

tuweze kubaini makosa ambayo pengine engine yanaweza yakaja kugundulika baadaye. Kwa hiyo, tumeona si vyema kuanza kuchukua hatua kabla hatujamaliza mchakato wa uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kwamba kila mmoja aliyehusika atawajibika iko pale pale. Namuomba Mheshimiwa Ester aiamini Serikali, aiachilie shilingi ili nikitoka hapa nikaanze kushughulika nao. Naomba atuamini, tutachukua hatua kama ambavyo nimesema. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili si suala geni, Mheshimiwa Waziri tunakuamini sana, umeambiwa na pande zote wewe sio mwanasiasa. Mwaka jana tulikupa msamaha hapa, tuliona changamoto hizi, leo tena Waziri tunayekutegemea, kweli unatuambia umejipanga kushughulikia?

Mheshimiwa Waziri, kwa kweli Wabunge wenzangu ninaomba msimame, mniunge mkono hoja, Taifa hili litaangamia kama hatutasema. Naomba kutoa hoja, ahsante.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Philip Mulugo, Mheshimiwa Doto Biteko, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Pascal Haonga. Sasa mnakuwa wengi halafu baadae mnasema... ngojeni basi sasa ninyi vipi?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MHE. CECILIA D. PARESSO: Paresto.

MWENYEKITI: Paresso kaa chini! Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Mwijage.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Chegeni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Raphael Chegeni nimeshakuandika, Mheshimiwa Selemani Jafo. Haya, tunaanza na Phillipo Mulugo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii ya vitabu nilikuwa nataka tu Serikali au Mheshimiwa Waziri sijui itakuwaje, jambo hili mimi linanipa kigugumizi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyo *declare Interest* jana, mimi ni mdau wa wamiliki wa shule binafsi na angalau mimi nimebahatika kuingia Bungeni naweza nikasema, lakini wenzangu waliobaki huko nje ni zaidi ya 1000. Vitabu hivi tumeshanunua na vipo shulenii na mimi jana nimeshaagiza kule shulenii wachome kabisa moto. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekopa hela Benki, shilingi milioni 22, *CRDB* na ushahidi upo, nimenunua vitabu darasa la tatu, darasa la nne na sekondari. Sasa nataka njue Serikali itanirudishia fedha au mimi nafanyaje? Ni hicho tu. (*Makof/ Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Doto Biteko.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nieleze tu masikitiko yangu, Profesa Joyce Ndalichako ninayemfahamu mimi ambaye ana *zero tolerance* kwenye *blah blah* leo anazungumza ataenda kulifanyia kazi. Nimesimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mmasi. Kwanza vitabu hivi viko kwenye mfumo wa elimu yetu, kwa maneno mengine

vinaendelea kueneza sumu kwenye mfumo wa elimu yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitarajia tunazungumza namna fulani ya kuvisitisha vitabu hivi *ku-operate* kwenye mfumo wa elimu ili tuokoe. Mimi ni mwalimu, ninajua mtoto anapofundishwa jambo ambalo haliko sahihi ambavyo inakuwa gharama sana kuliondoa kwenye akili yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuamini sana Profesa Ndalichako, umeonesha ukomavu mkubwa mkubwa wa kushughulikia *blah blah* nyangi kwenye sekta ya elimu kwenye nchi hii toka ukiwa *NECTA*. Ninakuomba kwenye jambo hili, nakuomba kabisa kwa dhati, tunaomba jambo hili lipatiwe suluhu ya kudumu hapa hapa Bungeni kwa sababu hakuna fursa nyingine ya kufanya hivyo. Nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na namuomba Mheshimiwa Mmasi usirudishe shilingi kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la vitabu ni jambo nyeti sana. Kama alivyosema Biteko, Joyce Ndalichako namfahamu, ni mchapakazi mzuri sana, lakini anaposema anaenda kuwachukulia hatua, nataka atuambie hivi vitabu ye ye ameviona lini? Kwa sababu hivi vitabu vimetoka toka mwaka jana na Mwongozo unasema Kamishna wa Elimu atavipitia vitabu kwa ajili ya ithibati, *ku-approve then Waziri mwenye Wizara yake atavipitia ku-approve.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka kujuu, Mheshimiwa Ndalichako ulikuwa wapi mpaka vitabu hivi vikatoka, vikaenda mpaka shulen na leo unasema unaenda kuwachukulia hatua, hii hatua ni pamoja na wewe mwenyewe? Kwa sababu na wewe unahuksika, kwa sababu wewe ultakiwa ndiyo u-*approve.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kitabu hiki, mtoto wa darasa la tatu anaambiwa ua ni mdudu halafu leo tukubali? Haiwezekani! Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana hili jambo ni lazima ama iundwe Kamati Maalum ipitie hivi vitabu vyote au Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ipitie ili itoe, tena itoe Maazimio hayo ndani ya Bunge hili ili hivi vitabu visiendelee kutumika shuleni. Nakushukuru. (*Makofii*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mmasi. Kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, ninaamini kabisa vitabu amesema hicho cha kiingereza, hiki cha kuhesabu ni balaa tupu, yaani ni sumu ni janga kwa Taifa, vya kujifunza ni janga la Taifa, cha kuandika wala usiseme, cha mazingira, vyote hivi hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelisema tangu tumevunja *EMAC* hapa, tarehe 5 Juni, 2013. Afadhalii vitabu vya *EMAC* kuliko hivi vitabu viliviyopitishwa na Taasisi ya Elimu hapa. Sasa hili ni janga na Kanuni ya kwanza janga likitokea wote mnakuwa ni kitu kimoja mnapambana na lile janga. Mwaka jana na wewe ulikuwa Mwenyekiti hapo hapo, uliagiza Wizata twende kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii ili tuweze tukachambua kitabu kwa kitabu na tutoe taarifa hapa Bungeni ambayo haikufanyika hapa Azimio la Bunge lillikiukwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect*, vitabu vingine hapa hata ithibati yenyewe havina na vipo ni sumu imesambaa nchi nzima, vitabu vyote vinatakiwa vitolewe. Si hivyo tu, shilingi bilioni 108 tunaomba kwa sababu hatuwezi tukapata muda, basi tuvipeleke kwenye Kamati ya Huduma za Jamii ndani ya Bunge hili hili itoe taarifa tuazimie hapa ili haki itendeke bila kupiga kelele nydingi sana. Namuunga mkono Mheshimiwa Mmasi. (*Makofii*)

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kuunga hoja ya ndugu yangu Ester Mmasi, kwamba kwanza hizi fedha shilingi bilioni 108 ambazo

zimetumika ni fedha nyingi sana na upotevu mkubwa sana wa kodi za Watanzania. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba jambo la kwanza vitabu hivi vingeondolewa vyote, yaani leo tunataka Serikali iweze kutoa tamko kwamba kuanzia sasa vitabu hivi viache kutumika kwa sababu tukiendelea kuvitumia vitabu hivi, Watanzania wenzetu, watoto wetu wataendelea kupata sumu ambayo mwisho wa siku hiyo sumu haitatusaidia kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwanza wangezuia hivyo vitabu na vile ambavyo havijasambazwa bado visisambazwe, ambavyo vimeshasambazwa viache kutumika, iwe ni tamko la Serikali haraka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali iangalie, iende mbele zaidi kwa sababu fedha hizi ni fedha za wavuja jasho; wote ambao wamehusika waweze kuchukuliwa hatua haraka sana. Kama leo hii katika Taifa kuna watu ambao wameshasimamishwa kazi kwa sababu ya makosa madogo. Mimi nadhani kwenye fedha hizi shilingi bilioni 108 inatakiwa tuchukue hatua kali zaidi na liwe fundisho wakati mwagine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, kama ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri kwa kweli ana historia nzuri sana, wote tunamfahamu akiwa pale Baraza la Mitihani. Mimi naomba tu, si aibu kwa sababu hata kwenye hotuba yako ulizungumza mle ukasema kwamba hili suala unalifahamu. Kama ulikuwa unalifahamu mimi niseme tu kwamba si aibu kama Mwinyi amewahi kuijuzulu kwa sababu ya watendaji wake, hata wewe unaweza uka-step down kwa nia njema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa

Ester. Wakati anajenga hoja, Mheshimiwa Ester ameeleza vizuri kwamba kutunga vitabu ambavyo una-*mislead* vijana ni sawa na uhaini na ni kweli kabisa, ukitaka kuliangamiza Taifa, chezea mfumo wa elimu. Kesho utawapa wapi wanasheria watakaoingia mikataba ya Taifa hili ya uhusu madini, kesho tutapata wapi Wabunge watakao kuja hapa kuja kujenga hoja za kulisaidia Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndalichako nadhani pamoja na mambo mengine, Wabunge wanahitaji *commitment* ya aina mbili ambayo mimi nadhani. Aina ya kwanza tunahitaji hivi vitabu kuanzia kesho viondoke shulenii, visitumike tena kwa sababu vitatumika kutunga mitihani ya muhula ambayo kesho kutwa tu itaanza, halafu sisi tunaenda kuchukua hatua baadaye tayari watoto wameshafanya mitihani tutakuwa tumechelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili pamoja na haya aliyojasema Mheshimiwa Waziri Kivuli ni kwamba tunahitaji utueleze ni namna gani hawa waliohusika utawashughulikia haraka iwezekanavyo; na katika hili, wewe unaweza. Kwa hiyo tunahitaji *commitment* ya namna hiyo, kwamba hawa waliohusika wanashughulikiwa ipasavyo haraka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mmasi, na nimo umbe Mheshimiwa Waziri atusaidie. Mheshimiwa Waziri unaelewa sana, vitabu kuna waandishi. Mwandishi akimaliza kuna Mkurugenzi wa Uandishi pale kwenye Taasisi ya Elimu, baada ya yeye kuna Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu, baada ya yeye kuna Kurugenzi ya Shule ya Msingi na Shule ya Sekondari, baada ya yeye kuna Kamishna wa Elimu, kuna Katibu Mkuu.

Sasa hawa wote kwa kweli kwenye jambo hili wamehusika. Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwa mfano kuna huyu Kigba, kuna huyu Profesa Balalusesa, naweza

nikawataja kwa majina wako wengi wameshiriki kwenye hivi vitabu na saini zao zimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na si cha darasa la tatu, hiki ni kitabu cha *english* cha *form four* ni makosa matupu, hiki kitabu cha *geography* cha *form three* ni makosa matupu. Umesema unaunda Kamati kupitia hivi vitabu, Kamati yako haiwezi kutoka kwenye Wizara ya Elimu maana hawa ndio waliopitisha hivi vitabu. Tuambiane ukweli, inawezekana mama wanakuumiza. Haiwezekani waliofanya hivi vitabu vitoke ndiyo uwapelekee waka *review*, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka uje utuambie, nani unampa kazi ya ku-*review* hivi vitabu ili ujiridhishe makosa yote, pili baada ya hapo utuambie wakati mna-*review* hawa *ma-director* wote niliowataja watupishe wakae pembeni wakati mna *review*, na tatu naomba utupe *commitment* ya muda ambao mtakuwa mmemaliza jambo hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naongeza nusu saa kwa mujibu wa Kanuni na sasa namuita Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mmasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitabu wenzangu wameshalichangia lote, wamezungumza, madhara tunayaafahamu. Hata hivyo mimi nimeguswa zaidi na *commitment* ya Waziri. Kwa sababu tuangalie kwamba kwanza Mheshimiwa Waziri ameshatambua tatizo liko wapi na Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kuainisha kwamba ni akina nani wamesababisha tatizo hilo. Mheshimiwa Mulugo amepoteza zaidi ya shilingi milioni 25, hapa hakuna shida kwa sababu gani waliochapisha vitabu wapo, pesa walilipwa, Wakurugenzi wanaotajwa na Mheshimiwa Serukamba wapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ambacho ningesema ni kwamba Mheshimiwa Serukamba ni Mwenyekiti wa Kamati

ya Huduma za Jamii, nadhani angetusaidia zaidi kupitia Kamati yake amsaidie Mheshimiwa Waziri katika suala hili ili Kamati ya Huduma za Jamii iweze kumsaidia Mheshimiwa Waziri kuainisha nini cha kufanya, kwa sababu hawa Wakurugenzi kuwafanya wawe ndio *team* ya kuchunguza na kubaini tatizo hawatafanikisha vile inavyotakiwa, kwanza haitawezekana. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri, mimi nafurahi kwa *commitement* yako...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waitara, Jiandae Mheshimiwa Matiko, halafu jiandae Mheshimiwa Jafo.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Mmasi, na nimuombe tu Mheshimiwa Waziri kwamba tatizo hilo si dogo kiasi hicho. Mimi pia nimepitia vitabu vyatuhusu ambavyo vinatolewa, vina makosa ya *ki-mathematics*, kuna majibu ya uongo. Bahati nzuri sasa hivi Katibu Mkuu ni mwali muhimo wangu amenifundisha *chemistry*. Kule milimani ukikosea *point* kidogo maana yake umeumia. Sasa niunge mkono, kwanza ningeshauri kwamba vitabu hivi vizuiliwe visiendelee kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni muhimu hawa ambao ni wahusika, kwa sababu wakisimamishwa si kwamba ndiyo wamehukumiwa, kuonesha kwamba jambo hili ni baya, wamelihujumu Taifa hili, wametumia fedha za Taifa hili vibaya wangesimamishwa kazi kuanzia sasa wakati uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine la mwisho ni kwamba hapa kuna mlolongo wa wafanyabiashara...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Menyekiti, nakushukuru, na mimi nasimama kuunga hoja ya Mheshimiwa Mmasi kwa masikitoko makubwa sana kama Taifa.

Kwanza tunatia aibu sana, vitabu hivi vimegawiwa takriban ni zaidi ya mwaka, hata kusema tunawawajibisha haisaidii kwa sababu unawawajibisha hao watu, watoto wamefundishwa kwa mwaka mzima na zaidi, je hao watoto utaenda kuwafundisha kwa vitabu ambavyo havijakosewa, ina maana hapo tunakuwa tunajenga Taifa sio la watu walioelimika na tusitegemee kwamba uchumi wetu utaenda kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi Serikali msije mkaona kigugumizi shilingi bilioni 108 ni nyngi mkaamua kusema kwamba viendelee, vifanyiwe marekebisho kidogo, tunaenda kujenga taifa ambalo kwa kweli tutashindwa kuja kueleza hapo baadae tulifanya nini sisi kama Wabunge humu.

Mheshimiwa Mwentekiti, ni fedheha zaidi kwa Mama ya Profesa Ndalichako kusema amesoma kitabu kimoja tu, na kwamba anaunda watu ku-review, hamna haja ya ku-review ukichukua vitabu hivi ukifungua *page* ya 1, 2 ni makosa, tukisema tunaunda tume si kwenda ku-review ni kupoteza hela za Watanzania zaidi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Jafo, jiandae Mwijage, ajiandae AG.

NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hoja hii aliyotoa dada yangu Ester, ni hoja kubwa sana

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba ukiwa na furaha sana usitoe ahadi na ukiwa na hasira sana

usifanye maamuzi ya haraka, hii ndiyo busara ambayo tumefundishwa sana siku zote. Jambo hili ni kubwa lakini nikifanya *reference* ya *commitment* ya Mheshimiwa Waziri na hili jambo sisi tunavyolizungumza, kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao shule hizi zote zipo kwetu na sisi sote ni waathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme kwamba hoja ya Mheshimiwa Mmasi ndiyo hoja ya msingi na Waheshimiwa Wabunge wamesema wameguswa ni jinsi gani wanaguswa na mustakabari wa elimu ya nchi yetu hii. Mimi nina amani na naamini kabisa Mheshimiwa Waziri amesikia hoja hizi kwa upana wake, na amepima uzito wa jambo hili kwa mustakabali wa nchi yetu. Mimi ninaamini Wajumbe wa Bunge hili naomba kwanza ikiwezekana, kwa kauli ya Mheshimiwa Waziri hapa tuweze kuungana naye kwa kadri atakavyozungumza, nina amini atakuwa na njia ya kututolea wapi tunakwenda kwa mstakabiri wa nchi yetu hii. (*Makofii*)

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Bahati mbaya kwa sababu ya muda, Mheshimiwa Mwitaa Waitara alitaka kusema neno muda ukaisha. Hata hivyo Mheshimiwa Mbatia amesema neno, kwamba hili ni janga kubwa. Waheshimiwa Wabunge niwashawishi tukubaliane kwa mawazo mliyoyatoa, hata aliyoysasema Mheshimiwa Serukamba kwamba Kamati ifanye kazi, mimi ninashawishika kwamba isiwe Kamati ya kutoka Wizara ya Elimu, lakini tuiache chini ya dhamana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunaloliona ni janga hili, hili linahusisha na watu wengine aliotaka kuwasema Mheshimiwa Waitara, tuweze kulishughulikia na niwahakikishie na mimi niko kwenye Serikali kila aliyejhuisika atabeba bei ya mauti yake. Tumuachie mama huyu, tumuachie Mheshimiwa Waziri nina uhakika tutapata usuluhisho. Wataalamu wakae, nakubali wasiwe wa Wizaraya Elimu, mtu huwezi ukajishtaki ukajihukumu, tuweze kupata jibu, madhara makubwa yamefanyika na hili ni janga, ndio mapendekezo yangu. (*Makofii*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza tunayo Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Taifa, Taasisi ambayo ndio hii inayoshughulika na mitaala. Kwa mujibu wa sheria hii kifungu cha 4 Taasisi inawajiba yenyewe kwa maamuzi yake ya kusimamia mitaala ya elimu. Licha ya hiyo pia kuna baraza ambalo ndio linalotawala hii taasisi inayosimamia uendelezaji wa hii mitaala. Vile vile chini ya kifungu cha 8 hili baraza linaunda pia Bodi mbalimbali za kusimamia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kushauri zile hoja kwamba Mheshimiwa Waziri na mwenzake wawajibike kwa kweli si hoja mahsus kwa sababu kuwajibika kwa taasisi ambayo kisheria masuala haya yamewekwa kwenye taasisi nyingine, yako kwenye sheria ninayo sheria hapa someni kifungu cha 4, 6 na kifungu cha 8; kwa hiyo, ushauri huu Mheshimiwa Bunge lako linapaswa liupuuze. Waziri ameliona hilo tatizo amelileta hapa anaeleza...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa mbona mnashindwa uvumilivu!

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: ... mnataka tena ye ye awajibishwe, na watu tunajua *seriousness* ya serikali hii kushughulikia kasoro, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba kuna hoja hapa inayozungumzwa kwamba vitabu vimenunuliwa, atafidiwa namna gani? Moja ukitaka kununua kitabu lazima kitabu lazima ujiridhishe na ubora wa hicho kitabu, *let's be aware, so long* Serikali haikumuelekeza anunue vile vitabu, Serikali haiwezi kubeba dhamana ya fidia ya vitu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu hili suala la mashtaka, kuna mapendekezo hapa kwamba..

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Ahsante Mheshimiwa AG
ahsante

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja
mwenyewe tupe maneno yako.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza kwa makini michango
yote ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao
wanaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ester Mmasi ambaye
amenishikia shilingi kutokana na tatizo hili la vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaeleza *commitment* ya
Serikali, na tayari nilishaeleza juu ya hatua za kuchukua dhidi
ya walihusika kwamba zinafanyika. Nimeeleza kwamba ili
niweze kupata taarifa kamili na kufahamu ukubwa wa tatizo
tayari nimeshaunda kamati ya wataalam. Niwatoe wasi wasi
Waheshimiwa Wabunge, hii kamati haihusishi hata mtu
mmoja ambaye alifanya hii kazi mwanzoni. Nimechukua
wataalamu kutoka vyuo vikuu ambao hawakushiriki katika
hii kazi na ninaamini wana uzalendo na wana mapenzi mema
na nchi yetu, na wanasiakia hata hiki kilio na ninaamini kazi
hiyo kwa uadilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inasikitishwa
sana kama nilivyosema na makosa hayo, na tusingependa
wanafunzi wajifunze vitu ambavyo vina makosa. Kwa hiyo,
baada ya kazi hii ya kuititia vitabu vyote kukamilika na
kuainisha makosa, Wizara yangu itachukua hatua na sasa
hapa Mheshimiwa Mwenyekiti hatua zitategemeana na
ukubwa wa makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viro vitabu ambavyo
tunaweza tukaweka *errata* na vile ambavyo vitaonekana
kama havikidhi kabisa Wizara yangu itaviondoa katika soko.
Hatuwezi tukaruhusu vitabu ambavyo vitadhibitishwa na
watumiaji kwamba havifai viendelee kutumika.

Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Ester Mmasi, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote muendelee kuniamini. Mheshimiwa Ester Mmasi niachie shilingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuonesha kwamba Serikali iko *serious* na hili jambo, nina samba kwamba kwa mamlaka niliyonayo kama Waziri mwenye dhamana, ninaziagiza mamlaka ambazo zinahusika na Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania na Kaimu Kamishna wa Elimu wawapishe wakae pembedi kwa sababu nao wamehusika, wasimamishwe kazi mara moja ili kupisha uchunguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba baada ya uchunguzi watu wote waliohusika kuanzia aliyeandika *content*, aliyeihariri kila mmoja atabeba msalaba wake mwenyewe. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Ester, anirudishie shilingi yangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Baada ya *commitment* hii ya Serikali ambayo umezungumza kwa hisia kubwa sana na tatizo ni kubwa sana lakini nichue nichukue kukupongeza Mheshimiwa Waziri umekuwa *bold enough* na umeyasema haya kwa sababu umechukua ushauri mkubwa wa Wabunge ambao wameutoa humu ndani, na mimi sasa nakuagiza ripoti na taarifa hiyo ya utekelezaji wa shughuli yote hii unayoifanya, naitaka uilete Ofisi ya Spika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mmasi, baada ya *commitment* ya Serikali na yote haya.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu nimepata *confidence* nimepata *relief*. Kwa nini ninasema hivi, *of course*, si kwa sura mbaya, tofauti na Naibu Waziri Mheshimiwa Waziri aliposimama cha kwanza alikataa kuomba radhi na akaahidi kuwajibisha wahusika. Si hilo tu, ametuahidi kwamba ataunda Tume huru ya *experts* kutoka vyuo vikuu, hilo linanipa *comfort* kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo isitoshe kilio chetu sisi na maoni yangu mimi na kilio changu mimi kama Ester, nilikuwa nauliza ni vipi hawa watu mpaka leo hawajasitishiwa ukomo wa ajira zao. Lakini pia nimepata jibu kwa Mheshimiwa Waziri. Ninaomba kusema kwamba kwa kauli hii pamoja na *commitment* hii ninaomba nimrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri, ukatende kazi ya Taifa hili. Sisi tunakuamini, Taifa linakuamini, walipakodi wanakuangalia wewe, tunaomba uongoze elimu yetu ya Tanzania. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, haya majina yapo haya mengine mengi tu. Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja; na naomba niseme kabisa mapema kabla sijasahau, kwamba nisipopata majibu mazuri na yanayoridhisha na yanayoleta misingi na mikakati maalum kutoka kwa Serikali kwa kweli nitashika shilingi na kutoa hoja ili Wabunge waweze kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni kuhusiana na wanafunzi ambao wanapata ujauzito wanapokuwa mashuleneni wanatakiwa kurudi shuleneni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili halijaanza leo, suala hili limekuwa likipigiwa kelele na wadau mbalimbali wa elimu, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilipigia kelele kila siku ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi pili mwaka 2017 Mheshimiwa Mama Margret Sitta alisimama ndani Bunge hili akauliza swali la nyongeza ambalo liliikuwa linahusiana na wanafunzi wanaopata ujauzito shuleneni warudi shuleneni, na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu alitoa majibu kwenye *podium* pale na akasema serikali inaenda kuandaa muongozo na kufikia mwezi wa tatu muongozo utakuwa umetoka, ili hawa wanafuzi waweze kurudi shuleneni kuendelea na shule...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE: KITETO Z. KOSHUMA: ...lakini Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nimalizie hoja yangu.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha sasa wewe umeshatoa shilingi kaa tu toa hoja.

MHE: KITETO Z. KOSHUMA: Natoa hoja ili wabunge waweze kujadili

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa waziri

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo aliyoyazungumza Mheshimiwa Koshuma kuhusu ahadi yangu, kama atakumbuka wakati najibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, nilimweleza jambo hili ni jambo linahitaji kuangalia kwa mapana. Vilevile nikasema kwamba kuna sheria nyingi ambazo tumezitunga zinazohusiana na masuala haya na nikamueleza kwamba wadau mbalimbali wamesha kaa na tutaendelea kukaa na wadau wengine kuona namna gani wadau wanachukulia suala hili na vilevile tukasema kwamba endapo litakuwa limekubalika muongozo umeanza kuandaliwa, halafu tukishakubaliana ndio tunaweza tukajua tufanye nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kutafakari na kuangalia sheria nyingi ambazo sisi wenyewe tumezitunga, na kuangalia namna gani tunaweza kuona Taifa letu linaendelea kuwa na maadili, lakini vilevile thamani ya Mtanzania inaendelea kulindwa, vilevile kwa kutambua kwamba nchi yetu ilishafikiria juu ya suala hili kwa sababu kuititia Sera yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014 inaweka utaratibu wa mafunzo endelevu na mafunzo nyumbufu ambayo inamuwezesha huyu mtoto ambaye

anakuwa hakubahatika kuendelea kutokana na kupata ujauzito akiwa mtoto mdogo sana; anaweza kutumia njia nyingine na kumfikisha kwenye Elimu yoyote anayohitaji kufika. Tanzania tayari ilishaweka hilo kuititia Taasisi za Elimu ya Watu Wazima, kuititia *FBCs* na kadhalika, kwa hiyo, mimi naomba utuachilie shilingi tuweze kuendelea.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Koshuma.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti nitaendelea kushika shilingi ya Wizara hiyo ya Elimu kwa sababu kama Serikali tayari ilikuwa imeshasema kabisa kwamba mwezi Machi atatuletea majibu hayo na kwamba mwongozo utakuwa umeshatoka. Mimi naomba Wabunge wenzangu, wanawake kwa wanaume bila kujali itikadi naomba msimame mniunge mkono kwa hoja hii tuweze kujadili, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Joseph Kakunda, Mheshimiwa Mama Salma, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Masoud Salim, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Tuanze na hawa jamani muda wenyewe mnauona na AG. Tunaanza na hawa kwanza, muda wetu mnauona unavyokwenda. Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana kunipa nafasi hii. Mimi napinga hoja kabisa Wanafunzi kupewa mimba shuleni, sababu ninazo, nimezungumza mara ya kwanza hapa na huyu anasema Mama Sitta, Mama Sitta alikuwa Waziri wa Elimu alishindwa hiyo ajenda, mimi wanitajie, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wapo humu wakina mama na wasichana wangapi walianza mapenzi wako shuleni? Na je, elimu yao ilipanda au ilishuka, wanataka kutuletea watoto wa mitaani...?

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MWENYEKITI: Hakuna taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: ...wanataka kutuletea watoto wa zinaa barabarani? *Hiyo napinga hoja moja kwa moja. Kuna watu wamepewa hela na wazungu, wanataka kutuletea ajenda za uongo uongo, tunawafahamu mchana kweupe, wamepewa hela na wazungu, wazungu wale pale juu mmepepesa pesa.* [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ALLY K. MOHAMED: ...hatukubali hoja zenu, mnataka kutuletea ndoa za jinsia moja za kusagana hapa hatukubali.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Masoud.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Kaeni chini, hakuna taarifa.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Hairuhusiwi hiyo kabisa, afute kauli yake, anatugombanisha nchi kwa nchi.

MWENYEKITI: No, no, no, kaeni chini.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Wazungu gani wametoa hela? Kama ye ye hana watoto wa kike anyamaze, aombe radhi.

MWENYEKITI: Kaeni chini!

MHE. PAULINE P. GEKUL: Aombe radhi huyo adhalilisha watu, nani kapewa hela?

MWENYEKITI: Kaeni chini.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mtu gani aliyempa hela yeye, hasemi?

MWENYEKITI: Waheshimiwa kaeni chini.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu atake radhi, atake radhi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Waheshimiwa kaeni chini, kaeni chini! Ngojeni sasa,

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)

MWENYEKITI: Kaeni nitoe nitoe maamuzi yangu? Kaeni chini! Kaeni chini! Wote kaeni chini! Kaeni chini, Bilago kaa chini. Haiwezekani wote msimame mkiendeshe Kiti. Kwa hiyo, kaeni wote chini, tulieni. Mheshimiwa *Chief Whip*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa jambo la utaratibu, na jambo la utaratibu linaongozwa kwa Kanuni ya 64 na Kanuni ya 64 inatuelekeza Waheshimiwa Wabunge kuhusu kutumia vizuri haki yetu ya uchangiaji Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na uhuru wa mawazo ya Mheshimiwa Keissy kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni sina mamlaka ya kuzuia, lakini ninaomba Mheshimiwa Keissy afute tu kauli yake inayohusu wageni ambao wametutembelea katika ukumbi wetu wa Bunge na *Hansard* ibaki na maneno yake yale ya msimamo na mtazamo wake katika hoja ambayo ipo mbele yetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy nilikuwa naomba afute kauli yake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafuta hoja ya wale wazungu, lakini mimi sikumtaja mtu aliyekasirika huyo ndiyo atajijua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, yamekwisha wewe kaa sasa. Tunaendelea kila jambo lina utaratibu wake, hamuwezi wote mkasimama tunaona Serikali ilivyoingilia, kila kitu kinataka subira. Haya Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi kupata mimba halikubaliki, wanaowapa mimba lazima washughulikiwe. Tulitunga sheria sisi wenyewe, hatutaki kuhalalisha wanafunzi kupata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwamba kwa mtindo huu ambao upo, kwamba wanaowapa mimba waachiwe lakini wanafunzi wakipata mimba waende shuleni, tuangalie chanzo chake kwa nini na tatizo ni nini? Tuangalie mambo ambayo yanababisha wanafunzi kupata mimba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napanga kabisa mwanafunzi kupata mimba halafu arudi shuleni hili halikubaliki. Ni lazima wanaowapa mimba washughulikiwe watafutiwe namna nyingine na ikiwezekana wahasiwe.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba watoto wa kike wako ndani ya moyo wangu, ninawapenda sana watoto wa kike na ninapenda sana watoto wa kike wafanikiwe waende mbele katika malengo yao mbalimbali katika maisha yao.

Kwa hiyo naunga mkono sana na nimekuwa nikifanya jitihada na Waheshiwa Wabunge mashahidi katika sehemu ambazo kumekuwa na changamoto za miundombinu ya mabweni nimekuwa mstari wa mbele pale inapowezekana kuweka mazingira mazuri ya watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, ni suala ambalo linagusa hisia na ni suala ambalo pia lina taratibu ambazo sisi kama Wabunge tumeziwekea. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba tunayo mifumo ya kuhakikisha kwamba wanafunzi baada ya kujifungua wanaweza kurejea shulenii na sisi kama Wabunge ambao tunatunga sheria ni vyema tukazisimamia.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa dada yangu Kiteto tuhakikishe kwamba hii sheria ambayo tumeitunga ya mtu anayempa mtoto wa kike anaenda jela miaka 30, tuwapate kwanza wakafungwe, halafu tuone kwamba je, baada ya kutekeleza hii sheria suala litaendelea? Lakini wakati huo huo wale ambao wanaathirika nakuhakikishia kwamba milango iko wazi, tuna njia nyingi za kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itahakikisha kwamba itakuwa inawapa elimu na kwa sababu suala hili limezungumziwa nitoe *commitment* nitafanya utaratibu kwa kushirikiana na Halmashauri ili kuangalia namna mahususi ya kuweza kuhamasisha wanafunzi ambao wanapata ujauzito watumie mifumo mingine ya elimu ambayo tunayo. Kwa hiyo dada yangu naomba tafadhali nirudishie shilingi yangu ili niendelee kutekeleza hili, tafadhali sana.

MWENYEKITI: Ahsante, hili nalo Mheshimiwa Waziri taarifa zako na maamuzi yote unayoyafanya tunataka taarifa zije Ofisi ya Spika ili ishughulikiwe kiutaratibu wa Kibunge. Mheshimiwa Koshuma.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, zime...

MWENYEKITI: Washa *microphone* ili uingie kwenye *Hansard*.

MBUNGE FULANI: Hii inafanya kazi, njoo uongelee hapa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa hebu tuwe wastaarabu kuna mtu anachezea hizi,

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa wakati nahitimisha hoja yangu ninaomba nioneshe masikitiko yangu makubwa sana, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ambao umewaruhusu wamesimama wote wameruhusiwa ambao wamepinga hoja hii. Ninasikitika kwa sababu Kiti chako hakikuweza ku-balance. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha hoja hii nimeshatoa masikitiko yangu na *record* itawekwa. Niliwahi kusema hapa nitakuwa *champion* wa kutetea watoto wa kike na hata siku moja sitarudi nyuma. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Koshuma, wewe amua unarudisha shilingi au unakaa kwa sababu usileté mambo mengine.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unipe nafasi nihitimishe hoja yangu.

MWENYEKITI: Huna muda, hitimisha sasa.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhitimisha hoja hii, naiomba Serikali iwe inakumbuka maneno yake inayokuwa inasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaamini Kamati ya Bunge inafanya kazi kwa niaba ya Wabunge wote. Kamati ya Bunge imeishauri Serikali kwamba mwongozo ule ambao Serikali imekuwa ikuandaa na imesema kwamba itauandaa na kuuleta mwezi Machi, itahakikisha mwongozo ule unaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Wabunge na tayari imekwisha ishauri Serikali, ninaamini kabisa kwamba kabla maneno haya hayajaletwa hapa Bungeni na Kamati, ushauri huu tayari Kamati ilikaa na

Waziri husika na kuyajadili mambo haya. Kwa hiyo mimi nitarudisha shilingi lakini nataka niseme, mnielewe Waheshimiwa Wabunge, nataka niseme kwamba Serikali ihakikishe inakuwa ina-*lead the talk*. mkisema muendane na kile ambacho mnaki...

MWENYEKITI: Ahsante shilingi umesharudisha nakushukuru. Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu!

Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Kif. 1001 – <i>Administration and HR Management</i>	Shs. 8,936,885,000/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 749,200,600/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Shs. 1,316,187,800/=
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Shs. 511,229,000/=
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i>	Shs. 280,886,000/=
Kif. 1006 – <i>Government Communication Unit</i>	Shs. 89,598,200/=
Kif. 1007 – <i>Legal Unit</i>	Shs. 97,416,000/=
Kif. 1008 – <i>Information, Comm, Tech and Elearning</i>	Shs. 771,540,000/=
Kif. 2001 – <i>Basic Education Development Office</i>	Shs. 28,704,565,230/=
Kif. 2002 – <i>School Quality Assurance</i>	Shs. 36,152,797,156/=
Kif. 2003 – <i>Regional & Inter, Edu, Affairs Coord Unit</i>	Shs. 85,334,000/=
Kif. 2004 – <i>Edu Sector Performance Coordination Unit</i>	Shs. 53,164,000/=
Kif. 3001 – <i>Basic Education</i>	Shs. 208,044,000/=
Kif. 3002 – <i>Adult Education & Non Formal Education</i>	Shs. 1,069,472,282/=
Kif. 4001 – <i>Secondary Education</i>	Shs. 352,092,000/=
Kif. 5001 – <i>Teacher Education</i>	Shs. 28,868,283,600/=
Kif. 7001 – <i>Higher Education</i>	Shs. 267,743,957,776/=
Kif. 7002 – <i>Techn. And Vocational Training Division</i>	Shs. 14,012,554,380/=

Kif. 8001 – *Science, Technology
and Innovation*.....Shs. 29,840,211,976/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO

Kif. 1001 – *Administration and
HR Management* Shs. 663,123,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Kif. 1001 – *Administration and
HR Management*..... Shs. 500,000,000/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* Shs. 125,422,978,200/=

Kif. 1008 – *Information, Comm.
Tech and Elearning* Shs.0/=

Kif. 2001 – *Basic Education Development
Office*.....Shs. 123,098,211,381/=

Kif. 2002 – *School Quality
Assurance* Shs. 11,000,000,000/=

Kif. 4001 – *Secondary Education*.....Shs. 0/=

Kif. 5001 – *Teacher Education*.....Shs. 23,860,041,582/=

Kif. 7001 – *Higher Education* Shs. 597,727,456,086/=

Kif. 7002 – *Tech. & Vocational Training
Division*.....Shs. 14,562,110,000/=

Kif. 8001 – *Science, Technology &
Innovation*..... Shs. 20,671,024,751/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Tukae, Mtoa Hoja. (*Makofii*)

TAARIFA

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako likikaa kama kamati ya matumizi imekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)
(Hoja liliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Nachukua nafasi hii kukupongeza Waziri na Naibu wako lakini kuwapongeza na Wabunge kwa mijadala mizuri, ndio Bunge lilitivyo kuna kukubali kuna kukataa.

Kwa hiyo, narudia tena Mheshimiwa kwa *ruling* uliyotoa zote kwa hoja zote mbili, taarifa zote zifike Ofisi ya Spika, haraka iwezekanavyo ili aweze kufanya maamuzi kwa mujibu wa taratibu zetu.

Baada ya maneno haya nawashukuru na Wabunge wote mlioshiriki, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 02.08 Usiku Bunge lillahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 16 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)